**24 MEI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Thelathini na Tatu – Tarehe 24 Mei, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Dkt. Joseph K. Mhagama) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. ASIA A. HALAMGA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya

Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Asia Halamga.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaingia kipindi cha maswali na tunaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, aulize swali lake.

Na. 426

### Kukamilisha Ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata – Maguliwa

**MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Maguliwa ambapo Wananchi wameshakamilisha ujenzi wa Boma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ilipeleka shilingi milioni 201 katika Kata ya Maguliwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD)* ambalo limekamilika na linatoa huduma. Aidha, ujenzi wa wodi mbili unaendelea na umefikia hatua ya linta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mradi wa Usafi wa Mazingira *(Sustainable Rulal Water Supply and Sanitation Program),* katika

mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ilitoa shilingi milioni 74.9, kwa ajili ya uboreshaji wa vyoo, mifumo ya maji safi na majitaka pamoja na ujenzi wa kichomeataka ambapo maboresho ya miundombinu hiyo yamekamilika na inatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kukamilisha ujenzi wa miundombinu iliyosalia katika kituo hicho cha afya kwa awamu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza naishukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa zinazofanyika katika Jimbo la Kalenga. Hivi karibuni tumepokea *ambulance* mbili na vituo vitatu vya afya vimekamilika, kwa sehemu, katika kipindi cha miaka minne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Katika Kituo cha Maguliwa wananchi wamejenga wodi mbili na imekamilika kwa nguvu za wananchi hasa ambayo nimeuliza. Je, Serikali ina mpango gani ije kumalizia angalau tupate wodi ya wanaume na wanawake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Katika Kituo cha Afya cha Kibena, tunaishukuru Serikali imejenga jengo la wagonjwa wa nje, lakini kuna majengo mengine pale ambayo tayari wananchi wameyajenga miaka mingi kidogo. Je, Serikali haioni haja ya kutuunga mkono, ili tumalizie hayo majengo? Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Jackson Kiswaga kwa kazi kubwa anayofanya ya kuwasemea wananchi wa Jimbo la Kalenga. Namhakikishia kwamba, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tutaendelea kumpa ushirikiano na ninapokea pongezi ambazo amempa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa hakika Mheshimiwa Rais

amefanya kazi kubwa sana katika sekta ya afya, amepeleka magari ya wagonjwa katika halmashauri zote 184 na zipo halmashauri ambazo zimepokea gari la wagonjwa zaidi ya moja na magari ya usimamizi. Zoezi hili linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kuhusiana na ukamilishaji wa wodi mbili ambazo wananchi wamechangia na ziko hatua ya linta, Serikali tayari imeshafanya tathmini na tumeona kwamba, tunahitaji shilingi milioni 60 kukamilisha zile wodi. Nakuhakikishia kwamba, tunatafuta fedha, tutapeleka kwa ajili ya kukamilisha wodi hizo mbili ili wananchi wa Maguliwa wapate huduma bora za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, kuhusiana na Kituo cha Afya cha Kibena ambacho majengo yamejengwa hayajakamilika, naomba nitumie nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa waanze kutenga fedha za mapato ya ndani kwa awamu ili kuendeleza ujenzi wa majengo hayo wakati Serikali Kuu ikitafuta fedha kwa ajili ya kuunga mkono juhudi hizo za wananchi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaenda swali linalofuata, Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, aulize swali lake.

Na. 427

**Kuongeza Barabara za Lami – Wilaya ya Kigamboni**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa Serikali kuongeza wigo wa barabara za lami katika Wilaya ya Kigamboni?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2023/2024 Serikali, kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)*, ilitenga shilingi bilioni 2.88 ambazo zilitumika kujenga Barabara ya Tungi – Mjimwema na Chagani Polisi kilomita 2.3 na mifereji yenye urefu wa mita 3,800. Mwaka 2024/2025 zimetengwa shilingi bilioni 2.215 ambazo zitatumika kujenga Barabara ya *Rombo Bar – RC Church,* Kivukoni, *Kivukoni P/S* na umaliziaji wa Barabara ya Chagani – Polisi kwa kiwango cha lami kilomita 1.52 na mifereji yenye urefu wa mita 3,040.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia mkopo kutoka Benki ya Dunia inatekeleza Mradi wa Uendelezaji Jiji la Dar es Salaam Awamu ya Pili *(DMDP II)*. Mradi huo utahusisha ujenzi wa kilomita 42.1 wa barabara za lami, mifereji ya maji ya mvua na madaraja. Hadi sasa mradi huo upo katika hatua za usanifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi wa barabara za lami katika miji, hivyo itaendelea kujenga barabara hizo zikiwemo za Manispaa ya Kigamboni kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, kwa niaba ya Mheshimiwa Faustine.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri. Pamoja na majibu mazuri ninayo maswali miwili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Kwa kuwa, hali ya Barabara za Kigamboni ni mbaya sana, watu wanashindwa kwenda kufanya kazi. Barabara ya kutoka Mji Mwema kwenda Kimbiji Pemba Mnazi haipitiki kabisa. Barabara ya Kibada – Pemba Mnazi mpaka Tundwi Songani haipitiki kabisa, hali ambayo inafanya wananchi wa Kigamboni sasa washindwe kufanya kazi na pia, kupandishiwa nauli za daladala. Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi kuhakikisha barabara hizo zinakwenda kupitika na watu wanaendelea na shughuli zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa, mzunguko wa lami wa barabara za Kigamboni ni mdogo sana ukizingatia

sasa Kigamboni ni eneo ambalo lina viwanda na ni eneo ambalo linakua kiuchumi, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wanajenga barabara mpaka kufika kwenye viwanda hivyo, ili wawekezaji wetu waweze kufanya kazi zao vizuri sana? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza maswali yenye tija sana. Naomba nimhakikishie kwamba, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa miundombinu ya barabara hizi za *TARURA*. Natumia nafasi hii kumwagiza Meneja wa *TARURA* wa Wilaya aweze kwenda kufanya tathmini kuona anachosema Mheshimiwa Mbunge kwa sababu, kama barabara hizi hazipitiki, kipaumbele cha Serikali ni kuhakikisha inarudisha mawasiliano sehemu ambazo hamna mawasiliano.

Kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kumwagiza Meneja aweze kwenda kufanya tathmini ya barabara alizozitaja Mheshimiwa Mbunge kwenye eneo la Mji Mwema, Kibada na Pemba Mnazi ili kuona hali ilivyo na hatua za dharura ziweze kuchukuliwa kuleta mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge ukiacha kwamba, Serikali inatenga fedha katika bajeti ya *TARURA,* lakini nakuhakikishia kwamba, kupitia Mradi wa *DMDP* ambao ni mradi utakaojenga barabara zenye urefu wa kilometa 250 Jimbo la Kigamboni na lenyewe litakuwa ni mnufaika mkubwa sana wa mradi huu. Kwa hiyo, ukiacha tu ujenzi ambao utafanyika kupitia *TARURA,* pia huu Mradi wa *DMDP* ambao unagharimu *US Dollar* milioni 438 utaleta tija kubwa sana katika miundombinu ya Jimbo la Kigamboni.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Mbagala, aulize swali lake.

Na. 428

**Mfereji wa Shegho – Mbagala**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia ujenzi wa Mfereji wa Shegho ambao unaathiri Wakazi wa Kata ya Kiburugwa Jimbo la Mbagala?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfereji wa Shegho una urefu wa kilomita 4.645 ambapo ulianza kujengwa kilomita 3.345 za awali katika awamu ya kwanza, kuanzia mwaka 2015 na kukamilika 2023. Kipande cha urefu wa kilomita 1.3 kufika Mto Mzinga hakikujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kipande kilichobaki cha kilomita 1.3 utatekelezwa kupitia Mradi wa *DMDP,* awamu ya pili, ambao hatua za kumpata mshauri mwelekezi atakayesimamia ujenzi huu zinaendelea. Serikali itaendelea kuihudumia miundombinu ikiwemo mifereji, Wilaya ya Temeke, kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nifanye marekebisho kidogo katika majibu niliyotumiwa hapa. Mfereji huo upo katika Kata ya Charambe, Kilungule, pamoja na Kata ya Kiburugwa tofauti na ilivyoandikwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Kwa kuwa, mfereji huo umeelekeza maji katika makazi ya wananchi na kusababisha familia zaidi ya 50 kupoteza makazi yao, je, Serikali ina mpango gani wa kuzisaidia familia hizo kupata makazi ambayo yameelekezewa maji na mfereji huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri upo tayari kuongozana nami kwenda kujionea familia hizo zinavyoathirika na zinavyoishi katika maisha magumu baada ya kuondokewa na nyumba zao na kuona Serikali itafanya nini, ili kuwarudishia makazi yao?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge, anafanya kazi kubwa sana kuwatetea wananchi wake. Kuhusiana na swali lake la kwanza, naomba nitumie nafasi hii kuikumbusha Halmashauri ya Temeke jukumu lake la msingi la kufanya tathmini ya athari za mvua ambazo zimesababisha mafuriko kwenye mfereji huo na kuathiri wananchi ili kuchukua hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana swali lake la pili. Mheshimiwa Mbunge, mimi nipo tayari, tutakaa, tutazungumza, tutakubaliana ili niweze kuja kujionea mwenyewe athari ambayo imepatikana kwa wananchi wetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dorothy Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Je, ni lini mifereji ya maji Kata za Kilakala, Makangarawe, Vituka na Buza itakuja kurekebishwa ili athari hizi ambazo zinaendelea ziweze kukoma?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali kupitia miradi yake tofauti tofauti, kwa mfano, Mradi wa *DMDP II* ambao unakaribia kuanza katika mwaka wa fedha 2024/2025, ina mpango wa kuja kufanya marekebisho na maboresho ya miundombinu katika jimbo lake.

Kwa hiyo, ukiacha tu kwamba kuna fedha za *TARURA*, lakini bado kuna miradi mbalimbali ya Serikali ambayo inakusudia kuboresha miundombinu katika Mkoa wa Dar es Salaam.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhali.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sina tabia ya kusimama *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Karibu Mheshimiwa Naibu Spika.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Dar es Salaam unachangia pato la Serikali kwa zaidi ya 75% na miundombinu yake ya barabara na mifereji imeharibika sana. Kutokana na shida hii mapato ya nchi yanaweza yakapungua kutokana na miundombinu hii kuchelewesha kuendesha uchumi kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Serikali isitoe Kauli kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri ya Dar es Salaam kuzingatia Sheria ya Manunuzi kwa kutumia Kipengele cha *Emergency Procurement,* ili barabara hizi zitengenezwe kwa fedha za Serikali ambazo zimechangiwa kutoka kwenye Halmashauri zetu na *own source* ambazo tunazo wenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nikizungumzia Manispaa ya Ilala tumeshatenga fedha, lakini mchakato wa kutafuta wakandarasi unachukua muda mrefu sana na kuchelewesha maendeleo ya Dar es Salaam na kuchangia mikoa mingine mapato yanayotoka Dar es Salaam? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa barabara zetu hizi za Wilaya katika uchumi wa Taifa letu. Ni dhahiri kwamba kumekuwa na mvua kubwa sana ambayo imeleta madhara mbalimbali katika miundombinu. Serikali pamoja na kwamba, kuna fedha nyingi ambazo zimetengwa na zinaendelea

kutengwa, inakusudia kuhakikisha inaboresha miundombinu hii. Aidha, kutokana na mvua ambayo bado inaendelea kunyesha katika kipindi hiki, hatua za manunuzi zinaendelea huku tukisubiri mvua ikatike ili wakandarasi waingie uwandani kuanza kufanya marekebisho ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upekee kabisa kwa sababu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tayari imeshatoa maelekezo kwa baadhi ya Halmashauri, na hasa za majiji, ziweze kutenga fedha kutoka kwenye *own source* kwa ajili ya marekebisho mbalimbali ya barabara na kwa sababu, kuna mazingira mengine ambayo barabara zinakuwa hazina mawasiliano kabisa, kwa hiyo, kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa huko awali na Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, basi natumia nafasi hii kukumbusha maagizo yale kwamba Halmashauri za majiji ziweze kuchukua hatua za kidharura kwa sababu, tayari zimeshatenga fedha kwenye *own source* ili ziweze kwenda kufanya marekebisho na hasa kwenye maeneo ambayo mawasiliano yamekatika kabisa na barabara hazipitiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunahamia Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, aulize swali lake.

Na. 429

**Fidia kwa Wananchi Waliopisha Mradi wa Umeme Kakono – Misenyi**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza: -

Je, lini Serikali italipa fidia kwa wananchi waliopisha Mradi wa Umeme Kakono – Misenyi?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, Mheshimiwa Judith Kapinga.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la tathmini ya fidia kwa wananchi wanaopisha mradi wa njia ya kusafirisha umeme Msongo wa kilovoti 220 kutoka Kakono – Kyaka umekamilika na gharama za fidia kwa wananchi wanaopisha mradi huu ni fedha za Kitanzania shillingi billioni 1.543. Malipo haya yanategemewa kuanza kulipwa hivi karibuni, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Florent Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa majibu mazuri. Mradi huu umechukua muda mrefu na wananchi wa Wilaya ya Misenyi wamekuwa wavumilivu, lakini kupitia Serikali sikivu wameendelea kufanya kazi ili kuhakikisha wananchi wanapata haki yao. Sasa nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kwa kuwa fidia hii imechukua muda mrefu na tathmini ilishafanyika, ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba tathmini hii inakidhi muda wa kisheria wa tathmini ili wananchi hao waweze kupata fidia ambayo inaendana na wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, niwaambie nini wananchi wa Misenyi kwamba watalipwa hiyo fidia kwa kuwa wameisubiri kwa muda mrefu sana? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia fidia ya wananchi wake kwa karibu sana. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Serikali tunahakikisha fidia ambayo inalipwa kwa wananchi ni ile ambayo inaakisi muda na wakati. Kwa sasa tupo tayari kwa ajili ya kuanza kulipa na wenzetu wa Wizara ya Fedha wametuhakikishia mpaka ifikapo mwishoni mwa Juni, labda tutakuwa tunaanza kulipa fedha hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa jimbo lake wakae kwa

utulivu, Serikali ni sikivu sana na tupo tayari kwa ajili ya kuanza kulipa fedha hizi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa ni mara ya tatu sasa nasimama ndani ya Bunge kuulizia fidia ya wananchi zaidi ya 246 waliopisha mradi wa umeme toka mwaka 2011. Mheshimiwa Waziri nataka kupata kauli ya Serikali, kwa kuwa sasa ni miaka 13 imepita, ni lini wananchi hawa watalipwa fidia yao kwa mujibu wa sheria?

**MWENYEKITI:** Majibu ya Serikali tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Chege amekuwa akifuatilia suala la fidia la wananchi hawa ambao wako 246 ambapo gharama ya fidia yao ni shilingi 220,000,000. Nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa jimbo lake kwamba, tayari fedha hizi tunazo na tunaanza kulipa wananchi 211 ambao taarifa zao zipo vizuri. Wale wananchi 35 ambao taarifa zao haziko vizuri, tumeielekeza halmashauri jimboni kwake waweze kuzifanyia kazi ili na wenyewe wakae katika mpango wa kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mpaka tunafika Juni 30, wananchi hawa watakuwa wameshaanza kulipwa kwa sababu fedha tayari tunazo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mradi wa *REA*, kuna vijiji vitatu vya Wilaya ya Chemba vilisahaulika; Kijiji cha Kelema Kuu, Kijiji cha Birise na Kijiji cha Muungano na bahati nzuri hatuhitaji sisi fidia, tunahitaji umeme tu. Naomba kujua, ni lini sasa vijiji hivyo vitawekewa umeme? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Monni amekuwa akifuatilia kweli vijiji hivi vitatu ambavyo vilisahaulika katika mpango, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeshafanyia kazi na vijiji hivi vya Kelema Kuu, Birise na Muungano, tayari tumeshaongea na mkandarasi kwa ajili ya kumwongezea wigo ili aweze kuanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa hakuna kijiji kitaachwa kupelekewa umeme katika mradi huu ambao unaendelea. Kwa hiyo, wakae kwa utulivu, Serikali tumesikia na tutapeleka umeme katika hivi vijiji vitatu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Wilaya ya Makete wamepisha ujenzi wa Bwawa la Lumakali na ni takribani mwaka mzima umeisha toka watu wa ardhi wafanye tathmini. Wanauliza, ni lini Serikali itawalipa fedha ili wananchi wetu waendelee na shughuli za kiuchumi kwenye eneo lile?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti ya mwaka unaokuja wa fedha 2024/2025, tumetenga fedha kwa ajili ya kulipa fidia wananchi hawa ambao wamepisha Mradi wa Lumakali. Tunaendelea kufanya tathmini ili kuweza kuelekea kwenye zoezi la fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa malipo ya fidia yapo katika bajeti kwa sababu mradi wa Lumakali ni mradi mmojawapo ambao sisi kama Serikali tunautegemea katika kuzalisha umeme, kwa hiyo, wananchi hawa watalipwa fidia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, sasa aulize swali lake.

Na. 430

**Kumaliza Mgao wa Umeme – Kilombero**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamaliza mgao wa umeme unaokatika kila Jumanne na Alhamisi katika Jimbo la Kilombero?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukatika kwa umeme katika Jimbo la Kilombero kulisababishwa na ujenzi wa barabara ya Ifakara – Kidatu ambapo *TANESCO* ilikuwa na zoezi la kuhamisha nguzo za umeme zilizokuwa ndani ya barabara. Lengo lilikuwa kuruhusu ujenzi wa barabara kufanyika na zoezi hilo kwa sasa limekamilika. Aidha, kukamilika kwa Kituo cha Kupooza Umeme cha Ifakara kumepelekea kuimarika kwa upatikanaji wa umeme wa uhakika katika Jimbo la Kilombero, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Abubakari Asenga tafadhali.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa maswali mawili ya nyongeza. Nataka kukiri mbele yako, kwamba lazima tuuseme ukweli kwamba umeme umepungua kukatika na tangu Waziri wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Biteko afike Kilombero atoe tamko lile kwamba tuna mgodi wa kuzalisha umeme, umeme usikatike, umeme haujakatika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikiri mbele yako, ukiona umekatika ujue basi yule anayeshika *switch* amezoea tu kukatakata lakini haukatiki umeme sasa hivi. Tunaishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Zaidi ya mara mbili nimeuliza maswali mawili madogo ya nyongeza katika Bunge lako kuhusu bei. Kwangu kunaitwa Halmashauri ya Mji wa Ifakara, lakini nina vijiji 48. Katika vijiji hivyo 48, kuna maeneo ya vijiji Kata ya Katindiuka na Kata ya Kidatu wanatozwa bei ya mjini kwa sababu ya hilo jina la Halmashauri ya Mji wa Ifakara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, tuliomba Kata ya Katindiuka na Kata ya Kidatu katika hivyo vijiji ambavyo wanatozwa bei ya mjini, warudushiwe bei ya zamani. Je, ni lini Serikali itarudisha bei hiyo? Hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, niliiomba Serikali vijiji vyangu 15, nikaleta na orodha kwamba viunganishiwe umeme. Je, ni lini vitaanza kuunganishiwa umeme? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Asenga amekuwa akifuatilia sana maendeleo na hususan masuala ya umeme katika jimbo lake. Nakiri kwamba ni kweli hizi kata mbili za Kidatu na Katindiuka amekuwa akizifuatilia kwa karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo yanapaswa kufanyiwa marejesho kwa Tanzania nzima ni mengi sana. Mwaka 2023 wakati Mheshimiwa Rais anafanya ziara Mtwara, alituelekeza Aizara kwamba tupitie maeneo haya upya ili tuone yale ambayo yanatakiwa kulipa shilingi 27,000 na yale ambayo yanatakiwa kulipa shilingi 320,960. Zoezi hili tumeshalifanyia kazi, tumeshaainisha maeneo 1,500 na kwenye jimbo la Mheshimiwa Mbunge, tumeainisha maeneo 10, lakini nakiri, maeneo ya Kidatu na Katindiuka, bado tunaendelea kuyachakata ili kuona na yenyewe kama yanaweza kuingia katika *list* ya yale maeneo 10 na yenyewe tuweze kuyaweka katika mchakato wa kupunguza bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi na Waheshimiwa Wabunge wote, yale maelekezo

ya Mheshimiwa Rais tumeanza kuyafanyia kazi. Tumeshaainisha maeneo 1,500 na tunaendelea kufanya hivyo ili baadaye tutafute mafungu kwa ajili ya kubadilisha kutoka shilingi 320,960 hadi shilingi 27,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la pili la vitongoji 15, tunamaliza, tupo katika hatua za mwisho za zoezi la zabuni ili kuweza kumpata mkandarasi kwa ajili ya kuanza kufanya kazi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kabla ya mwezi huu kwisha, tutakuwa tumepata mkandarasi kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa kupeleka umeme katika vitongoji hivi 15, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kumekuwa na changamoto kwenye miundombinu ya *line* za umeme hasa Mkoa wa Iringa na kusababisha kukatikakatika mara kwa mara na hii kuleta adha kwa wananchi wetu. Je, ni lini mtamaliza changamoto hizi ili wananchi waweze kupata umeme wa uhakika?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Grace Tendega. Suala la kukatikakatika kwa umeme ni kweli linaweza kuwa hivyo kutokana na changamoto ya miundombinu. Kwa kila mwaka wa fedha, tunatenga bajeti kwa ajili ya kurekebisha miundombinu ya umeme kwa ajili ya kupunguza na kumaliza kabisa changamoto ya kukatika katika kwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wa Iringa kwa kiasi kikubwa, tumekuwa tukifanya matengenezo makubwa kwa ajili ya kupunguza kukatikakatika kwa umeme. Mheshimiwa Mbunge ni shahidi, suala la kukatikakatika kwa umeme kwa upande wa Iringa, limepungua kwa kiasi kukubwa sana. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mkoa wa Iringa, tunaendelea kufanyia marekebisho kwenye miundombinu yetu ya umeme ili kuweza kuiondoa kabisa changamoto hii ya kukatika katika kwa umeme.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Ishengoma Christine.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kukatikakatika kwa umeme katika Jimbo la Kilombero ni sawasawa na kukatikakatika kwa umeme katika Manispaa ya Morogoro. Je, ni lini umeme utaacha kukatikakatika katika Manispaa ya Morogoro?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Manispaa ya Morogoro, tumekuwa tukiboresha miundombinu na hata pale katika Kituo cha Kupooza Umeme cha Morogoro, tumefanya *extension* ya kuongeza *transformer* nyingine kwa ajili ya kuimarisha nguvu ya umeme na kuimarisha upatikanaji wa umeme katika Manispaa ya Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa katika Manispaa ya Morogoro, kutokana na kuongeza miundombinu hii, tumeweza kupunguza tatizo la kukatikakatika kwa umeme. Kama nilivyosema hapo awali, kukatikakatika kwa umeme ni changamoto ya miundombinu, na kadiri ambavyo tunaendelea kutenga bajeti, tunaendelea kufanya kazi changamoto hii ili mwisho wa siku tuondoe kabisa changamoto hii katika Manispaa ya Morogoro.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Naomba tuendelee na Wizara ya Katiba na Sheria. Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, aulize swali lake.

Na. 431

**Ujenzi Mahakama ya Wilaya Mbinga**

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga jengo la kisasa la Mahakama ya Wilaya ya Mbinga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jonas Wiliam Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, kama ifuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mbinga inalo jengo la Mahakama ya Wilaya ambalo lilijengwa mwaka 1969, ni kweli kwamba jengo hilo siyo la kisasa. Hata hivyo, jengo hilo bado lina hali nzuri kwa kuwa linafanyiwa ukarabati mara kwa mara. Aidha, huduma za kimahakama zinazotolewa hapo, zinatolewa bila changamoto katika jengo hilo ambalo limeunganishwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kuwezesha utoaji wa huduma kupitia mifumo ya kielektroniki inayotumiwa na Mahakama ikiwemo uendeshaji wa mashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na ukubwa wa changamoto tulizonazo za uhaba na uchakavu wa majengo, kwa sasa, kipaumbele ni kujenga majengo ya Mahakama katika Wilaya ambazo hazina kabisa majengo ya Mahakama, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jonas William Mbunda, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naishukuru Serikali kwa majibu, lakini kama Serikali ilivyokiri kwamba jengo hilo lilijengwa mwaka 1969, ni wazi kwamba jengo hili limechakaa na lipo katika hali ambayo siyo nzuri sana ukilinganisha na majengo mengine yanayojengwa sasa hivi katika maeneo yetu ya wilaya. Bado nasisitiza Serikali ione umuhimu wa kujenga jengo jipya katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja la nyongeza, Kata za Mpepai, Mbangamao, Kikolo, Kihungu pamoja na Kagugu ziko mbali, nyingine zaidi ya kilometa 40 kutoka Mbinga Mjini. Kwa hiyo, bado kuna changamoto kubwa ya kupata huduma za kimahakama katika maeneo haya. Serikali ina mpango gani wa

kuhakikisha kwamba inajenga jengo la Mahakama ya Mwanzo katika maeneo hayo niliyoyatamka?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakiri kwamba uwekezaji kwenye sekta ya Mahakama haukujitokeza kuwa na kipaumbele katika miaka mingi iliyopita, lakini kufuatia mabadiliko ya Serikali ya Awamu ya Sita ambapo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesisitiza zaidi masuala ya haki jinai kuwafikia wananchi, kipaumbele sasa ni kujenga Mahakama hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa ya Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla, hivi sasa katika mwaka ujao, tunajenga Mahakama Jumuishi, Vituo Jumuishi vya Utoaji Haki vinane kwa maana zile Mahakama ngazi ya mkoa zinazochukua, zinajumuisha kuanzia Mahakama ya Mwanzo, Mahakama ya Wilaya, Hakimu Mkazi mpaka Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tunazo Mahakama za Wilaya mpya ambazo zinajengwa jumla 23. Pia tuna Mahakama za Mwanzo zitakazojengwa 78. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunda, nakiri kwamba kwenye eneo lako, kata zilizo mbali namna hii, Mahakama itaona uwezekano wa kuingiza kwenye mpango wake wa ujenzi ili eneo hilo liweze kupata Mahakama, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza. Fedha za kujenga Mahakama ya Wilaya ya Uyui zipo, naogopa sasa bajeti inaisha, bado mwezi mmoja. Lini Serikali itaanza kujenga Jengo la Wilaya ya Uyui?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kwamba ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa

Mbunge, fedha zipo na hatua iliyofikiwa sasa hivi ni ya kumpata mkandarasi. Napenda kumhakikikishia, kwa sababu Mahakama imeona changamoto hiyo, hivi sasa Mtendaji Mkuu wa Mahakama kupitia idara zake za manunuzi, wanaharakisha michakato ya manunuzi ili Mahakama hiyo ujenzi wake uweze kuanza mara moja pamoja na Mahakama nyingine.

**MWENYEKITI:** Tunahamia swali linalofuata, Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Mbunge wa Kilosa, aulize swali lake.

Na. 432

**Ujenzi wa Barabara ya Chanzuru – Melela – Kilosa**

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Chanzuru hadi Melela – Kilosa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Chanzuru - Melela – Kilosa yenye urefu wa kilometa 64.5 imekamilika. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Prof. Palamagamba Kabudi.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, je, Serikali haioni kwamba pamoja na kutafuta fedha za kujenga barabara yote, itafute fedha za kuanza kujenga barabara hiyo awamu kwa awamu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, ni lini Serikali itaanza kutengeneza Barabara ya Ludewa – Batini – Kimamba ambayo imeharibika, ina mashimo na haipitiki? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Kabudi kwa kazi kubwa anayowafanyia wananchi wa Jimbo lake la Kilosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na swali lake la kwanza, Serikali imepokea ushauri na tumekuwa na kawaida, pale ambapo tunashindwa kupata fedha ya kujenga barabara yote, tunaanza kuijenga barabara hiyo kwa awamu na tukianzia hasa maeneo ya miji na maeneo korofi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hilo ombi lake Serikali tumelipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakiri kwamba barabara nyingi sana zimeharibika kutokana na mvua ambayo imenyesha na hususan katika jimbo lake ambapo ni kati ya Ludewa na Kimamba. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Meneja wa Mkoa wa Morogoro ameshaleta maombi na tathmini ya barabara za Mkoa wa Morogoro ikiwepo na eneo hili pamoja na Daraja la Mto Mkondoa ambapo maeneo hayo yaliathirika sana na mvua. Tayari Serikali ipo kwenye hatua za mwisho kabisa kupata fedha ili kwenda kurekebisha maeneo mbalimbali yakiwepo na eneo hili la Ludewa na Kimamba.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Newala – Mbuyuni kupitia Makong'onda, mwaka 2023 ilipata bajeti kiasi cha fedha za kuwezesha upembuzi yakinifu. Ni nini hatima ya barabara hii kwa mwaka huu wa fedha? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa tumekamilisha upembuzi yakinifu na Usanifu wa kina, hatua inayofuata sasa ni kutafuta fedha kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, ninachoweza kumwambia tu Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, baada ya kukamilisha usanifu, basi Serikali inatafuta fedha ili kuijenga kwa kiwango cha lami hiyo barabara. Hiko ndicho tunachofanya Serikali na tutafanya hivyo kwa barabara ya Mheshimiwa Mbunge, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutupatia barabara ya kutoka Tarime Mjini – Nyamongo yenye kilometa 25. Mheshimiwa Naibu Waziri amefika, barabara hii ilikuwa iishe kwa kiwango cha lami Januari, 2024 sasa wameomba ongezeko la muda mpaka Desemba mwaka huu, 2024 wanadai fedha shilingi bilioni 6.8. Shughuli zimesimama kabisa, hakuna kazi ya ujenzi ambayo inaendelea. Je, nini kauli ya Serikali ili barabara ikamilike wananchi wa Tarime Vijijini wapate huduma? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli barabara nyingi zilikuwa zimesimama. Moja, siyo tu kwa sababu ya kutokulipwa, kwa sababu Wakandarasi hawa bilioni sita, haiwezi kumfanya asimame, lakini sehemu kubwa tulikuwa tumesimama kwa sababu ya mvua nyingi inayonyesha na hasa maeneo ambako anatoka Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Wakandarasi wote waliokuwa wamesitisha shughuli kwa sababu ya mvua ama shughuli nyingine, moja ni kwamba Serikali inapeleka fedha warudi kwenye maeneo ili waweze kukamilisha barabara kama walivyoomba zile *extension* kwamba kufika Desemba awe amekamilisha kipande hicho cha barabara, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aysharose Mattembe, swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Kwa kuwa, barabara inayoanzia Sepuka – Ndago hadi Kizaga imechukua muda mrefu kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami, je, ni lini Serikali itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya Serikali kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa barabara hiyo yenye kilomita kama 78, tayari Mkandarasi ameshapatikana na sasa hivi kinachosubiriwa tu ni kumkabidhi *site* ili aanze kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunahamia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 433

**Somo la Uraia na Uzalendo Kuwekwa kwenye Mtaala**

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali isiweke kwenye mitaala somo la uraia na uzalendo ili kizazi kijacho kiwe na uelewa wa haki na wajibu wa raia nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua umuhimu wa kutoa elimu ya uraia na uzalendo kwa kizazi cha sasa na kijacho, ilifanya maboresho ya Mitaala ya Elimu mwaka 2023, ambapo katika maboresho hayo, tayari maudhui kuhusu elimu ya uraia na uzalendo yameingizwa katika mitaala hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kupitia somo jipya la Historia ya Tanzania na Maadili, litakalofundishwa kuanzia Elimu ya Awali hadi Kidato cha Sita, somo la Historia na Maadili litabeba maudhui yanayolenga kumjenga Mtanzania kuwa mzalendo na mwajibikaji anayefahamu historia, desturi, mila na maadili ya nchi yake, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, maswali ya nyongeza.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa sina budi kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya uongozi wa Rais wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo inakuwa sikivu na ni mwaka jana tu tulishauri hapa Bungeni kuhusu elimu hii ya uraia na uzalendo na mwaka huo huo 2023 kazi imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza kwa lengo la kuboresha zaidi. Swali langu la kwanza je, mtaala huu umeshaanza kutumika ama unakaribia kutumika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili ni kwamba, kama umeshaanza kutumika ama utatumika karibuni, kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kurudisha vitabu vilivyokuwa vikitumika zamani? Kwa mfano, Msichana Jifahamu, vitabu ambavyo vina maudhui yanayomjenga kijana wa kiume na wa kike kuweza kujikinga na masuala ya mahusiano yasiyo rasmi wakati wa umri mdogo na yanayosababisha kuharibikiwa kimasomo pamoja na kupotoka kimaadili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Najma Giga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Giga, amekuwa akifuatilia kwa karibu kuhusiana na suala la maadili ya vijana wetu. Kwenye eneo lake la kwanza ambalo anahitaji kufahamu juu ya utaratibu wa mitaala na

utekelezaji wake, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Giga na Bunge lako Tukufu kwamba mitaala yetu mipya imeanza kutekelezwa tokea Januari mwaka huu 2024 na tumeanza kutekeleza kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaanza na elimu ya awali wataanza na mtaala mpya, darasa la kwanza pamoja na darasa la tatu, vilevile kwa kidato cha kwanza. Kwa hiyo mtaala wetu kimsingi umeishaanza kutekelezwa hivi tunavyozungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la pili kwenye masuala ya vitabu vile vya zamani. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba vipo vitabu vya zamani ambavyo tunaendelea kuvitumia mpaka sasa kama vitabu vya kiada na ziada, vilevile yapo maudhui ya vitabu vya zamani vile vitabu havitumiki lakini maudhui yake yameweza kuchomekwa kwenye vitabu vipya ambavyo vimetungwa hivi sasa ambavyo tunatumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile stadi hizi unazozingumza za vijana wetu zimeendelea kufundishwa. Kwa upande wa elimu ya awali, tuna klabu mbalimbali za masomo wanafundishwa vijana wetu stadi mbalimbali zikiwepo na hizi za maisha. Upande wa Sekondari na Msingi stadi hizi za masomo zimeweza kuchomekwa kwenye masomo mbalimbali. Kwa hiyo, nikuondoe wasiwasi mambo haya yote Serikali imezingatia na tutatekeleza kwa kadri ninyi Wabunge mnavyoona inafaa, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea na Mheshimiwa Agnes Hokororo kwa niaba ya Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda sasa aulize swali lake.

Na. 434

**Kutumika kwa Majengo ya Chuo cha *VETA* Chikundi - Ndanda**

**MHE. AGNES E. HOKORORO K.n.y. MHE. CECIL D. MWAMBE** aliuliza:-

Je, lini majengo ya Chuo cha *VETA* Chikundi – Ndanda yataanza kutumika?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa elimu ya mafunzo ya ufundi stadi katika kuimarisha ustawi wa uchumi wa wananchi katika Wilaya ya Masasi. Katika kutambua hilo, Serikali imejenga Chuo cha Ufundi Stadi katika eneo la Chikundi, Ndanda, Chuo ambacho kina jumla ya majengo 17 ambayo ni jengo la utawala, karakana nne, jengo la madarasa, majengo matatu ya maliwato, stoo ya vifaa, bwalo la chakula na jiko, jengo la mlinzi, jengo la kupokelea umeme, bweni la wavulana, bwei la wasichana, nyumba ya Mkuu wa Chuo na nyumba pacha kwa ajili ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo hiki kwa sasa kimeshafunguliwa na majengo yote katika chuo hicho yanatumika. Aidha, katika mwaka 2023/2024 Chuo kimedahili wanafunzi na kuanza kutoa mafunzo, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kumwuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa, majengo hayo yameanza kutumika na amekiri kwamba chuo ni kipya, je, Wizara ina mpango gani wa kuongeza fani zinazofundishwa katika Chuo cha Ufundi *VETA* – Chikundi hasa zitakazowajumuisha vijana wa kike ikiwemo upishi na ushonaji?

(b) Wizara ina mpango gani wa kuongeza majengo kwa ajili ya watumishi ili iendane na mafunzo yanatolewa na idadi ya watumishi ili waweze kufanya kazi zao vizuri? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu mafupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hokororo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoshasema kwenye majibu ya swali la msingi kwamba Chuo hiki kimeishafunguliwa na majengo yote yanatumika, nianze kwanza na swali la fani. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwa sababu chuo hiki ndiyo kwanza tumefungua na tunajua kwamba kuna mahitaji ambayo yanahitajika yakiwemo walimu. Kwa hiyo, nimwondoe hofu kwamba fani hizi zitakuwa zinaendelea kuongezeka kwa kadri mahitaji ya vifaa pamoja na wataalamu kwa maana ya walimu tutakapokuwa tunawapeleka pale, basi fani zitakuwa zinaendelea kuongezeka na tumesema fani ziendane na shughuli za kiuchumi eneo lile ambalo chuo hiki kimejengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa eneo la pili kuhusiana na uongezaji wa miundombinu kwa maana ya majengo, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba vyuo hivi vimejengwa 25 katika awamu ya kwanza katika Wilaya pamoja na Mikoa Minne na tunajenga kwa awamu. Kwa hiyo, awamu ya kwanza ilikuwa tujenge majengo ambayo yatawezesha chuo kuanza kutoa mafunzo, lakini awamu ya pili itakuwa sasa ni kuongeza miundombinu ikiwemo na nyumba za watumishi pamoja na miundombinu mingine ambayo itakuwa inahitajika kwa ajili ya kutoa mafunzo kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo niwaondoe wasiwasi, siyo tu hapa Chikundi lakini kwa vile vyuo vyote 25 ambavyo tumejenga na vile vinne vya mikoa na hivi sasa Mheshimiwa Rais ameishatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyuo 64 katika Wilaya 64 na Chuo kimoja cha Mkoa kule Songwe, tunaendelea na ujenzi huo na unakwenda kwa awamu, nakushukuru.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo aulize swali lake.

Na. 435

**Mbegu ya Ng'ombe ya Asili ya Ufipa**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha mbegu ya Ng'ombe ya asili ya Ufipa haipotei?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, tafadhali.

Waheshimiwa Wabunge, maswali ya nyongeza yawe mafupi inavyowezekana na Serikali mjielekeze kwenye hoja moja kwa moja kwa sababu tuna changamoto ya muda. Karibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha mifugo ya asili ikiwemo ng'ombe aina ya Ufipa haipotei, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mifugo *(TALIRI)* ilianzisha vituo viwili vya Kongwa na *West* Kilimanjaro kwa ajili ya kuhifadhi mifugo ya asili ambapo Kituo cha Kongwa kinahifadhi mbari za ng'ombe wa asili na kituo cha *West* Kilimanjaro kinahifadhi mbari za mbuzi na kondoo wa asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati mwingine unaotekelezwa na Wizara wa kuhifadhi mifugo ya asili ni kuvuna na kuhifadhi mbegu za mifugo ya asili ikiwemo mbari aina ya ufipa katika kituo cha Taifa cha Uhimilishaji cha *NAIC* – Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara imepanga kununua madume nane ya ng'ombe wa asili aina ya Ufipa, Gogo, Iringa *red,* Singida *White,* Ankole, Tarime, Sukuma na Maasai kwa ajili ya kuvuna mbegu na kuanza uhifadhi wa vinasaba vya mbari za mifugo ya asili iliyo hatarini kutoweka hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Josephat Kandege swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila inapofikia msimu wa masika kumekuwa kukitokea milipuko ya magonjwa aina tatu ambayo imekuwa ikiua mifugo hii kwa wingi sana. Aina ya kwanza ya ugonjwa ni *black quarter* ambayo wafugaji huita ugonjwa wa kamkono kwa sababu ng'ombe huvimba mkono mmoja wa mbele; aidha kulia ama kushoto. Pia, kuna homa ya mapafu na ugonjwa wa ndiganakali ili kuhakikisha kwamba magonjwa haya yanatibika ni pale ambapo chanjo inafanywa kwa wakati.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba chanjo inafika kwa wakati na inaenezwa katika Wilaya yote ya Kalambo? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa chanjo hizi zimekuwa na bei kubwa, Je, Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba inaweka ruzuku ya kutosha ili wananchi wawe na waweze kumudu kununua chanjo hizi?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anavyosema Mheshimiwa Mbunge. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Kandege kwa jinsi ambavyo amekuwa ni mdau mkubwa sana wa hii sekta ya mifugo na katika swali lake hili anataka kujua jinsi ambavyo Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba inadhibiti hii milipuko ya magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mikakati ya Serikali ni pamoja na kuleta chanjo ya lazima kwa mifugo kuanza mwaka huu na chanjo hii itatolewa bure kwa wafugaji wote walioko ndani ya nchi yetu. Mheshimiwa Rais kupitia bajeti yetu hii ya mwaka 2024/2025 tumetenga zaidi ya shilingi bilioni 27 ambazo zitaelekezwa kwenye chanjo ya mifugo ambayo itasaidia kuzuia hii milipuko ya magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *solution* ya magonjwa haya ya milipuko ni kuhakikisha kwamba wafugaji wetu wanachanja mifugo yao popote pale walipo na chanjo hii itakuwa ni ya lazima, lakini mfugaji atakuwa hachangii chochote, Serikali itasimamia kila kitu katika chanjo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili anataka kujua kwa nini chanjo ziko bei ya juu? Kama nilivyosema, ni kwamba bei ya chanjo inategemea na aina ya ugonjwa ambao mfugaji anataka kuchanja lakini kama nilivyosema kwamba kwa kuanza mwaka huu tutachanja mifugo yetu bure na tunapoendelea wafugaji watapaswa kuwa wanachangia kidogo kigogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *concern* yake ya chanjo yetu kuwa juu, basi tutaendelea kuangalia namna ambavyo tutazungumza na wadau wanaoingiza dawa hizi za chanjo ili kuona namna ambavyo wanaweza wakapunguza bei ya chanjo kwa ajili ya kumrahisishia mfugaji ili aweze kuchanja kwa bei rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ni kwamba wafugaji lazima wafahamu kwamba chanjo hizi ni lazima ili kuifanya mifugo yetu iweze kuendana na soko la dunia kadri ambavyo maelekezo ya Serikali yamekuwa yakitolewa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Fatma Toufiq, kwa ufupi.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo *breed* nane tofauti zitakazohifadhiwa, je, zitatosha kwa ajili ya matumizi ya nchi nzima? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu kwa ufupi Serikali tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi *breed* nane zinatosha kwa sababu ni mbegu ambazo zimehifadhiwa katika kituo chetu cha *NAIC*. Mbegu hizi ikifika muda wa matumizi hutumika, siyo mbegu ya *breed* nane,

hii ni aina nane ya mbegu zilizohifadhiwa, lakini mbegu hizo zinazo uwezo wa kuzalisha ng'ombe hata 10,000, kwa sababu ni mbegu ambazo zimehifadhiwa na huzalishwa kwa njia ya uhimilishaji kwa ajili ya kupandikiza mifugo ambayo ipo katika Taifa letu kadri ya mahitaji yanavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, siyo kwamba ni mbegu nane tu, hapana. Hizo ni aina nane za ng'ombe lakini mbegu hizo zina uwezo wa kuzalisha zaidi ya ng'ombe hata 100,000 kadri ambavyo mfugaji anataka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante. Tunahamia Wizara ya Afya, Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 436

**Kuajiri Kada Tofauti kwenye Hospitali Nchini**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Je, kwa nini Kada zinazowezesha utendaji kazi katika Hospitali hazijumuishwi pindi ajira zinapotangazwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa utaratibu wa ajira wa kada ambazo ni saidizi mfano Wahasibu, Maafisa Ugavi na Madereva unafanywa na Sekretarieti ya Ajira na Utumishi na hivyo hazijumuishwi katika kada za Watumishi wa Afya mfano Madaktari, Wauguzi, Wafamasia na Maabara ambao utaratibu wa ajira husimamiwa na Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza tatizo hili tutaboresha mikakati ya mawasiliano ndani ya Serikali kwa kuonesha mahitaji halisi ya kada hizi ili vibali vya ajira vinavyotolewa vizingatie pia mahitaji ya kada hizo kwa Wizara ya Afya, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rwamlaza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba Serikali imetambua kuwepo kwa kada hizi ambazo zinawezesha hospitali zetu kufanya kazi. Pamoja na kutaja wale uliowataja lakini kuna watu wa TEHAMA, watu wa mifumo ya maji, mifumo ya umeme, ma-*engineer* wa ujenzi na Maafisa Habari.

Je, ni kwa nini Wizara ya Afya isiweze yenyewe kuajiri watu hawa na kuwapa ajira za kudumu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Katika Hospitali ya Mkoa wa Kagera hawa wote niliowataja wameajiriwa na hospitali na inawezekana hata katika sehemu nyingine. Hospitali kutokana na mapato yao wanaelemewa mzigo, wanashindwa kuwalipa mishahara mizuri na kwa wakati unaotakiwa…

**MWENYEKITI:** Swali Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Je, Serikali haioni sasa iwapunguzie kabisa mzigo hospitali ili iweze kuwalipa hawa wawezeshaji na wenyewe wafaidi mishahara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu kwa namna ambavyo ameuliza maswali yake, inaonekana ni kwa namna gani anafuatilia vizuri eneo hili letu la afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge na nimtoe wasiwasi, kwanza ajira ya kudumu haitokani na kuajiriwa na Wizara ya Afya. Ajira ya kudumu haipatikani kwa sababu wameajiriwa na Wizara ya Afya ila kwa kushirikiana na Utumishi, tumekuwa tukiwaajiri watu wote hawa. Kwa mfano, leo ndani ya Wizara ya Afya na hospitali zetu zote kuna watu wa *IT,* watu wa kada nyingine zote ambao wana ajira za kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa juhudi za watumishi wetu na Wakurugenzi wa hospitali zetu, wamekuwa wenyewe wakizalisha mapato yao ya ndani na wakiweza kuajiri kuziba yale ma-*gap* ambayo Serikali haijaweza kuajiri watu hao, lakini Serikali imeweka utaratibu kila wakati vibali vya ajira vinapotoka wanahakikisha hao ambao tayari wanajitolea wanakuwa *accommodated* kwenye ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kufanya mawasiliano na Serikali kama nilivyosema ili kwa kweli hawa wenzetu ambao tayari wamewaajiri wameshazoea mazingira na wanafanya kazi ndani ya hospitali zetu wawe kila wakati wanakuwa *accommodated* ndani ya vibali vinavyotoka kila wakati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunahamia Wizara ya Maji, Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 437

**Uhitaji wa Mradi Mkubwa wa Maji Mikoa ya Lindi na Mtwara**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA K.n.y. MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza:-

Je, lini Mikoa ya Lindi na Mtwara itapata Mradi mkubwa wa Maji kutoka Mto Rufiji ambao upo jirani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na jitihada mbalimbali za kufikia malengo ya kufikisha huduma ya majisafi na salama kwa wananchi kwa 95% mijini na 85% vijijini ifikapo 2025 kwa kutekeleza miradi mikubwa ya maji kwa kutumia vyanzo vya maji vya uhakika ikiwemo maziwa, mito na mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azima hiyo, Serikali inaendelea na mapitio ya usanifu wa mradi wa kutoa maji katika Mto Ruvuma kwenda kwenye Mikoa ya Lindi na Mtwara pamoja na maeneo ya pembezoni yatakayopitiwa na bomba kuu. Aidha, Serikali inaendelea na tathmini ya awali ya usanifu wa mradi wa maji wa kutoka Mto Rufiji kupeleka kwenye Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa lengo la kuhakikisha inaongeza hali ya upatikanaji wa maji katika Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zote hizo zinatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza naipongeza Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina mambo mawili. Jambo la kwanza, naiomba Serikali iendelee na hilo zoezi la kufanya tathmini ya awali kama ilivyoji-*commit* leo ili wananchi wa mikoa tajwa wapate hizo huduma za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kwa kuwa zoezi la usanifu wa kuchukua maji kutoka Mto Ruvuma kwenda Mtwara limehusisha uchukuaji wa maeneo ya watu wa maeneo ya Nanyamba, *Mtwara DC* na Mtwara Manispaa na linahitaji fidia, je, mkakati wa Serikali wa kulipa fidia kwa wananchi wale ambao maeneo yao yamechukuliwa ni upi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, naomba kufanya marekebisho. Nadhani swali limeulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Maimuna Mtanda. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Maimuna, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Maimuna na aliyeuliza swali kwa niaba pamoja na Wabunge wa Mikoa ya Kusini. Hii imekuwa ni ajenda yao kuu ya kuhakikisha kwamba mradi huu wa kutoka Mto Ruvuma

unaharakishwa ili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tayari Serikali imeshaanza kufanya tathmini ya awali ya usanifu na Mheshimiwa Mbunge ametuomba tuendelee nayo, sisi tutaharakisha zoezi hili likamilike ili tuweze kujua kwamba mradi huu utagharimu shilingi ngapi ili tuweze kuchukua hatua za kupata fedha kwa ajili ya kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili. Kama ambavyo nimejibu katika majibu yangu ya msingi, Serikali inaendelea kufanya mapitio ya usanifu ili kuendelea kujiridhisha na pale ambapo bomba kuu litapita na watakaoathirika tuweze kulipa kwa pamoja badala ya kuanza kulipa nusu nusu wakati mapitio yanaendelea. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali italipa fidia pale ambapo mapitio ya usanifu yatakamilika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri.

Tunahamia Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Abdi Hija Mkasha, Mbunge wa Micheweni, swali lake linaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Omar Issa Kombo.

Na. 438

**Kukamilisha Huduma za Kibenki za *CRDB, NMB* na *PBZ* Micheweni**

**MHE. OMAR ISSA KOMBO K.n.y. MHE. ABDI HIJA MKASHA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kurejesha huduma za Kibenki za *CRDB, NMB* na *PBZ* katika Wilaya ya Micheweni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kabla ya benki kufanya uamuzi wa kufungua tawi jipya, benki husika hufanya upembuzi yakinifu ukiwa na lengo la kuangalia kama kuna uwepo wa biashara ya kutosha ambayo italeta faida kwa benki husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki za *CRDB, NMB* na *PBZ* kwa sasa hazina matawi katika Wilaya ya Micheweni. Hata hivyo, Wananchi wa Wilaya ya Micheweni wanapata huduma za kibenki kutoka benki hizo kupitia jumla ya mawakala 27 (*CRDB* 11, *NMB* 12 na *PBZ* 4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika Benki Kuu tayari imetoa idhini kwa Benki ya *PBZ* kufungua tawi katika eneo la Konde lililopo katika Wilaya ya Micheweni, na matayarisho ya kufungua tawi hilo yanaendelea, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Omar Issa Kombo, swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa awali huduma hii ilikuwa inapatikana kwenye Jimbo la Micheweni ambalo lipo Wilaya ya Micheweni; sambamba na hilo, Serikali ya Awamu ya Nane ya Mheshimiwa Dkt. Mwinyi imeweka maeneo ya Maziwang'ombe kama maeneo ya uwekezaji; miundombinu tayari ipo lakini pia kuna ujenzi wa Bandari Rasmi Shumba Mjini ambapo tunatarajia mzunguko wa fedha utakuwa mkubwa. Je, Serikali haioni haja ya kupeleka huduma hii ya Benki kwenye Makao Makuu ya Wilaya ambayo yako kwenye Jimbo la Micheweni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Micheweni wanatumia benki nyingine ikiwemo *CRDB* na *NMB* na Mheshimiwa Waziri amesema wametia mkazo kwenye *PBZ,* je, hawaoni haja ya kuwapelekea wananchi wa Wilaya ya Micheweni huduma ya Benki nyingine ikiwemo *CRDB* na *NMB*? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Omar Issa, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana kwa namna anavyofanya kazi kwa ufanisi na kwa ufuatiliaji wa maendeleo ama wa huduma hizi za kibenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la kwanza. Serikali inatambua ukuaji wa uchumi uliopo katika Mji wa Micheweni ambao umechochewa na uongozi thabiti wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba benki hizi zitaendelea kufanya utafiti na upembuzi yakinifu katika eneo la Mji wa Micheweni. Ikionekana tija ipo, basi huduma hiyo itafunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili. Benki zote hizo nyingine ambazo amezitaja *CRDB* na *NMB* zinaendelea kufanya tathmini katika Wilaya hiyo ya Micheweni, hivyo inawezekana baadaye kufungua Tawi la *CRDB* na *NMB* katika Wilaya hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Tumemaliza kipindi chetu cha maswali ya Wabunge na majibu ya Serikali. Kuna matangazo machache yanayohusu wageni waliopo Bungeni asubuhi ya leo.

Kwanza, tunao wageni waliokaa Jukwaa la Spika ambao ni wageni wa Mheshimiwa Jerry William Silaa, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Tunaye Mhandisi Anthony Sanga - Katibu Mkuu, Bi. Lucy Kabyemera - Naibu Katibu Mkuu; Ndugu Nathaniel Nhonge - Kamishna wa Ardhi; Dkt. Sophia Kongela - Mwenyekiti wa Bodi Shirika la Nyumba la Taifa na Ndugu Hamad Abdallah, Mkurugenzi Mkuu Shirika la Nyumba la Taifa. *(Makofi)*

Pia tunaye Ndugu Charles Saguda - Mkuu wa Chuo cha Ardhi, Morogoro; Ndugu Hamdun Mansoor - Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani; Profesa Wakuru Magigi - Mkurugenzi Mkuu Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi na Ndugu Evelyne Mugasha - Mthamini Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Vilevile tunaye Ndugu Stella Tullo - Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya; Ndugu Andrew Kato - Rais wa *AREPTA* (Chama cha Wataalam wa Milki Kuu Tanzania); Ndugu Hamidu Hemed Mvungi - Mkurugenzi wa *Hamidu City Kigamboni* na Sheikh Mussa Hemed Mfaume - Sheikh Mkuu wa Kata ya Msongola, Wilaya ya Ilala. *(Makofi)*

Tunaye pia Mheshimiwa Edward Mpogolo - Mkuu wa Wilaya ya Ilala; *Comrade* Abbas Mtemvu - Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Dar es Salaam; *Comrade* Adam Ngalawa - Katibu wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam na *Comrade* Juma Simba, *MNEC* Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo pia Mheshimiwa Omary Kumbilamoto - Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Ndugu Ojambi Didas Masaburi - Naibu Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao pia *Comrade* Said Sultan Side - Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Ilala; *Comrade* Ally Bananga Mwatiga - Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo ya Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Dar es Salaam. *Comrade* Bananga naomba usimame. Ahsante nadhani utambulisho umekamilika. *(Makofi/Kicheko)*

Tunaye pia Mheshimiwa Shabaan Mussa - Diwani wa Kata ya *Pugu Station*. *(Makofi)*

Naomba nirejee tu kwa *Comrade* Ally Bananga Mwatiga, sisi shemeji zako tupo, karibu sana Bungeni. Nimetaarifiwa pia na mawifi wapo. *(Makofi/Kicheko)*

Tunao pia Ndugu Mwinyimkuu Sangaraza - Katibu Siasa na Uenezi Wilaya ya Ilala; Ndugu Mohamed Msophe - Mwenyekiti Jumuiya ya Wazazi Ilala; Ndugu Mtiti Jirabi - Katibu wa Wazazi

Wilaya na Ndugu Juma Mizungu - Mwenyekiti wa Vijana Ilala. Hizi zote ni Jumuiya ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Jesca Msengi - Katibu wa Vijana Ilala; Ndugu Neema Kiusa - Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania, Ilala; Ndugu Mariam Bakari - Katibu wa UWT Ilala; Ndugu Salma Fumbwe - Mjumbe Kamati ya Siasa Wilaya ya Ilala; Ndugu Yusuph Lima - Mjumbe Kamati ya Siasa Wilaya ya Ilala; Ndugu Mwantumu Ditopile - Mjumbe Kamati ya Siasa Wilaya ya Ilala na Ndugu Selemani Kaniki, mdau wa michezo Jimbo la Ukonga. *(Makofi)*

Yupo pia Bi. Mariam Makulo Silaa - Mke wa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Tafadhali usimame tena wifi yetu na shemeji yetu. Ahsante sana shemeji na wifi yetu, karibu sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Tunaye pia *Comrade* Simba Jerry Silaa, mtoto wa Mheshimiwa Jerry Silaa na Mjumbe wa Kamati Tendaji ya Chipukizi Chama Cha Mapinduzi Taifa. Hongera sana *Comrade* Simba naona unatosha sana, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni viongozi wa CCM kutoka Wilaya ya Ilala Jijini Dar es Salam. Wote wasimame kwa pamoja. Wale wote wanaotoka Jijini Dar es Salaam kifupi wote wasimame tena. Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi Ilala, wote msimame. Ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 18 wa Mheshimiwa Jumanne Sagini ambaye ni Naibu Waziri wa Katiba na Sheria ambao ni wakufunzi na wanafunzi kutoka Chuo cha Ualimu *Area* "A" cha Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu ambaye ni Mjumbe wa Baraza Kuu Umoja wa Vijana Taifa kutoka Mkoa wa Geita, Ndugu Reuben Emmanuel Sagayika. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mheshimiwa Taska Mbogo ambaye ni mtoto wa kaka yake kutoka Mpanda, Mkoa wa Katavi, ahsante. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mohamed Said Issa ambaye ni mtoto wa rafiki yake kutoka Konde, Pemba Kaskazini. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambao ni watumishi kutoka Kampuni ya Utalii ya Moshi Mjini *African Scenic Safaris* wakiongozwa na Ndugu Elisimbo Natai ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni hiyo. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni watumishi kutoka Halmashauri ya Mbozi, kutoka Vwawa Mkoa wa Songwe. Sijui wapo? Nadhani hawajaingia.

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula ambao ni waumini wa Kanisa la *Ekklesia Revival Ministry* kutoka Dar es Salaam na Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Mhandisi Samweli Hhayuma ambao ni Wachungaji kutoka Jimbo la Hanang, Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 25 wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ambao ni Kikundi cha *Brave Women* kutoka Jimbo la Kigamboni, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 63 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni *Kihesa's Mamas* kutoka Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 44 na walimu watano kutoka Shule ya Msingi *Capstones Christian* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 58 na walimu 10 kutoka Shule ya Msingi *Marangu Hills Academy* kutoka Wilaya ya Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Mwisho, tunao wanafunzi 50 kutoka Chuo cha Uhasibu cha Arusha, ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Kama kuna wageni ambao wapo hawajatangazwa, basi watatangazwa kwa nafasi nyingine.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**MWENYEKITI:** Hoja za Serikali, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo ndani Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyochambua na kujadili bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 3), Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024…

**WABUNGE FULANI:** Omba fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge mmemwambia Waziri aombe fedha, lakini Kanuni zinamtaka asome kwanza. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa, naomba tumpe muda, tumwazime masikio na tumsikilize kwa utulivu. Karibu Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha makadirio

ya mapato na matumizi ya mafungu hayo mawili kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge la Kumi na Mbili ambao ni mahususi kwa ajili ya kujadili Bajeti ya Serikali. Aidha, kwa heshima na taadhima ninaomba kutumia fursa hii kipekee kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ninamwahidi kuwa nitaendelea kutekeleza majukumu aliyonikabidhi kwa juhudi, uadilifu na weledi ili kuleta ufanisi na kukuza ustawi wa maendeleo ya wananchi kupitia sekta ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka mitatu tangu ashike madaraka ya kuongoza Taifa letu. Katika kipindi hiki cha uongozi wake, sekta ya ardhi imepata mafanikio mbalimbali ambayo yanajumuisha uboreshaji wa sera, sheria, taratibu na mifumo ya utoaji wa huduma, kuongezeka kwa kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi nchini, uendelezaji wa makazi, kurahisishwa kwa taratibu za upatikanaji wa haki za ardhi, utatuzi wa migogoro ya ardhi na utoaji wa elimu kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri wao katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia na kuratibu shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninawashukuru kwa maelekezo na ushauri wanaonipa ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu ya kuiongoza sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake mahiri katika kusimamia maslahi na ustawi wa wananchi wa Zanzibar na kuendelea kudumisha Muungano wetu ambao umetimiza miaka 60. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nampongeza Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu pamoja na Naibu Spika Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa kuliongoza na kusimamia kwa umahiri shughuli za Bunge. Aidha, ninakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Dkt. Joseph Kitizo Mhagama kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge. Vilevile, ninampongeza Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge kama Mwenyekiti wa Bunge na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb) kwa kuendelea kusimamia kwa ufanisi shughuli za Bunge kama Wenyeviti wa Bunge. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu awajalie afya njema na hekima ili muweze kutekeleza majukumu ya kusimamia shughuli za Bunge kwa maslahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake ya Bajeti ambayo imewasilisha utekelezaji wa malengo ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika hotuba hiyo imetoa mwelekeo wa utekelezaji wa majukumu ya sekta ya ardhi katika kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi pamoja na upimaji na uhakiki wa mipaka ya vijiji kama njia mojawapo ya kudhibiti migogoro ya ardhi. Ninaahidi kuwa, Wizara itayafanyia kazi masuala yote yaliyoainishwa katika hotuba hiyo ili kufikia malengo ya Serikali yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uongozi wa Mwenyekiti Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge kwa utekelezaji wa majukumu ya usimamizi wa

sekta ya ardhi. Maoni na ushauri ambao wamekuwa wakiutoa mara kwa mara vimesaidia kuongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma za sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaahidi kuendelea kuzingatia maoni na ushauri wao ili kutimiza azma ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuhakikisha kuwa sekta ya ardhi inachangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi wa nchi, kuimarisha usalama wa milki na kudhibiti migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge walioaminiwa na kuteuliwa na Mheshmiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kushika nyadhifa mbalimbali za uongozi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawatakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani na pongezi za dhati kwa viongozi wa Chama cha Mapinduzi katika ngazi zote kwa maelekezo, miongozo, ushauri na ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Ukonga kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa kwa kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa naishukuru familia yangu; mke wangu Bi. Maryam Bakar Silaa na mwanangu *Comrade* Simba William Silaa, kwa kuwa karibu nami na kuendelea kuniunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yangu. Halikadhalika, nawashukuru viongozi wa dini kwa sala na dua ambazo zinanipa nguvu katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wanafamilia wote, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa, marafiki na

Watanzania kwa ujumla kwa kuondokewa na kiongozi wetu mpendwa Hayati Ali Hassan Mwinyi aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika tutaendelea kumuenzi kwa kuleta mageuzi ya kiuchumi na kisiasa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Februari, 2024 Taifa letu lilipata msiba wa kuondokewa na aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Monduli na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa. Natumia fursa hii kumpa pole Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanafamilia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa kumpoteza kiongozi huyo mahiri. Kipekee natoa pole kwa Mheshimiwa Fredrick Edward Lowassa kwa kuondokewa na baba yake mpendwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pole kwako wewe binafsi, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge, na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Wabunge, watumishi wa Ofisi ya Bunge, familia na Watanzania kwa ujumla kwa kuondokewa na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil, aliyekuwa Mbunge wa Kwahani – Zanzibar na Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, aliyekuwa Mbunge wa Mbarali. Hakika michango yao itaendelea kukumbukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mwenyezi Mungu awajalie uponyaji wa haraka Watanzania wenzetu waliojeruhiwa ili waweze kupona na kurejea katika shughuli zao za kila siku za ujenzi wa Taifa. Aidha, tunamwomba Mwenyezi Mungu awalaze Marehemu wote mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Wizara imeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, Mpango wa Tatu

wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026), mpango mkakati wa Wizara, mikataba, itifaki, mipango na makubaliano ya kikanda na kimataifa, sera, sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali ya sekta ya ardhi na maelekezo ya viongozi wakuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kipaumbele yatakayotiliwa mkazo na Wizara katika mwaka 2024/2025 ni kama ifuatavyo: -

(a) Kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi mijini na vijijini;

(b) Kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi;

(c) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika utunzaji wa kumbukumbu, utoaji wa huduma na upatikanaji wa taarifa za ardhi;

(d) Kuhakikisha uwepo wa nyumba bora, ukuaji wa sekta ya milki na maendeleo ya makazi kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii; na

(e) Kuimarisha mipaka ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 163.17 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 43.3 ziliidhinishwa kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 37.61 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 82.13 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za miradi ya maendeleo, shilingi bilioni 14.01 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 68.12 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mahitaji, Wizara iliongezewa bajeti ya shilingi bilioni 287.66 kwa ajili ya kulipa madeni ya wazabuni, watumishi na wakandarasi. Ongezeko hilo limefanya bajeti ya Wizara kufikia shilingi bilioni 405.83.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi tarehe 15 Mei, 2024, jumla ya shilingi bilioni 423.13 zilipokelewa, sawa na 93.86% ya bajeti ya shilingi bilioni 450.83. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 34.72 ni mishahara ya watumishi wa Wizara na taasisi sawa na 79.94% ya bajeti husika, shilingi bilioni 21.94 ni matumizi mengineyo ya Wizara na taasisi, sawa na 56.24% ya bajeti husika na shilingi bilioni 366.47 ni miradi ya maendeleo sawa na 99.48%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha za miradi ya maendeleo zilizopokelewa, shilingi bilioni 309.53 ni fedha za ndani, sawa na 99.52% na shilingi bilioni 56.94 ni fedha za nje sawa na 99.26%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara kupitia Fungu 48 ilipanga kukusanya shilingi bilioni 300. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2024, Wizara imekusanya shilingi bilioni 136 sawa na 45.3% ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jukumu la ukusanyaji wa maduhuli kuhamishiwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara imeendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha kupendekeza jukumu la kukusanya kodi ya pango la ardhi liendelee kutekelezwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na iwezeshwe kwa kurudishiwa sehemu ya fedha *(retention)* kwa ajili ya makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo hili linatokana na sababu mbalimbali zikiwemo; ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi ni jukumu la kisheria lililoainishwa chini ya Kifungu cha 25 na 33 cha Sheria ya Ardhi Sura ya 113, ukusanyaji unahitaji wataalamu wa sekta ya ardhi ambao Wizara ndiyo mamlaka yao ya ajira na nidhamu, na mfumo wa TEHAMA wa Wizara unaotunza kumbukumbu za wamiliki umeunganishwa na shughuli kuu za kisekta za upangaji, upimaji, uthamini na umilikishaji ardhi na hivyo kupunguza changamoto za ukusanyaji zilizokuwepo hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara imepanga kukusanya shilingi bilioni 250 kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. Lengo hili litafikiwa kwa kuendelea

kuimarisha mifumo ya TEHAMA kwa lengo la kurahisisha ukusanyaji wa maduhuli kidigitali; kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na usajili wa ardhi; kuendelea kufuatilia madeni ya kodi ya pango la ardhi kutoka katika mashirika, taasisi za Umma na wamiliki binafsi na kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 8.2. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 2.49 ni mishahara ya watumishi, shilingi bilioni 2.29 ni fedha za matumizi mengineyo na shilingi bilioni 3.41 ni fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi tarehe 15 Mei, 2024, Tume imepokea jumla ya shilingi bilioni 7.33 kati ya bajeti ya shilingi bilioni 8.82, sawa na 83.11% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi bilioni 1.37 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi bilioni 2.55 ni mishahara na shilingi bilioni 3.41 fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya upangaji wa matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Tume ilipanga kukusanya shilingi milioni 18 kutokana na kodi ya pango la nyumba zilizopo Tabora. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2024, shilingi milioni 9.5 zimekusanywa sawa na 53% ya lengo. Aidha, Tume ilipanga kuhamasisha wadau kuchangia kiasi cha shilingi milioni 700 kwa ajili ya shughuli za upangaji wa matumizi ya ardhi. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2024, jumla ya shilingi bilioni 2.77 zilipokelewa kutoka kwa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara iliahidi kuandaa hatimiliki 500,000, hatimiliki za kimila 520,000 na hati za sehemu ya jengo 1,000. Aidha, Wizara iliahidi kusajili miamala ya hatimiliki na nyaraka za kisheria 100,000 na kutoa vyeti vya ardhi 100,000. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, Wizara imeandaa na kusajili hatimiliki 87,240 sawa na 17.4% ya lengo, na hatimiliki za kimila 21,953 sawa na 4.5% ya lengo. Kwa upande wa vyeti vya ardhi ya kijiji, jumla ya vyeti 56 vimeandaliwa sawa na 56% ya lengo; hati za sehemu ya jengo 324 sawa na 32.4% ya

lengo na miamala ya hatimiliki na nyaraka za kisheria 95,456 sawa na 95.46% ya lengo zimesajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza kasi ya umilikishaji, Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji wa Milki za Ardhi, Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (K.K.K), kuboresha mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma na kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi na kampuni zinazofanya kazi za urasimishaji zilizokiuka maadili. Aidha, Serikali kupitia Sheria ya fedha ya mwaka 2023 ilichukua hatua ya kupunguza gharama za umilikishaji kwa zaidi ya 50%. Hatua hiyo zimeongeza kasi ya umilikishaji wa ardhi ambapo hatimiliki zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka hatimiliki 76,746 kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Mei 2023, hadi hatimiliki 87,240 kwa kipindi cha Julai 2023 mpaka Mei, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, utoaji wa hatimiliki umeongezeka kutoka hatimiliki 67,331 mwaka wa fedha, 2020/2021 hadi hatimiliki 86,398 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kutokana na huduma za ardhi kuanza kutolewa katika ofisi za ardhi za mikoa. Ninawahimiza wananchi kote nchini kuendelea kutumia ofisi za ardhi za mikoa kupata huduma ya punguzo la tozo za umilikishaji, kuhakikisha wanamilikishwa maeneo yao kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imepanga kuandaa hati za hakimiliki za kimila 520,000, hatimiliki 500,000, vyeti vya kijiji 1,000 na hati za sehemu ya jengo 1,000. Vilevile, miamala ya hatimiliki na nyaraka za kisheria 100,000 zitasajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaratibu na kusimamia ardhi ya uwekezaji kwa kushirikiana na taasisi za uwekezaji nchini ili kuhakikisha ardhi kama rasilimali muhimu inaleta tija kiuchumi na kijamii. Usimamizi huu unahusisha ugawaji na usimamizi wa ardhi kwa wawekezaji wa ndani na nje ya kupitia Kamati ya Kitaifa ya Ugawaji Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi tarehe 15 Mei, 2024, maombi 191 ya ardhi ya uwekezaji yenye ukubwa wa hekta 11,613.08

yaliidhinishwa kwa ajili ya uwekezaji, ambapo kati ya hayo maombi 65 ni ya raia wa Tanzania na 151 ni ya wawekezaji kutoka nje ya nchi. Uwekezaji wa nje una mtaji wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 704.21, sawa na shilingi trilioni 1.82 za Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kliniki za Ardhi ni mpango wa Wizara wenye lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wote wenye kuhitaji huduma au wenye changamoto za ardhi wanapatiwa huduma karibu na maeneo wanayoishi kwa haraka na ufanisi unaotarajiwa na jamii. Kwa kutambua hilo, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali imekuwa ikiendesha zoezi la Kliniki za Ardhi kwenye mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo wataalamu wa kada zote za ardhi wanakuwepo eneo moja kwa wakati mmoja hivyo kuwezesha upatikanaji wa huduma zote za ardhi papo kwa papo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Mei, 2024 kliniki za ardhi zimefanyika katika mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, chini ya viongozi wa Wizara, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa kliniki za ardhi na matokeo chanya yaliyopatikana, Viongozi Wakuu wa Wizara wamefanya ziara kwenye majiji yote nchini na kushirikiana na viongozi wa maeneo hayo kushughulikia changamoto za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi. Majiji hayo ni Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Dodoma na Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kwa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kote nchini ambao wameshirikiana kwa karibu sana na Makamishina wa Ardhi Wasaidizi wa Mikoa na Wataalamu wa Sekta ya Ardhi katika kuendesha na kusimamia kliniki za ardhi katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kliniki za ardhi zimeonesha mafanikio kutokana na wananchi wengi kujitokeza kusikilizwa kwa uhuru na uwazi kisha changamoto zao kupatiwa ufumbuzi wa

haraka. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 wananchi 35,963 walihudumiwa katika mikoa 22 inayoendesha kliniki za ardhi, migogoro na malalamiko 7,444 yalipokelewa ambapo migogoro na malalamiko 4,565 yalishughulikiwa. Aidha, hatimiliki 17,553 zilikamilishwa na kukabidhiwa kwa wamiliki na maombi mapya ya hati 13,289 yalipokelewa. Katika kliniki hizo jumla ya shilingi bilioni 3.03 zilikusanywa kama tozo na ada mbalimbali za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia uendeshaji wa zoezi la kliniki za ardhi, Wizara imebaini vyanzo mbalimbali vya malalamiko na migogoro ya ardhi. Vyanzo hivyo ni pamoja na madai ya fidia, utolewaji wa miliki pandikizi *(double allocation)*, uvamizi wa maeneo ya umma na binafsi, udanganyifu na utapeli kwa kutumia nyaraka za kugushi, ucheleweshaji wa huduma, mwingiliano wa mipaka, madai ya mali za urithi au wanandoa, utekelezaji wa miradi ya urasimishaji na upimaji shirikishi na uelewa mdogo wa baadhi ya wananchi kuhusu masuala ya umiliki wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali kuchukua hatua kwa wananchi wanaotumia nyaraka za kugushi au kuvamia viwanja vyenye umiliki kwa kuwafikisha Mahakamani na kurejesha maeneo hayo kwa wamiliki halali. Aidha, Wizara imeanzisha dawati maalum katika Ofisi za Ardhi za mikoa ili kuwawezesha wananchi wenye migogoro ya ardhi hasa wenye sura ya jinai kuwasilisha malalamiko yao ili yapatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa wananchi na wadau wote wa ardhi wenye changamoto zinazotokana na vitendo vya dhuruma kuendelea kujitokeza kutoa malalmiko yao ili kuiwezesha Wizara kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaratibu utekelezaji wa maelekezo ya Baraza la Mawaziri kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji na mitaa 975 nchini. Katika utekelezaji wa maamuzi haya, tathmini imebainisha kuwa vijiji na mitaa yenye migogoro ni 1,004 yaani vijiji 981 na mitaa 23 badala ya vijiji 975 kama ilivyobainishwa hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2024 utekelezaji wa uwamuzi katika vijiji 438 na mitaa 13 umekamilika na utekelezaji katika vijiji 543 na mitaa 10 unaendelea. Utekelezaji huo umewezesha ardhi yenye ukubwa wa ekari milioni 2.4 kumegwa na kurejeshwa kwa wananchi ikijumuisha ekari milioni 1.65 kutoka kwenye maeneo ya hifadhi, *ranch* na mashamba ya Serikali ekari 707,962 kutoka kwenye mapori tengefu 12 na ekari 46,715 kutoka kwenye hifadhi za misitu saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile maeneo 18 kati ya 20 yamefanyiwa uthamini na kiasi cha shilingi bilioni 178.57 kinahitajika kwa ajili ya kuhamisha wananchi kutoka kwenye maeneo ya hifadhi na vyanzo vya maji. Kati ya maeneo yaliyothaminiwa wananchi wa maeneo sita wamelipwa fidia kiasi cha shilingi bilioni 20.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha usimamizi wa mipaka ya hifadhi, vigingi 32,838 vimesimikwa na nguzo za kuchongwa kuzunguka maeneo ya hifadhi za Taifa 21. Mapori ya akiba 29 na hifadhi za misitu 416 pia Serikali kupitia Tangazo la Serikali Na. 754 la tarehe 20 Oktoba, 2023 imerekebisha mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa kumega eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 478 kwenda kwa wananchi. Utekelezaji wa maagizo Baraza la Mawaziri utakamilishwa kumalizia kazi ya uthamini na kulipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upimaji upya wa vijiji vilivyomegewa maeneo, kushughulikia maeneo yenye changamoto zaidi ambayo yanahusisha baadhi ya vijiji vitakavyoondolewa katika maeneo ya hifadhi, vyanzo vya maji na maeneo muhimu kwa ajili ya ulinzi na usalama wa nchi. Utekelezaji wa kazi hiyo umepangwa kukamilika ifikapo mwezi Juni mwaka 2024. Mwelekeo wa Wizara ni kuweka mifumo thabiti ya usimamizi na ufuatiliaji kwa kushirikiana na wadau wote muhimu ili kupunguza migogoro mikubwa kama hii kuendelea kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuhakikisha mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya yanaundwa na kufanya kazi katika wilaya zote nchini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2024

jumla ya mabaraza 139 yameundwa ambapo kati ya hayo mabaraza 104 yanatoa huduma. Napenda kutumia fursa hii kuziimiza Sekretarieti za Mikoa pamoja na Ofisi za Wilaya kuwezesha upatikanaji wa majengo ya ofisi na wajumbe wa baraza ili mabaraza 35 yaliyobaki yaweze kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ilipanga kushughulikia mashauri 33,250 hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2024 Wizara imeshughulikia mashauri 29,573 ambapo mashauri mapya ni 14,093 na mashauri ya zamani ni 15,480. Kati ya hayo mashauri 15,550 yemeshughulikiwa na kutolewa uwamuzi na mashauri 14,023 yanaendelea kushughulikiwa. Aidha, Wizara imeendelea kufanya maboresho ya mfumo wa kielektroniki wa kusimamia mashauri katika mabaraza ya ardhi, nyumba na wilaya ili kuongeza ufanisi. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara itashughulikia mashauri 14,023 yaliyobaki na mengine yatakayojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ilipanga kuratibu na kusimamia uandaaji na uwezeshaji wa taarifa za uthamini 54,000 ambapo kati ya hizo taarifa za uthamini za kawaida ni 20,000 na taarifa za fidia na wafidiwa ni 34,000 na kushughulikia malalamiko 30 ya uthamini wa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2024 Wizara imeidhinisha taarifa za uthamini 57,285 sawa na 111.66% ya lengo ambapo kati ya hizo taarifa za uthamini wa kawaida ni 22,311 na taarifa za uthamini wa fidia 34,974. Aidha, malalamiko 91 ya fidia yalipokelewa na kushughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara imeendelea kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kufanya uthamini wa mali za wananchi wa Ngorongoro wanaohama kwa hiyari kupisha shughuli za uhifadhi. Uthamini umefanyika kwa awamu sita katika kata 11 na vijiji 25 ambapo mali za kaya 650 zenye thamani ya shilingi bilioni 3.79 zimefanyiwa uthamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo malalamiko yanayohusu ulipaji wa fidia kutoka katika maeneo mbalimbali nchini. Malalamiko hayo yanatokana na wananchi kutofahamu

kwa hakika wadau wanaohusika na ulipaji wa fidia. Baadhi ya taasisi kufanya uthamini wa fidia bila ya kuwepo fedha kwa ajili ya malipo ya fidia na kutozingatia taratibu za uhakiki wa taarifa za uthamini wa fidia kwa mujibu wa sheria ya uthamini na usajili wa thamini sura ya 138.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa malalamiko ambayo yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara, Wizara imetoa Waraka wa Uthamini wa Fidia Na. 1 wa Mwaka 2024 ambao pamoja na mambo mengine unaelekeza taratibu zinazopaswa kuzingatiwa wakati wa shughuli ya uthamini, uhakiki wa taarifa za uthamini na ulipaji fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ifahamike kuwa jukumu la Wizara ni kuratibu uthamini na wajibu wa kulipa fidia ni wa taasisi na unufaika na uthamini huo. Aidha, natoa wito kwa wadau wote wa uthamini kuhakikisha wanazingatia waraka wa uthamini wa fidia. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara itaratibu na kusimamia uandaaji wa taarifa za uthamini 54,000 kati ya hizo taarifa za uthamini wa kawaida ni 20,000 na taarifa za uthamini wa fidia ni 34,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upangaji wa miji na makazi ni mojawapo ya majukumu ya msingi ya Wizara ambapo inaratibiwa na kutekelezwa kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na taratibu za uendelezaji miji. Utekelezaji wa jukumu hili unalenga kuwa na makazi yaliyopangwa kuhifadhi mazingira na kuwa na uhakika wa ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kumekuwepo na ongezeko la ukuaji wa miji na kusababisha hitaji kubwa la kubadili matumizi ya ardhi. Wizara imefanya marekebisho ya kanuni za viwango vya kupanga ukubwa wa ardhi kwa matumizi mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara imeboresha kanuni za makundi ya matumizi ya madaraja ya matumizi ili kuwezesha matumizi ya ardhi kushabihiana, hivyo kuondoa migogoro ya

matumizi ya ardhi. Vilevile katika kanuni hiyo mchakato wa mabadiliko ya matumizi ya ardhi umeboreshwa ambapo maombi yatajadiliwa katika ngazi ya mtaa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, ndiyo yajadiliwe na Kamati za Halmashauri ili kuimarisha ushirikishwaji wa wadau na hivyo kupunguza migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya wazi yanapaswa kusimamiwa, kutunzwa na kulindwa ili yatumike kwa masilahi mapana ya umma. Hata hivyo, maeneo hayo yamekuwa yakivamiwa na kubadilishwa matumizi au kutumiwa venginevyo kutokana na sababu nyingi zikiwemo uvamizi wa makusudi, kutolipwa fidia kwa wamiliki wa asili, kutumika kama vyanzo vya mapato ya halmashauri na usimamizi usiyoridhisha wa mamlaka zilizopewa kusimamia maeneo hayo. Ili kukabiliana na matumizi holela ya maeneo hayo, matumizi ya maeneo ya wazi yamewekewa utaratibu wa kuhidhinishwa na Wizara endapo yatahitajika kutumika kwa masilahi ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusisitiza kuwa maeneo yote ya wazi ni lazima yatunzwe, yalindwe na kudumishwa ili yatumike kwa manufaa ya umma yakiwemo kufanyia mikutano ya hadhara, kupendezesha mandhari na mazingira ya mji, michezo kwa watoto katika mitaa, watu kupumzika, kufanyia chanjo kwa umma na kutumika kama hifadhi kwa watu na misaada wakati wa maafa, majanga na dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ilipanga kuratibu na kuidhinisha mabadiliko ya matumizi ya ardhi 500 hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2024 maombi 465 sawa na 93.2% ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi yaliidhinishwa. Katika mwaka 2024/2025 Wizara itaendelea kupokea na kuidhinisha maombi ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi 500 kwa kuzingatia sheria na kanuni za mipango miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000 zinaelekeza kuwa maeneo ya makazi yaliyoendelezwa bila kupangwa yatarasimishwa. Katika kutekeleza matakwa ya sera hizi Wizara imeendelea kuratibu urasimishaji wa makazi

yaliyoendelezwa bila kupangwa kwa kushirikisha jamii, asasi za kiraia na sekta binafsi. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ilipanga kurasimisha makazi 300,000. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2024 jumla ya makazi 237,424 sawa na 79.1% yamerasimishwa katika Mamlaka za Upangaji 37.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara itarasimisha makazi 500,000. Pia Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji na sekta binafsi inaendelea kufanya uhamasishaji kwa wananchi ambao makazi yao hayajarasimishwa ili kukamilisha zoezi hilo na kuendeleza kliniki za ardhi ili kukwamua urasimishaji katika maeneo ambayo hayajakamilisha miradi ya urasimishaji. Ili kufikia lengo la kurasimisha makazi 500,000 katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara itaanza kwa kukwamua urasimishaji ambao ulikwama kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo uchangiaji hafifu wa wananchi na baadhi ya kampuni zilizofanya urasimishaji kutokamilisha kazi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani, katika Mkoa wa Dar es Salaam urasimishaji katika mitaa 270 ili kuamua kazi hiyo Wizara itaajiri wataalam wa muda wa Mipango Miji na Upimaji na kuhakikisha kazi hizo zinakamilika. Zoezi hili limeanza kutekelezwa katika mitaa 13 ya Mkoa wa Dar es Salaam. Natoa wito kwa wananchi ambao makazi yao hayajarasimishwa kujitokeza kurasimishiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majukumu mengine Wizara inajukumu la kusimamia miliki kuu nchini. Sekta ya miliki inajumuisha ardhi iliyopangwa na kupimwa kwa kujengwa nyumba za makazi, majengo ya biashara, viwanda, maeneo ya burudani na majengo ya matumizi maalum.

Mheshimiwa Menyekiti, wadau wa Sekta ya Miliki wanajumuisha wawekezaji, wamiliki wa majengo, wapangaji, taasisi za fedha, mawakala, wanunuzi wa nyumba na viwanja na watafiti wa soko la nyumba. Sekta hii imeendelea kukua na kuvutia wadau wengi zaidi kutokana na fursa za uwekezaji katika nyanja mbalimbali ikiwemo soko la fedha na nyumba za kupangisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha usimamizi wa sekta hii, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ilipanga kukamilisha uandaaji wa sheria na kanuni za kusimamia Sekta ya Miliki Kuu, kutoa elimu kwa wadau na kuandaa kanzidata ya waendelezaji Miliki pamoja na mawakala wa Miliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Miliki yameandaliwa na kuwasilishwa kwenye mamlaka za uamuzi. Mapendekezo hayo pamoja na mambo mengine yanalenga kuanzisha mamlaka ya kusimamia Sekta ya Miliki *(Real Estate Regulatory Authority)* ili kuongeza tija na ufanisi katika usimamizi na uratibu wa sekta hii muhimu kwa uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ilipanga kuratibu, kusimamia na kuidhinisha viwanja 500,000 na mashamba 500. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 viwanja 249,340 na mashamba 7,559 yamepimwa na kuidhinishwa sawa na 49.87% ya lengo la viwanja na 1,511.8% ya lengo la mashamba. Ongezeko kubwa la mashamba yaliyopimwa na kuidhinishwa inatokana na mpango wa Serikali wa kuhamisha wananchi kutoka eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kwenda Msomera na Saunyi Mkoa wa Tanga. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara itasimamia upimaji na uidhinishaji wa viwanja 500,000 na mashamba 500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ramani ni zao la kazi ya upimaji ardhi ambalo huweza kupatikana katika mfumo wa nakala ngumu au nakala tete. Ramani huzalishwa kutokana na taarifa za msingi za kijiografia. Ramani zinazotayarishwa zinajumuisha viwanja, mashamba, mipaka ya kiutawala na kimataifa na hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2024 ramani za mipaka ya kiutawala za wilaya 17 katika mikoa ya Dar es Salaam, tano; Kagera, saba; Dodoma, ramani mbili; Tanga, moja; Arusha, moja; na Mbeya, moja zimeandaliwa. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara itaendelea kuandaa ramani za mipaka ya kiutawala kwa Wilaya 25. MWelekeo wa Wizara ni

kuwa na ramani za kidijiti ili kurahisisha upatikanaji wa ramani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na changamoto za uandaaji wa ramani unaofanywa na baadhi ya taasisi na sekta binafsi bila ya kuzingatia sheria na ubora hali inayosababisha kuwepo kwa tafsiri zisizosahihi za mipaka ya Kimataifa na kiutawala. Matokeo yake ni kuwepo kwa migogoro ambayo ingeweza kuzuilika endapo taratibu za uandaaji wa ramani zingezingatiwa kwa mujibu wa Sheria ya Upimaji Sura Na. 324.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelekeza taasisi zote za umma na binafsi zizingatie takwa la kisheria linalompa mamlaka Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani kuandaa na kuidhinisha ramani zote zikiwemo za mipaka ya kiutawala na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina jukumu la kuratibu na kupima mipaka ya vijiji ambapo mwaka wa fedha 2023/2024 ilipanga kuhakiki na kupima mipaka ya vijiji 100. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2024 jumla ya vijiji 742 imehakikiwa na kupimwa mipaka. Kati ya hivyo, vijiji 475 vimehakikiwa na kupimwa mipaka upya na upimaji wa vijiji 267 ambavyo vilikuwa havijapimwa umefanyika. Aidha, migogoro ya mipaka ya vijiji vitano vya Bangalala, Mwembe, Makanya, Ng'wasi na Nasulu katika Wilaya ya Same imetatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile mgogoro wa mipaka katika shamba la Malonje na vijiji vitano vya Sikaungu, Msandamuungano A, Msandamuungano B, Songambele, Azimio na Malonje katika Wilaya ya Sumbawanga umetatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhakiki na kupima mipaka ya vijiji 1,000. Natoa rai kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa kuhakikisha kuwa vijiji vinavyoanzishwa vinapimwa mipaka yake kabla ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imekumbwa na maafa yaliyotokana na mvua nyingi ambazo zimeendelea kunyesha

katika maeneo mbalimbali nchini. Kufuatia maafa yaliyotokea katika Wilaya ya Hanang, kutokana na kuporomoka kwa sehemu ya mlima Hanang, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepanga na kupima viwanja mbadala kwa waathirika wa maporomoko hayo. Viwanja hivi vimepimwa katika eneo la ekari 100 zilizomegwa kutoka shamba la Jeshi la Magereza lililopo katika Kijiji cha Kidagamo Wilaya ya Hanang.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya viwanja 269 vimepimwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo makazi viwanja 235, makazi na biashara viwanja 15, biashara viwanja saba na huduma za jamii viwanja 12. Aidha, waathirika wote 108 wamepatiwa viwanja, kwa ajili ya makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, kupitia Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro inaendelea na upimaji wa viwanja na mashamba, kwa ajili ya makazi, kilimo na ufugaji. Kazi hii inafanyika katika Vijiji vya Msomera, Wilaya ya Handeni na Saunyi, Wilaya Kilindi, katika Mkoa wa Tanga ambapo lengo ni kupima viwanja 10,000 na mashamba 8,500. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 viwanja 5,031 vya makazi vyenye wastani wa ukubwa wa ekari 2.5 na mashamba 7,897 yenye ukubwa wa wastani wa ekari tano yamepimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, pamoja na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji ikiwemo mvua kubwa zilizonyesha, Wizara imejipanga kukamilisha upimaji wa mashamba ifikapo mwezi Juni, mwaka 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Wizara ni kuifanya TEHAMA kuwa nyenzo muhimu ya kuendesha shughuli za sekta ya ardhi. Lengo la hatua hiyo ni kuongeza uwazi, ufanisi, uwajibikaji na kupunguza gharama na muda wa utoaji huduma. Wizara imekamilisha usanikishaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Huduma za Ardhi kwa kutumia watalaam wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekti, hatua inayoendelea ni kuhamisha taarifa kutoka kwenye mifumo ya zamani na majalada kwa awamu kwenda kwenye mfumo ulioboreshwa. Aidha, mfumo

utaanza kutumika kwa awamu ya kwanza katika Mikoa ya Arusha, Tanga, Mbeya, Mwanza na Dodoma ifikapo Mwezi Juni, Mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara iliahidi kusimika na kusambaza miundombinu wezeshi ya TEHAMA katika Ofisi za Ardhi za Mikoa 25 na Halmashauri 132. Hadi Tarehe 15 Mei, 2024 usimikaji wa miundombinu wezeshi ya TEHAMA katika Halmashauri 44 imekamilika na kazi ya usimikaji wa miundombinu hiyo inaendelea katika Halmashauri 41. Pamoja na huduma nyingine, miundombinu hii itatumika katika utoaji wa huduma za ardhi kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Huduma za Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ilizikopesha Mamlaka za Serikali za Mitaa 57, Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Iringa, Chuo Kikuu Ardhi na Vyuo vya Ardhi vya Morogoro na Tabora jumla ya shilingi bilioni 50, kwa ajili ya kuongeza kasi ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Wizara imeendelea kufuatilia marejesho ya fedha hizo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi tarehe 15 Mei, 2024, jumla ya shilingi billioni 23.71 zimerejeshwa na Halmashauri 55 ambapo Halmashauri 13 zimerejesha mikopo yao kwa 100%; Halmashauri 42 zimerejesha sehemu ya fedha; na Halmashauri mbili za Manispaa ya Shinyanga na Wilaya ya Musoma hazijarejesha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzipongeza Halmashauri za Jiji la Mwanza, Manispaa za Morogoro, Ilemela na Kigamboni; Miji ya Tunduma na Bariadi; Halmashauri za Wilaya za Moshi, Meru, Kilosa, Geita, Kaliua na Mbozi; zilizotekeleza wajibu wa kurejesha fedha kwa mujibu wa makubaliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kuzitaka Halmashauri na Taasisi ambazo hazijarejesha au hazijakamilisha marejesho, kurejesha fedha wanazodaiwa ifikapo mwezi Juni, mwaka 2024, ili kuziwezesha Halmashauri nyingine kunufaika na fedha hizo. Kwa Halmashauri

ambazo hazitatekeleza agizo hilo, fedha hizo zitakatwa moja kwa moja kutoka kwenye ruzuku zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuepuka changamoto zilizojitokeza kwenye utaratibu wa utoaji wa mikopo kwa awamu ya kwanza, Wizara imefanya maboresho katika utaratibu huo. Maboresho yaliyofanyika yanahusisha fedha kutolewa kupitia Ofisi za Ardhi za Mikoa, fedha kutolewa kwa awamu kwa kuzingatia hatua ya kazi iliyofikiwa na fedha za mauzo ya viwanja kuwekwa kwenye akaunti maalum ya Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/24, Wizara imebuni na kusanifu Mradi wa Msalato *Satellite City* katika Jiji la Dodoma utakaokidhi mahitaji ya watu zaidi ya 14,776. Mradi huo utawezesha ujenzi wa makazi bora yenye miundombinu na huduma muhimu za jamii na biashara za aina mbalimbali hivyo, kupunguza msongamano wa wananchi wanaofuata mahitaji katikati ya mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imepanga kubuni na kusanifu miji ya satelaiti miwili katika Majiji ya Dodoma na Arusha, kwa maana ya Msalato, Dodoma na Mji wa *AFCON (AFCON City)* Arusha, ili kuwa na miji nadhifu na kudhibiti makazi holela. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia kikamilifu matumizi ya fedha za mfuko ili kuwezesha Halmashauri kupanga na kupima miradi iliyoandaliwa. Wizara kupitia Programu ya KKK itapanga, kupima na kumilikisha viwanja 100,000, kwa ajili ya matumizi mbalimbali kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji pamoja na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 1991/1992, Serikali ilianzisha Mfuko Maalum wa Kupima Viwanja *(Plot Development Revolving Fund – PDRF*) ambao ulilenga kuwezesha upangaji, upimaji na umilikishaji viwanja. Hata hivyo, mwaka 2016 Serikali ilisitisha matumizi ya akaunti za mifuko mbalimbali nchini ikiwemo akaunti ya Mfuko huu. Kusitishwa kwa matumizi ya akaunti kuliikosesha Wizara chanzo cha uhakika cha fedha za upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi nchini, Serikali imeridhia kurejeshwa kwa matumizi ya akaunti ya Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi. Kwa kuanzia, Serikali imetoa mtaji wenye thamani ya shilingi bilioni 15.4 na imeridhia marejesho ya fedha kiasi cha shilingi bilioni 50 za kupanga, kupima na kumilikisha zinazodaiwa kwenye mikopo ya Halmashauri ziingizwe kwenye mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha uendelevu wa mfuko na ufanisi katika utekelezaji, Mwongozo wa Uratibu na Usimamizi wa Mfuko umeandaliwa. Wizara inatoa shukrani za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kurejesha matumizi ya akaunti ya mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi *(LTIP)*. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara kupitia mradi huu ilipanga kupima mipaka ya vijiji 700, kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi na mipangokina ya vijiji 700, kuandaa na kuidhinisha Hati za Hakimiliki za Kimila 200,000 na kukarabati Ofisi za Ardhi za Halmashauri 41.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi tarehe 15 Mei, 2024, jumla ya mipaka ya vijiji 407 imepimwa na kuhakikiwa, na vyeti vya ardhi ya vijiji 320 vimetolewa na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 843 imeandaliwa katika Halmashauri 21. Aidha, vipande vya ardhi 381,509 vimetambuliwa, kwa ajili ya kutoa Hati za Hakimiliki za Kimila katika Wilaya sita za Tanganyika, Maswa, Mbinga, Mufindi, Songwe na Chamwino.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya makazi 500,000 yalipangwa kurasimishwa katika Halmashauri 23 kuanza kusimika vituo 22 vya upimaji na kuweka alama za msingi za upimaji 276. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 vipande vya ardhi 62,200 vimerasimishwa katika Halmashauri ya Dodoma, Chalinze, Manispaa ya Kigoma, Mji wa Nzega, Manispaa ya Kahama na Manispaa ya Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alama za msingi za upimaji 327 zimewekwa katika Halmashauri 26 sawa na 118% ya lengo. Aidha,

zabuni, kwa ajili ya urasimishaji makazi 400,000 imetangazwa. Vilevile, mkandarasi, kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya kieletkroniki vya upimaji 22 amepatikana na kazi ya ujenzi itaanza katika mwaka 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ilipanga kuanza ujenzi wa majengo 25 ya Ofisi za Ardhi za Mikoa na kujenga kumbi za mihadhara nne katika Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 washauri elekezi wa ujenzi wa majengo 25 ya Ofisi za Ardhi za Mikoa na kumbi nne za mihadhara za Vyuo vya Tabora na Morogoro wamepatikana na wameanza kazi za awali za ubunifu katika maeneo ambayo ujenzi utafanyika. Vilevile, mradi umeboresha mazingira ya kufanyia kazi na kuwezesha ununuzi wa samani za ofisi, vitendeakazi na magari 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2024/2025 kupitia Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi *(LTIP)* ni:-

(i) Kuhakiki na kupima mipaka ya vijiji na kutoa vyeti vya vijiji 1,000;

(ii) Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 1,000;

(iii) Kuandaa mipangokina ya vijiji 100 na kuandaa Hati za Hakimiliki za Kimila 300,000;

(iv) Kurasimisha vipande vya ardhi 100,000 kupitia wataalamu wa Serikali na vipande 400,000 kupitia kampuni zinazofanya kazi za urasimishaji;

(v) Kubadilisha Nyaraka za Ardhi *(Data conversion)* 1,921,758 kutoka analojia kwenda kidijitali;

(vi) Kuwezesha upatikanaji wa miundombinu kwa ajili ya usambazaji wa mfumo wa *ILMIS* kwa Ofisi za Ardhi 67;

(vii) Kusanifu na kusimika Vituo vya Kieletroniki vya Upimaji *(CORs)* 22;

(viii) Kujenga mfumo wa kidigitali wa vitalu vya thamani ya ardhi nchini;

(ix) Kazi nyingine zitakazotekelezwa kupitia mradi ni kujenga ofisi za ardhi za mikoa 25;

(x) Kujenga kumbi za mihadhara katika Vyuo vya Ardhi vya Tabora, viwili na Morogoro – kumbi mbili;

(xi) Kuwezesha ubunifu na ujenzi wa Jengo la Taifa la Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi;

(xii) Kukarabati Ofisi za Ardhi katika Halmashauri 34;

(xiii) Kukamilisha utaratibu ununuzi wa magari 52, kununua vifaa, kuhuisha mitaala na kuwezesha ukuzaji wa ujuzi wa watumishi wa Vyuo vya Ardhi Tabora na Morogoro;

(xiv) Kuboresha utendaji kazi wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya 30; na

(xv) Kuandaa na kuboresha Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuimarisha mipaka ya Kimataifa kwa kujenga na kuongeza alama, kuzipima, kukarabati zilizoharibika, kuandaa ramani za mipaka na kuandaa mikataba ya mipaka. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara iliahidi kuimarisha sehemu ya Mpaka wa Kimataifa kati ya Tanzania na Kenya yenye urefu wa kilomita 80, pamoja na Mpaka wa Tanzania na Burundi yenye urefu wa kilomita 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi tarehe 15 Mei, 2024 Wizara imeendelea na uimarishaji wa mipaka ya Tanzania na Kenya kwenye kipande cha kilomita 110 kutoka Namanga hadi Tarakea ambapo kazi hiyo imekamilika. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara itakamilisha uimarishaji wa sehemu ya Mpaka wa Tanzania na Kenya yenye urefu wa kilomita 100 kutoka

Tarakea mpaka Ziwa Jipe na sehemu ya Mpaka wa Tanzania na Burundi yenye urefu wa kilomita 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba la Taifa lina jukumu la kujenga nyumba za makazi na majengo mengine kwa ajili ya kuuza na kupangisha, kujenga majengo kulingana na mipango iliyoidhinishwa na Serikali, kuzalisha na kuwezesha uzalishaji wa vifaa vya ujenzi, kusimamia milki za majengo, kufanya ukarabati, kukusanya kodi ya pango, kutoa huduma ya ushauri elekezi, upangaji wa maeneo na ukandarasi wa majengo. Majukumu hayo yanatekelezwa kupitia Mpango Mkakati wa Shirika wa miaka 10 unaoanza 2015/2016 mpaka 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Shirika lilipanga kukwamua miradi mikubwa iliyopo Kawe iliyokuwa imesimama tangu mwaka 2018 ikiwemo mradi wa nyumba 422 wa Kawe 711 wenye thamani ya shilingi bilioni 169 na Mradi wa *Golden Premier Residence* wa nyumba 196 ambao una thamani ya shilingi bilioni 71.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ujenzi wa Mradi wa Kawe 711 unaendelea na umefikia 35% na unatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, mwaka 2026. Aidha, Mradi wa *Golden Premier Residence (GPR)* ambao umesimama na majadiliano kati ya shirika na mkandarasi yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shirika limeendelea na uuzaji na upangishaji wa majengo katika mradi uliokamilika wa *Morocco Square,* ambapo katika jengo lenye nyumba za makazi 100, nyumba 71 zimeshauzwa na mauzo ya nyumba zilizobakia yanaendelea. Aidha, upangishaji wa hoteli yenye vyumba 81 umefanyika kwa 100%, maduka kwa maana ya *(Retail Mall)* 94% na ofisi 42%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shirika limeanza utekelezaji wa mradi wa *Samia Housing Scheme* wenye nyumba 5,000 katika mwaka wa fedha 2023/2024. Shirika lilipanga kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 560, Kawe, Jijini Dar es Salaam, na nyumba 500

katika Jiji la Dodoma maeneo ya Njedengwa, Iyumbu na Medeli. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 ujenzi wa nyumba 560 awamu ya kwanza katika eneo la Kawe, Jijini Dar es Salaam, umefikia 60% na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 shirika lilipanga kuendelea na ujenzi wa majengo ya biashara katika Mikoa ya Kagera, Mwanza, Dodoma, Shinyanga, Morogoro, Mtwara na Lindi. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 ujenzi wa majengo ya maduka 50 katika Mji wa Kahama umefikia 14% na ujenzi wa jengo la biashara katika Mji wa Masasi umeshaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Shirika lilipanga kutekeleza miradi 24 ya ubia yenye thamani ya shilingi bilioni 340 kupitia Sera yake ya Ubia ambapo hadi tarehe 15 Mei, 2024 shirika limeidhinisha na kusaini mikataba ya miradi 21 yenye thamani ya shilingi bilioni 271. Miradi hii itatekelezwa kwa muda wa miezi 24 ambapo utekelezaji umeanza Januari, 2024 katika Mikoa ya Dar es Salaam kwa miradi 17, Mwanza miradi mitatu na Iringa mradi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia miradi hii, shirika linatarajia kupata manufaa mbalimbali ikiwemo kuongeza idadi ya nafasi za upangaji, mathalani katika eneo la Kariakoo nafasi za upangishaji zitaongezeka kutoka 324 hadi 2,691. Hivyo, mapato, thamani ya mali za shirika na faida ya uwekezaji kwa kuzingatia eneo *(Return on Investments)* itaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shirika limekamilisha ukarabati wa majengo 181 ambayo yana nyumba 311 katika mikoa 15 ya shirika. Aidha, jumla ya majengo 83 ambayo yana nyumba 451 yaliyopo katika mikoa mbalimbali ya shirika yanaendelea kufanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina jukumu la kusimamia shughuli za upangaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Utekelezaji wa majukumu ya tume unazingatia mpango mkakati wa Tume (2021/2022 - 2025/2026).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2023/2024 Wizara kupitia tume ilipanga kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwa wilaya tano na vijiji 210 katika Halmashauri mbalimbali nchini. Mipango hii huandaliwa kwa njia shirikishi na kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji na wadau. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 Wizara kupitia tume imewezesha uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji 339 katika Wilaya 27 sawa na 161.4% ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la vijiji vilivyoandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi linatokana na utekelezaji wa Mradi wa Uimarishaji Usalama wa Milki ya Ardhi na mwitikio wa wadau wa ndani na nje ya nchi kuchangia uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi. Uandaaji wa mipango hii umefanya kuwa na jumla ya vijiji 4,126 vilivyoandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi kati ya vijiji 12,318 vilivyopo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2024/2025 Wizara kupitia tume itaendelea kuratibu uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi inayotekelezwa kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Usalama wa Milki ya Ardhi *(LTIP)* na kuwezesha kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji 422.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nawashukuru Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, Mbunge na Naibu Waziri; Mhandisi Anthony Damian Sanga, Katibu Mkuu; na Bi. Lucy Dominico Kabyemera, Naibu Katibu Mkuu kwa kunisaidia kutekeleza majukumu ya kusimamia sekta hii muhimu. Aidha, nawashukuru Bwana Nathaniel Mathew Nhonge, Kamishna wa Ardhi; Bwana Hamad Abdallah Hamad, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa; Prof. Wakuru Magigi Maseka, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; Bi. Evelyne Mugasha, Mthamini Mkuu wa Serikali; na Bi. Stella Tullo, Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti wa Bodi na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa kutekeleza majukumu yao kwa bidii na maarifa na hivyo, kuleta ufanisi katika kufikia malengo ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Washirika wa Maendeleo ambao Serikali imekuwa ikishirikiana nao katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo zinazohusiana na Sekta ya Ardhi. Washirika hao ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya *EXIM* ya Korea Kusini, *UN-HABITAT, Shelter Afrique, African Union Boarder Program, Regional Centre for Mapping of Resources Development (RCMRD),* Benki ya Maendeleo Afrika, Benki Kuu ya Tanzania *(BOT), Tanzania Mortgage Refinancing Company (TMRC)*, Watumishi *Housing Company Limited,* taasisi za fedha za ndani, Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi na wananchi kwa michango yao katika utekelezaji wa majukumu ya sekta ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani kwa vyombo vya habari kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika kutoa elimu na hamasa kwa umma kuhusu masuala ya sekta ya ardhi. Kwa hakika wanahabari wameiwezesha Wizara kuwafikia wadau wengi zaidi kwa namna mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, napenda kuishukuru familia yangu hususan mke wangu Bi Mariam Bakari Silaa na mwanangu *Comrade* Simba William Silaa kwa uvumilivu na kunitia moyo katika utekelezaji wa majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara katika mwaka wa fedha 2024/2025 itaendelea kuimarisha utaratibu na usimamizi wa maendeleo ya sekta ya ardhi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, omba fedha sasa.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** …na kuboresha ili kutekeleza azma hiyo kwa vipaumbele nilivyovitaja pale awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na

Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Fungu la 48 na Tume ya Taifa ya Mipango ya Ardhi Fungu 03 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi jumla ya matumizi ya kawaida ya miradi ya maendeleo ni shilingi 157,455,085,000. Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi jumla ya matumizi ya kawaida na maendeleo ni jumla ya shilingi 12,173,330,000. Jumla kuu ya fedha zinazoombwa na ili Bunge liweze kujadili na kuidhinisha ni shilingi 171,372,508,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii inapatikana kwenye Wavuti ya Wizara na baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja.

## HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA JERRY W. SILAA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2024/25 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyochambua na kujadili Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**); Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kwa mwaka 2023/24. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu hayo mawili kwa mwaka 2024/25.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano wa **15** wa Bunge la **12** ambao ni mahsusi kwa ajili ya kujadili Bajeti ya Serikali. Aidha, kwa heshima na taadhima naomba kutumia fursa hii

kipekee kumshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ninamuahidi kuwa nitaendelea kutekeleza majukumu aliyonikabidhi kwa juhudi, uadilifu na uweledi ili kuleta ufanisi na kukuza ustawi na maendeleo ya wananchi kupitia sekta ya ardhi.

**Salamu za Pongezi**

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka mitatu tangu ashike madaraka ya kuongoza Taifa letu. Katika kipindi hiki cha uongozi wake, Sekta ya Ardhi imepata mafanikio mbalimbali ambayo yanajumuisha uboreshaji wa sera, sheria, taratibu na mifumo ya utoaji wa huduma; kuongezeka kwa kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi; uendelezaji wa makazi; kurahisishwa kwa taratibu za upatikanaji wa haki za ardhi; utatuzi wa migogoro ya ardhi; na utoaji wa elimu kwa umma.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri wao katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia na kuratibu shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawashukuru kwa maelekezo na ushauri wanaonipa ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake mahiri katika kusimamia maslahi na ustawi wa wananchi wa Zanzibar na kuendelea kudumisha Muungano wetu ambao umetimiza miaka **60**.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nakupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongoza na kusimamia kwa umahiri shughuli za Bunge. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.), kwa

kuendelea kusimamia kwa ufanisi shughuli za Bunge kama Mwenyekiti wa Bunge. Vilevile, nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb.) na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu awajalie afya njema na hekima ili muweze kutekeleza majukumu ya kusimamia shughuli za Bunge kwa maslahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii kumpongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Hotuba yake ya Bajeti ambayo imewasilisha utekelezaji wa malengo ya Serikali kwa mwaka 2023/24, pamoja na mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2024/25. Kwa hakika, hotuba hiyo imetoa mwelekeo wa utekelezaji wa majukumu ya sekta ya ardhi katika kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi pamoja na upimaji na uhakiki wa mipaka ya vijiji kama njia mojawapo ya kudhibiti migogoro ya ardhi. Ninaahidi kuwa, Wizara itayafanyia kazi masuala yote yaliyoainishwa katika hotuba hiyo ili kufikia malengo ya Serikali yaliyokusudiwa.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uongozi wa Mwenyekiti Mheshimiwa Timotheo Paul Mzava (Mb.) na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.) kwa utekelezaji wa majukumu ya usimamizi wa Sekta ya Ardhi. Maoni na ushauri ambao wamekuwa wakiutoa mara kwa mara umesaidia kuongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma za sekta ya ardhi. Tunawaahidi kuendelea kuzingatia maoni na ushauri wao ili kutimiza azma ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuhakikisha kuwa sekta ya ardhi inachangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi wa nchi, kuimarisha usalama wa milki na kudhibiti migogoro ya ardhi.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** nampongeza Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Mbunge wa Chamwino kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); Mheshimiwa Daniel

Baran Sillo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, Mbunge wa Misungwi kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi; Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Uchukuzi; na Mheshimiwa Zainab Athumani Katimba, Mbunge wa Viti Maalum kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali. Ninawatakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao.

**Salamu za Pole**

**9.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba nitumie fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wanafamilia wote, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania kwa ujumla kwa kuondokewa na kiongozi wetu mpendwa Hayati Ali Hassan Mwinyi aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika tutaendelea kumuenzi kwa kuleta mageuzi ya kiuchumi na kisiasa nchini.

**10.** ***Mheshimiwa* Spika**, mwezi Februari, 2024, Taifa letu lilipata msiba wa kuondokewa na aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Monduli na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa. Nitumie fursa hii kumpa pole Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanafamilia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa kumpoteza kiongozi huyo mahiri. Aidha, natoa pole kwa Mheshimiwa Fredrick Edward Lowassa, Mbunge wa Jimbo la Monduli kwa kuondokewa na Baba yake mpendwa.

**11.** ***Mheshimiwa* Spika**, natoa pole kwako wewe binafsi, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Wabunge, Watumishi wa Ofisi ya Bunge, familia na Watanzania kwa ujumla kwa kuondokewa na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil, aliyekuwa Mbunge wa Kwahani, Zanzibar na Mheshimiwa Francis

Leonard Mtega, aliyekuwa Mbunge wa Mbarali. Hakika michango yao itaendelea kukumbukwa.

**12.** ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kuwapa pole Watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa na mali kutokana na maafa, ajali na majanga yaliyosababisha athari mbalimbali zikiwemo vifo, majeruhi, uharibifu wa mali na mazingira yaliyotokea katika maeneo mbalimbali nchini. Tunamwomba Mwenyezi Mungu awajalie uponyaji wa haraka watanzania wenzetu waliojeruhiwa ili waweze kupona na kurejea katika shughuli zao za kila siku za ujenzi wa Taifa. Aidha, tunamwomba Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi. Amina.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2023/24 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2024/25. Bajeti ya Wizara imeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26); Mpango Mkakati wa Wizara; Mikataba; Itifaki; Mipango na Makubaliano ya Kikanda na Kimataifa; Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Sekta ya Ardhi; na maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali. Maeneo ya kipaumbele yatakayotiliwa mkazo na Wizara katika mwaka 2024/25 ni pamoja na:-

i) Kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi mijini na vijijini;

ii) Kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi;

iii) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika utunzaji wa kumbukumbu, utoaji wa huduma na upatikanaji wa taarifa za ardhi;

iv) Kuhakikisha uwepo wa nyumba bora, ukuaji wa sekta ya milki na maendeleo ya makazi kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii; na

v) Kuimarisha mipaka ya kimataifa.

**MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2023/24 NA MALENGO YA MWAKA 2024/25.**

**MAPATO NA MATUMIZI FUNGU 48**

**14.** ***Mheshimiwa*** **Spika**, katika mwaka 2023/24 Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni **163.17** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni **43.43** ziliidhinishwa kwa ajili ya Mishahara (PE); shilingi bilioni **37.61** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na shilingi bilioni **82.13** kwa ajili ya miradi ya maendeleo (DEV). Kati ya fedha za miradi ya maendeleo, shilingi bilioni **14.01** ni fedha za ndani na shilingi bilioni **68.12** ni fedha za nje. Aidha, Wizara iliongezewa bajeti ya shilingi bilioni **287.66** kwa ajili ya kulipa madeni ya Wazabuni, Watumishi na Wakandarasi. Ongezeko hilo limefanya bajeti ya Wizara kufikia shilingi bilioni **450.83**.

**15.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi tarehe 15 Mei, 2024, jumla ya shilingi bilioni **423.13** zilipokelewa, sawa na asilimia **93.86** ya bajeti ya shilingi bilioni **450.83.** Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **34.72** ni mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi sawa na asilimia **79.94** ya bajeti husika; shilingi bilioni **21.94** ni matumizi mengineyo ya Wizara na Taasisi sawa na asilimia **56.24** ya bajeti husika na shilingi bilioni **366.47** ni miradi ya maendeleo sawa na asilimia **99.48**. Kati ya fedha za miradi ya maendeleo zilizopokelewa, shilingi bilioni **309.53** ni fedha za ndani sawa na asilimia **99.52**; na shilingi bilioni **56.94** ni fedha za nje sawa na asilimia **99.26**. (**Jedwali Na.1**).

**Ukusanyaji wa Maduhuli**

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** ardhi ni miongoni mwa rasilimali muhimu ambazo zinachangia pato la Taifa kupitia ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na kodi ya pango la ardhi, ada na tozo nyingine za utoaji huduma za sekta ya ardhi. Katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia Fungu **48** ilipanga kukusanya shilingi bilioni **300**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2024, Wizara imekusanya shilingi bilioni **136** sawa na asilimia **45.3** ya lengo ***(Jedwali Na.2)***.

**17.** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na jukumu la ukusanyaji wa maduhuli kuhamishiwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Wizara imeendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha kupendekeza

jukumu la kukusanya kodi ya pango la ardhi liendelee kutekelezwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na iwezeshwe kwa kurudishiwa sehemu ya fedha (*retention*) kwa ajili ya makusanyo. Pendekezo hili linatokana na sababu mbalimbali zikiwemo: ukusanyaji wa kodi ya pango la Ardhi ni jukumu la kisheria lililoainishwa chini ya kifungu cha 25 na 33 cha Sheria ya Ardhi (Sura 113); ukusanyaji unahitaji wataalamu wa sekta ya ardhi ambao Wizara ndio mamlaka yao ya ajira na nidhamu; na mfumo wa TEHAMA wa Wizara unaotunza kumbukumbu za wamiliki umeunganishwa na shughuli kuu za kisekta za upangaji, upimaji, uthamini na umilikishaji ardhi na hivyo kupunguza changamoto za ukusanyaji zilizokuwepo hapo awali.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara imekadiria kukusanya shilingi bilioni **250**. Lengo hili litafikiwa kwa kuendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA kwa lengo la kurahisisha ukusanyaji wa maduhuli kidigitali; kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na usajili wa ardhi; kuendelea kufuatilia madeni ya kodi ya pango la ardhi kutoka katika mashirika, taasisi za umma na wamiliki binafsi; na kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati.

**MAPATO NA MATUMIZI YA FUNGU 03**

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (**Fungu 03**) iliidhinishiwa shilingi bilioni **8.19.** Kati ya fedha hizo shilingi bilioni **2.49** ni Mishahara ya watumishi (PE); shilingi bilioni **2.29** ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC); na shilingi bilioni **3.41** ni fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo. Aidha, wakati wa utekelezaji wa Bajeti, Tume ilipata nyongeza ya bajeti ya mishahara kiasi cha shilingi milioni **627.12** kwa ajili ya mishahara kutokana na ongezeko la watumishi hivyo kufanya Bajeti ya Tume kufikia shilingi bilioni **8.82**.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi tarehe 15 Mei, 2024, Tume imepokea jumla ya shilingi bilioni **7.33** kati ya bajeti ya shilingi bilioni **8.82** sawa na asilimia **83.11** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi bilioni **1.37** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC); shilingi bilioni **2.55** ni Mishahara; na shilingi bilioni

**3.41** fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Maendeleo (***Jedwali Na.3***).

**Ukusanyaji wa Maduhuli**

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume imeendelea kutekeleza jukumu la kukusanya maduhuli kutoka katika vyanzo mbalimbali. Katika mwaka 2023/24, Tume ilipanga kukusanya shilingi Milioni **18** kutokana na kodi ya pango la nyumba zilizopo Tabora. Hadi, tarehe 15 Mei, 2024 shilingi Milioni **9.5** zimekusanywa sawa na asilimia **52.78** ya lengo. Aidha, Tume ilipanga kuhamasisha wadau kuchangia kiasi cha shilingi milioni **700** kwa ajili ya shughuli za upangaji wa Matumizi ya Ardhi. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 jumla ya shilingi bilioni **2.77** zilipokelewa kutoka kwa wadau mbalimbali sawa na asilimia **395.71** ya lengo (**Jedwali Na.4**). Ongezeko hili limetokana na mwitikio mkubwa wa wadau kuchangia kazi za upangaji wa matumizi ya ardhi.

**UANDAAJI WA HATIMILIKI NA USAJILI WA NYARAKA**



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Phillip Isdori Mpango akiwa pamoja na wananchi wa Makete aliowakabidhi Hati za Kimila mkoani Njombe Oktoba 2023.*

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuandaa, kusajili na kutoa nyaraka mbalimbali ikiwemo Hatimiliki na Hati za Hakimiliki

za Kimila kwa wamiliki wa ardhi. Hati hizo huimarisha usalama wa miliki na hivyo kuwezesha udhibiti na kupunguza migogoro ya ardhi, kudhibiti umegaji wa ardhi kiholela, kuwezesha utambuzi wa maeneo katika zoezi la uwekaji wa Anwani za Makazi na kutumia ardhi kama dhamana katika Taasisi za fedha na vyombo vya sheria.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara iliahidi kuandaa Hatimiliki **500,000,** Hati za Hakimiliki za Kimila **520,000** na Hati za Sehemu ya Jengo **1,000.** Aidha, Wizara iliahidi kusajili miamala ya hatimiliki na Nyaraka za Kisheria **100,000** na kutoa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **100**. Hadi tarehe **15 Mei, 2024**, Wizara imeandaa na kusajili Hatimiliki **87,240** sawa na **asilimia 17.4** ya lengo na Hati za Hakimiliki za Kimila **86,994** sawa na asilimia **16.73** ya lengo. Kwa upande wa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji, jumla ya vyeti **362** vimeandaliwa sawa na asilimia **324** ya lengo, Hati za Sehemu ya Jengo **324** sawa na asilimia **32.4** ya lengo na miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria **95,456** sawa na asilimia **95.46** ya lengo zimesajiliwa (**Jedwali Na.5**).

**24.** ***Mheshimiwa* Spika**, zipo changamoto mbalimbali zilizosababisha kutofikia malengo ya uandaaji wa Hatimiliki. Changamoto hizo ni pamoja na uwepo wa madai ya fidia kwenye baadhi ya maeneo yaliyopangwa na kupimwa, uwepo wa migogoro ya ardhi kwenye baadhi ya maeneo, kutokamilishwa kwa malipo ya viwanja vilivyopangwa na kupimwa, wananchi wengi kutochangia gharama za urasimishaji na baadhi ya watumishi kutozingatia misingi ya haki, weledi na uadilifu.

**25.** ***Mheshimiwa Spika****,* ili kuongeza kasi ya umilikishaji, Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo utekelezaji wa Mradi wa Usalama wa Milki za Ardhi; Kushirikiana na sekta binafsi na Taasisi za Umma; Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi; kuboresha mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma; na kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi na kampuni zinazofanya kazi za urasimishaji zilizokiuka maadili. Aidha, Serikali kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2023 ilichukua hatua ya kupunguza gharama za umilikishaji kwa zaidi ya asilimia 50. Hatua hizo zimeongeza kasi ya umilikishaji wa ardhi ambapo hati

zilizomilikishwa zimeongezeka kutoka Hatimiliki **76,746** kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 mpaka Hatimiliki **87,240** kwa kipindi cha Julai, 2023 mpaka Mei, 2024. Vilevile, utoaji wa hatimiliki umeongezeka kutoka Hatimiliki **67,331** mwaka 2020/21 hadi Hatimiliki **86,398** mwaka 2022/23 kutokana na huduma za ardhi kuanza kutolewa katika Ofisi za Ardhi za Mikoa. **Nawahimiza wananchi kote nchini kuendelea kutumia Ofisi za Ardhi za Mikoa kupata huduma na fursa ya punguzo la tozo za umilikishaji kuhakikisha kuwa wanamilikishwa maeneo yao kwa mujibu wa sheria.**

**26.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2024/25, Wizara imepanga kuandaa na kutoa Hati za Hakimiliki za Kimila **520,000**, Hatimiliki **500,000,** Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **1,000** na Hati za Sehemu ya Jengo **1,000**. Vilevile, miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za kisheria **100,000** zitasajiliwa.

**Usimamizi wa Masharti ya Umiliki**

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** wamiliki wa ardhi wana wajibu wa kuzingatia masharti yanayoainishwa katika nyaraka za umiliki ikiwemo kuendeleza ardhi husika kwa wakati. Ukiukaji wa masharti ya umiliki, umekuwa ukisababisha athari hasi kiuchumi na kijamii ikiwemo kuibuka kwa migogoro ya ardhi inayotokana na maeneo husika kuvamiwa. Katika kusimamia utekelezaji wa masharti ya uendelezaji hususani wa mashamba, mwaka 2023/24, Wizara iliahidi kukagua mashamba na viwanja **230** ili kubaini uzingatiaji wa masharti ya umiliki. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, ukaguzi wa mashamba na viwanja **156** ulifanyika na kubaini kuwa viwanja na mashamba **124** hayajaendelezwa. Aidha, Wizara ilichukua hatua dhidi ya wamiliki waliokiuka masharti ya uendelezaji ambapo jumla ya milki za viwanja na mashamba **124** zimebatilishwa. Katika mwaka 2024/25, Wizara itakagua mashamba na viwanja **230** na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria kwa watakaobainika kukiuka masharti ya umiliki. **Natoa rai kwa wamiliki wote wa ardhi kuhakikisha wanazingatia masharti ya umiliki kama yalivyoainishwa kwenye nyaraka zao za umiliki. Aidha, natoa muda wa siku 90 kwa wamiliki wa ardhi ambao hawajaendeleza maeneo yao kwa mujibu wa sheria watekeleze**

**wajibu wao, baada ya muda huo nitapendekeza ubatilisho wa milki zao.**

**Usimamizi wa Ardhi ya Uwekezaji**

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaratibu na kusimamia ardhi ya uwekezaji kwa kushirikiana na taasisi za uwekezaji nchini ili kuhakikisha ardhi kama rasilimali muhimu inaleta tija kiuchumi na kijamii. Usimamizi huu unahusisha ugawaji na usimamizi wa ardhi kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kupitia Kamati ya Kitaifa ya Ugawaji Ardhi. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, maombi **216** ya ardhi ya uwekezaji yenye ukubwa wa hekta **11,292.14** yaliidhinishwa kwa ajili ya uwekezaji ambapo kati ya hayo maombi **65** ni ya raia wa Tanzania na **151** ni ya wawekezaji kutoka nje ya nchi. Uwekezaji wa nje una mtaji wenye thamani ya Dola za Marekani milioni **58.95** sawa na shilingi bilioni **152.98** ***(Jedwali Na.6***).

**29.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeshiriki katika Timu ya pamoja ya Wataalam wa Serikali inayoandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Ardhi ya Uwekezaji na Wawekezaji. Lengo la Mwongozo huo ni kuhahikisha kuwa ardhi iliyotolewa kwa uwekezaji inaleta tija iliyotarajiwa kiuchumi na kijamii. Timu ya Wataalam inahusisha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji; Ofisi ya Rais- TAMISEMI; Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA); Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA). Hadi tarehe 15 Mei, 2024 Timu hiyo imewatembelea wawekezaji **38** katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kwa lengo la kuona hatua za uwekezaji wao na kupokea maoni yao yenye lengo la kuboresha mazingira ya kiuwekezaji. Katika mwaka 2024/25, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia maeneo ya ardhi ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na uhakiki wa matumizi ya ardhi iliyotolewa kwa wawekezaji na kuwa na vikao na wadau wa uwekezaji wakiwemo wawekezaji wenyewe ili kuhakikisha ardhi ya uwekezaji inaleta tija inayotarajiwa.

**Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Kiutawala**

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na utatuzi wa migogoro ya ardhi kiutawala kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo uendeshaji wa Kliniki za ardhi kwenye Mikoa na Mamlaka

za Serikali za Mitaa, madawati ya kushughulikia kero na malalamiko, Timu na Kamati Maalum za Wataalam wa Serikali na ziara za viongozi wa Wizara katika maeneo mbalimbali nchini. Utatuzi huo unahusisha masuala ya fidia; utoaji wa viwanja mbadala; urekebishaji wa mipaka ya vijiji, viwanja au mashamba na utoaji elimu. Katika mwaka 2023/24 Wizara ilipanga kutatua migogoro **6,550** kiutawala ambapo hadi tarehe 15 Mei, 2024 migogoro **7,885** imetatuliwa **(*Jedwali Na.7*).**
Vilevile, rejista za migogoro katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri zimeendelea kuhuishwa ili kuwa na kumbukumbu sahihi za migogoro ya ardhi nchini.

**31. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2024/25, Wizara itaendelea kushughulikia malalamiko na migogoro ya ardhi kupitia moduli ya mfumo wa kielektroniki wa ILMIS inayotarajiwa kuanza kutumika mwezi Julai, 2024. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kupanga matumizi ya ardhi na kutoa elimu kwa umma kuhusu umiliki wa ardhi na madhara ya migogoro.

**Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Kupitia Kliniki za Ardhi**

**32.** ***Mheshimiwa Spika***, kliniki za Ardhi ni mpango wa Wizara wenye lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wote wenye kuhitaji huduma au wenye changamoto za ardhi wanapatiwa huduma karibu na maeneo wanayoishi kwa haraka na ufanisi unaotarajiwa na jamii. Kwa kutambua hilo, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali imekuwa ikiendesha zoezi la kliniki za ardhi kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo wataalam wa kada zote za ardhi wanakuwepo eneo moja kwa wakati mmoja hivyo kuwezesha upatikanaji wa huduma zote za ardhi papo kwa papo. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Mei, 2024 kliniki za ardhi zimefanyika katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa chini ya Viongozi wa Wizara, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya. Kwa kutambua umuhimu wa kliniki za ardhi na matokeo chanya yanayopatikana, Viongozi Wakuu wa Wizara wamefanya ziara kwenye majiji yote nchini na kushirikiana na viongozi wa maeneo hayo kushughulikia changamoto za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi. Majiji hayo ni Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Dodoma na Tanga. **Napenda kutoa pongezi kwa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na**

**Wilaya kote nchini ambao wameshirikiana kwa karibu sana na Makamishna wa Ardhi Wasaidizi wa Mikoa na wataalamu wa sekta ya ardhi katika kuendesha na kusimamia Kliniki za ardhi katika maeneo yao**.



*Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Jerry William Silaa (Mb.) akiwasikiliza wananchi wakati wa Kliniki ya Ardhi tarehe 6 Novemba 2023 iliyofanyika jijini Dodoma.*

**33.** ***Mheshimiwa Spika***, kliniki za ardhi zimeonesha mafanikio kutokana na wananchi wengi kujitokeza kusikilizwa kwa uhuru na uwazi kisha changamoto zao kupatiwa ufumbuzi kwa haraka. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, wananchi **35,963** walihudumiwa katika mikoa **22** iliyoendesha kliniki za ardhi. Migogoro na malalamiko **7,444** yalipokelewa ambapo **4,565** imetatuliwa na **2,879** inaendelea kushughulikiwa. Aidha, Hatimiliki **17,553** zilikamilishwa na kukabidhiwa kwa wamiliki na maombi mapya ya hati **13,289** yalipokelewa. Katika kliniki hizo, jumla ya shilingi bilioni **3.03** zilikusanywa kama tozo na ada mbalimbali za kisheria.



*Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Jerry Silaa (kushoto), Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii Mhe. Timotheo Mzava (wa pili kushoto) na wajumbe wa Kamati hiyo wakati wa Kliniki ya Ardhi Bunju jijini Dar es Salaam.*

**34.** ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia uendeshaji wa zoezi la Kliniki za Ardhi, Wizara imebaini vyanzo mbalimbali vya malalamiko na migogoro ya ardhi. Vyanzo hivyo ni pamoja na madai ya fidia, utolewaji wa milki pandikizi, uvamizi wa maeneo ya umma na binafsi, udanganyifu na utapeli kwa kutumia nyaraka za kughushi, ucheleweshaji wa huduma, mwingiliano wa mipaka, madai ya mali za urithi au wanandoa, utekelezaji wa miradi ya urasimishaji na upimaji shirikishi na uelewa mdogo wa baadhi ya wananchi kuhusu masuala ya umiliki wa ardhi.

**35.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali kuchukua hatua kwa wananchi wanaotumia nyaraka za kughushi au kuvamia viwanja vyenye umiliki kwa kuwafikisha mahakamani na kurejesha maeneo hayo kwa wamiliki halali. Aidha, Wizara imeanzisha Dawati Maalum katika Ofisi za Ardhi za Mikoa ili kuwezesha wananchi wenye migogoro ya ardhi hasa yenye sura ya jinai kuwasilisha malalamiko yao ili yapatiwe ufumbuzi. **Natoa wito kwa Wananchi na wadau wote wa ardhi wenye changamoto zinazotokana na vitendo vya dhuluma kuendelea kujitokeza kutoa malalamiko yao ili kuiwezesha Wizara kuchukua hatua stahiki** .

**Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi katika Vijiji 975**

**36.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaratibu utekelezaji wa Maelekezo ya Baraza la Mawaziri kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi ya vijiji na Mitaa **975** nchini. Katika utekelezaji wa maamuzi haya, tathmini imebainisha kuwa vijiji na mitaa yenye migogoro ni **1,004** (vijiji 981 na mitaa 23) badala ya **975** kama ilivyokuwa imebainishwa hapo awali.

**37.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi tarehe 15 Mei, 2024 utekelezaji wa uamuzi katika vijiji **438** na mitaa **13** umekamilika na utekelezaji katika vijiji **543** na mitaa **10** unaendelea (**Jedwali Na.8).** Utekelezaji huo umewezesha ardhi yenye ukubwa wa ekari milioni **2.4** kumegwa na kurejeshwa kwa wananchi ikijumuisha ekari milioni **1.65** kutoka kwenye maeneo ya hifadhi, ranchi na mashamba ya Serikali; ekari **707,962** kutoka kwenye Mapori Tengefu **12** na ekari **46,715** kutoka kwenye Hifadhi za Misitu saba (**7**). Vilevile, maeneo **18** kati ya **20** yamefanyiwa uthamini na kiasi cha shilingi bilioni **178.57** kinahitajika kwa ajili ya kuhamisha wananchi kutoka kwenye maeneo ya Hifadhi na vyanzo vya maji. Kati ya maeneo yaliyothaminiwa, wananchi wa maeneo sita (**6**) wamelipwa fidia kiasi cha shilingi bilioni **20.07 (Jedwali Na.9 A&B)**

**38. Mheshimiwa Spika,** ili kuimarisha usimamizi wa mipaka ya Hifadhi, vigingi **32,838** vimesimikwa na mkuza kuchongwa kuzunguka maeneo ya Hifadhi za Taifa **21** na Mapori ya Akiba 29 na Hifadhi za Misitu **416**. Pia, Serikali kupitia Tangazo la Serikali Na. 754 la tarehe 20/10/2023 imerekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa kumega eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba **478** kwenda kwa wananchi. Utekelezaji wa maagizo ya Baraza la Mawaziri utakamilishwa kwa kumalizia kazi za uthamini na kulipa fidia; upimaji upya wa vijiji vinavyomegewa maeneo; kushughulikia maeneo yenye changamoto zaidi ambayo yanahusisha baadhi ya vijiji vitakavyoondolewa katika maeneo ya hifadhi, vyanzo vya maji na maeneo muhimu kwa ajili ya ulinzi na usalama wa Nchi. Utekelezaji wa kazi hizo umepangwa kukamilika ifikapo Juni, 2024. Mwelekeo wa Wizara ni kuweka mifumo thabiti ya usimamizi na ufuatiliaji kwa kushirikiana na wadau wote muhimu ili kupunguza migogoro mikubwa kama hii kuendelea kujitokeza.

**Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya**

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ni miongoni mwa vyombo vilivyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sura 216 kwa ajili ya kushughulikia migogoro ya ardhi. Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa Mabaraza haya yanaundwa na kufanya kazi katika Wilaya zote nchini. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 jumla ya Mabaraza **139** yameundwa ambapo kati ya hayo Mabaraza **104** yanatoa huduma. ***Napenda kutumia fursa hii kuzihimiza Sekretarieti za Mikoa pamoja na Ofisi za Wilaya kuwezesha upatikanaji wa majengo ya ofisi na wajumbe wa baraza ili Mabaraza 35 yaliyobaki yaweze kutoa huduma.***

**41.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kushughulikia mashauri **33,250**. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 Wizara imeshughulikia mashauri **29,573** ambapo mashauri mapya ni **14,093** na mashauri ya zamani ni **15,480**. Kati ya hayo, mashauri **15,550** yameshughulikiwa na kutolewa uamuzi na mashauri **14,023** yanaendelea kushughulikiwa. Aidha, Wizara imeendelea kufanya maboresho ya Mfumo wa Kielektroniki wa Kusimamia Mashauri katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ili kuongeza ufanisi. Katika mwaka 2024/25 Wizara itashughulikia mashauri **14,023** yaliyobaki na mengine yatakayojitokeza.

**UTHAMINI WA MALI**

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pamoja na majukumu mengine ina jukumu la kuratibu, kusimamia na kutoa huduma za uthamini kwa madhumuni mbalimbali ikiwemo kuiwezesha Serikali na Taasisi nyingine katika ulipaji wa fidia, ukadiriaji tozo na kodi za Serikali, mizania ya hesabu, dhamana, rehani na mirathi. Katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kuratibu na kusimamia uandaaji na uidhinishaji wa taarifa za uthamini **54,000** ambapo kati ya hizo, taarifa za uthamini wa kawaida ni **20,000** na taarifa za fidia zenye wafidiwa **34,000** na kushughulikia malalamiko **30** ya uthamini wa fidia.

**43.** **Mheshimiwa Spika**, hadi tarehe 15 Mei, 2024, Wizara imeidhinisha taarifa za uthamini **57,285** sawa na asilimia **111.66** ya

lengo ambapo kati ya hizo, taarifa za uthamini wa kawaida ni **22,311** na taarifa za uthamini wa fidia **34,974**.

Aidha, malalamiko **91** ya fidia yalipokelewa na kushughulikiwa. Sehemu ya utekelezaji huu umehusisha mazoezi mbalimbali ya uthamini kwa ajili ya fidia kwa wananchi wanaopisha miradi ya kimkakati na maeneo ya hifadhi (**Jedwali Na.10**). Vilevile, Wizara imeendelea kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kufanya uthamini wa mali za wananchi wa Ngorongoro wanaohama kwa hiari kupisha shughuli za uhifadhi. Uthamini umefanyika kwa awamu sita **(6)** katika kata **11** na vijiji **25** ambapo mali za kaya **650** zenye thamani ya shilingi bilioni **3.79** zimefanyiwa uthamini.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** kumekuwa na changamoto ya uhalisia wa viwango vya thamani ya ardhi, hali inayoathiri ukadiriaji na ukusanyaji wa mapato ya sekta ya ardhi na utoaji wa huduma za uthamini. Kufuatia hali hii, Wizara imeanza kuandaa vitalu vya thamani ya ardhi vitakavyoakisi thamani halisi ya ardhi ili kuiwezesha Serikali kukusanya mapato stahiki yanayotokana na sekta ya ardhi. Aidha, vitalu vya thamani vitatumika kurahisisha kazi ya uthamini na hivyo kupunguza muda na gharama. Taarifa za vitalu hivyo zitatumika katika Mfumo Unganishi wa Taarifa za Ardhi (ILMISv3). Kazi ya kuandaa vitalu vya thamani ya ardhi kwa awamu ya kwanza imeanza katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Mwanza, Tanga, Pwani, Tabora na Kigoma.

**45.** ***Mheshimiwa Spika***, kumekuwepo malalamiko yanayohusu ulipaji wa fidia kutoka katika maeneo mbalimbali nchini. Malalamiko hayo yanatokana na wananchi kutofahamu kwa hakika wadau wanaohusika na ulipaji wa fidia; baadhi ya taasisi kufanya uthamini wa fidia bila kuwepo fedha kwa ajili ya malipo ya fidia; na kutozingatiwa kwa taratibu za uhakiki wa taarifa za uthamini wa fidia kwa mujibu wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Sura 138. Ili kuondoa malalamiko ambayo yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara, Wizara imetoa Waraka wa Uthamini na Fidia Na. 1 wa Mwaka 2024 ambao pamoja na mambo mengine unaelekeza taratibu zinazopaswa kuzingatiwa wakati wa shughuli za uthamini, uhakiki wa taarifa za uthamini na ulipaji

wa fidia. **Naomba ifahamike kuwa, jukumu la Wizara ni kuratibu uthamini na wajibu wa kulipa fidia ni wa taasisi itakayonufaika na uthamini huo. Aidha, natoa wito kwa wadau wote wa uthamini kuhakikisha wanazingatia Waraka wa Uthamini na Fidia.**

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara itaratibu na kusimamia uandaaji wa taarifa za uthamini **54,000.** Kati ya hizo, taarifa za uthamini wa kawaida ni **20,000** na taarifa za uthamini wa fidia **34,000**. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa mazoezi mbalimbali ya uthamini wa mali na kushiriki katika miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali. Vilevile, malalamiko yatokanayo na uthamini wa fidia yataendelea kushughulikiwa kadri yatakavyojitokeza.

## UPANGAJI NA UENDELEZAJI WA MIJI NA MAKAZI

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imedhamiria kuboresha usimamizi na utekelezaji wa upangaji wa miji na makazi. Upangaji miji na makazi ni mojawapo ya majukumu ya msingi ya Wizara ambayo yanaratibiwa na kutekelezwa kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na taratibu za uendelezaji miji. Utekelezaji wa jukumu hili unalenga kuwa na makazi yaliyopangwa, kuhifadhi mazingira na kuwa na uhakika wa ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo uwekezaji.

### Utangazaji wa Maeneo ya Upangaji Miji

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** makazi ya vijiji ni miji ya baadaye. Baadhi ya makazi hayo yanakua kwa haraka katika sura ya kimji kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ongezeko la idadi ya watu, shughuli za kiuchumi, mabadiliko ya mitazamo ya kimaisha, kuboreshwa kwa huduma za kijamii na miundombinu ya msingi mathalan; barabara, umeme, maji, shule, huduma za afya na uwekezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati katika maeneo hayo. Kufuatia hali hiyo, Wizara imeendelea kutangaza katika Gazeti la Serikali maeneo ya vijiji yaliyoiva na kuwa na sifa ya kupangwa, kusimamiwa na kuendelezwa kimji kwa mujibu wa Sheria ya Mipangomiji, Sura 355. Maeneo haya hutangazwa baada ya kupokea na kuridhia mapendekezo kutoka Mamlaka za Upangaji kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa. Aidha, makazi ya vijiji

ambayo hayajakidhi vigezo vya kuendelezwa kimji, yataendelea kuendelezwa na kusimamiwa kwa kuzingatia Mwongozo wa Upangaji na Ujenzi wa Nyumba Bora Vijijini wa mwaka 2021.

**49.** ***Mheshimwa Spika***, katika mwaka 2023/24, Wizara iliendelea kushirikiana na Mamlaka za Upangaji kutambua na kutangaza maeneo yaliyoiva kwa ajili ya kupangwa, kusimamiwa na kuendelezwa kimji. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 jumla ya maombi ya maeneo **317** kutoka kwenye mamlaka za upangaji **49** yalipokelewa ambapo maombi **88** yalitangazwa katika Gazeti la Serikali na maombi **229** yapo katika hatua mbalimbali za utangazaji. Kati ya hayo, maombi **65** ni maeneo mapya na maombi **252** ni maeneo ya urasimishaji makazi **(Jedwali Na.11).** ***Nazihimiza Mamlaka za Upangaji nchini kuendelea kutambua na kuwasilisha mapendekezo ya maeneo yaliyoiva kupangwa, kusimamiwa na kuendelezwa kimji ili yatangazwe katika Gazeti la Serikali kuwa maeneo ya upangaji kwa mujibu wa Sheria.***

**Uandaaji wa Mipango Kabambe**

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mipango Kabambe hutoa dira ya matumizi ya jumla ya ardhi na hivyo kuzisaidia Mamlaka za upangaji (Majiji, Manispaa, Miji na Miji Midogo) katika udhibiti, usimamizi, ukuaji na uendelezaji wa miji. Mipango Kabambe ni dira ya utoaji wa huduma mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kimazingira pamoja na usalama wa ustawi wa miji na watu wake. Mipango hii huandaliwa kwa mujibu wa Sheria ya Mipangomiji, Sura 355 ambapo Wizara ina jukumu la utoaji wa mwongozo wa uandaaji wa mipango kabambe, uidhinishaji wa mipango, ufuatiliaji wa utekelezaji, uidhinishaji wa marekebisho ya matumizi ya ardhi pamoja na uhuishaji wa mipango hiyo pindi utekelezaji wake unapofikia ukomo au kujitokeza kwa mahitaji ya ulazima.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia umuhimu huo, Wizara katika mwaka 2023/24, iliahidi kuendelea kushirikiana na Mamlaka za Upangaji katika uandaaji na utekelezaji wa Mipango Kabambe kwa mujibu wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 Mpango Kabambe wa Mji wa Bagamoyo umekamilika na kuidhinishwa. Mipango Kabambe mitatu (**3**) ya Miji ya Kahama na Mafinga na Jiji la Kibiashara la Kwala ipo katika


hatua mbalimbali za uandaaji. Aidha, ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mipango Kabambe ya Miji mitano (**5**) katika Halmashauri za Jiji la Arusha, Manispaa ya Iringa, Miji ya Babati, Tunduma na Njombe umefanyika.

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** ufuatiliaji huo ulibaini utekelezaji usioridhisha, ushirikishwaji duni wa wadau na wananchi, upungufu wa wataalam na vitendea kazi. Kutokana na changamoto hizo, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI imezielekeza Mamlaka za Upangaji kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Mipango Kabambe na Mipangokina na kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuihuisha na kuifanyia marekebisho ya matumizi kadri ya mahitaji yanavyojitokeza.

**53.** ***Mheshimwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara itaendelea kushirikiana na Mamlaka za Upangaji kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Mipango Kabambe katika Mamlaka za Upangaji minne (4) ambayo ni Jiji la Tanga, Manispaa ya Moshi na Halmashauri za Miji ya Korogwe na Kibaha. Vilevile, Wizara itasimamia ukamilishaji wa uandaaji wa Mipango Kabambe miwili (2) ya Halmashauri za Mji wa Mafinga na Manispaa ya Kahama. Pia, Wizara itaratibu uandaaji wa mipango ya uendelezaji wa maeneo matatu (3) yaliyochakaa katika Majiji ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha kwa lengo la kuyaboresha maeneo hayo ili yaendane na mahitaji ya kijamii na kiuwekezaji ya sasa na baadae.

**Uandaaji wa Mipangokina**

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kuratibu uandaaji na uidhinishaji wa Mipangokina ili kuelekeza ukuaji, uboreshaji wa makazi, hifadhi ya mazingira, kuondoa ukinzani wa matumizi ya ardhi na kutoa uhakika wa upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali yakiwemo ya uwekezaji, makazi, biashara, miundombinu na huduma za jamii. Mipangokina huandaliwa kama sehemu ya utekelezaji wa mapendekezo ya matumizi ya ardhi yaliyomo katika mipango kabambe kupitia Mamlaka za Upangaji. Mipangokina inawezesha upimaji wa viwanja ardhini na uendelezaji wa maeneo ya huduma kama barabara, simu, umeme, mawasiliano na kurahisisha umilikishaji.




*Mpango kina wa makazi Kijiji cha Kapanga kilichopo halmashauri ya wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi*

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kuidhinisha michoro ya Mipangokina **2,000** kutoka kwenye Mamlaka za Upangaji nchini.
Hadi tarehe 15 Mei, 2024 michoro ya Mipangokina **1,783** yenye jumla ya viwanja **244,519** vya matumizi mbalimbali imeidhinishwa sawa na asilimia **89.1** ya lengo. Katika mwaka 2024/25, Wizara inatarajia kuidhinisha Mipangokina **2,000** kutoka katika Mamlaka za Upangaji nchini.

**Urasimishaji wa Makazi**

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 zinaelekeza kuwa maeneo ya makazi yaliyoendelezwa bila kupangwa yatarasimishwa. Katika kutekeleza matakwa ya sera hizi, Wizara imeendelea kuratibu urasimishaji wa makazi yaliyoendelezwa bila kupangwa kwa kuishirikisha jamii, asasi za kiraia na sekta binafsi.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kurasimisha makazi 300,000. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, jumla ya makazi **237,424** sawa na asilimia **79.14** yamerasimishwa (***Jedwali Na.12***). Katika mwaka 2024/25 Wizara itarasimisha makazi **500,000**. Aidha, Wizara itakamilisha tathmini ya utekelezaji wa Programu ya

Kurasimisha Makazi na Kudhibiti Makazi yasiyopangwa Mijini (2013-2023) ili kubaini mafanikio, changamoto zilizojitokeza na matarajio ya baadaye. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji na Sekta Binafsi inaendelea kufanya uhamasishaji kwa wananchi ambao bado makazi yao hayajarasimishwa ili kukamilisha zoezi hilo na kuendeleza kliniki za ardhi ili kukwamua urasimishaji katika maeneo ambayo hayajakamilisha miradi ya urasimishaji makazi yasiyopangwa.

**58.** ***Mheshimiwa Spika***, Ili kufikia lengo la kurasimisha makazi **500,000** katika mwaka 2024/25, Wizara itaanza na kukwamua urasimishaji ambao ulikwama kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo uchangiaji hafifu wa wananchi na baadhi ya kampuni zilizofanya urasimishaji kutokamilisha kazi kwa wakati. Mathalan, katika mkoa wa Dar es Salaam urasimishaji haukukamilika katika mitaa **270**. Ili kukwamua kazi hizo Wizara itaajiri wataalam wa muda wa mipangomiji na upimaji na kuhakikisha kazi hizo zinakamilika. Zoezi hili limeanza kutekelezwa katika mitaa **13** ya mkoa wa Dar es Salaam. ***Natoa Wito kwa wananchi ambao makazi yao hayajarasimishwa kujitokeza kurasimishiwa.***

**Udhibiti na Usimamizi wa Uendelezaji Miji (mabadiliko ya matumizi ya ardhi)**

**59.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kumekuwepo na ongezeko la ukuaji wa miji na kusababisha hitaji kubwa la kubadili matumizi ya ardhi, Wizara imefanya marekebisho ya Kanuni za Viwango vya Kupanga Ukubwa wa Ardhi kwa matumizi mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye. Pia, imeboresha Kanuni ya Makundi ya Matumizi na Madaraja ya Matumizi ili kuwezesha matumizi ya ardhi kushabihiana hivyo kuondoa migogoro ya matumizi ya ardhi. Vilevile, katika Kanuni hiyo mchakato wa mabadiliko ya matumizi ya ardhi umeboreshwa ambapo maombi yatajadiliwa katika ngazi ya mtaa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ndipo yajadiliwe na Kamati za Halmashauri ili kuimarisha ushirikishwaji wa wadau hivyo kupunguza migogoro ya ardhi.

**60.** ***Mheshimiwa Spika***, maeneo ya wazi yanapaswa kusimamiwa, kutunzwa na kulindwa ili yatumike kwa maslahi

mapana ya umma. Hata hivyo, maeneo hayo yamekuwa yakivamiwa na kubadilishwa matumizi au kutumiwa vinginevyo kutokana na sababu nyingi zikiwemo uvamizi wa makusudi, kutolipwa fidia kwa wamiliki wa asili, kutumika kama vyanzo vya mapato ya Halmashauri na usimamizi usioridhisha wa Mamlaka zilizopewa kusimamia maeneo hayo. Ili kukabiliana na matumizi holela ya maeneo hayo, matumizi ya maeneo ya wazi yamewekewa utaratibu wa kuidhinishwa na Wizara endapo yatahitajika kutumika kwa maslahi ya umma. **Napenda kusisitiza kuwa maeneo ya wazi ni lazima yatunzwe, yalindwe na kudumishwa ili yatumike kwa manufaa ya umma yakiwemo kufanyia mikutano ya hadhara, kupendezesha mandhari na mazingira ya mji, michezo kwa watoto katika mitaa, watu kupumzika, kufanyia chanjo kwa umma na kutumika kama hifadhi ya watu na misaada wakati wa maafa, majanga au dharura.**

**61.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kuratibu na kuidhinisha mabadiliko ya matumizi ya ardhi **500**. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, jumla ya maombi **465** sawa na asilimia **93.2** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi yaliidhinishwa. Katika mwaka 2024/25 Wizara itaendelea kupokea na kuidhinisha maombi ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi **500** kwa kuzingatia sheria na kanuni za mipangomiji.

**Usimamizi na Uratibu wa Sekta ya Nyumba**

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya nyumba imeendelea kuwa na mchango muhimu kiuchumi na kijamii kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Upatikanaji wa nyumba ni mojawapo ya kiashiria cha kukua kwa uchumi wa nchi na kupungua kwa umasikini wa kipato. Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa huduma za uendelezaji nyumba ikiwemo upatikanaji wa mikopo ya nyumba yenye masharti nafuu. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 Serikali kupitia *Tanzania Mortgage Refinancing Company (TMRC)* imewezesha taasisi za fedha **31** kutoa mikopo ya nyumba yenye riba nafuu kiasi cha shilingi bilioni **587.**

**Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali**

**63. *Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali unalenga kuongeza upatikanaji wa makazi bora kwa watumishi wa Serikali, kuwawezesha kukarabati, kukamilisha au kujenga nyumba mpya. Katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia Mfuko ilipanga kukopesha watumishi **100**. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 mfuko umewezesha watumishi **87** kupata mikopo ya nyumba yenye thamani ya shilingi Billioni **1.06** hivyo kufanya watumishi waliopata mikopo kufikia **1,706** ikiwa na thamani ya shilingi bilioni **10.75.** Katika mwaka 2024/25 watumishi wa Serikali **100** watawezeshwa kupata mikopo ya nyumba yenye thamani ya shilingi billioni **2.2.**

**Ushirikiano na Taasisi za Kimataifa katika Uendelezaji wa Makazi**

**64. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali za kimataifa ikiwemo Shirika la Makazi Duniani (*UN-Habitat*) katika masuala ya uendelezaji makazi nchini. Ushirikiano huo, licha ya kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia baina ya nchi yetu na nchi nyingine Duniani, umekuwa ni jukwaa la kujifunza na kupata uzoefu katika kutekeleza Ajenda Mpya ya Makazi Duniani ambayo inatekelezwa na nchi zote wanachama wa umoja wa mataifa.

**65. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ya makazi iliandaa maadhimisho ya Siku ya Makazi Duniani yaliyofanyika tarehe 02 Oktoba, 2023 Jijini Dodoma yakiongozwa na kauli mbiu ya "*Resilient Urban Economies - Cities as Drivers of Growth and Recovery*" ikimaanisha "*Uchumi Himilivu wa Miji - Miji Kichocheo cha Ukuaji na Ufufuaji wa Uchumi.* Maadhimisho haya yalitolewa kwa njia ya mjadala na mafunzo ambapo wawakilishi **150** kutoka Wizara, Taasisi za elimu, Jiji la Dodoma, Taasisi zinazotoa huduma, NHC na WHC walishiriki. Katika mkutano huo, wadau walijadili namna ya kufanya miji kuwa kichocheo cha ukuaji na ufufuaji wa uchumi hasa baada ya janga la UVIKO 19 na namna ya kujipanga na majanga yajayo.

**66.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ilishiriki Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu uliofanyika mwezi Julai, 2023 Jijini New York, Marekani. Mkutano huo ulilenga kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa hiari wa Malengo ya Mendeleo Endelevu (SDGs) ya Umoja wa Mataifa ambayo kwa hapa nchini, malengo hayo huratibiwa na Wizara ya Fedha. Katika wasilisho hilo, Wizara sambamba na Wizara nyingine, imehusika kitaalamu na Lengo Na. 11 kati ya malengo 5 yaliyokuwa yanatolewa taarifa katika mkutano huo kuhusu kufanya "Majiji na Makazi kuwa Jumuishi, Salama, Stahimilivu na Endelevu". Katika mwaka 2024/25, Wizara itaendelea kuimarisha uhusiano na taasisi hizo za kimataifa katika masuala ya maendeleo ya makazi.

**USIMAMIZI WA SEKTA YA MILKI**

**67.** ***Mheshimiwa Spika*,** pamoja na majukumu mengine, Wizara ina jukumu la kusimamia Sekta ya Milki nchini. Sekta ya Milki inajumuisha ardhi iliyopangwa na kupimwa kwa kujengwa nyumba za makazi, majengo ya biashara, viwanda, maeneo ya burudani na majengo ya matumizi maalum. Wadau wa Sekta ya Milki wanajumuisha wawekezaji, wamiliki wa majengo, wapangaji, taasisi za fedha, mawakala, wanunuzi wa nyumba na viwanja na watafiti wa soko la nyumba. Sekta hii imeendelea kukua na kuvutia wadau wengi zaidi kutokana na fursa za uwekezaji katika nyanja mbalimbali ikiwemo soko la fedha na nyumba za kupangisha.

**68.** ***Mheshimiwa Spika*,** ili kuimarisha usimamizi wa sekta hii, katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kukamilisha uandaaji wa Sheria na kanuni za kusimamia Sekta ya Milki, kutoa elimu kwa wadau na kuandaa kanzidata ya Waendelezaji Milki pamoja na mawakala wa Milki. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mapendekezo ya Kutunga Sheria ya Milki yameandaliwa na kuwasilishwa kwenye mamlaka ya uamuzi. Mapendekezo hayo pamoja na mambo mengine yanalenga kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Sekta ya Milki '*Real Estate Regulatory Authority*' ili kuongeza tija na ufanisi katika usimamizi na uratibu wa sekta hii muhimu kwa uchumi wa nchi.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu Mkutano wa wadau wa Sekta ya Milki uliofanyika tarehe 19 – 20 Januari, 2024 jijini Dar es Salaam ukiwa na lengo la kuwatambua mawakala na kujadili namna bora ya utekelezaji wa shughuli zao. Kauli mbiu ya Mkutano huo ilikuwa ni "*Urasimishaji wa Shughuli za Mawakala wa Milki kwa Maendeleo ya Taifa*". Mkutano huo ulihudhuriwa na wawakilishi kutoka kampuni za uendelezaji milki; mawakala wa milki; na taasisi za umma na binafsi. Aidha, kupitia mkutano huu Wizara imeweza kuboresha taarifa za kanzidata ya mawakala na wadau mbalimbali wa sekta ya milki.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara imepanga kuanzisha kanzidata kwa ajili ya usajili wa miradi ya uendelezaji milki. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu shughuli za sekta ya milki ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha katika kuboresha mazingira ya kuvutia uwekezaji na biashara katika Sekta ya Milki. ***Natoa wito kwa wadau wote wa sekta ya milki kuhakikisha wanajitokeza ili shughuli zao ziweze kutambuliwa na Serikali.***

**UPIMAJI NA RAMANI**

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli za upimaji ardhi wa nchi kavu na ndani ya maji; utayarishaji wa ramani kwa ajili ya utekelezaji wa mipango mbalimbali ya Serikali; na kutoa miongozo, kanuni na taratibu zinazohusu upimaji ardhi kulingana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji.

**Uwekaji wa Alama za Msingi za Upimaji Ardhi**

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** alama za msingi ni miongoni mwa miundombinu muhimu katika kazi za upimaji ardhi. Wizara inaendelea kuratibu na kuongeza alama za msingi za upimaji ili kuwezesha na kurahisisha kazi, kupunguza muda pamoja na gharama za upimaji ardhi. Katika mwaka 2023/24, Wizara iliahidi kuweka alama mpya za msingi **267** katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 alama za msingi za upimaji **378** zimewekwa katika mikoa ya Dodoma (**47**), Manyara (**13**), Tanga (**40**), Tabora (**22**), Singida (**10**), Iringa (**26**), Pwani (**27**), Mara (**14**),

Kigoma (**12**), Geita (**24**), Kagera (**12**), Kilimanjaro (**10**) na Shinyanga (**47**) na hivyo kuwa na jumla ya Alama za Msingi za Upimaji **1,423**. Katika mwaka 2024/25, Wizara itaweka alama mpya za msingi **150** katika Halmashauri mbalimbali nchini. Lengo la Wizara ni kuwekeza zaidi kwenye usimikaji wa Vituo vya Kielektroniki vya Upimaji (*Continuously Operating Reference Station- CORS*) ambavyo vitawezesha kazi za upimaji kufanyika kwa ufanisi zaidi.



*Alama za Msingi za upimaji wa ramani.*

**73.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24, Wizara iliahidi kuanza hatua za awali za ujenzi wa vituo **22** vya kielektroniki vya upimaji (*Continuously Operating Reference Station - CORS*) katika makao makuu ya mikoa **22**. Vituo hivyo ni maalum kwa ajili ya kutuma taarifa za upimaji (GNSS *signals*) kwa wapima ardhi. Mkandarasi atakayefanya kazi ya kusimika vituo hivyo amepatikana, makubaliano yamefanyika na kazi ya usimikaji wa vituo hivyo itafanyika katika mwaka 2024/25.

**Upimaji wa viwanja na mashamba**

**74.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kuratibu, kusimamia na kuidhinisha viwanja **500,000** na mashamba **500**. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, viwanja **249,340** na mashamba **7,559** yamepimwa na kuidhinishwa sawa na asilimia **49.87** ya lengo la viwanja na asilimia **1,511.8** ya lengo la mashamba (***Jedwali Na.13***). Ongezeko kubwa la mashamba yaliyopimwa na

kuidhinishwa linatokana na mpango wa Serikali wa kuhamisha wananchi kutoka katika eneo la hifadhi ya Ngorongoro kwenda Msomera na Saunyi mkoani Tanga. Katika mwaka 2024/25, Wizara itasimamia upimaji na uidhinishwaji wa viwanja **500,000** na mashamba **500**.

**Utayarishaji wa Ramani**

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ramani ni zao la kazi za upimaji ardhi, ambalo huweza kupatikana katika mfumo wa nakala ngumu au nakala tete. Ramani huzalishwa kutokana na taarifa za msingi za kijiografia. Ramani zinazotayarishwa zinajumuisha za viwanja, mashamba, mipaka ya kiutawala na kimataifa na Hifadhi za Taifa. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, ramani za mipaka ya kiutawala ya Wilaya **17** katika Mikoa ya Dar es Salaam (**5**), Kagera (**7**), Dodoma (**2**), Tanga (**1**), Arusha (**1**) na Mbeya (**1**) zimeandaliwa. Katika mwaka 2024/25, Wizara itaendelea kuandaa ramani za mipaka ya kiutawala ya Wilaya **25**. Mwelekeo wa Wizara ni kuwa na Ramani za kidigitali ili kurahisisha upatikanaji wa ramani.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** kumekuwepo na changamoto ya uandaaji wa ramani unaofanywa na baadhi ya taasisi na sekta binafsi bila kuzingatia sheria na ubora hali inayosababisha kuwepo kwa tafsiri zisizo sahihi za mipaka ya kimataifa na kiutawala. Matokeo yake ni kuwepo kwa migogoro ambayo ingeweza kuzuilika endapo taratibu za uandaaji wa ramani zingezingatiwa kwa mujibu wa Sheria ya Upimaji, Sura 324. **Naelekeza taasisi zote za umma na binafsi zizingatie takwa la kisheria linalompa mamlaka Mkurungenzi wa Upimaji na Ramani kuandaa na kuidhinisha ramani zote zikiwemo za mipaka ya kiutawala na kimataifa**.

**Upimaji wa Mipaka ya Vijiji**

**77.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ina jukumu la kuratibu na kupima mipaka ya vijiji ambapo katika mwaka 2023/24 ilipanga kuhakiki na kupima mipaka ya vijiji **100.** Hadi tarehe 15 Mei, 2024, jumla ya vijiji **742** vimehakikiwa na kupimwa mipaka. Kati ya hivyo, vijiji **475** vimehakikiwa mipaka na vijiji **267** vimepimwa (**Jedwali Na.14**). Aidha, migogoro ya mipaka ya vijiji vitano (**5**) vya Bangalala,

Mwembe, Makanya, Mgwasi na Nasuro katika Wilaya ya Same imetatuliwa. Vilevile, mgogoro wa mipaka kati ya shamba la Malonje (Efatha) na vijiji vitano (**5**) vya Sikaungu, Msandamuungano "A", Msandamuungano "B", Songambele Azimio na Malonje katika Wilaya ya Sumbawanga umetatuliwa. Katika mwaka 2024/25, Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI kuhakiki na kupima mipaka ya vijiji **1,000** nchini. ***Natoa rai kwa mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa kuhakikisha kuwa Vijiji vinavyoanzishwa vinapimwa mipaka yake kabla ya kutangazwa katika gazeti la Serikali.***

**Tafsiri na Uhakiki wa Mipaka ya Kiutawala na Hifadhi**

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kutafsiri ardhini Matangazo ya Serikali (GNs) ya mipaka ya utawala na hifadhi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara za kisekta na Mamlaka mbalimbali ili kutatua changamoto za mipaka. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, matangazo ya mipaka ya kiutawala saba (**7**) yametafsiriwa katika
Wilaya za Sumbawanga na Momba (**2**), Wanging'ombe na Makete (**2**), Shinyanga na Nyang'hwale (**2**), Kilindi na Kiteto (**1**). Vilevile, Tangazo la Serikali namba 235 la mwaka 1968 la Hifadhi ya Taifa ya Serengeti limetafsiriwa na kuwezesha utatuzi wa mgogoro wa mpaka wa vijiji saba (**7**) vya Nyambuli, Machochwe, Mbalibali, Bisarara, Bonchugu, Nyamakendo na Merenga katika Wilaya ya Serengeti.

***Upangaji na Upimaji wa Viwanja Mbadala vya Waathirika wa Maporomoko ya Mlima Hanang'***

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu imekumbwa na maafa yaliyotokana na mvua nyingi ambazo zimeendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini. Miongoni mwa maeneo yaliyokumbwa na maafa hayo ni Wilaya ya Hanang'. Kufuatia maafa yaliyotokea katika Wilaya ya Hanang' kutokana na kuporomoka kwa sehemu ya Mlima Hanang', Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI imepanga na kupima viwanja mbadala vya waathirika wa maporomoko hayo. Viwanja hivi vimepimwa kutoka katika eneo la ekari 100 zilizomegwa kutoka shamba la Jeshi la Magereza lililopo katika kijiji cha

Gidagamowd, Wilaya ya Hanang'. Jumla ya viwanja **269** vimepimwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo makazi (235), makazi na biashara (15), biashara (7) na huduma za jamii (12). Aidha, waathirika wote **108** wamepatiwa viwanja kwa ajili ya makazi.

**Upangaji na Upimaji wa Viwanja na Mashamba kwa Ajili ya Wananchi Wanaohama kwa Hiari Kutoka Katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro**

**80. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii (Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro) inaendelea na upimaji wa viwanja na mashamba kwa ajili ya makazi, kilimo na ufugaji. Kazi hii inafanyika katika vijiji vya Msomera (Handeni) na Saunyi (Kilindi) katika Mkoa wa Tanga ambapo lengo ni kupima viwanja **10,000** na mashamba **8,500.** Hadi tarehe 15 Mei, 2024, viwanja **5,031** vya makazi vyenye wastani wa ukubwa wa ekari **2.5** na mashamba **7,897** yenye ukubwa wa wastani wa ekari **5** yamepimwa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, pamoja na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji ikiwemo mvua kubwa zilizonyesha, Wizara imejipanga kukamilisha upimaji wa mashamba ifikapo Juni, 2024.




*Muonekano wa mpango wa matumizi ya ardhi katika eneo la Msomera wilayani Handeni mkoa wa Tanga.*

**HUDUMA ZA TEHAMA**

**81. *Mheshimiwa Spika,*** mpango wa Wizara ni kuifanya TEHAMA kuwa nyenzo muhimu ya kuendesha shughuli za sekta ya ardhi. Lengo la hatua hiyo ni kuongeza uwazi, ufanisi, uwajibikaji na kupunguza gharama na muda wa utoaji huduma. Wizara imekamilisha usanikishaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Huduma za Ardhi kwa kutumia watalaam wa ndani. Hatua inayoendelea ni kuhamisha taarifa kutoka kwenye mifumo ya zamani na majalada kwa awamu kwenda kwenye Mfumo ulioboreshwa. Aidha, mfumo utaanza kutumika kwa awamu ya kwanza katika Mikoa ya Arusha, Tanga, Mbeya, Mwanza na Dodoma ifikapo Juni, 2024. Manufaa ya mfumo huu ni pamoja na: -

(i) Kuwezesha wananchi kuomba huduma bila kulazimika kwenda Ofisi za Ardhi;

(ii) Kufahamu muda ambao huduma inayoombwa itakamilika. Hii itawapa wananchi uwezo wa kutoa taarifa endapo watacheleweshewa huduma;

(iii) Kuondoa changamoto ya upotevu wa nyaraka zinazowasilishwa na wananchi kwani zitakuwa zinawasilishwa kupitia mfumo (online);

(iv) Kuongeza uwazi na uwajibikaji katika ngazi zote za utendaji kazi kwa kuwa viongozi wataweza kufuatilia mwenendo wa utekelezaji wa majukumu unavyoendelea;

(v) Kuunganishwa na mifumo mingine ya Serikali ili kurahisisha utoaji wa huduma; na

(vi) Kuondoa changamoto ya miliki pandikizi na hivyo kudhibiti migogoro ya ardhi.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara iliahidi kusimika na kusambaza miundombinu wezeshi ya TEHAMA katika Ofisi za Ardhi za Mikoa **25** na Halmashauri **132**. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, usimikaji wa miundombinu wezeshi ya TEHAMA katika Halmashauri **44** imekamilika na kazi ya usimikaji wa miundombinu

hiyo inaendelea katika Halmashauri **41**. Pamoja na huduma nyingine, miundombinu hii itatumika katika utoaji wa huduma za ardhi kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Huduma za Ardhi.

**83.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara pia, iliahidi kuanzisha wavuti ya wateja (*Self-Service Web Portal*) kwa lengo la kuwawezesha wananchi kupata huduma kupitia wavuti hiyo bila kulazimika kwenda ofisi za ardhi na hivyo kupunguza gharama na muda wa kupata huduma. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba usanikishaji wa Wavuti hiyo pamoja na *Mobile App* umekamilika na huduma zimeanza kutolewa kupitia wavuti hiyo. Katika mwaka 2024/25, Wizara itakamilisha usambazaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Huduma za Ardhi katika Mikoa iliyobaki hatua kwa hatua. Pia, itawajengea uwezo watumiaji wa Mfumo huo katika ngazi ya Wizara, Mikoa na Halmashauri. Vilevile, wananchi watajengewa uwezo kuhusu matumizi ya Mfumo kwa njia mbalimbali ikiwemo vipeperushi, mitandao ya kijamii, vyombo vya habari, mabango na kwa njia ya video zitakazopatikana kwenye Mfumo.

**MAPITIO YA SERA NA SHERIA**

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa, Sera, Sheria na Kanuni za Sekta ya Ardhi zinafanyiwa marekebisho ili kukidhi mahitaji. Katika kutekeleza azma hiyo, Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 zimeendelea kufanyiwa marekebisho ambapo Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 (Toleo la mwaka 2023) imeidhinishwa. Hatua inayofuata ni kutoa elimu kwa umma, kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali na kuanza utekelezaji wa mkakati wa kutekeleza Sera. Aidha, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 inaendelea kufanyiwa marekebisho ambapo pamoja na kuhuisha masuala ya makazi, itajumuisha masuala mahsusi ya usimamizi wa sekta ya nyumba ili kuongeza tija na ustawi wa wananchi na Taifa kwa ujumla.

**85.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kukamilisha taratibu za kutunga na kurekebisha sheria mbalimbali za sekta ya ardhi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mapendekezo ya Kutunga Sheria ya Chuo cha Ardhi, Sheria Mpya ya Upimaji na Usajili wa Wapima Ardhi na Sheria ya Milki

yameandaliwa na yapo katika hatua za ukamilishaji. Aidha, marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji, Sura 426 yamefanyika ili pamoja na masuala mengine, kuainisha na kuongeza wigo wa madaraja ya Wataalam wa Mipangomiji na sifa za usajili kwa kila daraja.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha utaratibu wa utekelezaji wa shughuli za Madalali na Wasambaza Nyaraka wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, Kanuni za Uteuzi, Malipo na Nidhamu kwa Madalali wa Baraza na Wasambaza Nyaraka zimefanyiwa marekebisho na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 61 la tarehe 26 Januari, 2024. Aidha, Kanuni za Ada kwa Huduma za Uthamini na Ushauri wa Kitaalam za mwaka 2023 zimetungwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 548 la tarehe 4 Agosti, 2023. Kanuni hizi zinalenga kuboresha huduma za uthamini na zitatumika kwa Wathamini waliosajiliwa na kutoa huduma za uthamini na ushauri wa kitaalam kwa sekta binafsi. Vilevile, Kanuni za Uthamini na Usajili wa Wathamini (Mafunzo na Mitihani) za mwaka 2023 zimefanyiwa marekebisho na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 450 la tarehe 7 Julai, 2023.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetunga upya Kanuni mbili (2) za Sheria ya Mipangomiji, Sura 355. Kanuni hizo ni Kanuni ya Viwango vya Kupanga Maeneo kwa Matumizi Mbalimbali ya Ardhi na Kanuni ya Makundi ya Matumizi na Madaraja ya Matumizi. Madhumuni ya kutunga upya kanuni hizi ni kujumuisha matumizi mapya ambayo hayakuzingatiwa katika kanuni zilizokuwepo; baadhi ya vigezo na viwango vya upangaji kutokidhi mahitaji; mabadiliko ya miji yaliyoainishwa katika taarifa ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 pamoja na Sensa ya Majengo ya Mwaka 2022 yanayohitaji kufanyika kwa mabadiliko ya kanuni; kukidhi mahitaji ya kila matumizi ya ardhi; na mabadiliko ya kiuchumi na sura za miji kuhitaji mwongozo mpya wa kikanuni. Taratibu za kukamilisha utungaji wa kanuni hizo zinaendelea.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Wizara itakamilisha marekebisho ya Sera ya Maendeleo ya Makazi pamoja na kufanya marekebisho ya sheria na kanuni mbalimbali za sekta ya ardhi kadri itakavyohitajika.

**MIRADI YA MAENDELEO**
**Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi**

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Wizara iliidhinishiwa shilingi bilioni **4.5** kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, Wizara imepokea shilingi bilioni **3.6** kwa ajili ya utekelezaji wa Programu sawa na asilimia **80**. Katika kipindi hicho, viwanja **10,463** vimepangwa, viwanja **9,463** vimepimwa na viwanja **8,177** vimemilikishwa kwenye Halmashauri **14**.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22 Wizara ilizikopesha Mamlaka za Serikali za Mitaa **57**, Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Iringa, Chuo Kikuu Ardhi na Vyuo vya Ardhi vya Morogoro (ARIMO) na Tabora (ARITA) shilingi bilioni **50** kwa ajili ya kuongeza kasi ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Wizara imeendelea kufuatilia marejesho ya fedha hizo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, shilingi billioni **23.71** zimerejeshwa na Halmashauri **55** ambapo Halmashauri **13** zimerejesha mikopo yao kwa asilimia **100**; Halmashauri **42** zimerejesha sehemu ya fedha; na Halmashauri mbili (**2**) za Manispaa ya Shinyanga na Wilaya ya Musoma hazijarejesha kabisa (**Jedwali Na.15).** Napenda kuzipongeza Halmashauri ya Jiji la Mwanza; Manispaa za Morogoro, Ilemela na Kigamboni; Halmashauri za Moshi, Meru, Kilosa, Geita, Kaliua, Mbozi; na Halmashauri za Miji ya Tunduma na Bariadi zilizotekeleza wajibu wa kurejesha fedha kwa mujibu wa makubaliano. ***Naungana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, kuzitaka Halmashauri na Taasisi ambazo hazijarejesha au hazijakamilisha marejesho, kurejesha fedha wanazodaiwa ifikapo Juni, 2024 ili kuziwezesha Halmashauri nyingine kunufaika na fedha hizo. Kwa halmashauri ambazo hazitatekeleza agizo hilo, fedha hizo zitakatwa moja kwa moja kutoka kwenye ruzuku zao.***

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuepuka changamoto zilizojitokeza kwenye utaratibu wa utoaji wa mikopo kwa awamu ya kwanza, Wizara imefanya maboresho katika utaratibu huo. Maboresho yaliyofanyika yanahusisha fedha kutolewa kupitia Ofisi za Ardhi za Mikoa; fedha kutolewa kwa awamu kwa kuzingatia hatua ya kazi

iliyofikiwa; na fedha za mauzo ya viwanja kuwekwa kwenye akaunti maalum ya Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi.

**92. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara imebuni na kusanifu Mradi wa *Msalato Satellite City* katika Jiji la Dodoma utakaokidhi mahitaji ya watu zaidi ya **14,776**. Mradi huo utawezesha ujenzi wa makazi bora yenye miundombinu na huduma muhimu za jamii na biashara za aina mbalimbali hivyo kupunguza msongamano wa wananchi wanaofuata mahitaji katikati ya mji. Katika mwaka 2024/25, Wizara imepanga kubuni na kusanifu miji ya Satelaiti miwili (2) katika majiji ya Dodoma (Msalato) na Arusha (AFCON City) ili kuwa na miji nadhifu na kudhibiti makazi holela. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia kikamilifu matumizi ya fedha za mfuko ili kuwezesha halmashauri kupanga na kupima miradi iliyoandaliwa.




*Muonekano wa Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi wa Msalato Satellite City jijini Dodoma*

**93. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa mpango wa uendelezaji wa maeneo ya mijini yenye thamani kubwa yaliyochakaa ambayo hayatumiki kwa tija. Utekelezaji wa mpango huu utawezesha uboreshaji mandhari ya miji, kuchochea shughuli za kiuwekezaji na kuongeza thamani ya ardhi katika maeneo hayo. Ili kuwezesha utekelezaji, Wizara imeandaa

Mwongozo wa Upangaji na Uendelezaji Upya wa Maeneo Yaliyochakaa unaoweka utaratibu wa utekelezaji ambao utasambazwa kwenye Mamlaka za Upangaji ili uweze kutumika. Katika mwaka 2024/25, Wizara itaanza utekelezaji wa Mpango wa Uendelezaji Upya wa Maeneo Yaliyochakaa katika majiji ya Mbeya na Dar es Salaam.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Wizara kupitia Programu ya KKK itapanga, kupima na kumilikisha viwanja **100,000** kwa ajili ya matumizi mbalimbali kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji pamoja na sekta binafsi. Aidha, Wizara itaandaa mipango ya uendelezaji upya wa maeneo kongwe katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha. Vilevile, utafanyika uhakiki wa matumizi ya ardhi katika Majiji matano (5) ya Dodoma, Mbeya, Mwanza, Arusha na Tanga na Manispaa tatu (3) za Kahama, Morogoro na Kigoma.

**Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi**

**95.** ***Mheshimiwa Spika;*** mwaka 1991/92, Serikali ilianzisha Mfuko Maalum wa Kupima Viwanja (Plot Development Revolving Fund – PDRF) ambao ulilenga kuwezesha upangaji, upimaji na umilikishaji viwanja. Hata hivyo, mwaka 2016 Serikali ilisitisha matumizi ya akaunti za mifuko mbalimbali nchini ikiwemo akaunti ya Mfuko huu. Kusitishwa kwa matumizi ya akaunti kuliikosesha Wizara chanzo cha uhakika cha fedha za upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi.

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia umuhimu wa upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi nchini, Serikali imeridhia kurejeshwa kwa matumizi ya akaunti ya Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi. Kwa kuanzia, Serikali imetoa mtaji wenye thamani ya shilingi bilioni **15.4** na imeridhia marejesho ya fedha kiasi cha shilingi bilioni **50** za Kupanga, Kupima na Kumilikisha zinazodaiwa kwenye mikopo ya Halmashauri ziingizwe kwenye Mfuko huu. Ili kuwezesha uendelevu wa mfuko na ufanisi katika utekelezaji, Mwongozo wa Uratibu na Usimamizi wa Mfuko umeandaliwa. ***Wizara inatoa shukrani za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kurejesha matumizi ya akaunti ya mfuko.***

**Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP)**

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP). Mradi huu unatekelezwa kwa miaka mitano (**5**) (2022/23 – 2026/27) katika mikoa yote **26** na unalenga kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta ya Ardhi ikiwemo uboreshaji wa miundombinu ili kurahisisha utoaji huduma za kupanga, kupima, kumilikisha ardhi, uthamini na maboresho ya sera na sheria mbalimbali.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipokea na kutekeleza maelekezo ya Bunge ya kufanya mapitio ya mpango wa utekelezaji wa Mradi wa LTIP ili kuongeza mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara ilifanya mapitio ya mpango wa utekelezaji wa Mradi na kuongeza mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji kutoka mpango wa awali wa vijiji **250** hadi kufikia vijiji **1,667**.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia Mradi huu ilipanga kupima mipaka ya vijiji **700**; kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi na mipangokina ya vijiji **700**; kuandaa na kuidhinisha Hati za Hakimiliki za Kimila **200,000** na kukarabati ofisi za ardhi za Halmashauri **41**. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, jumla ya mipaka ya vijiji **407** imepimwa na kuhakikiwa, vyeti vya ardhi ya kijiji **320** vimetolewa na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **843** imeandaliwa katika Halmashauri **21 (Jedwali Na.16)**. Mipango hii imewezesha kupangwa kwa ardhi yenye ukubwa wa jumla ya Hekta **5,013,087** kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo malisho (**564,691),** makazi (**267,595**), hifadhi za misitu (**363,935**), makazi na kilimo (**1,230,898**), kilimo (**2,538,750**), huduma za kijamii (**44,476**) na ardhi ya akiba (**2,742**). Aidha, vipande vya ardhi **381,509** vimetambuliwa kwa ajili ya kutoa Hati za Hakimiliki za Kimila katika Wilaya sita (**6**) za Tanganyika (**69,216**), Maswa (**85,182**), Mbinga (**56,547**), Mufindi (**72,991**), Songwe (**77,514**) na Chamwino (**20,059**).

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 jumla ya makazi **500,000** yalipangwa kurasimishwa katika Halmashauri **23;** kuanza kusimika vituo **22** vya upimaji na kuweka alama za msingi za upimaji **276**. Hadi tarehe 15 Mei 2024, vipande vya ardhi **62,200** vimerasimishwa katika Halmashauri za Jiji la Dodoma (**7,545),**

Wilaya ya Chalinze (**12,112*)***, Manispaa ya Kigoma (**6,171**), Mji wa Nzega (**11,796**), Manispaa ya Kahama (**10,860**) na Manispaa ya Shinyanga (**13,716**)**;** na Alama za Msingi za Upimaji **327** zimewekwa katika Halmashauri **26** sawa na asilimia **118** ya lengo. Aidha, zabuni kwa ajili ya urasimishaji makazi **400,000** imetangazwa Vilevile, Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa vituo **22** vya upimaji amepatikana na kazi ya ujenzi itaanza katika mwaka 2024/25. **101.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kuanza ujenzi wa majengo **25** ya Ofisi za Ardhi za Mikoa na kujenga kumbi za mihadhara nne (**4**) katika vyuo vya ardhi vya Tabora na Morogoro. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 washauri elekezi wa ujenzi wa majengo **25** ya Ofisi za Ardhi za Mikoa na kumbi nne (**4**) za mihadhara za Vyuo vya Tabora na Morogoro wamepatikana na wamekamilisha rasimu za ubunifu wa majengo. Washauri elekezi waliopatikana ni wataalam wa ndani. Hii ni katika kuendeleza azma ya Awamu ya Sita ya kuimarisha sekta binafsi nchini.

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwajengea uelewa wananchi kuhusu utekelezaji wa mradi katika ngazi za Mitaa, Kata na Wilaya katika maeneo ya mradi. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 wananchi **282,593** wamejengewa uelewa kuhusu sheria za ardhi na utekelezaji wa Mradi ambapo wanaume walikuwa **158,118** na wanawake **124,475**. Vilevile, katika kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro, Mradi umewezesha kumaliza mashauri **496** katika mabaraza matano (**5**) ya Bagamoyo, Musoma, Tarime, Tabora na Ifakara na hivyo kupunguza mlundikano wa kesi katika mabaraza hayo. Vilevile, mradi umeboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuwezesha ununuzi wa samani za ofisi, vitendeakazi na magari **18.** Aidha, taratibu za ununuzi wa magari mengine **52** zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika mwaka 2024/25. Hatua hii itapunguza changamoto ya usafiri iliyopo katika sekta ya Ardhi.



*Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Jerry William Silaa, akimkabidhi magari Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhandisi. Anthony Damian Sanga kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa LTIP.*

**103. *Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2024/25 kupitia Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP) ni: -

i). Kuhakiki na kupima mipaka ya vijiji na kutoa vyeti vya vijiji **1,000**;

ii). Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **1,000**;

iii). Kuandaa Mipangokina ya vijiji **100** na kuandaa Hati za Hakimiliki za Kimila **300,000**;

iv). Kurasimisha vipande vya ardhi **100,000** kupitia wataalam wa Serikali na vipande **400,000** kupitia kampuni zinazofanya kazi za urasimishaji;

v). Kubadilisha Nyaraka za ardhi (Data conversion) **1,921,758** kutoka analojia kwenda kidijitali;

vi). Kuwezesha upatikanaji wa miundombinu kwa ajili ya usambazaji wa mfumo wa ILMIS kwa Ofisi za Ardhi **67**;

vii). Kusanifu na kusimika Vituo vya Kieletroniki vya Upimaji (CORs) **22**;

viii). Kujenga mfumo wa kidigitali wa Vitalu vya Thamani ya Ardhi nchini;

ix). Kujenga Ofisi za Ardhi za Mikoa **25**;

x). Kujenga kumbi za mihadhara katika Vyuo vya Ardhi vya Tabora - ARITA (2) na Morogoro - ARIMO (**2**);

xi). Kuwezesha ubunifu na ujenzi wa Jengo la Taifa la Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi;

xii). Kukarabati Ofisi za ardhi katika Halmashauri **34**;

xiii). Kununua vifaa, kuhuisha mitaala na kuwezesha ukuzaji wa ujuzi wa watumishi wa Vyuo vya Ardhi Tabora na Morogoro;

xiv). Kuboresha utendaji kazi wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya **30**; na

xv). Kuandaa na kuboresha sera, sheria na miongozo mbalimbali.

**Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani (Land Data Infrastructure – LDI)**

**104.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani una thamani ya Dola za Kimarekani **milioni 65** na unalenga kuweka miundombinu ya upimaji na ramani ambayo itaongeza kasi ya upangaji, upimaji ardhi na uandaaji wa ramani kwa matumizi mbalimbali. Pamoja na shughuli nyingine, Mradi utawezesha ujenzi wa Vituo vya Kielektroniki vya Upimaji (CORs) **30**, ununuzi wa vifaa vya kisasa vya upimaji na uandaaji wa ramani ikiwemo ndege moja (**1**) yenye rubani na ndege **17** zisizo na rubani (drones) na vifaa vya kisasa vya

kielektroniki vya kuchakata ramani. Utaratibu wa kumpata mshauri mwelekezi wa mradi umekamilika na mkataba kati ya Wizara na Mshauri Mwelekezi uliwekwa saini tarehe 9 Mei, 2024. Kazi atakazofanya ni usanifu wa mradi, kuandaa viwango na miongozo ya upimaji na uandaaji wa ramani za kidigitali pamoja na kusimamia utekelezaji wa mradi kwa kushirikiana na wataalam wa ndani.

**105.** ***Mheshimiwa Spika***, katika hatua za awali za utekelezaji wa mradi wa LDI, Wizara imeanzisha Kituo cha Mafunzo na Ubunifu (TNGC) kitakachotumika kuwajengea uwezo watumishi katika matumizi ya teknolojia ya mifumo ya taarifa za kijiografia na kumbukumbu za ardhi. Aidha, Kituo hicho kitaongeza uwezo wa wataalamu wa ndani kutekeleza miradi ya ardhi na hivyo kuokoa matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kuajiri wataalam kutoka nje ya nchi. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 watalaam **10** wamepata mafunzo ya ukufunzi nchini Tanzania na Korea Kusini.




*Mtaalamu wa kurusha Ndege isiyo na Rubani akijiandaa kurusha ndege.*

**106.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/25, Wizara itaendelea na utekelezaji wa mradi kwa kukamilisha ununuzi wa vifaa na kuandaa ramani za msingi za uwiano wa **1:2,500** kwa miji mikuu ya mikoa na uwiano wa **1:25,000** kwa nchi nzima.

**Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa**

**107. *Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuimarisha mipaka ya kimataifa kwa kujenga na kuongeza alama, kuzipima, kukarabati zilizoharibika, kuandaa ramani za mipaka na kuandaa mikataba ya mipaka. Katika mwaka 2023/24, Wizara iliahidi kuimarisha sehemu ya mpaka wa kimataifa kati ya Tanzania na Kenya yenye urefu wa kilomita **80** pamoja na mpaka wa Tanzania na Burundi yenye urefu wa kilomita **100**. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, Wizara iliendelea na uimarishaji wa mpaka wa Tanzania na Kenya kwenye kipande cha kilomita **110** kutoka Namanga hadi Tarakea ambapo kazi hiyo imekamilika. Kazi ya uimarishaji wa sehemu ya mpaka wa Tanzania na Kenya yenye urefu wa kilomita **100** kutoka Tarakea mpaka Ziwa Jipe inaendelea na itakamilika katika mwaka 2024/25. Aidha, ramani **65** za sehemu ya mpaka wa Tanzania na Kenya kutoka Ziwa Viktoria (Rorya) hadi Tarakea (Rombo) yenye urefu wa kilomita **238** kati ya kilometa **458** zilizoimarishwa zimekamilika. Katika mwaka 2024/25, Wizara itakamilisha uimarishaji wa sehemu ya mpaka wa Tanzania na Burundi yenye urefu wa kilomita **100** pamoja na kuendelea na uandaaji wa ramani za mipaka ya kimataifa.




*Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Geophrey Pinda (wa nne kushoto) akiwa na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii wakikagua mpaka wa Tanzania na Kenya eneo la Namanga mkoani Arusha.*

**USHIRIKI WA WIZARA KATIKA MIRADI YA KIMKAKATI**
**Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta**

**108. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilifanya kazi ya upimaji wa mkuza wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) katika upande wa Tanzania wenye urefu wa Kilomita **1,146**. Mkuza uliopimwa unaanzia Mtukula (Kagera) hadi Chongoleani (Tanga). Ramani za mkuza huo unaopita katika mikoa nane (**8**) na Halmashauri **28** zimeandaliwa na kuidhinishwa. Aidha, Wizara imeshiriki katika kukamilisha utwaaji wa ardhi ya nyongeza ya hekta **12.75** iliyopo katika vijiji vya Mwighanji (Singida), Serya (Kondoa) na Kelema Mashariki (Chemba).

**109. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuhakikisha kunakuwepo na usalama wa milki kwenye njia ya Mradi, Wizara imekamilisha uandaaji na usajili wa Hatimiliki kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) katika Halmashauri **28** za mikoa nane **(8)** inayopitiwa na bomba hilo. Katika mwaka 2024/25, Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi zote za utekelezaji wa mradi huu na miradi mingine ya kimkakati kuhakikisha inakuwa na milki salama kwa kadri itakavyotakiwa.

**TAASISI NA BODI ZILIZO CHINI YA WIZARA**
**SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA (NHC)**

**110. *Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Nyumba la Taifa lina jukumu la kujenga nyumba za makazi na majengo mengine kwa ajili ya kuuza na kupangisha; kujenga majengo kulingana na mipango iliyoidhinishwa na Serikali; kuzalisha na kuwezesha uzalishaji wa vifaa vya ujenzi; kusimamia milki za majengo; kufanya ukarabati; kukusanya kodi ya pango; kutoa huduma ya ushauri elekezi, upangaji wa maeneo na ukandarasi wa majengo. Majukumu hayo yanatekelezwa kupitia Mpango Mkakati wa Shirika wa miaka 11 (2015/16 – 2025/26).

**Ujenzi wa Nyumba za Makazi na Majengo Mengine kwa ajili ya Kuuza na Kupangisha**

**(i) Mradi wa Kawe 711, Golden Premier Residence na Morocco Square**

**111.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka 2023/2024 Shirika lilipanga kukamilisha ujenzi wa miradi mikubwa ikiwemo mradi wa nyumba **422** wa Kawe 711 wenye thamani ya shilingi bilioni **169** na nyumba **196** wa *Golden Premier Residence* wenye thamani ya shilingi bilioni **71** iliyokuwa imesimama tangu mwaka 2018. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ujenzi wa Mradi wa Kawe 711 unaendelea na umefikia asilimia **35** na unatarajiwa kukamilika mwezi Aprili 2026. Aidha, mradi wa *Golden Premier Residence* (GPR) bado umesimama na majadiliano kati ya Shirika na mkandarasi yanaendelea.

**112.** ***Mheshimiwa Spika;*** Shirika limeendelea na uuzaji na upangishaji wa majengo katika Mradi uliokamilika wa Morocco Square, ambapo katika jengo lenye nyumba za makazi **100**, tayari nyumba **71** zimeshauzwa na mauzo ya nyumba zilizobakia yanaendelea. Aidha, upangishaji wa Hoteli yenye vyumba **81** umefanyika kwa asilimia **100**, Maduka (Retail Mall) asilimia **94** na ofisi asilimia **42**.



*Hotel ya King Jada ni moja ya majengo ya Mradi wa Morocco Square jijini Dar es salaam*

**(ii) Mradi wa *Samia Housing Scheme***

**113. *Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka 2023/24 Shirika lilipanga kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba **560** uliopo Kawe Jijini Dar es Salaam na nyumba **500** katika Jiji la Dodoma maeneo ya Njedengwa, Iyumbu na Medeli. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, ujenzi wa nyumba **560** awamu ya kwanza katika eneo la Kawe Jijini Dar es Salaam umefikia asilimia **60** na unatarajiwa kukamilika mwaka 2024/25.

**Ujenzi wa Majengo ya Biashara**

**114. *Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka 2023/24 Shirika lilipanga kuendelea na ujenzi wa majengo ya biashara katika Mikoa ya Kagera (Bukoba), Mwanza, Dodoma, Shinyanga (Kahama), Morogoro, Mtwara (Masasi) na Lindi. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 ujenzi wa majengo ya maduka **50** katika Mji wa Kahama umefikia asilimia **14** na ujenzi wa jengo la biashara katika mji wa Masasi umeanza. **Utekelezaji wa Sera ya Ubia ya Shirika**

**115. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Shirika lilipanga kutekeleza miradi **24** ya ubia yenye thamani ya shilingi bilioni **340** kupitia Sera yake ya Ubia ambapo hadi tarehe 15 Mei, 2024, Shirika limeidhinisha na kusaini mikataba ya miradi **21** yenye thamani ya shilingi bilioni **271**. Miradi hii itatekelezwa kwa muda wa miezi **24** ambapo utekelezaji umeanza Januari, 2024 katika Mikoa ya Dar es Salaam (**17**), Mwanza (**3**) na Iringa (**1**).

**116. *Mheshimiwa spika,*** kupitia miradi hii, Shirika linatarajia kupata manufaa mbalimbali ikiwemo kuongeza idadi ya nafasi za upangaji, mathalan katika eneo la Kariakoo nafasi za upangishaji zitaongezeka kutoka **324** hadi **2,691**. Hivyo, mapato, thamani ya mali za Shirika na faida ya uwekezaji kwa kuzingatia eneo (Return on Investments) itaongezeka.

**(iii) Ukarabati wa Nyumba za Shirika**

**117. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Shirika limekamilisha ukarabati wa majengo **181** ambayo yana nyumba **3,111** katika mikoa **23** ya Shirika. Aidha, jumla ya majengo **83**

ambayo yana nyumba **451** yaliyopo katika mikoa mbalimbali ya Shirika yanaendelea kufanyiwa ukarabati (**Jedwali Na. 17**).

**(iv) Ukusanyaji wa Mapato ya Shirika**

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2023/24, Shirika lilipanga kukusanya shilingi bilioni **274** kutokana na vyanzo mbalimbali ambavyo ni kodi ya pango shilingi bilioni **105**, ukandarasi shilingi bilioni **99 na** shilingi bilioni **70** kutokana na mauzo ya nyumba na viwanja. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, Shirika limekusanya jumla ya Shilingi bilioni **208.5** sawa na asilimia **76.1** ya lengo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **90.4** ni makusanyo ya kodi ya pango, makusanyo ya mauzo ya nyumba na viwanja ni shilingi bilioni **50.8** na shilingi bilioni **60.9** ni mapato yanayotokana na miradi ya ukandarasi pamoja na ushauri elekezi na shilingi bilioni **6.4** ni mapato mengineyo.

**(v) Ukusanyaji wa Madeni ya Shirika**

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, shirika limekusanya shilingi bilioni **7.2** ambapo kiasi cha shilingi bilioni **4.1** ni deni la pango la nyumba, shilingi bilioni **2.7** kutoka kwenye miradi ya ukandarasi na shilingi milioni **400** ni madeni mengineyo ikiwemo ya uuzaji wa nyumba. Madeni hayo yamepungua kutoka shilingi bilioni **25.7** Julai**,** 2023 hadi shilingi bilioni **18.5** Mei**,** 2024 sawa na asilimia **28**. Hata hivyo, Shirika bado linakabiliwa na changamoto ya wadaiwa sugu wa kodi ya pango; miradi ya ukandarasi na wanunuzi wa nyumba kutokukamilisha malipo yao kwa wakati. Hivyo, Shirika limeweka mikakati ifuatayo ili kukabiliana na changamoto hizo;

i). Kuingia mikataba na wapangaji ili kuwaruhusu kulipa madeni yao kwa awamu;

ii). Kuvunja mikataba ya upangaji kwa wapangaji waliokaidi kulipa madeni yao na kuwaondoa kwenye nyumba na kukamata mali zao kwa ajili ya kuuza ili kufidia madeni yao;

iii). Kuwatangaza wadaiwa sugu katika vyombo vya habari;

iv). Kuhakikisha kuwa, kila mpangaji mpya anayepangishwa analipa amana ya pango ya miezi mitatu (security deposit); na

v). Kuingia makubaliano na *Credit Information Reference Bureau* ili kusajili majina ya wadaiwa sugu na kuwanyima fursa ya kupata mikopo katika taasisi za fedha.;

vi). Kuingia mikataba na wapangaji ili kuwaruhusu kulipa madeni yao kwa awamu;

vii). Kuvunja mikataba ya upangaji kwa wapangaji waliokaidi kulipa madeni yao na kuwaondoa kwenye nyumba na kukamata mali zao kwa ajili ya kuuza ili kufidia madeni yao;

viii). Kuwatangaza wadaiwa sugu katika vyombo vya habari;

ix). Kuhakikisha kuwa, kila mpangaji mpya anayepangishwa analipa amana ya pango ya miezi mitatu (security deposit); na

x). Kuingia makubaliano na *Credit Information Reference Bureau* ili kusajili majina ya wadaiwa sugu na kuwanyima fursa ya kupata mikopo katika taasisi za fedha.

**Natoa wito kwa wapangaji kulipa ankara zao kwa wakati na wadaiwa wote kulipa madeni yao mapema kabla hatua zaidi hazijachukuliwa kwa ukiukaji wa mikataba.**

**(vi) Ujenzi wa Miradi ya Ukandarasi**

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2023/24 Shirika limendelea na utekelezaji wa miradi ya ukandarasi ikiwemo ujenzi wa Majengo ya Ofisi za Wizara nane (8) Jijini Dodoma, ujenzi wa Jengo la Shule ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Ujenzi wa majengo manne (4) ya Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA), Kituo cha biashara ya madini ya Tanzanite Mirerani, ujenzi wa Jengo la Kitengo cha Moyo cha Jakaya Kikwete (JKCI) ambapo hadi tarehe 15 Mei, 2024, utekelezaji wake ni kama ifutavyo:-

i). Ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara nane (**8**) yenye thamani ya shilingi bilioni **194** Katika Mji wa Serikali Mtumba umefikia wastani wa asilimia **81**;

ii). Ujenzi wa jengo la Shule ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wenye thamani ya shilingi bilioni **9.8** umefikia asilimia **75**;

iii). Ujenzi wa majengo manne (**4**) ya Wakala wa Ununuzi wa Serikali (GPSA) katika mikoa ya Simiyu, Songwe, Dodoma na Pwani yenye thamani ya shilingi bilioni **2.8** umekamilika kwa asilimia **100**;

iv). Ujenzi wa Kituo cha biashara ya madini ya Tanzanite wenye thamani ya shilingi bilioni **5.5** katika mji wa Mirerani Mkoa wa Manyara umefikia asilimia **85**; na

v). Ujenzi wa jengo la Kitengo cha Moyo cha Jakaya Kikwete (JKCI) wenye thamani ya shilingi bilioni **3.1** Jijini Dar Es Salaam umefika asilimia **99**.

**Mpango wa Utekelezaji wa Shughuli za Shirika kwa mwaka 2024/25**

**121. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, shirika limepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

(i) Kuendelea na ujenzi wa nyumba **422** katika mradi wa Kawe 711 ambapo unatarajiwa kufikia asilimia **75** ya utekelezaji ifikapo Juni, 2025. Lengo ni kukamilisha ujenzi ifikapo Aprili, 2026;

(ii) Kuendelea na ujenzi wa nyumba **196** katika mradi wa Golden Premier Residence (GPR) ifikapo Juni, 2025;

(iii) Kuanza ujenzi wa nyumba **560** za Mradi wa *Samia Housing Scheme* (SHS) awamu ya pili katika eneo la Kawe Jijini Dar es Salaam;

(iv) Kuendelea na ujenzi wa nyumba **150** za *Samia Housing Scheme* katika eneo la Medeli na Iyumbu Jijini Dodoma kwa ajili ya kuuzia wananchi;

(v) Kukamilisha ujenzi wa majengo ya biashara katika mkoa wa Shinyanga (Kahama) na kuanza ujenzi katika mji wa Masasi (Mtwara);

(vi) Kuanza ujenzi wa majengo ya biashara katika miji ya Moshi, Arusha, Tanga, Tabora, Lindi, Morogoro, Bukoba na Dar es Salaam;

(vii) Kuendelea na ujenzi na kusimamia miradi **21** ya ubia yenye thamani ya shilingi billioni **271** na kukaribisha wawekezaji wengine kutoka sekta binafsi ili kufanya uendelezaji wa majengo ya biashara na makazi kupitia sera ya ubia;

(viii) Kuendelea kukusanya mapato ikiwemo madeni ya kodi ya nyumba, miradi ya ukandarasi, uuzaji wa nyumba, viwanja na madeni mengineyo ambapo mikakati madhubuti imewekwa ili kukusanya madeni hayo;

(ix) Kuendelea kutekeleza mpango wa matengenezo kwa kukarabati majengo **250**;

(x) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya ukandarasi ikiwemo kukamilisha ujenzi wa jengo la Shule ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kituo cha biashara ya madini ya Tanzanite Mirerani na miradi mingine itakayojitokeza;

(xi) Kuendelea kutekeleza shughuli za utaalam elekezi/ushauri katika miradi mbalimbali nchini;

(xii) Kuendelea na ujenzi wa mradi wa jengo la Ofisi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) Jijini Dodoma na Zanzibar;

(xiii) Kukamilisha uandaaji wa Mpango Kabambe wa matumizi ya ardhi katika maeneo ya Mwashiwawala – Mbeya, Kwala – Pwani na kufanya mapitio ya mpango wa Kitovu cha Mji eneo la Kawe; na

(xiv) Kufanya utafiti kuhusu teknolojia sahihi katika ujenzi wa nyumba za gharama nafuu.

## TUME YA TAIFA YA MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia shughuli za Upangaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Aidha, Tume hii, ina jukumu la kuandaa, kuratibu, kuwezesha na kusimamia utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini, Kufanya Ufuatiliaji, Tathmini, Uzingativu wa Mipango pamoja na kufanya tafiti za Matumizi ya Ardhi zinazohusiana na ardhi. Utekelezaji wa majukumu hayo unazingatia Mpango Mkakati wa Tume (2021/22-2025/26).

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mipango ya matumizi ya ardhi huwezesha kutenga maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo maeneo ya malisho, kilimo, makazi, uwekezaji, miundombinu ya barabara, huduma za jamii, hifadhi za misitu na mapitio ya wanyamapori (shoroba). Upangaji huu huleta tija katika uzalishaji, kuimarisha usalama wa milki na kudhibiti migogoro baina ya watumiaji wa ardhi. Mipango hii huandaliwa katika ngazi ya Vijiji, Wilaya, Mkoa, Kanda na Taifa.

### Uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya na Vijiji

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia Tume ilipanga kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya tano **(5)** na Vijiji **210** katika Halmashauri mbalimbali nchini. Mipango hii huandaliwa kwa njia shirikishi na kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji na wadau. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, Wizara kupitia Tume imewezesha uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **339** katika wilaya **30** sawa na asilimia **161.4** ya lengo la mwaka ***(Jedwali Na.18)***. Ongezeko la vijiji vilivyoandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi linatokana na utekelezaji wa Mradi wa Uimarishaji Usalama wa Milki za Ardhi na mwitikio wa wadau wa ndani na nje ya nchi kuchangia uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi. Uandaaji wa Mipango hii umefanya kuwa na jumla ya Vijiji **4,126** vilivyoandaliwa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kati ya vijiji **12,318** vilivyopo nchini.



*Wananchi wa Kijiji cha Kibuye, kilichopo katika Kata ya Bukuba, Wilayani Buhigwe wakimsikiliza Bw. Emmanuel Mbula, mtaalamu kutoka Tume ya Matumizi ya Ardhi akitoa elimu juu ya Sheria za Usimamizi Rasilimali Ardhi ikiwa ni maandalizi ya upangaji matumizi ya ardhi ya Kijiji hicho*

**125. *Mheshimiwa Spika,*** Mipango ya Matumizi ya Ardhi iliyoandaliwa kwa mwaka 2023/24 imewezesha kupangwa maeneo ya matumizi ya ardhi katika Vijiji vya Halmashauri za Wilaya mbalimbali nchini. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 jumla ya hekta **1,287,534.46** zimepangwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo uwekezaji **(12,167.27)**, malisho **(91,611.28)**, hifadhi za misitu (**150,377.92)**, misitu ya uvunaji **(24,394.10)**, makazi (**107,426.30)** kilimo na makazi (**229,767.75)**, kilimo **(608,586.81)**, huduma za jamii **(15,494.13)**, miundombinu **(12,866.02)** na hifadhi za vyanzo vya maji **(34,842.88)**. Katika mwaka 2024/25, Wizara kupitia Tume itaendelea kuratibu na kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya Ardhi ya Vijiji **422** kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji na wadau wa kimkakati katika maeneo mbalimbali ya miradi ya kimkakati, migogoro, mpakani na yenye uzalishaji mkubwa wa mazao.

**126. *Mheshimiwa Spika,*** pamoja na uandaaji wa Mipango ya Vijiji, Wizara kupitia Tume ilipanga kuandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Wilaya moja katika mwaka fedha 2023/24. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 Tume imewezesha uandaaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Wilaya katika Halmashauri ya Bukombe

Mkoani Geita. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/25, Tume itaendelea kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya tano (**5**). ***Natoa wito kwa Halmashauri za Wilaya zote nchini kutoa kipaumbele katika kutenga fedha za uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ili kuongeza kasi ya uaandaji wa mipango ya matumizi ya ardhi.***

**Uandaaji wa Mipangokina ya Vijiji Katika Makazi na Mashamba**

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka **2023/24,** Tume ilipanga kuandaa mipango kina ya makazi na mashamba katika vijiji vitano (**5**) itakayowezesha utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila **5,200**. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, jumla ya mipangokina ya makazi na mashamba katika vijiji **66** imeandaliwa katika Halmashauri za Wilaya **19** na kufikisha jumla ya Vijiji **88** vilivyoandaliwa Mpangokina nchini. Aidha, mipango hii imewezesha uwekaji wa miundombinu ya huduma za jamii na utoaji wa Hati za Hakimilki za Kimila **18,125** katika Halmashauri za Wilaya **17**. Hati hizi zimewawezesha wananchi kuwa na milki salama na kuwawezesha asilimia **15** ya wananchi kuzitumia kama dhamana kupata mikopo kutoka Taasisi za Fedha.

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa Fedha 2024/25, Tume itaendelea kuwezesha uandaaji wa mipangokina **40** katika maeneo yanayotengwa kwa matumizi ya makazi, mashamba, misitu na hivyo kuwezesha utoaji wa Hati za Hakimilki za Kimila **8,200**. Hii itawawezesha wananchi kiuchumi na kuimarisha usalama wa milki.

**Uwezeshaji wa Mamlaka za Upangaji**

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24 Tume ilipanga kuzijengea uwezo timu shirikishi za upangaji **255** katika Mamlaka za Upangaji za Wilaya na Vijiji na kutoa elimu kwa umma. Elimu iliyopangwa kutolewa ilihusu Sheria za Ardhi, Miongozo na Taratibu za uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi, usuluhishi wa migogoro, uhifadhi wa mazingira, wanyamapori, vyanzo vya maji na uzingatiaji wa mipango na mabadiliko ya tabianchi.

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi tarehe 15 Mei, 2024, Wizara kupitia Tume imezijengea uwezo Mamlaka za upangaji za Vijiji **339** na Halmashauri za Wilaya **30** kuhusu uandaaji, usimamizi na utekelezaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Jumla ya wajumbe **16,090** wakiwemo wajumbe **241** wa Halmashauri za Wilaya **30**, Wajumbe **7,797** wa Halmashauri za Vijiji (VC) ikiwemo Wajumbe **2,712** wa Kamati za Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi za Vijiji (VLUM); Wajumbe **2,373** wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji (VLC); Wajumbe **594** wa Kamati ya Uhakiki wa Maslahi ya Ardhi (VLAC) na wajumbe **2,373** wa Kamati za Uhakiki wa Mipaka walijengewa uwezo katika Halmashauri mbalimbali nchini. Aidha, katika mwaka 2024/25 Tume itaendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Upangaji **420.**



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhandisi Antony Sanga (aliyesimama) akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Kigala, mkoa wa Njombe wakati wa zoezi la uandaji wa mpango wa matumizi ya ardhi ya Kijiji hicho.*

**Elimu kwa Umma**

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24 Tume ilipanga kurusha vipindi **30** vya elimu kwa umma kuhusu upangaji wa matumizi ya ardhi. Hadi tarehe 15 Mei 2024, vipindi **102** vimerushwa kupitia runinga, redio, tovuti na mitandao ya kijamii. Aidha, Tume iliendesha mikutano mbalimbali uwandani yenye lengo la uelimishaji Jamii kuhusu majukumu na kazi zinazotekelezwa na Tume. Katika mwaka 2024/25, Tume

itaendelea kuziwezesha Mamlaka za upangaji na kutoa elimu kwa umma kwa vipindi **40** kuhusu sheria za ardhi, miongozo na taratibu za upangaji, usimamizi na utekelezaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi nchini.

**Uhuishaji na uhakiki wa Mipaka ya Vijiji**

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Tume imewezesha uhuishaji na uhakiki wa mipaka ya kiutawala ya vijiji **194** katika Halmashauri za Wilaya **20**. Aidha, migogoro ya Ardhi ya vijiji **183** imetatuliwa katika Halmashauri za Wilaya **20** (***Jedwali Na.19***). Vilevile, Vyeti vya Ardhi ya Vijiji **46** vimeandaliwa na kutolewa kwa kushirikiana na wadau katika Halmashauri za Wilaya Saba **(7)** za Tunduru **(11)**, Makete **(1)**, Ruangwa **(1)**, Liwale **(5)**, Butiama **(23)**, Morogoro **(2)**, Mpimbwe **(3)**. Katika mwaka 2024/25, Tume itaendelea kuhakiki na kuhuisha mipaka ya vijiji wakati wa uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi, kushirikiana na Mamlaka za Upangaji kutoa vyeti vya ardhi vya vijiji na kuimarisha mipaka ya kiutawala ya vijiji.



*Wapima Ardhi wa Wizara wakishirikiana na wananchi katika zoezi la kupima mipaka ya vijiji katika halmashauri ya Ushetu Septemba, 2023.*

**Tafiti**

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume imeendelea kufanya tafiti mbalimbali zinazohusiana na Sekta ya Ardhi na upangaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Tafiti hizi husaidia kujenga uelewa kwa wadau na kuhuisha Sheria na Miongozo mbalimbali ndani ya

Sekta ya Ardhi. Katika mwaka 2023/24, Tume ilipanga kufanya tafiti mbili (**2**) zinazohusu matumizi ya Ardhi na Maendeleo ya Vijiji katika Halmashauri mbalimbali nchini.

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imekamilisha kufanya tafiti mbili zinazohusiana na matumizi ya Ardhi kuhusu changamoto na fursa za upangaji wa matumizi ya ardhi na matokeo yake katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Tafiti zilifanyika katika vijiji saba **(7)** vya Mgaraganza, Mkongoro, Mwamgongo katika Mkoa wa Kigoma; Vijiji vya Kizerui, Mbomole na Sakale katika Mkoa wa Tanga na Makuka katika Mkoa wa Iringa. Tafiti hizi zililenga katika kubaini masuala chanya au hasi yanayoweza kuathiri uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi na athari zinazoweza kujitokeza ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwa maeneo yenye umuhimu kwa uhifadhi nchini.

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** matokeo ya tafiti hizi yamebainisha kuwa kuandaliwa kwa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kumepunguza migogoro kati ya wakulima na wafugaji, shughuli za kibinadamu na uhifadhi katika maeneo. Mipango ya Matumizi ya Ardhi imesaidia kuhifadhi vyanzo vya maji na misitu na kusababisha kuboreshwa kwa hali ya uzalishaji wa mazao ya kilimo na upatikanaji wa maji katika maeneo yao. Vilevile, Mipango ya Matumizi ya Ardhi imesaidia kutengwa kwa maeneo ya misitu ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa kupungua kwa hali joto na kuongezeka kwa mvua na upatikanaji wa maji. Serikali itaendelea kuimarisha mbinu shirikishi za uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa uzingatiaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi nchini. Aidha, mikakati endelevu itaendelea kuwekwa ili kuwezesha wananchi kumilikishwa maeneo yao na kuendelea kupewa elimu inayolenga kutunza maeneo yao na kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa kuzingatia kanuni ndogo. Katika mwaka 2024/25, Wizara kupitia Tume itafanya tafiti mbili (**2**) zinazohusiana na upangaji na Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi.

**Uimarishaji wa Mfumo wa Taarifa na Utunzaji wa Kumbukumbu za Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imeendelea kuboresha na kusimamia

Mfumo wa Taarifa na Utunzaji wa Kumbukumbu za Mipango ya Matumizi ya Ardhi (NLUIS). Mfumo huu unawezesha kuandaa na kuhifadhi kumbukumbu za Mipango ya Matumizi ya Ardhi ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Aidha, katika mwaka 2024/25 Tume itaendelea kuboresha Mfumo wa Taarifa na Utunzaji wa Kumbukumbu za Mipango ya Matumizi ya Ardhi, kusambaza katika Halmashauri za Wilaya na kuwezesha utumiaji wa mfumo.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/24, Wizara kupitia Tume ilipanga kuhifadhi Mipango ya Matumizi ya Ardhi **810** katika Mfumo wa Taifa wa Utunzaji wa Taarifa na Kumbukumbu za Mipango ya Matumizi ya Ardhi pamoja na kuendelea kuboresha mfumo huu. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, jumla ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **534** imehifadhiwa hivyo kuwa na mipango iliyohifadhiwa kufikia **1,252** kati ya Mipango **3,283** iliyoandaliwa na Tume na wadau mbalimbali. Aidha, katika mwaka 2024/25, Wizara kupitia Tume itaendelea kuhifadhi taarifa za Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **850** na Wilaya **10** katika mfumo.

**Ufuatiliaji na Tathmini ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/24 Tume imeendelea kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya uzingatiaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **62** katika maeneo yaliyopitiwa na Miradi ya Kimkakati katika Halmashauri za Bahi, Chemba, Singida, Bunda, Makete, Sumbawanga, Igunga, Kibaha, Tarime, Chamwino, Ngorongoro, Kilombero, na Misungwi. Ufuatiliaji na Tathmini umebaini kuwa, Mipango ya Matumizi ya Ardhi inayoandaliwa haizingatiwi ipasavyo. Sababu ya kutokuzingatiwa ni pamoja na changamoto ya kimuundo kati ya Kamati za Halmashauri za vijiji hususan Kamati ndogo za huduma za jamii na Kamati ya Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi (VLUM). Hii inatokana na Mwongozo wa Ushirikishwaji wa Uaandaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi kuzuia wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji kuteuliwa kuwa wajumbe wa Kamati ya Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi ya Kijiji (VLUM) hali inayosababisha mgongano katika utekelezaji wa majukumu na hatimae kuacha ombwe katika usimamizi wa utekelezaji wa mipango ya Matumizi ya Ardhi.

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na changamoto hiyo, Wizara kupitia Tume imeanza kufanya marekebisho ya mwongozo wa uaandaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa masuala ya Ardhi ili kuwianisha majukumu ya Kamati ya Huduma za Jamii na VLUM.

**BODI ZA KITAALAM**

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia Bodi za Wataalam wa Sekta ya Ardhi. Bodi hizo ni Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji; Bodi ya Usajili wa Wathamini; na Baraza la Taifa la Wapima Ardhi. Majukumu ya Bodi hizi yanajumuisha kusajili wataalam wa sekta na kampuni za kitaalam, kusimamia weledi na maadili ya kitaaluma.

**Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji**

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wataalam **39** na kampuni **11** za Mipangomiji zimesajiliwa, hivyo kuwa na jumla ya Wataalam **499** na kampuni **101** zilizosajiliwa. Aidha, Wataalam wawili (**2**) wamefutiwa usajili na Bodi kwa ukiukwaji wa sheria na maadili katika utendaji kazi. Pia, Bodi inaendelea kufanya uchunguzi kuhusu tuhuma za ukiukaji wa maadili ya utendaji kazi dhidi ya wataalam saba (**7**) na Kampuni sita (**6**) za mipangomiji katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Lindi na Songwe.

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi imefanya ufuatiliaji wa utendaji kazi na uzingatiaji Sheria za Mipangomiji katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, Dar es Salaam, Mwanza, Shinyanga, Geita na Dodoma, na kufanya ukaguzi wa jumla ya michoro ya mipangomiji **935** pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam katika Ofisi za Ardhi za Mikoa hiyo.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imeandaa mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kusajili miradi inayofanywa na wataalam na kampuni za mipangomiji na wataalam wa mipangomiji. Mfumo huu utarahisisha upatikanaji wa taarifa zinazohusiana na miradi na wataalam wa mipangomiji na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Bodi itaendelea kusajili Wataalam na kampuni za mipangomiji zitakazokidhi vigezo ili kuimarisha utendaji kazi. Aidha, usimamizi na ufuatiliaji wa utendaji kazi na uzingatiaji wa sheria za mipangomiji utaendelea kufanyika ili kuimarisha ustawi wa sekta ya mipangomiji.

**Bodi ya Usajili wa Wathamini**

**145.** ***Mheshimiwa* spika,** hadi tarehe 15 Mei, 2024 jumla ya Wathamini **94** wamesajiliwa katika ngazi ya Usajili Kamili, Wathamini **84** katika ngazi ya Usajili wa Awali, Wathamini Wasaidizi **52** wameorodheshwa na Kampuni za Uthamini nane (**8**) zimesajiliwa. Idadi hii inafanya jumla ya Wathamini **389** wenye Usajili Kamili, Wathamini **775** wenye Usajili wa Awali, Kampuni za Uthamini **75** na Wathamini Wasaidizi **162**. Bodi pia inashughulika na masuala ya kinidhamu na kimaadili ambapo wathamini **28** na kampuni **16** zimetolewa taarifa kuhusu masuala ya kinidhamu na hatua kuanza kuchukuliwa. Hivyo, kufanya jumla ya Wathamini ambao wamechukuliwa hatua kufikia **41** na kampuni **36**; kati ya masuala haya ya kinidhamu, masuala yanayohusu wathamini **27** na kampuni **29** yamekamilishwa na kufungwa.

**146.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/25, Bodi imepanga kuendelea kusajili wathamini **150** katika ngazi zote, kutengeneza Mfumo wa TEHAMA kwa ajili ya usajili wa wathamini, kufanya mapitio ya mitaala ya mafunzo ya kujiandaa na mitihani ya Usajili Kamili, kufanya kaguzi za kitaalam, kuendesha mafunzo endelevu kwa wathamini na kufanya Mkutano Mkuu wa Mwaka. Aidha, Bodi imepanga kukusanya kiasi cha shilingi milioni **740.55** kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato ya ndani.

**Baraza la Taifa la Wapima Ardhi**

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Baraza lilipokea maombi **98** kwa ajili ya usajili wa wapima ardhi na maombi ya leseni za kampuni. Kati ya maombi yaliyowasilishwa, wapima ardhi **74** wamesajiliwa na kampuni **24** zilipewa leseni hivyo, kufanya jumla ya wapima ardhi waliosajiliwa nchini kuwa **793** na kampuni zenye leseni **119**. Katika mwaka 2024/25, Baraza litasajili wapima ardhi **80** na kutoa leseni kwa Kampuni **30**. Aidha, Baraza

litaendelea kuchukua hatua kwa wapima ardhi na kampuni zitakazokiuka taaluma ya maadili ya kazi za upimaji kwa kusitisha leseni ya upimaji.

**Vyuo vya Ardhi vya Morogoro na Tabora**

**148.** ***Mheshimiwa Spika***, Vyuo vya Ardhi Morogoro (ARIMO) na Tabora (ARITA) vimeendelea kutekeleza majukumu ikiwemo kufanya utafiti, kutoa mafunzo ya muda mrefu katika ya fani za mipangomiji, upimaji ardhi, urasimu ramani, ubunifu na uchapishaji, usimamizi wa ardhi, uthamini na usajili. Katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia vyuo hivyo iliahidi kudahili wanafunzi **2,000** (ARITA **1,500** na ARIMO **500**). Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa jumla ya wanafunzi **1,744** walidahiliwa ambapo Chuo Ardhi Tabora kilidahili wanafunzi **1,256** na Chuo cha Ardhi Morogoro kilidahili wanafunzi **488** katika mafunzo ya Astashahada na Stashahada. Aidha, wanafunzi **1,602** wamehitimu mafunzo yao. Aidha, Chuo cha Ardhi Morogoro kimeongeza miundombinu ya Madarasa kwa kujenga vyumba vitatu (**3**) vya mihadhara. Vilevile, Wizara iliahidi kukamilisha ujenzi wa Maktaba ya Chuo cha Ardhi Tabora ifikapo Juni, 2024. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, ujenzi wa Maktaba hiyo unaendelea na utakamilika kama ilivyopangwa.

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Wizara kupitia vyuo vyake inatarajia kudahili wanafunzi **2,670** (ARITA **1,580** na ARIMO **1,090**). Aidha, kutokana na ongezeko la mahitaji ya wataalam wa sekta ya ardhi, Chuo cha Ardhi Morogoro kitaongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi **489** hadi **1,090**. Vilevile, Wizara itakamilisha ujenzi wa vyumba viwili (2) vya madarasa ya Chuo cha Ardhi Morogoro.



*Naibu Waziri wa Ardhi Mhe. Geophrey Pinda (kushoto) akipata maelezo kutoka kwa mwanafunzi wa Chuo cha Ardhi Morogoro (ARIMO) wakati wa mahafali Novemba 2023*

**MASUALA MTAMBUKA**
**Utawala na Rasilimali Watu**

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** Utawala na Rasilimali Watu ni sehemu muhimu katika usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 Wizara ina jumla ya watumishi **2,395** kati ya hao wanaume **1,679** na wanawake **716**. Aidha, katika kipindi hicho Wizara ilipata kibali cha kuajiri Watumishi **98** wa fani za Upimaji wa Ardhi, Uthamini na Utawala wa Ardhi. Kwa kuzingatia muundo na majukumu ya Wizara, idadi halisi ya mahitaji ya watumishi ni **5,028** na hivyo kuwa na upungufu wa watumishi **2,633** ***(Jedwali Na.20).*** Katika kukabiliana na upungufu huo, Wizara imeendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kupatiwa watumishi kwa idadi inayokidhi mahitaji. Aidha, watumishi **347** wamepandishwa vyeo na watumishi **37** wamebadilishwa kada. Watumishi **1,166** watapandishwa vyeo katika mwaka 2024/2025.

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia nidhamu na uadilifu katika utoaji wa huduma za Sekta ya Ardhi nchini. Katika kusimamia nidhamu za watumishi, hatua mbalimbali kwa watumishi waliotuhumiwa kwa makosa mbalimbali zilichukuliwa

ambapo watumishi **22** wamesimamishwa kazi kupisha uchunguzi wa tuhuma za ukosefu wa maadili ya utendaji kazi katika Utumishi wa Umma; Watumishi saba (**7**) waliachishwa kazi na watumishi wawili (**2**) walipewa onyo na kuwekwa chini ya uangalizi.

**Kuwajengea Uwezo Watumishi**

**152. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwawezesha kushiriki katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa lengo la kuwaongezea utaalam, ujuzi na maadili ili kuhakikisha wanakuwa na weledi zaidi katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Katika mwaka 2023/24, Wizara iliahidi kuwawezesha watumishi **215** kupata mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa kuzingatia mahitaji na Mpango wa Mafunzo wa Wizara. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, Wizara imewezesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi **330.** Katika mwaka 2024/25, Wizara itaendelea kuwawezesha watumishi kushiriki mafunzo kwa kuzingatia Mpango wa Mafunzo wa Wizara.

**Habari na Elimu kwa Umma**

**153. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24, Wizara iliahidi kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali ya Sekta ya Ardhi. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, Wizara imetoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya sekta ya ardhi kupitia vipeperushi, majarida, mitandao ya kijamii, makala za magazeti, kliniki za ardhi, mikutano ya hadhara na vipindi vya redio na luninga. Aidha, Wizara ilifanya mkutano mmoja (**1)** na wahariri wa vyombo vya habari pamoja na mikutano **11** ya waandishi wa habari kuhusu masuala ya Sekta ya Ardhi. Vilevile, elimu kwa umma imetolewa kupitia tovuti ya Wizara (www.lands.go.tz) na maonesho mbalimbali. Pia, elimu kwa umma imeendelea kutolewa kupitia kipindi cha Televisheni cha '*Maisha ni Nyumba*' kinachoratibiwa na Shirika la Nyumba la Taifa.

**154. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma kwa njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, mikutano ya hadhara na maonesho mbalimbali.

**SHUKRANI**

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nawashukuru Mhe. Geophrey Mizengo Pinda (Mb), Naibu Waziri; Mhandisi Anthony Damian Sanga, Katibu Mkuu; na Bi. Lucy Dominico Kabyemera, Naibu Katibu Mkuu; kwa kunisaidia kutekeleza majukumu ya kusimamia sekta hii muhimu. Aidha, nawashukuru Bw. Nathaniel Mathew Nhonge, Kamishna wa Ardhi; Bw. Hamad Abdallah Hamad, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa; Prof. Wakuru Magigi Maseka, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; Bi. Evelyne Mugasha, Mthamini Mkuu wa Serikali; na Bi. Stella Tullo, Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Pia, nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti wa Bodi; na watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa kutekeleza majukumu yao kwa bidii na maarifa na hivyo kuleta ufanisi katika kufikia malengo ya Wizara.

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Washirika wa Maendeleo ambao Serikali imekuwa ikishirikiana nao katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo zinazohusiana na Sekta ya Ardhi. Washirika hao ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya EXIM ya Korea Kusini, UN-HABITAT, Shelter Afrique, African Union Boarder Program, Regional Centre for Mapping of Resources Development (RCMRD), Benki ya Maendeleo Afrika, Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Tanzania Mortgage Refinancing Company (TMRC), Watumishi Housing Company Limited, taasisi za fedha za ndani, Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi na wananchi kwa michango yao katika utekelezaji wa majukumu ya sekta ya ardhi.

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa shukrani kwa vyombo vya habari kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika kutoa elimu na hamasa kwa umma kuhusu masuala ya sekta ya ardhi. Kwa hakika wanahabari wameiwezesha Wizara kuwafikia wadau wengi zaidi kwa namna mbalimbali.

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kuishukuru familia yangu hususan mke wangu Bi Mariam Bakari Silaa na mwanangu Simba William Silaa kwa uvumilivu na kunitia moyo katika utekelezaji wa majukumu yangu.

## HITIMISHO

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara katika mwaka 2024/25, itaendelea kuimarisha uratibu na usimamizi wa maendeleo ya Sekta ya Ardhi kwa kuboresha huduma zinazotolewa. Ili kutekeleza azma hiyo, Wizara itazingatia vipaumbele vilivyoainishwa awali ambavyo ni:-

i). Kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi mijini na vijijini;

ii). Kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi;

iii). Kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika utunzaji wa kumbukumbu, utoaji wa huduma na upatikanaji wa taarifa za ardhi;

iv). Kuhakikisha uwepo wa nyumba bora, ukuaji wa sekta ya milki na maendeleo ya makazi kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii; na

v). Kuimarisha mipaka ya kimataifa.

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2024/25

**160.** ***Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha*** Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kama ifuatavyo: -

**Fungu 48: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

| Na | Maelezo | Aina | Makisio ya Bajeti |
|---|---|---|---|
| A | Mapato ya Serikali | | 250,000,000,000.00 |
| | **Makisio ya Matumizi ya mwaka 2024/25** | | |
| B | Matumizi ya Kawaida | Mishahara (PE) | 48,435,318,000 |
| | | Taasisi (PE) | 1,720,210,000 |
| | | **Jumla ya Mishahara** | **50,155,528,000** |
| | | Matumizi Mengineyo (OC) | 35,399,978,250 |
| | | Taasisi (OC) | 1,243,068,750 |
| | **Jumla ya Matumizi Mengineyo** | | **36,643,047,000** |
| | **(Jumla ya Matumizi ya Kawaida** | | **86,798,575,000** |
| C | Matumizi ya Maendeleo | Ndani | 10,601,757,000 |
| | | Nje | 60,054,753,000 |
| | **Jumla ya Miradi ya Maendeleo** | | **70,656,510,000** |
| | **Jumla Kuu** | | **157,455,085,000** |

Jumla ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Fungu **48** ni shilingi **157,455,085,000.00**.

**Fungu 03: Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.**

| AINA | AINA YA MATUMIZI | SHILINGI |
|---|---|---|
| **A** | **Mapato** | |
| | **Mapato ya Serikali** | **18,000,000** |
| **B** | Matumizi ya Kawaida; | |
| | Mishahara | 3,887,780,000 |
| | Matumizi Mengineyo | 3,244,318,000 |
| | **Jumla Ndogo** | **7,132,098,000** |
| **C** | **Matumizi ya Maendeleo** | |
| | Fedha za ndani | 5,041,232,000 |
| | **Jumla Ndogo** | **5,041,232,000** |
| **JUMLA KUU (B+C)** | | **12,173,330,000** |

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla kuu ya fedha zinazoombwa na Wizara (Fungu **48** na Fungu **03**) ili Bunge liweze kujadili na kuidhinisha ni shilingi **171,372,508,000.00**.

**162.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba imeambatana na majedwali yanayoainisha kwa ufasaha takwimu zinazohusiana na shughuli zilizotekelezwa na Wizara. Aidha, hotuba hii inapatikana pia kwenye tovuti ya Wizara ambayo ni ***www.lands.go.tz.***

***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Jerry William Silaa, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, makofi haya ni *credit* ya Watanzania kwa kazi kubwa na nzuri ambayo Wizara yako unayoiongoza inafanya kwa niaba ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa niaba yake ni Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti na Mwenyekiti wa Bunge Mheshimiwa Najma Murtaza Giga.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndiye muweza wa kila jambo na sasa naomba kwa sababu ya changamoto ya muda naomba Taarifa yote ya Kamati iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa na Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge yanayohusu Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu kama ifuatavyo: -

(i) Sehemu ya kwanza inatoa msingi wa uchambuzi na mawanda ya uchambuzi;

(ii) Sehemu ya pili inayohusu uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(iii) Sehemu ya tatu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2024/2025;

(iv) Sehemu ya nne inahusu maoni na ushauri; na mwisho ni

(v) Hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa majukumu na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya hii umejengwa katika Masharti ya Kanuni za Bunge Kifungu cha 6(8)(a)(b) kikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 7(1)(a) na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge Toleo la Februari, 2023, kinaitambua Kamati hii kuwa na wajibu wa kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi uliofanyika uligusa maeneo yafuatayo: -

(i) Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(ii) Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na

(iii) Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yaliyochambuliwa yalijitokeza katika randama ya Mpango na Bajeti ya Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na randama ya Mpango na Bajeti ya Fungu 03 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa bajeti na uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Maelezo ya jumla, ili kukidhi masharti hayo tarehe 21 Machi, 2024, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2024/2025. Taarifa hiyo ilijumuisha majukumu na Mpango na Bajeti ya Wizara yenyewe - Fungu 48 pamoja na Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi - Fungu 03.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hatua hiyo, Kamati inatoa taarifa kuhusu mambo yafuatayo: -

(i) Uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati;

(ii) Ukaguzi wa miradi;

(iii) Utekelezaji wa vipaumbele;

(iv) Hali ya ukusanyaji wa maduhuli; na

(v) Hali ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzingatiaji wa ushauri wa Kamati, wakati wa Bunge lilipojadili Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 tarehe 23 Mei, 2023, Kamati ilitoa ushauri katika mambo 10 kwa Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na kwa maeneo mahsusi matatu kwa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03). Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, sehemu kubwa ya ushauri imezingatiwa na sehemu nyingine inaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa ushauri uliozingatiwa unahusu kuongeza bajeti ya miradi ya maendeleo chini ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Maelezo ya Waziri yalionesha kuwa bajeti ya miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imeongezeka kwa 48% ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa ushauri ambao unaendelea kufanyiwa kazi ni kuhusu taasisi, mashirika ya umma na wananchi kutokulipa Kodi ya Pango la Ardhi hivyo kuathiri kwa kiwango kikubwa makusanyo katika sekta hiyo. Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa hadi Februari, 2024, Serikali ilikuwa imekusanya 23.4% tu ya madai halisi ya kodi hiyo. Kiasi hicho ni kidogo ukilinganisha na muda wa utekelezaji wa bajeti ambapo kwa makadirio Serikali ilitakiwa kuwa imekusanya 67%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha. Katika utekelezaji wa masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, tarehe 11 hadi tarehe 19 Machi, 2024, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa miradi mitatu inayotekelezwa katika mikoa mitatu ambayo ni Lindi, Pwani na Dar es Salaam. Miradi hiyo ni sehemu ya miradi iliyotengewa fedha kiasi cha shilingi 220,559,270,000 kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Naomba kubainisha ufafanuzi kuhusu miradi hiyo pamoja na kufanya majumuisho ya mambo yaliyojitokeza katika ukaguzi wa miradi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi wa miradi; Mradi Namba 4951 -Upangaji wa Matumizi ya Ardhi. Mradi huu unatekelezwa na Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi,

kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Eneo la utekelezaji wa mradi linagusa Vijiji 219 vya halmashauri za wilaya 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Wizara ilionesha kuwa katika Wilaya ya Ruangwa, utekelezaji wa mradi ulijumuisha kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi katika vijiji 16, kikiwemo Kijiji cha Namkatila ambacho Kamati ilipata nafasi ya kutembelea katika ukaguzi wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla utekelezaji wa mradi unaendelea vizuri na unafanyika kwa kuwashirikisha wananchi na viongozi wa vijiji, hali ambayo inaongeza uelewa wa kutosha miongoni mwa wananchi kuhusu mipango ya matumizi ya Ardhi. Jambo hilo linastahili kupongezwa na liendelee kuwa mfano wa kuigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Na. 2326 - Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK) katika Halmashauri ya Chalinze. Mradi huu unatekelezwa kwa kiasi cha shilingi 2,500,000,000 ikiwa ni mkopo usio na riba kutoka Wizara ya Ardhi kwenye Halmashauri ya Chalinze Mkoa wa Pwani ambapo Kamati ilitembelea maeneo ya Msolwa na Chamakweza ambapo mradi huu umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauriya ya Wilaya ya Chalinze inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 4,500,000,000 hivyo kupata faida ya shilingi 2,000,000,000. Hata hivyo, hali ya urejeshwaji wa fedha hizo kutoka kwenye halmashauri hiyo ni wa kusuasua ikiwa imerejesha 15% tu ya fedha iliyokopeshwa na Wizara. Katika ukaguzi wa Mradi huo Kamati iliitaka Halmashauri hiyo kuanza kurejesha haraka kiasi inachodaiwa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Na. 4953 - Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi *(LTIP)*, Kamati ilielezwa kuwa ili kufikia lengo, mradi umejielekeza katika kuboresha utawala na usimamizi wa ardhi nchini na usalama wa milki za ardhi nchini kwa wanawake na wanaume. Kwa mfano, katika Mkoa wa Dar es Salaam mradi unatekelezwa kwa kusogeza huduma jirani na wananchi kupitia vituo vya kutolea huduma za ardhi katika eneo moja maarufu kama Ardhi Kliniki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea Eneo la Bunju tarehe 17 Machi, 2024 na kujionea uendeshaji wa kliniki hiyo. Pia, Kamati ilishuhudia urasimishaji wa ardhi katika maeneo manne; utoaji wa hati 16 za ardhi kwa wananchi; na kusikiliza migogoro ya ardhi tisa. Aidha, hati miliki za ardhi 67 zilitolewa kupitia kampuni binafsi za upimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yatokanayo na ukaguzi wa miradi; kutokana na taarifa za utekelezaji wa miradi iliyokaguliwa pamoja na hali halisi ilivyobainika wakati wa ziara, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

(i) Utekelezaji wa sehemu kubwa ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati umefikia hatua nzuri hali inayoonesha kuwa miradi hiyo itakamilika kwa wakati. Hata hivyo, mradi wa *LTIP* bado unasuasua hali inayoweza kupelekea kuchelewa kupatikana tija iliyokusudiwa; na

(ii) Wakati wa utekelezaji wa miradi, Wizara na Tume walizingatia ushirikishwaji wa wadau na wananchi ambao ni wanufaika wa miradi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48), ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 300,000,000,000. Hadi kufikia Februari, 2024, Wizara ilikuwa imekusanya shilingi 101,848,128,229.56 sawa na 34% ya lengo la makadirio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, uchambuzi umebaini kwamba hali ya makusanyo hafifu imetokana na uamuzi wa Serikali kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023 *(Finance Act, 2023)* kutaka Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kukusanya Kodi ya Pango la Ardhi *(Land Rent)*. Jambo hilo limeathiri kiasi cha jumla ya makusanyo ya Kodi ya Pango la Ardhi ambacho ndiyo chanzo kikuu cha makusanyo katika Fungu hili. Hali hiyo imetokana na mamlaka hizo (halmashauri) kushindwa kukusanya kodi hiyo kwa sababu mbalimbali ikiwemo ya kukosa nguvu ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03), ilikadiriwa kukusanya

shilingi 718,000,000. Hadi kufikia Februari, 2024, Tume ilivuka malengo kwa kukusanya shilingi 1,698,678,150 sawa na 265.9% ya lengo. Ziada kubwa inaonesha kuwa upangaji wa makadirio ya makusanyo ndani ya Tume hauzingatii uwezo wa vyanzo vya mapato yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina (Fungu 48) Wizara ya Ardhi. uchambuzi wa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa Fungu 48 hadi kufikia mwezi Februari, 2024, umeonesha mambo yafuatayo: -

(i) Fedha za matumizi ya kawaida zilipatikana kwa 44.6% ikiwa ni pungufu ya fedha zilizotakiwa kupatikana katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti ambacho ni 66.6%;

(ii) Katika kiasi hicho cha fedha za kawaida, fedha za uendeshaji *(OC)* zilikuwa 45% ya fedha zote, huku mishahara ikiwa imepatikana kwa 64%;

(iii) Fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo zilipatikana kwa 80% ya bajeti; na

(iv) Katika fedha za kugharamia miradi ya maendeleo, fedha za ndani zilifikia 95% na fedha za nje zilikuwa 47%. Hata hivyo, katika kiasi hicho cha fedha za ndani, 77% ilikuwa ni fedha ya kulipia madeni mbalimbali ya Wizara. Taswira halisi ya mwenendo wa fedha inaonekana kwenye Jedwali Na. 2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 03 - Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; kwa upande wa Fungu 03 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, uchambuzi wa mwenendo wa upatikanaji wa fedha hadi kufikia Februari, 2024 ulionesha mambo yafuatayo: -

(i) Tume ilipokea 67% ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge ikiwa inaendana na uwiano katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti ambacho ni 66.6%;

(ii) Fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa zilikuwa 58.7% ya bajeti yote;

(iii) Katika kiasi hicho cha fedha za matumizi ya kawaida, fedha za matumizi mengineyo *(OC)* zilipokelewa kwa 52.63%, huku mishahara ikiwa imepokelewa kwa 80.69%;

(iv) Fedha za miradi ya maendeleo zilipokelewa kwa 66% huku fedha zote zikiwa fedha za ndani. Taswira halisi ya mwenendo wa fedha inaonekana katika Jedwali Na. 03.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ni uchambuzi wa mpango wa makadirio na mapato ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Katika mwaka wa fedha 20224/2025 Fungu 48 (Wizara) imekadiriwa kukusanya maduhuli ya shilingi 250,000,000,000. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makadirio hayo yamepungua kwa shilingi 50,000,000,000 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi zaidi umebaini kuwa pamoja na kupungua kwa lengo la makusanyo kwa upande wa Fungu 48, uwezekano wa lengo hilo kufikiwa ni mdogo. Hali hii inatokana na ukweli kuwa, katika kipindi cha miaka miwili mfululizo, ukusanyaji wa maduhuli katika Wizara hii haukufikia 50% ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi - Fungu 03 inakadiria kukusanya jumla ya shilingi 1,018,000,000. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makadirio haya yameongezeka kwa shilingi 300,000,000 sawa na 41.8% ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu – 48) inaomba jumla ya shilingi 157,455,085,000 ili kuimarisha sekta ya ardhi na nyumba nchini na kukuza mchango wake katika maendeleo ya Taifa, uchumi wa nchi na ustawi wa wananchi. Uchambuzi na matokeo ya matumizi ya fedha hizo unaonesha yafuatayo: -

(i) Jumla ya bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imeshuka kwa 3.5% ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2023/2024;

(ii) Bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na imeongezeka kwa shilingi 5,755,340,000 sawa na 7.1% ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2023/2024; na

(iii) Bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imeshuka kwa kiasi cha shilingi 11,470,135,000 sawa na 14% ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2023/2024. Taswira ya makadirio ya matumizi kwa Fungu 48 la Wizara inaonekana katika Jedwali Na. 5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu - 03) Serikali inaomba jumla ya shilingi 12,173,330,000 ili kuendelea kupanga matumizi ya ardhi katika vijiji na miji yetu kwa maendeleo ya Taifa, uchumi wa nchi na ustawi wa wananchi. Uchambuzi na matokeo ya matumizi ya fedha hizo unaonesha yafuatayo: -

(i) Jumla ya bajeti ya Fungu hili kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imeongezeka kwa 48.1% ikilinganishwa na ya mwaka 2023/2024;

(ii) Bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa kiasi cha shilingi 2,339,470,000.00 sawa na 48.9% ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2023/2024; na

(iii) Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa kiasi cha shilingi 1,631,232,000 sawa na 47.8% ikilinganishwa mwaka wa fedha 2023/2024. Taswira ya makadirio ya matumizi kwa Fungu 03 Wizara inaonekana katika Jedwali Na. 5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo muhimu yanayogusa sekta ya ardhi; wakati wa kujadili mpango wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025, mambo kadhaa yanayogusa sekta ya ardhi yalijadiliwa kama ifuatavyo: -

(i) Mradi wa Kuboresha Usalama wa Miliki za Ardhi *(Mradi wa LTIP)* unatekelezwa kutokana na mkataba kati Serikali na Benki

ya Dunia, mradi wa kiasi cha bilioni 346 na unatekelezwa kupitia vipengele vinne, ambavyo ni kuongeza usalama wa milki za ardhi kwa kutoa hatimiliki 1,000,000 maeneo ya mijini kwa njia ya urasimishaji na hatimiliki za Kimila 500,000 vijijini, kuimarisha mifumo ya taarifa za ardhi, kujenga miundombinu ya ardhi na usimamizi wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, kasi ya utekelezaji wa mradi huu ukilinganisha na shughuli za muda uliopangwa katika kutekeleza mradi huu hairidhishi.

(ii) Shirika la nyumba la Taifa *(National Housing Cooperation)* katika kutekeleza majukumu yake, shirika kwa sasa linatekeleza miradi kadhaa ya ujenzi wa nyumba ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Baadhi ya miradi hiyo ni Mradi wa Samia *Housing Scheme,* Mradi wa Kawe 711 *(Seven – eleven)* na Mradi wa *Golden Premium Residence*. Aidha, Shirika limeanza kutekeleza miradi mbalimbali ya ubia kupita sera ya ubia ya shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeza majukumu yake, shirika linadai madeni toka kwa wateja wake ambao ni watu binafsi pamoja na taasisi za umma na taasisi binafsi.

(iii) Maboresho ya Mfumo wa Usimamizi wa Ardhi nchini. Mfumo wa Usimamizi wa Ardhi nchini unaonesha kuwa uboreshaji huo wa mfumo utawapa wananchi uwezo wa kutoa taarifa endapo watacheleweshewa huduma. Mfumo utaondoa changamoto ya upotevu wa nyaraka zinazowasilishwa na wananchi kuomba huduma, kwani zitakuwa zinawasilishwa kupitia mfumo wa *online* na mfumo utaongeza uoni *(visibility)* kwa viongozi wa ngazi mbalimbali za Wizara na kuona utendaji wa majukumu unavyoendelea katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo huu unakusudia kuanzisha Ardhi Kiganjani *App*, itakayomwezesha mwananchi anayeomba huduma husika kulipiwa na atapata namba ya malipo *(Control Number)* kwenye *dashboard* au simu yake ya kiganjani bila kuhitaji kwenda ofisini. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha

inatenga fedha za kutosha ili mfumo huu uweze kuanza kazi nchi nzima.

(iv) Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi kwa kuzikopesha taasisi na Halmashauri mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijulishwa kuwa kumekuwa na kusuasua katika kurejesha fedha za mikopo kwa Halmashauri nyingi na Kamati inaitaka Serikali kufuatilia marejesho ya mikopo ili kuhakikisha proramu hii inakuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Halmashauri 44 zimerejesha sehemu ya fedha, huku Halmashauri za Manispaa ya Shinyanga na Musoma *DC* zikiwa hazijarejesha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Wizara kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuhakikisha wanazibana Halmashauri zilizobaki ziweze kurejesha fedha zote ili ziende zikasaidie kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika maeneo mengine ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto katika kulipa fidia ya ardhi kwenye maeneo yanayotwaliwa kwa ajili ya miradi ya Serikali na uwekezaji, kumekuwa na ucheleweshaji fidia wakati ambapo Serikali au taasisi zake zinapotaka kutwaa maeneo ya wananchi kwa manufaa ya umma au kupangiwa matumizi mengine tofauti na yale yaliyopo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya ucheleweshaji wa kulipa fidia hizo inachangia katika kuzalisha migogoro kati ya wananchi na Serikali au mwekezaji, kulipa riba kutokana na kuchelewesha kulipia fidia, mrundikano wa kesi za ardhi katika mabaraza ya ardhi na mahakamani na kuwafanya wananchi kuwa maskini kinyume na kusudio la Serikali la kuhakikisha ustawi katika maisha ya wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naenda kwenye maoni na ushauri. Kamati inaipongeza Serikali, kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa ufanisi mkubwa wa

utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2023/2024. Kipekee kabisa Kamati inapongeza Wizara kwa kusimamia vyema shughuli zote za Sekta za Ardhi hapa nchini. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuifanya sekta ya ardhi kuwa moja ya vipaumbele vikubwa katika mipango yake ya maendeleo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, Kamati ina maoni na ushauri kwenye baadhi ya masuala yanayopaswa kuzingatiwa na Wizara kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la ukusanyaji wa maduhuli, Kamati ina maoni kuwa ukusanyaji mdogo wa mapato yatokanayo na kodi ya pango la ardhi *(Land Rent)*, unatokana na Sheria ya Fedha *(Finance Act)* ya Mwaka 2023 ambayo ilizitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya wakati Halmashauri hizo hazina kanzidata, watumishi na hata nyenzo za kisheria za ukusanyaji. Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri kuwa Serikali ipitie upya uamuzi huo na kuleta Bungeni mapendekezo ya kurekebisha hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni urejeshwaji wa Fedha za Mradi wa Kupima, Kupanga na Kumilikisha Ardhi. Kamati imebaini kuwepo kwa ucheleweshaji wa baadhi ya Halmashauri kurejesha fedha ilizokopeshwa ili kutekeleza mradi wa Kupima, Kupanga na Kumilikisha Ardhi. Hivyo basi, Kamati inashauri kuwa Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ishirikiane na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuhimiza Wakurugenzi wa Halmashauri ambao hawajarejesha fedha hizo kurejesha ili Halmashauri nyingine ambazo hazijakopa zikopeshwe kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa mradi na kuleta tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba la Taifa linakabiliwa na changamoto ya baadhi ya wateja wake ambao ni taasisi za Serikali kushindwa kulipa kodi ya pango kiasi cha 2,148,864,361.35. Kamati inaishauri Serikali kuzisimamia taasisi hizo zinazodaiwa na Shirika hilo kwa kuhakikisha zinatenga bajeti ya kulipa deni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto ya upungufu wa watumishi katika Sekta ya Ardhi Nchini. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ina upungufu wa watumishi wakiwemo wakaguzi wa majengo *(building inspectors)*, hali inayochangia ujenzi usiofuata matumizi bora ya ardhi. Kamati inashauri kuwa Serikali iongeze watumishi katika sekta ya ardhi ili kusaidia kudhibiti ujenzi holela na kusimamia matumizi bora ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni changamoto ya upangaji wa matumizi bora ya ardhi. Kumekuwepo na migogoro mingi ya ardhi nchini inayotokana na Serikali kushindwa kupima na kupanga matumizi bora ya ardhi kwa maeneo mengi nchini. Kamati inashauri kwamba Serikali iendelee kutoa fedha kwa Tume ya Taifa ya Mipango na Matumizi Bora ya Ardhi kwa ajili ya kupima na kupanga, hali itakayosaidia kuondoa migogoro na kudhibiti ukuaji wa miji kiholela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni ucheleweshaji wa fidia ya ardhi katika maeneo yaliyofanyiwa uthamini. Kumekuwepo na changamoto ya Serikali kuchelewa kulipa fidia inapotaka kutwaa ardhi kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo, hali inayochangia migogoro kati ya wananchi na Serikali. Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kuwa kunakuwa na uthibitisho wa uwepo wa fedha za kulipa fidia ambao utatolewa na Wizara, taasisi mtwaaji au mwekezaji anayekusudia kutwaa ardhi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali ihakikishe kuwa inashirikiana na wadau wote muhimu wa utwaaji na inafanya uhakiki kabla ya Mthamini Mkuu kuidhinisha majedwali ya fidia na kabla ya hatua au zoezi la uoneshaji majedwali hayo kwa wananchi kufanyika. Hii itasaidia kurekebisha dosari zote ndani ya muda sahihi na kuhakikisha wananchi wanalipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni changamoto ya ujenzi wa makazi katika maeneo hatarishi. Kumekuwepo na ujenzi wa makazi katika maeneo oevu *(wetlands),* maeneo ya mabonde, maeneo ya karibu na hifadhi za Taifa na shoroba za wanyama. Hali hii inahatarisha maisha ya wananchi katika

maeneo hayo. Kamati inaishauri Serikali iandae mipango ya matumizi ya ardhi inayoendana na hali halisi ya maeneo husika ili kuwaepusha wananchi na athari hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na kasi ndogo ya utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi - *LTIP,* hali inayoweza kuathiri tija ya malengo ya mradi kufikiwa kama ilivyokusudiwa. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi katika usimamizi na utekelezaji wa mradi huo. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kliniki za ardhi zinakuwa endelevu hata baada ya mradi huu ili kutatua changamoto za migogoro ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nahitimisha kwa kusema kwamba, Kamati inapenda kumpongeza Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, ukiwemo wewe mwenyewe kwa namna ambavyo tunatekeleza majukumu yetu katika kulisimamia na kuliwezesha Bunge letu kutekeleza wajibu wake wa kusimamia na kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati napenda kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Jerry William Silaa, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pia Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, Naibu Waziri wa Wizara hii kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawashukuru watendaji wote wa Wizara chini ya Katibu Mkuu, Mhandisi Anthony Sanga, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Lucy Kabyemela, kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake na usimamizi mzuri wa majukumu ya Wizara kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nawapongeza na kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kazi kubwa iliyofanyika chini ya Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava hadi taarifa hii inaingia Bungeni. Majina ya Wajumbe hao yameorodheshwa katika taarifa hii, ila kwa sababu ya muda, naomba yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naomba nimalize kwa kuwashukuru Watumishi wote wa Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na Mtoa hoja hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII, KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 (Kanuni za Bunge), naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge yanayohusu taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya kwanza inayotoa, Msingi wa Uchambuzi na Mawanda ya Uchambuzi;

(ii) Sehemu ya pili inayohusu Uchambuzi na tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; na

(iii) Sehemu ya tatu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2024/2025;

(iv) Sehemu ya nne inayohusu Maoni, Ushauri; na

(v) Hitimisho.

## 1.2 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa taarifa ya utekelezai wa Majukumu na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya hii umejengwa katika Masharti ya Kanuni za Bunge. Kifungu cha 6(8)(a)(b) kikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge Toleo la Februari,2023, kinaitambua Kamati hii kuwa na wajibu wa kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yaliyotaka Taarifa za Utekelezaji Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi masharti hayo, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara hii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na kuja na matokeo kama yalivyoainishwa katika taarifa hii.

## 1.3 Mawanda ya Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi uliofanyika uligusa maeneo yafuatayo:-

i. Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

ii. Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

iii. Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

**Mheshimiwa Spika,** mambo yaliyochambuliwa yalijitokeza katika randama ya Mpango na Bajeti ya **Fungu 48** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na randama ya Mpango na Bajeti ya **Fungu 03** Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Wakati wa uchambuzi, Kamati iliongozwa na kigezo cha asilimia na uwiano. Aidha, njia iliyotumika ni tathmini ya jumla na ulinganisho wa mambo mbalimbali. Mambo hayo yaliiwezesha Kamati kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji na mantiki ya mpango na makadirio kwa mwaka wa fedha unaokuja.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii ya taarifa inaripoti matokeo ya utekelezaji wa masharti ya Kanani ya 117(2) ya Kanuni za Bunge. Kanuni hiyo ilizitaka Kamati za Bunge za Kisekta kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoisha na kufanya ulinganisho wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi masharti hayo tarehe 21 Machi, 2024, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2024/2025. Taarifa hiyo ilijumuisha majukumu na Mpango na Bajeti ya Wizara yenyewe **Fungu 48** pamoja na Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi **Fungu 03**.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya hatua hiyo, Kamati inatoa taarifa kuhusu mambo yafuatayo:-

(i) Uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati;
(ii) Ukaguzi wa Miradi;
(iii) Utekelezaji wa Vipaumbele;
(iv) Hali ya ukusanyaji wa maduhuli;
(v) Hali ya upatikanaji wa fedha;

**2.1.1 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa Bunge lilipojadili Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa fedha 2023/2024 tarehe 23 Mei, 2023, Kamati ilitoa ushauri katika mambo kumi (10) kwa **Fungu 48** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na kwa maeneo mahsusi matatu (3) kwa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi **(Fungu 03).** Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, sehemu kubwa ya Ushauri imezingatiwa na sehemu nyingine inaendelea kufanyiwa kazi.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano wa ushauri uliozingatiwa unahusu kuongeza bajeti ya miradi ya Maendeleo chini ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Maelezo ya Waziri yalionesha kuwa bajeti ya miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imeongezeka kwa **asilimia 48** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa ushauri ambao unaendelea kufanyiwa kazi ni kuhusu Taasisi, Mashirika ya Umma na Wananchi kutokulipa kodi ya Pango la Ardhi hivyo kuathiri kwa kiwango kikubwa makusanyo katika sekta hiyo. Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa hadi Feburari, 2024, Serikali ilikuwa imekusanya **asilimia 23.4** ya madai halisi ya kodi hiyo. Kiasi hicho ni kidogo ukilinganisha na muda wa utekelezaji wa bajeti ambapo kwa makadirio Serikali ilitakiwa kuwa imekusanya **asilimia 67.**

**Mheshimiwa Spika,** Jambo muhimu la kusisitiza kutokana na taarifa hiyo ni kuwa, ushauri unaotolewa Bungeni unalenga kuboresha shughuli za umma kwa sekta inayohusika. Ni maoni ya

Kamati kuwa, Serikali inapozingatia ushauri wa Kamati inatimiza azma ya kufanikisha ustawi wa wananchi ambao ndio lengo kuu la Serikali. Kuchelewa kuzingatia ushauri kunaweza kuathiri ustawi wa wananchi na kuwa kinyume na matarajio ya wananchi kwa Serikali yao.

**2.1.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha**

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya miradi ya maendeleo hupitishwa na Bunge kwa lengo la kuimarisha sekta inayohusika ili itoe mchango mkubwa zaidi katika uchumi, maendeleo, ustawi na kuboresha maisha ya wananchi. Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi linahitaji kujiridhisha na hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayoidhinishiwa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, tarehe 11 hadi tarehe 19 Machi, 2024, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa miradi mitatu (03) inayotekelezwa katika mikoa mitatu ambayo ni Lindi,Pwani na Dar es Salaam. Miradi hiyo ni sehemu ya miradi iliyotengewa fedha kiasi cha **shilingi 220,559,270,000** kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Naomba kubainisha ufafanuzi kuhusu miradi hiyo pamoja na kufanya majumuisho ya mambo yaliyojitokeza katika ukaguzi wa miradi kama ifuatavyo:-

**A) Ufafanuzi wa Miradi**

(a) Mradi Namba 4951: Upangaji wa Matumizi ya Ardhi

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatekelezwa na Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Eneo la utekelezaji wa mradi linagusa Vijiji 219 vya Halmashauri za Wilaya 14 ikiwemo Halmashauri ya Wilaya Ruangwa, (16); Tunduma (20); Kilindi (1); Ludewa (16); Makete (04); Singida (20); Ushetu (20); Shinyanga (12); Igunga (20); Bunda (16); Rorya (20); Magu (18); Buchosa (24); na Sumbawanga (12).

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Wizara ilionesha kuwa, katika Wilaya ya Ruangwa, utekelezaji wa mradi ulijumuisha kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi katika vijiji 16. Vijiji hivyo ni

Chikwale, Chiundu, Nambilanje, Mkaranga, Namkatila, Namkonjela, Nangandala, Nanjaru, Mbecha, Chikoko, Likwachu, Mibure, Chilangalile na Litama.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla utekelezaji wa mradi unaendelea vizuri na unafanyika kwa kuwashirikisha wananchi na viongozi wa vijiji. Hali hiyo inaongeza uelewa wa kutosha miongoni mwa wananchi kuhusu mipango ya matumizi ya Ardhi. Jambo hilo linastahili pongezi na liendelee kuwa mfano wa kuigwa.

(b) Mradi Namba 2326: Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi – KKK katika halmashuri ya Chalinze

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatekelezwa kwa utaratibu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutoa mikopo ya fedha isiyo na riba kwa Halmashauri nchini. Bunge liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 4,500,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza mradi huu kwenye halmashauri mbalimbali nchini kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Katika ziara ya ukaguzi, Kamati ilitembelea mradi wa KKK kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze hususan, maeneo ya Msolwa na Chamakweza Mkoani Pwani.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Utekelezaji ilionesha kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze ilipatiwa Mkopo usio na riba wa **Shilingi 2,500,000,000.00.** Mkopo huo ulitumika kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika maeneo ya Msolwa na Chamakweza yenye ukubwa wa ekari 440.34.

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa mradi huu umekamilika kwa maeneo yote ya Msolwa na Chamakweza. Kwa hali hiyo, Halmashauriya ya Wilaya ya Chalinze inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 4,500,000,00.00** kutoka kwenye mradi huo. Kwa makusanyo hayo, faida inayotarajiwa kupatikana itakuwa ni **Shilingi 2,000,000,000.00**. Faida hiyo ni sawa na **asilimia 44.45.** Pamoja na faida inayotarajiwa kupatikana hadi kamati inatembelea Halmashauri ya Chalinze hali ya urejeshwaji wa mkopo ni ya kusuasua kwani walikuwa wamelejesha **shilingi 300,000,000.00** tu.

(c) Mradi Na.4953: Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP)

**Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kutekeleza Mradi wa LTIP ambao unatekelezwa kwa Fedha za Mkopo kiasi cha Dola za Marekani **Milioni 150** kutoka Benki ya Dunia katika kipindi cha miaka mitano (2022/2023 – 2027/2028). Lengo la mradi ni kuboresha Usalama wa miliki na utoaji wa huduma za ardhi kwa wananchi. Mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri 67 katika mikoa 15 nchini. Kwa Mkoa wa Dar es Salaam mradi unatekelezwa katika jumla ya mitaa 272 iliyopo katika halmashauri tano ambazo ni Temeke, Ilala, Kigamboni, Ubungo na Kinondoni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa ili kufikia lengo, mradi unajielekeza katika kuboresha utawala na usimamizi wa ardhi nchini, na Usalama wa milki za ardhi nchini kwa wanawake na wanaume. Kwa mfano, katika Mkoa wa Dar es Salaam mradi unatekelezwa kwa kusogeza huduma jirani na wananchi kupitia vituo vya kutolea huduma za ardhi katika eneo moja maarufu kama **Ardhi Kliniki.** Aidha, huduma zinazotolewa ni pamoja na Kupanga, Kupima, Kumilikisha Ardhi; kutatua migogoro mbalimbali ya ardhi; kuongeza idadi ya wanawake wanaomiliki ardhi kisheria kwa kuwamilikisha hati za ardhi; na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala mbalimbali ya ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata nafasi ya kutembelea eneo la Bunju tarehe 17 Machi, 2024 na kujionea uendeshaji wa kliniki hiyo. Pia, Kamati ilishuhudia Urasimishaji wa Ardhi katika meneo manne (04) tofauti; Utoaji wa hati kumi na sita (16) za ardhi kwa wananchi; na kusikiliza Migogoro ya Ardhi tisa (09). Aidha, hati miliki za ardhi sitini na saba (67) zilitolewa kupitia makampuni binafsi ya upimaji.

**B)** Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na Taarifa za utekelezaji wa miradi iliyokaguliwa pamoja na hali halisi ilivyobainika wakati wa ziara, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

(i) Utekelezaji wa sehemu kubwa ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati imefikia hatua nzuri hali inayoonesha kuwa miradi hiyo itakamilika kwa wakati. Hata hivyo

mradi wa LTIP bado unasuasua hali inayoweza kupelekea kuchelewa kupatikana tija iliyokusudiwa; na

(ii) Wakati wa utekelezaji wa miradi, Wizara na Tume walizingatia ushirikishwaji wa wadau na wananchi ambao ni wanufaika wa miradi husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo. Hata hivyo, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Wizara iongeze usimamizi katika miradi hiyo ili ikamilike ndani ya muda na kuleta tija iliyokusudiwa.

**2.1.3 Utekelezaji wa Majukumu na Mipango ya Wizara**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Katika kufanya hivyo, kamati ilizingatia vipaumbele vya wizara kwa mwaka husika ambavyo ni:-

(i) Kusimamia miradi ya ubia na kukaribisha wawekezaji kutoka sekta binafsi ili kufanya uendelezaji wa majengo ya biashara na makazi kupitia sera ya ubia;

(ii) Kukamilisha kanuni na miongozo ya uendelezaji wa milki;

(iii) Kutoa elimu ya Sheria, Kanuni na Miongozo ya usimamizi wa uendelezaji miji katika Ofisi za ardhi;

(iv) Kufanya tafiti kuhusu makazi yasiyo rasmi;

(v) Kuwezesha Shughuli za Ofisi ya Msajili wa Bodi ya Wataalam wa Mipangomiji; na

(vi) Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya urasimishaji na kuzuia makazi yasiyo rasmi;

(vii) Kufanya Ukaguzi wa uzingativu wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi iliyoandaliwa katika vijiji;

(viii) Kufanya tathimini na ufuatiliaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji vilivyoandaliwa mipango ya matumizi

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla wake shughuli nyingi zilizopangwa katika Mpango wa Mwaka 2023/2024 zinaendelea kutekelezwa vizuri na ufanisi unaonekana. Baadhi ya shughuli hizi na matokeo yake ni: -

(i) Kusajili Hati za Hatimiliki 500,000 katika halmashauri 22, Viwanja 23,503 vimepangwa na kupimwa katika Halmashauri za Jiji la Dodoma (7,474), Wilaya ya Chalinze (9,865) na Kigoma (6,164), Hatimiliki za Ardhi 6,303 zimetolewa katika mkoa wa Dar es Salaam kupitia zoezi la kliniki za Ardhi;

(ii) Kuratibu ugawaji wa hekta 5000 kwa ajili uwekezaji ambapo hekta 509.62 zimegawiwa kwa wawekezaji kwa matumizi mbalimbali yakiwemo viwanda, kilimo, ujenzi wa nyumba na uwekezaji mwengine;

(iii) Kuongeza vipindi 50 vya Luninga,257 vya redio, Makala magazetini 250 pamoja na habari 1,642 kwenye mitandao ya kijamii vilirushwa kwa umma kuhusu masuala ya sekta ya ardhi;

(iv) Kutatua Migogoro kwa kupima Vijiji 128 vya Halmashauri za Wilaya 14 kwa kuonesha Mipaka kwa kupitia uhakiki na upimaji; na

(v) Mipango ya matumizi ya Ardhi ya vijiji 219 imendaliwa katika Halmashauri 14 nchini.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo ya Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto kama vile upungufu mkubwa wa watendaji wa sekta ya ardhi na upungufu wa fedha za miradi ya maaendeleo. Kamati inahimiza Serikali kuwekeza katika kuajiri sambamba na kuongeza fedha za maendeleo kwa Tume ya Taifa ya mipango ya matumizi ardhi ili waweze kupima vijiji vingi hapa nchini.

**2.1.4 Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika,** maduhuli ni sehemu ya msingi katika utekelezaji wa bajeti, Kamati ilipokea maelezo kuhusu hali ya ukusanyaji wa maduhuli kwa **Fungo 48** na **Fungu 03**. Ili kupata uhalisia unaoweza kulisaidia Bunge kuwa na picha kamili kuhusu maduhuli, Kamati ilichambua maelezo ya serikali kuhusu ukusanyaji wa maduhuli. Uchambuzi huo, ulifanyika kwa kuzingatia masuala yafuatayo:-

(i) Kiasi kilichokusanywa ikilinganishwa na lengo la makusanyo;

(ii) Makadirio ya uwiano wa aina ya maduhuli ikilinganishwa na uwiano wa aina hizo kwenye makusanyo halisi; na

(iii) Ulinganisho wa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi **Fungu 48,** ilikadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 300,000,000,00.00.** Hadi kufikia Februari, 2024, Wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 101,848,128,269.56** sawa na **asilimia 34** ya lengo la makadirio. Aidha, uchambuzi umebaini kwamba hali ya makusanyo hafifu imetokana na uamuzi wa Serikali kupitia **Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023** (Finance Act, 2023) kutaka Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kukusanya Kodi ya Pango la Ardhi (Land Rent). Jambo hilo limeathiri kiasi cha jumla ya makusanyo ya Kodi ya Pango la Ardhi, ambacho ndio chanzo kikuu cha makusanyo katika Fungu hili. Hali hiyo imetokana na Mamlaka hizo (Halmashauri) kushindwa kukusanya kodi hiyo kwa sababu mbalimbali ikiwemo ya kukosa nguvu ya kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi **(Fungu 03)**, ilikadiriwa kukusanya **Shilingi 718,000,000**. Hadi kufikia februari, 2024, Tume ilivuka malengo kwa kukusanya **Shilingi 1,698,678,150** sawa na **asilimia 265.9** ya lengo. Kamati inaipongeza Tume kwa hatua hii ya kuvuka lengo la ukusayaji wa maduhuli. Hata hivyo, ni maoni ya Kamati

kwamba, upo uwezekano wa kutokuwa na makadirio halisi ya mapato kwa Tume hii. Ziada kubwa inaonyesha kuwa upangaji wa makadirio ya makusanyo ndani ya Tume hauzingatii uwezo wa vyanzo vyake vya mapato.

Kielelezo Na.01 Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Februari, 2024

| Fungu | Makadirio | Makusanyo | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Fungu 48 (Wizara) | 300,000,000,000.00 | 101,848,128,269.56 | 34 |
| Fungu 03 (Tume) | 718,000,000 | 1,696,678,150 | 265.9 |

*Chanzo: Randama za Wizara na Usanifu wa Kamati*

**2.1.5 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika,** upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwenye bajeti ni muhimu katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Ili kujiridhisha na uwezo wa kifedha wa Wizara kutekeleza majukumu yake, Kamati ilichambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa Fungu 48 na Fungu 03 Tume.

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuonyesha hali halisi ya kila fungu, Kamati ilichambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa fungu moja moja kama ifuatavyo:-

a) Fungu 48: Wizara ya Ardhi

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa **Fungu 48** hadi kufikia mwezi Februari, 2024, umeonesha mambo yafuatayo:-

(i) Fedha za matumizi ya kawaida zilipatikana kwa **asilimia 49.6** ikiwa ni pungufu ya fedha zilizotakiwa katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti ambacho ni asilimia **66.6;**

(ii) Katika kiasi hicho cha fedha za kawaida, fedha za uendeshaji (OC) zilikuwa **asilimia 45** ya fedha zote, huku mishahara ikiwa imepatikana kwa **asilimia 64**;

(iii) Fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo zilipatikana kwa **asilimia 80** ya bajeti;

(iv) Katika fedha za kugharamia miradi ya maendeleo, fedha za Ndani zilifikia **asilimia 95** na fedha za nje **asilimia 47.** Hata hivyo, katika kiasi hicho cha fedha za ndani, **asilimia 77** ilikuwa ni fedha ya kulipia madeni mbalimbali ya Wizara. Taswira halisi ya mwenendo wa fedha inaonekana kwenye **Jedwali Na. 2.**

Jedwali Na.2 Upatikanaji wa Fedha kwa Fungu 48

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | KIASI KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 43,428,651,000.00 | 27,670,697,672.78 | 64 |
| Matumizi Mengineyo | 37,614,584,000.00 | 12,110,029,963.70 | 45 |
| JUMLA (A) | 81,043,235,000 | 39,780,727,636.48 | 64 |
| Miradi ya Maendeleo | 82,126,645,000.00 | 177,313,385,501 | 80 |
| Kulipa madeni ya Serikali | 138,432,625,000.00 | 138,432,625,000.00 | 100 |
| **JUMLA** | **301,602,505,000** | **217,094,113,137.5** | **72** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo wa upatikanaji wa mapato kwa ujumla unaonesha changamoto ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kwa ujumla hali hiyo ilichangia kutokutekelezwa ipasavyo kwa majukumu yaliyopangwa. Kwa mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha, ni wazi kuwa itakuwa vigumu kwa Wizara kutekeleza majukumu kama yalivyoainishwa kwenye taarifa hii.

b) Fungu 03: Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa **Fungu 03,** Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Uchambuzi wa mwenendo wa upatikanaji wa fedha hadi kufikia Februari, 2024 ulionesha mambo yafuatayo:-

i. Tume ilipokea **asilimia 67** ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge ikiwa inaendana na uwiano katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti ambacho ni **asilimia 66.6**; ii. Fedha za matumizi ya Kawaida zilizopokelewa zilikuwa **asilimia 58.7** ya bajeti yote. Kiasi hiki ni pungufu ya kipindi cha utekelezaji wa bajeti ambacho ni **asilimia 66.6;** iii. Katika kiasi hicho cha fedha za matumizi ya kawaida, fedha za matumizi mengineyo (OC) zilipokelewa kwa **asilimia 52.63**, huku mishahara ikiwa imepokelewa kwa **asilimia 80.69;** iv. Fedha za miradi ya Maendeleo zilipokelewa kwa **asilimia 66** huku fedha zote zikiwa fedha za ndani. Taswira halisi ya Mwenendo wa Fedha inaonekana katika **Jedwali Na. 03.**

Kielelezo Na.3: Upatikanaji wa Fedha (FUNGU 03)

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | KIASI KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 2,498,904,000 | 2,016,588,000 | 80.69 |
| Matumizi mengineyo | 2,293,724,000 | 1,207,192,463.97 | 52.63 |
| Miradi ya Maendeleo | 3,410,000, 000 | 2,266,408,000 | 66.46 |
| **JUMLA** | **8,202,628,000** | **5,490, 188,463.97** | **66.93** |

Chanzo: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo huo kwa ujumla unaonesha kuwa vipaumbele na majukumu yaliyopangwa kutekelezwa na Tume yalifanyika kwa ufanisi. Hali hii imechangia katika kupatikana kwa tija katika majukumu hayo.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,**ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilichambua na kujadili Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

i. Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2024/2025; na
ii. Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025;
iii. Mambo muhimu yanayogusa sekta ya ardhi.

### 3.1.1 Makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kutambua uhusiano uliopo kati ya Mapato na Matumizi, Kamati ilipokea ufafanuzi wa kuhusu lengo la maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Uchambuzi wa ufafanuzi huo ulizingatia uzoefu uliopatikana katika ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 20224/2025 Fungu 48 (Wizara) imekadiriwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi 250,000,000,000.00** Uchambuzi wa kamati umebaini kuwa makario hayo yamepungua kwa Shilingi **50,000,000,000.00** ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi zaidi umebaini kuwa, pamoja na kupungua kwa lengo ya makusanyo kwa upande wa Fungu 48, uwezekano wa lengo hilo kufikiwa ni mdogo. Hali hii inatokana na ukweli kuwa, katika kipindi cha miaka miwili mfululizo, ukusanyaji wa maduhuli katika Wizara hii haukufikia asilimia 50 ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi **Fungu 03** inakadia kukusanya jumla ya **Shilingi 1,018,000,000.00.** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makadirio haya yameongezeka kwa

**Shilingi 300,000,000.00** sawa na **asilimia 41.8** ukilinganisha na mwaka wa fedha 2023/2024.

Jedwali Na.4 Mchanganuo wa makadirio ya Maduhuli

| FUNGU | 2023/2024 | 2024/2025 | Ongezeko/punguzo | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Wizara (48) | 300,000,000,000 | 250,000,000,000 | 50,000,000,000 | 16.66 |
| Tume (03) | 718,000,000 | 1,018,000,000 | 300,000,000 | 41.8 |

***3.1.2 Makadirio ya Matumizi***

**Mheshimiwa Spika,** masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge yamelenga kuliwezesha Bunge kutumia uzoefu wa utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha ili kuchambua makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa kuzingatia lengo hilo, Kamati imechambua makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Kulinganisha makadirio kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na makadirio kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Kulinganisha mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na makadirio kwa mwaka wa fedha 2024/2025; na

(iii) Kulinganisha uwiano wa aina za matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na mwaka wa fedha 2024/2025; na

(iv) Kulinganisha upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo na makadirio ya fedha za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

a) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu – 48)

**Mheshimiwa Spika,** Wizara hii inaomba jumla ya **Shilingi 157,455,085,000.00** ili kuimarisha sekta ya ardhi na nyumba nchini

na kukuza mchango wake katika maendeleo ya Taifa, uchumi wa nchi na ustawi wa wananchi. Uchambuzi na matokeo ya matumizi ya fedha hizo unanesha yafuatayo:-

i. Jumla ya bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imeshuka kwa **asilimia 3.5** ikilinganishwa na ya mwaka wa fedha 2023/2024;

ii. Bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imeongezeka kwa **Shilingi 5,755,340,000** sawa na **asilimia 7.1** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2023/2024; na

iii. Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imeshuka kwa kiasi cha **Shilingi 11,470,135,000** sawa na **asilimia 14** ikilinganishwa mwaka wa fedha 2023/2024. Taswira ya makadirio ya matumizi kwa **Fungu 48** Wizara inaonekana katika **Jedwali Na. 5**

Jedwali Na 05: Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na mwaka 2024/2025 Fungu 48

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA MWAKA 2023/2024 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2024/2025 | %ONGEZEKO |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 43,428,651,000 | 50,155,528,000 | 15.49 |
| Matumizi mengineyo | 37,614,584,000 | 36,643,047,000 | 2.58 |
| JUMLA | 81,043,235,000 | 86,798,575,000 | 7.1 |
| Miradi ya maendeleo | 82,126,645,000 | 70,656,510,000 | -13.96 |
| **JUMLA KUU** | **163,169,880,000** | **157,455,085,000** | **-3.5** |

**b) Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu –03)**
**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Fungu 03, Serikali inaomba jumla ya **Shilingi 12,173,330,000** ili kuendelea kupanga matumizi

ya ardhi katika vijiji na miji yetu kwa maendeleo ya Taifa, uchumi wa nchi na ustawi wa wananchi. Uchambuzi na matokeo ya matumizi ya fedha hizo unaonesha yafuatayo:-

i. Jumla ya bajeti kwa fungu hili kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imeongezeka kwa **asilimia 48.1** ikilinganishwa na ya mwaka wa fedha 2023/2024;

ii. Bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imeongezeka kwa Shilingi 2,339,470,000.00 sawa na **asilimia 48.9** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2023/2024; na

iii. Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imeongezeka kwa kiasi cha **Shilingi 1,631,232,000** sawa na **asilimia 47.8** ikilinganishwa mwaka wa fedha 2023/2024. Taswira ya makadirio ya matumizi kwa **Fungu 03** Wizara inaonekana katika Jedwali Na. 5

Jedwali Na.06: Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa 2023/2024 na mwaka 2024/2025 Fungu 03

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA MWAKA 2023/2024 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2024/2025 | % Ongezeko |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 2,498,904,000 | 3,887,780,000 | 55.58 |
| Matumizi Mengineyo | 2,293,724,000 | 3,244,318,000 | 41.44 |
| JUMLA | 4,792,628,000 | 7,132,098,000 | 48.81 |
| Miradi ya Maendeleo | 3,410,000,000 | 5,041,232,000 | 47.83 |
| JUMLA KUU | 8,220,628,000 | 12,173,330,000 | 48.08 |

*Chanzo:* Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Fungu 03 halina fedha za maendeleo kutoka nje. Hali hii nzuri kwani inapunguza utegemezi. Hata hivyo, ili kuongeza kasi ya kupima na kupanga matumizi ya ardhi nchini, ni vizuri Serikali ikaona uwezo wa kushirikisha wadau wa maendeleo katika sekta ya ardhi.

### 3.1.3 Mambo muhimu yanayogusa sekta ya ardhi

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kujadili mpango wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025, mambo kadhaa yanayogusa sekta ya ardhi yalijadiliwa mambo kadhaa:-

#### i) Mradi wa Kuboresha Usalama wa Miliki za Ardhi (LTIP)

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa kutokana na Mkataba kati Serikali na Benki ya Dunia – kiasi cha Bilioni 346 ikiwa unatekelezwa kupitia vipengele vinne (4) ambavyo ni kuongeza usalama wa milki za ardhi kwa kutoa hati miliki milioni moja maeneo ya mijini kwa njia ya urasimishaji na Hati miliki za Kimila laki tano vijijini; kuimarisha mifumo ya taarifa za ardhi, kujenga miundombinu ya ardhi; na usimamizi wa mradi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa taarifa za Wizara, Katika mwaka 2023/2024 jumla ya makazi 500,000 yalipangwa kurasimishwa katika Halmashauri 23 kupitia wataalam wa ndani makazi 100,000 na kampuni binafsi za upangaji na upimaji makazi 400,000; kuanza kujenga Vituo 22 vya Upimaji na kusimika Alama za Msingi za Upimaji 400 katika muda wote wa mradi.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa mradi Jumla ya makazi 102,276 yametambuliwa na vipande vya ardhi 62,200 vimerasimishwa kwa kutumia wataalam wa ndani kusimika alama za Msingi za Upimaji 327 zimesimikwa katika Halmashauri 26 sawa na asilimia 82. Aidha, Wizara kupitia Mradi ilipanga kupima/kuhakiki mipaka ya vijiji 700; kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi na mipangokina ya vijiji 700 kati ya lengo la Mradi la kupanga matumizi ya ardhi ya vijiji 1,667 (kutoka lengo la awali la vijiji 250 kufuatia utekelezaji wa ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii).

**Mheshimwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo, kasi ya utekelezaji wa mradi huu ukilinganisha na shughuli na muda uliopangwa katika kutekeleza mradi huu hairidhishi.

ii) Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake, Shirika kwa sasa linatekeleza miradi kadhaa ya Ujenzi wa Nyumba ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Baadhi ya miradi hiyo ni Mradi wa Samia Housing Scheme (SHS), Mradi wa Kawe 711(Seven – eleven) na Mradi wa Golden Premium Residence (GPR). Aidha, Shirika limeanza kutekeleza miradi mbalimbali ya ubia kupita sera ya ubia ya Shirika.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeza majukumu yake, Shirika linadai madeni toka kwa wateja wake ambao ni watu binafsi pamoja na taasisi za umma na binafsi.

**iii) Maboresho ya Mfumo wa Usimamizi wa Ardhi nchini**
**Mheshimiwa Spika,** uboreshaji huo wa mfumo utawapa wananchi uwezo wa kutoa taarifa endapo watacheleweshewa huduma; Mfumo utaondoa changamoto ya upotevu wa nyaraka zinazowasilishwa na wananchi kuomba huduma, kwani zitakuwa zinawasilishwa kupitia mfumo (online); na Mfumo utaongeza uoni (visibility) kwa viongozi wa ngazi mbalimbali wa Wizara kuona utendaji wa majukumu unavyoendelea katika ngazi mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Mfumo huu unakusudia kuanzisha Ardhi Kiganjani App itakayomuwezesha mwananchi anayeomba huduma inayotakiwa kulipiwa atapata Namba ya Malipo (Control Number) kwenye dashboard au simu yake ya kiganjani bila kuhitaji kwenda Ofisini kuipata. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inatenga fedha za kutosha ili mfumo huu uweze kuanza kazi nchi nzima.

**iv) Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK)**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi kwa kuzikopesha Taasisi na Halmashauri mbalimbali nchini na miradi ya Wizara. Hadi kufikia

Disemba, 2023, Viwanja 1,017 vimepimwa katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Viwanja 7,945 na mashamba 46 vimemilikishwa kati ya viwanja 246,136 vilivyopimwa mwaka 2022/23.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa kumekuwa na kusuasua katika kurejesha fedha za mikopo kwa halmashauri nyingi ili kuhakikisha proramu hii inakuwa endelevu. Hata hivyo, Wizara imeandaa mwongozo wa utekelezaji wa Mfuko wa Mzunguko wa Maendeleo ya Ardhi (Plot Development Revolving Fund) ambao utatoautaratibu wa namna ya fedha katika Mfuko huu utakavyotumika ili kutekeleza program ya KKK.

**Mheshimwa Spika,** katika kurejesha fedha ambazo halmashauri zilipewa kwa ajili ya kutekeleza program hii, Shilingi bilioni 21.7 zimerejeshwa kati ya Shilingi bilioni 50 zilizotolewa kwa halmashauri sawa na asilimia 43. Aidha, halmashauri 12 za Ofisi ya ardhi Mkoa wa Iringa zimerejesha fedha zote, halmashauri 44 zimerejesha sehemu ya fedha huku halmashauri za Manispaa ya Shinyanga na Musoma DC zikiwa hazijarejesha kabisa. Kamati inaitaka Wizara kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI kuhakikisha wanazibana Halmashauri zilizobaki ziweze kurejesha fedha zote ili ziende zikasaidie Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi katika maeneo mengine ya nchi yetu.

**v) Changamoto katika Kulipa Fidia ya Ardhi kwenye maeneo yanayotwaliwa kwa ajili ya Miradi ya Serikali na Uwekezaji**

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na ucheleweshaji fidia wakati Serikali au taasisi zake zinapotaka kutwaa maeneo ya wananchi kwa manufaa ya umma au kupangiwa matumizi mengine tofauti na yale yaliyopo kwa sasa. Ili kukadiria kiasi cha fidia kitakacholipwa kwa mwananchi ambaye mali zake zimetwaliwa kwa manufaa ya umma, sheria inaelekeza kuwa thamani ya mali hizo zinapaswa kukadiriwa na mthamini aliyesajiliwa na bodi ya wathamini.

**Mheshimiwa Spika,** hali ya ucheleweshaji wa kulipa fidia hizo inachangia katika kuzalisha migogoro kati ya wananchi na Serikali au muwekezaji, kulipa riba kutokana na kuchelewesha kulipia fidia, mlundikano wa kesi za Ardhi katika mabaraza ya Ardhi na

Mahakamani na kuwafanya wananchi kuwa masikini kinyume na kusudio la Serikali la kuhakikisha ustawi katika maisha ya wananchi wake.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI

### 4.1 Maoni na Ushauri

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza serikali, kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa ufanisi mkubwa wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2023/2024. Kwa kipekee kabisa Kamati inapongeza Wizara kwa kusimamia vyema shughuli zote za Sekta za Ardhi hapa nchini.Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuifanya sekta ya ardhi kuwa moja ya vipaumbele vikubwa katika mipango yake ya maendeleo hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na pongezi hizi, Kamati ina maoni na ushauri kwenye baadhi ya masuala yanayopaswa kuzingatiwa na Wizara kama ifuatavyo;

#### 4.1.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa ukusanyaji mdogo wa mapato yatokanayo na kodi ya pango la ardhi (Land Rent) unatokana na sheria ya fedha (Finance Act) ya Mwaka 2023 iliyoitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya wakati halmashauri hizo hazina kanzidata, watumishi na hata nyenzo za kisheria za ukusanyaji. Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri kuwa Serikali ipitie upya uamuzi huo na kuleta Bungeni mapendekezo ya kurekebisha hali hiyo;

#### 4.1.2 Urejeshwaji wa Fedha za mradi wa Kupima, Kupanga na Kumilikisha Ardhi (KKK)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwepo kwa ucheleweshaji wa baadhi ya halmashauri kurejesha fedha ilizokopeshwa ili kutekeleza mradi wa Kupima, Kupanga na Kumilikisha Ardhi. Hivyo

bas, Kamati inashauri kuwa Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ishirikiane na OR TAMISEMI kuhimiza wakurugenzi wa Halmashauri ambao hazijarejesha fedha hizo kurejesha ili halmashauri zingine ambazo hazijakopa zikopeshwe kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa mradi na kuleta tija iliyokusudiwa.

### 4.1.3 Madeni ya Kodi ya Pango kwa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) linakabiliwa na changamoto ya baadhi ya wateja wake ambao ni taasisi za Serikali kushindwa kulipa kodi ya pango kiasi cha shilingi 2,148,864,361.35. Kamati inashauri Serikali kuzisimamia taasisi zinazodaiwa na Shirika hilo kwa kuhakikisha zinatenga bajeti ya kulipa deni hilo.

### 4.1.4 Changamoto ya Upungufu wa Watumishi katika Sekta ya Ardhi Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ina upungufu wa watumishi wakiwemo wakaguzi wa majengo (building inspectors) hali inayochangia ujenzi usiofuata matumizi bora ya ardhi. Kamati inashauri kuwa Serikali iongeze watumishi katika sekta ya ardhi ili kusaidia kudhibiti ujenzi holela na kusimamia matumizi bora ya ardhi nchini;

### 4.1.5 Changamoto ya Upangaji wa Matumizi bora ya Ardhi

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo na migogoro mingi ya ardhi nchini inayotokana na Serikali kushindwa kupima na kupanga matumizi bora ya ardhi kwa maeneo mengi nchini. Kamati inashauri kwamba Serikali iendelee kutoa fedha kwa ajili ya kupanga kwa Tume ya taifa ya Mipango na Matumizi Bora ya Ardhi kwa ajili ya Kupima na Kupanga hali itakayosaidia kuondoa migogoro na kudhibiti ukuaji wa miji kiholela

**4.1.6 Ucheleweshaji wa Fidia ya Ardhi katika maeneo yaliyofanyiwa uthamini**

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo na changamoto ya Serikali kuchelewa kulipa fidia inapotaka kutwaa ardhi kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo, hali inayochangia migogoro kati ya wananchi na Serikali. Kamati inashauri Serikali ihakikishe kuwa kunakuwa na uthibitisho wa uwepo wa fedha za kulipa fidia ambao utatolewa na Wizara/taasisi mtwaaji au mwekezaji anaekusudia kutwaa ardhi husika. Aidha, Serikali ihakikishe kuwa kwa kushirikiana na wadau wote muhimu wa utwaaji inafanya Uhakiki kabla ya Mthamini Mkuu kuidhinisha majedwali ya fidia, na kabla ya hatua ya Uoneshaji majedwali hayo kwa wananchi (Disclosure Stage) kufanyika, hii itasaidia kurekebisha dosari zote ndani ya muda sahihi na kuhakikisha wananchi wanalipwa kwa wakati.

**4.1.7 Changamoto ya Ujenzi wa Makazi katika Maeneo hatarishi**

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo na ujezi wa Makazi katika maeneo oevu (wetlands), maeneo ya mabonde, maeneo karibu na hifadhi za Taifa, shoroba za Wanyama. Hali hii inahatarisha Maisha ya wananchi katika maeneo hayo. Kamati inashauri Serikali iandae Mpango wa Matumizi ya Ardhi inayoendana na hali halisi ya maeneo husika ili kuwaepusha wananchi na athari hizo.

**4.1.8 Kasi ya Utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP)**

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na kasi ndogo ya utekelezaji wa mradi wa LTIP hali inayoweza kuathiri tija ya malengo ya mradi kufikiwa kama ilivyokusudiwa. Kamati inashauri Serikali kuongeza kasi katika usimamizi na utekelezaji wa mradi huo. Aidha, Kamati inashuari Serikali kuhakikisha Kliniki za Ardhi zinakuwa endelevu hata baada ya mradi huu ili kutatua changamoto za migogoro ya ardhi nchini.

## SEHEMU YA TANO

### 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya kamati inapenda kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na wenyeviti wa Bunge kwa namna mnavyotekeleza majukumu yenu katika kulisimamia na kuliwezesha Bunge letu kutekeleza wajibu wake wa kusimamia na kuishauri Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumpongeza na kumshukuru sana **Mhe Jerry William Silaa (Mb**), Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mhe. Geophrey M. Pinda (Mb) Naibu Waziri wa Wizara hii kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, nawashukuru watendaji wote wa Wizara chini ya Katibu Mkuu Mhandisi Anthony Sanga, Naibu Katibu Mkuu Ndg Lucy Kabyemela, kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake na usimamizi mzuri wa majukumu ya wizara kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee nawapongeza na kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kazi kubwa walioyofanya hadi taarifa hii inaingia Bungeni. Majina ya wajumbe hao yameorodheshwa katika taarifa hii, ila kwa sababu ya changamoto ya muda, naomba majina yao yaingie kwenye taarifa rasmi za Bunge, yaani hansard. Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo: -

1. Mhe. Timotheo Mnzava,Mb- M'kiti
2. Mhe. Najma Murtaza Giga – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Asia Abdukarimu Halamga,Mb
4. Mhe. Cecilia Daniel Pareso,Mb
5. Mhe. Innocent Seba Bilakwate,Mb
6. Mhe. Ester Lukago Midimu,Mb
7. Mhe. Alaudin Hasham Salim,Mb
8. Mhe. Josephine Thabita Chagula,Mb
9. Mhe. Khalifa Salum Suleiman,Mb
10. Mhe. Lucy Tomas Mayenga,Mb
11. Mhe. Maida Hamad Abdallah,Mb
12. Mhe. Munira Mustafa Khatib,Mb
13. Mhe. Neema William Mgaya,Mb

14. Mhe. Oliver Daniel Semguruka,Mb
15. Mhe. Shaabani Omari Shekilindi,Mb
16. Mhe. Taska Restuta Mbogo,Mb
17. Mhe. Festo Richard Sanga,Mb
18. Mhe. Dkt. Florence George Samizi,Mb
19. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman,Mb
20. Mhe. Askofu Josephat Mathias Gwajima,Mb
21. Mhe. Emmanuel Adamson mwakasaka,Mb
22. Mhe. Asha Abdallah Juma,Mb

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhiimu, naomba nimalize kuwashukuru Watumishi wote wa Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg.Nenelwa Joyce Mwihambi, ndc kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha, na naunga Mkono Hoja

Timotheo P. Mnzava, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Najma Giga, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii na Mwenyekiti wa Bunge kwa kusoma vizuri sana taarifa ya Kamati yako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, tunao wageni walioongezeka kwenye ukumbi wetu huu wa Bunge. *(Makofi)*

Kwanza, tunao wageni waliokaa katika Jukwaa la Spika, ambao ni Wageni wa Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mbunge na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; tunaye

Ndugu David Mushendwa - Msajili wa Hati; Dkt. Upendo Matotola - Mkurugenzi wa Milki na tunaye Ndugu Netto Ndilito - Mkurugenzi wa Sera na Mipango. Ahsanteni sana na karibuni nyote. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wageni wengine wa Mheshimiwa Mheshimiwa Jerry William Silaa - Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni Wakurugenzi na watumishi kutoka katika taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ardhi, naomba msimame mliopo, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanachama wa Chama Cha Mapinduzi na wadau kutoka Jimbo la Ukonga. Simameni tuwatambue, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao viongozi wa dini ambao wamekuja pamoja na wadau mbalimbali wa Sekta ya Ardhi na Taasisi za Fedha ambao wamekuja kwa heshima ya Mheshimiwa Waziri Jerry Silaa, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 20 wa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mbunge na Waziri wa Fedha ambao ni Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania, karibuni sana, tumefurahi kuwaona. *(Makofi)*

Tunao wageni 40 wa Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, Mbunge na Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni Vijana Jazz kutoka Makao Makuu ya CCM, karibuni sana, tumefurahi kuwaona. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Venant Daud ambaye ni kaka yake kutoka Jijini Mwanza, karibu sana kaka yetu. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Seif Gulamali ambao ni rafiki zake kutoka Manonga, Mkoa wa Tabora, karibuni sana rafiki zetu. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni Wanachama wa Taasisi Isiyo ya Kiserikali *(TAWENI)*

ambayo inahusika na matumizi ya nishati safi na salama, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo hapa kwa sasa ni Ndugu Hamis Sadiki Rajab, Afisa Utumishi kutoka *TBS,* karibu sana na ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumeshapata hotuba mbili, hotuba ya Mheshimiwa Waziri na hotuba ya Kamati, nawashukuru wote, Mheshimiwa Waziri na Mwenyekiti wa Kamati, tutakuwa na wachangiaji nane asubuhi hii na nitajiatahidi kwa kadiri inavyowezekana kumaliza, tujielekeze kwenye hoja.

Waheshimiwa Wabunge, asubuhi yetu hii tutaanza na Mheshimiwa Livingstone Lusinde, atafuatia Mheshimiwa Godwin Kunambi na Mheshimiwa Edward Olelekaita ajiandae. Mheshimiwa Livingstone Lusinde, tafadhali. *(Makofi)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ya kuchangia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mafungu yote mawili, Fungu Na. 48 na Fungu Na. 03. Pia, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili nami niweze kusimama kwenye Bunge letu Tukufu ili niweze kutoa mchango wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uteuzi wa Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Ardhi, Mheshimiwa Jerry Silaa. Mheshimiwa Rais kama kocha, amechagua mshambuliaji mzuri, mtu mwenye uwezo na mtu ambaye kwa kweli amewa-*prove wrong* watu wengi ambao walikuwa hawamfahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama namna Wizara imewekwa vizuri kuanzia Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu wake, Katibu Mkuu, Kamishna pamoja na watumishi wengine, utakubaliana nami kwamba Mheshimiwa Rais anakusudi kubwa la kuhakikisha kwamba ardhi ya nchi yetu siyo tu inapoimwa na kupangwa, bali inakuwa kichocheo kikubwa cha maendeleo ya Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi kubwa za Mheshimiwa Waziri, tumeona viongozi wa dini karibu zote ambazo ziko katika Taifa letu wakimwombea dua. Ni ombi langu Mheshimiwa Waziri huyu awekeze ulinzi, ambao utamsaidia kumlinda katika kufanya kazi zake, maana kupambana na majambazi papa ya ardhi siyo kitu kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kliniki ya ardhi aliyoianzisha Mheshimiwa Waziri imejibu vilio vingi vya Watanzania. Sasa ni ushauri wangu kwamba kila Mkoa hauwezi kusubiri Mheshimiwa Waziri afike, kila Mkoa hauwezi kusubiri kliniki ya ardhi ifike. Napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri kuweka *system* maalum ya kushughulikia matatizo ya ardhi, ambayo yeye akisema akiwa ofisini, ile *system* yote inafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake watendaji wake wote kuanzia Mwenyekiti wa Kijiji, Diwani mpaka kufika Taifa kuwe na utaratibu maalum wa kutoa haki kwa wananchi kuliko kusubiri mtu mmoja afike na kliniki kutwa nzima. Kuna kipindi ameendesha kliniki mpaka saa tano ya usiku, hii siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, jambo lingine ni kuhusu mabaraza ya migogoro, unajua kuna kitu ambacho sielewi, labda leo Mheshimiwa Waziri atanisaidia. Hivi haya mabaraza, ni mabaraza ya kutatua migogoro au ya kuongeza migogoro? Kwa sababu Mabaraza ya Ardhi ya Kata yamekuwa kichocheo kikubwa cha kuongeza migogoro ya ardhi kwenye maeneo yao, kwa sababu mapato yake hayafahamiki na bajeti ya kuendesha vikao vya baraza haifahamiki. Kwa hiyo, imekuwa mtu mwenye fedha ndiyo mwenye haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu yeyote mwenye fedha akienda kushitaki kwenye Baraza la Ardhi la Kata, yeye ndio mshindi kwa sababu yeye ndio atalilisha baraza, atalisafirisha baraza kwenda kuona eneo, yeye ndio atawarudisha na yeye ndio atawagharimia chakula na posho. Sasa hii haiwezekani. Ni lazima kufanya utaratibu maalum, tujue chanzo cha mapato cha haya mabaraza ni kipi na haya mabaraza yanalipwa posho kutoka kwenye fungu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ni lazima kuwe na msaada wa uwezeshaji kielimu kutoka Wilaya kushuka kwenye Kata. Maana hawa watu hawajui Sheria za Ardhi, wanachaguliwa tu pale na wakati mwingine wananchi wanalazimisha, “Diwani mtoe huyu au Diwani vunja baraza.” Kwa hiyo, utaratibu wake umekuwa mgumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema chombo hiki kikawekewa nguvu kubwa ili kiweze kufanya kazi kisheria na mapato yake yafahamike kwamba wakikutana posho wanatoa wapi? Hivi kweli posho ya shilingi 5,000 unalipa Mjumbe wa Baraza la Kata anayeshughulikia mgogoro wa shilingi milioni 100 au anashughulikia mgogoro wa shilingi milioni 10, halafu yeye analipwa posho shilingi 5,000! Ataacha kuchukua mpunga kwa huyu mtu mwenye hela na kumpa haki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni ushauri wangu, kama kweli tunataka tuone haki inatendeka kwa upande wa ardhi, kwanza haya Mabaraza ya Ardhi ya Kata wawezeshwe msaada wa elimu, wajue taratibu na elimu ya Sheria za Ardhi ili huyu Mwenyekiti wa Baraza la Mgogoro awe ni Mwenyekiti wa Baraza la utatuzi wa mgogoro badala ya kuwa Mwenyekiti wa kuendeleza migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kikosi kazi cha Mheshimiwa Rais kinafanya kazi kwenye vijiji. Mimi nataka kumpongeza sana Mheshimiwa Rais na ninachukua fursa hii kama Mjumbe wa *NEC*. Hawa watu wamekuwa wakipima ardhi mpaka vijijini, na Mheshimiwa Samia ameonesha tofauti kubwa. Sasa hivi kuna baadhi ya vijiji vinatembelewa mashamba, yanapimwa na wananchi wa vijijini wanapimiwa makazi yao. Hili ni jambo kubwa ambalo kama likiendelea, nataka niwaambie litatupa urahisi sana kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, CCM inakwenda kuchukua ushindi yaani kwa mtelezo kama vile ilikuwa imeweka, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwakumbuka watu wa vijijini, ila ni rai yangu kwa wananchi kutumia vizuri hizi hati wanazopewa, ni hati za miaka 50, lakini kama wote watakimbilia kuzikopea bila kuwa na utaratibu maalum, wanaweza kujikuta tena mashamba yao

yanakuja kufilisiwa na kuuzwa kwa utaratibu ambao utakuwa mbaya sana mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nawaomba sana wananchi badala ya kukimbilia kwenda kukopea hizi hati, uwe na uhakika kwamba una biashara na kwamba biashara yako inaweza kulipa huo mkopo unaoenda kuukopa, vinginevyo tutajiingiza kwenye matatizo makubwa sana ambayo hayana sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi ikipima vizuri maeneo ya vijijini, tukajua wapi makazi, wapi mashamba, wapi maeneo ya malisho? Hii ni Wizara mtambuka, hata hayo majani bora kwa mifugo ambayo juzi yalikuwa yanazungumzwa, tutajua tuyapande wapi lakini kama tutakuwa hatujapima na kutenga ardhi yetu vizuri itakuwa ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimesimama kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameipanga hii Wizara ya Ardhi na kwa *speed* yao ambayo wanafanya kazi kuhakikisha kwamba hati zinapatikana. Pia, utoaji wa haki na kusimamia kuona watu wanyonge nao wakipatiwa haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona taasisi za dini zikirudishiwa viwanja vyao, watu wa dini hawawezi wakaenda Mahakamani wakaanza kusumbuana na watu kutwa nzima, lakini wengine wanaomba dua tu, Mwenyezi Mungu atajalia ardhi yetu itarudi lakini tumeona Mheshimiwa Waziri akisimama na kutoa haki kwa taasisi zetu za dini ambazo zimekuwa zikiombea Taifa hili, Mheshimiwa Rais na amani ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango na kwa kujali muda. Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, atafuatia Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu ajiandae.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na ninamshukuru

Mheshimiwa Rais. Pia, nimpe pole Mheshimiwa Waziri maana amepewa Sekta nyeti na muhimu kwa Taifa letu, lakini ni Sekta ambayo ililaaniwa na Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirejee Kitabu cha Mwanzo aya ya 17: "Akamwambia Adam, 'kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nilikuagiza nikisema usiyale, ardhi imelaaniwa kwa ajili yako." Haya ni maneno matakatifu. Ndiyo maana nikasema ninampa pole na ameanza vizuri. Naomba nijikite kwenye mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu leo nitaeleza kwa namna gani ardhi ni muhimu katika kujenga uchumi wa Taifa letu. Hapa nieleze na nirejee maneno ya Hayati Baba wa Taifa aliwahi kusema, "Nchi yoyote ili iweze kupiga hatua za maendeleo lazima iwe na ardhi, watu, siasa safi na utawala bora." Sasa leo nitazungumzia Sekta ya Ardhi namna gani kwa maono yake Baba wa Taifa ardhi ni rasilimali muhimu kwa uchumi wa Taifa letu, lakini bado haitusaidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dhana ya upangaji, upimaji na umilikishaji. Kinachofanywa na Wizara ya Ardhi haipangi, haipimi mwisho wake inafanya urasimishaji. Nchi yetu haijapimwa, kinachofanyika sasa ni kurasimishwa siyo kupimwa. Naomba nitoe elimu hapa. Dhana ya upimaji inaanza na nyaraka muhimu mbili; ya kwanza inaitwa *land use masterplan* na ya pili inaitwa *infrastructure masterplan*. Sasa nikimwuliza Mheshimiwa Waziri ni halmashauri gani zina *infrastructure masterplan*? Naomba nitafsiri Kiswahili ili Watanzania wanielewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyosema *land use masterplan* maana yake ni mpango kabambe wa matumizi bora ya ardhi na *infrastructure masterplan* ni mpango kabambe wa miundombinu kwenye ardhi. Sasa hilo halifanyiki na ukiuliza halmashauri ngapi zina mpango kabambe wa matumizi bora ya ardhi na mpango kabambe wa miundombinu jibu litakuja sintofahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nimshauri Mheshimiwa Waziri, kazi yako ni ndogo sana. Tengenezeni mpango wa pamoja na Waziri wa TAMISEMI, halmashauri zielekezwe chini kila

halmashauri iwe na mpango kabambe wa matumizi bora ya ardhi na mpango kabambe wa miundombinu. Leo hii eneo pekee ambalo limefanikiwa ni Dodoma Jiji. Tuna *masterplan* 25 zinasemekana na mwaka huu nimeambiwa tano zimeongezeka lakini hizo *masterplan* ni *land use masterplan* na siyo *infrastructure masterplan.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri, Dar es Salaam ni *squatter city,* Mwanza ni *squatter city* na Arusha ni *squatter city*. Narejea, jiji pekee ililopangwa japo wengine hawapendi kusikia, Dodoma kwa sababu ndiyo mfano bora, nitasema. Sasa naeleza haya ili Mheshimiwa Waziri uchukue na kwa sababu una nia njema *brother* utafika mbali sana, nisikilize kwa makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimeeleza hapo kwa nini nasema *land use masterplan*. *Land use masterplan* yenyewe inaeleza wapi kuna maeneo hatarishi, wapi tujenge nyumba za makazi, wapi tuweke viwanda, wapi tuweke wawekezaji na wapi tuweke mashamba. Haya hayafanyiki, tunachofanya ni urasimishaji nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Waziri nikushauri, urasimishaji ubaki kwenye miji na majiji kwa sababu tumechelewa. Upangaji na upimaji uende kwenye halmashauri za wilaya bado hatujachelewa. Majiji ni matano tu na Manispaa kadhaa lakini halmashauri ni nyingi sana na nimesikitika kidogo Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yako. Unasema unaalika miji ilete mipango ya maeneo yaliyoiva, siyo kweli na siyo sawasawa hapo. Tusisubiri maeneo yaive, yakiiva maana yake ni *squatter* tunakwenda kufanya *upgrading.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba wote nchi nzima walete mipango kabambe kwa Mheshimiwa Waziri, tuipime nchi yetu, nahisi kama kumsukuma mlevi hivi. Mheshimiwa Waziri shirikiana na TAMISEMI utafika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite kwenye migogoro. Ameeleza vizuri sana Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake kuhusiana na aina ya migogoro nchini. Sasa nimsaidie migogoro miwili. Ipo migogoro inayosababishwa amesema na wataalamu

wake wa Sekta ya Ardhi. Hii kudhibitiwa, na ni rahisi sana, na mwarobaini wake ni *ILMIS (Integrated Land Management Information System)*. Huu ni mfumo fungamanishi wa kuhifadhi taarifa za Sekta ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu watumishi hawawezi ku-*tamper* kwa sababu hakuna hati pandikizi, huwezi kupata huko. Mfano mzuri Kinondoni huko nyuma wana historia, Kinondoni ilikuwa ni hatari sana, lakini wana *ILMIS* na sasa kidogo imepunguza migogoro kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. Sasa Mheshimiwa Waziri ahakikishe *ILMIS* inakuwa nchi yote, atakuwa amewabana watumishi wake wa Sekta ya Ardhi na hawataweza kufanya *double allocations.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *double allocation* naomba nitoe elimu hapa Bungeni na ikikupendeza unaweza kuongeza dakika nyingine za mtu mwingine kwa sababu natoa elimu. Hati pandikizi zinapatikaje? Hati pandikizi wataalamu wa ardhi wanafanyaje? Anakuja mtu mwenye fedha na anakuja mtu aliyetangulia mmiliki halali anaanza kuomba umiliki. Sasa yeye katika hatua za umiliki akija mtu mwenye fedha kile kiwanja kwa sababu ni muhimu anamwambia sikiliza bwana mdogo, kabla hatujazungumza kuna shilingi milioni tano mezani halafu jioni tutaonana. Kijana anachanganyikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yule anayekuja na fedha mfukoni nyaraka zile zinakuwa *backdated* (anapewa nyaraka zinazorudishwa nyuma ukilinganisha na yule mmiliki halali). Matokeo yake anakuwa wa kwanza kupata hati huyu anakuwa wa pili lakini *ILMIS* ndiyo mwarobaini, huo mchezo haufanyiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda pia nieleze namna utatuzi wa migogoro ya ardhi. Kuna utatuzi wa migogoro ya ardhi kiutawala na utatuzi wa migogoro ya ardhi kimahakama. Mheshimiwa Waziri siyo mamlaka ya mwisho ya utatuzi wa migogoro ya ardhi. Mamlaka ya mwisho ni Mahakama na ndiyo maana mimi Mheshimiwa Kunambi ukisema ardhi siyo yangu ukanitoa, naenda Mahakamani nakushtaki, nasema sijatendewa

haki. Mahakama ndiyo mwamuzi wa mwisho wa migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri tengeneza mfumo. Uzuri nchi yetu ina utawala bora; kuna kijiji, kuna kata na Waziri ni mamlaka ya rufaa. Sasa unakwenda na wewe utamaliza wilaya ngapi Mheshimiwa Waziri? Hotuba yangu ya mwaka 2023 nilisema kaka yangu nimeona ameanza kuwa na mvi. Sasa wasiwasi wangu, shemeji yupo hapa, hebu punguza hiyo. Tengeneza mfumo, yaani wewe ukiwa Wizarani pale ukikohoa, Mwenyekiti wa Kijiji cha pale kwangu Utengule aseme, naam! *Simple,* wala huhangaiki. Tutamshauri hata nje ya Bunge atafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa alivyonieleza kwamba ana siku 200 za kutatua migogogoro ya ardhi, nikajiuliza maswali, *my brother* anatumia nini au ni kalumanzila? Kwa kweli migogoro ya ardhi nchi hii ili iishe tupange, tupime, tumilikishe na tuwe na mpango wa Taifa kwenye jambo hili na tuwe *serious.* Eneo lingine mamlaka zote zinazohusika zitimize wajibu wake. Wewe uwe mamlaka ya rufaa pale, usimamie Sera ya Ardhi, ukifanya hivyo Mheshimiwa Waziri *I'm telling you my brother* utafika mbali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni migogoro ya vijiji 975. Nimeona kwenye hotuba yake kwamba ni migogoro 350 tu mpaka sasa. Kasi hiyo siyo sahihi. Mheshimiwa Rais hataki hayo. Dhamira ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuona wananchi wake wanaishi bila migogoro ya ardhi. Vijiji 975 sasa ni mwaka wa pili kama siyo wa tatu, tuna vijiji 350; *are we serious*? Sasa Mheshimiwa Waziri amepokea kijiti, nashauri kasi iongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano kule Jimbo langu la Mlimba, mpaka jana wananchi wangu wanachomewa mazao, wanachomewa nyumba zao kwa sababu ya migogoro ya ardhi na hawana amani. Mgogoro wa ardhi kati ya wananchi na *TAWA* na mgogoro wa ardhi kati ya wafugaji na wakulima, mwarobaini ni upangaji na matumizi bora ya ardhi. Mheshimiwa Waziri kwa kuwa ana nia njema, *all starts well ends well my brother* na nimekwambia nitakusaidia kukushauri vyema.

*(Hapa kengele ililia kushiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kunambi, naomba hitimisha tafadhali.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimishe. Ukisoma Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ukurasa wa 119...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, tuna changamoto ya muda na unatambua.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitimisha. Ibara ya 74 unaelekeza Wizara ya Ardhi kusajili vipande vya ardhi 2,500,000 kwenye miji na hatimiliki za kimila 2,600,000...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, naomba hitimisha hoja yako.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye vijiji; kasi ni ndogo. Sasa tunakwenda mwakani uchaguzi, tunafikia lengo la Ilani ya Chama Cha Mapinduzi? Kaka bado una kazi kubwa ya kufanya na Mungu akusaidie, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kunambi kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge wote mlioanza kuchangia tunawashukuru sana, tunafurahi michango yenu ni mizuri sana na inamsaidia Mheshimiwa Waziri.

Sasa namwita Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, ajiandae Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota. *(Makofi)*

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Nami niungane na waliompongeza Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Waziri Jerry Silaa. Mheshimiwa Jerry Silaa tangu umeteuliwa tumeona kazi yako

kubwa. Hizi *clinic* unazofanya na umekutana na wananchi wanavyolalamika, endelea hivyo hivyo na matarajio ya Mheshimiwa Rais na Watanzania walio wengi wanataka hii migogoro iishe na tuwasikilize wananchi. Endelea hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Pinda naye amekuwa akienda kwenye mikoa na wilaya na alikuja pia Kiteto. Endeleeni hivyo hivyo, mkiwasikiliza Watanzania na migogoro hii ikaisha, ndicho anachotamani Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na ndicho wanachotamani Watanzania wote. Tunataka migogoro ya ardhi iishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakupongeza Katibu Mkuu na timu nzima ya wataalamu, endeleeni hivyo. Ninyi ni Sekta ya Ardhi kwa hiyo mtoke sana mwende *field,* ndiyo matarajio ya Watanzania. Endeleeni hivyo hivyo. Ombi langu moja tu ni kwamba Kiteto tunamtaka Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi la Wilaya, mtuletee huyo kwa haraka sana. Kiteto ni kubwa na migogoro ni mingi, mkituletea Mwenyekiti wa kututembelea siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, leo nitajikita kwenye migogoro ya ardhi. Hii dhana ya migogoro ya ardhi ni kubwa. Ardhi ni uhai, ardhi ni mali, ardhi ni tamaduni za watu na maisha ya watu, hivyo, inahitaji utulivu, umakini, weledi mkubwa sana, utawala wa sheria na sheria itafsiriwe kama ilivyotakiwa na Bunge. Vilevile, inahitaji teknolojia kwa sababu nchi yetu ni kubwa, ili tuweze kupima na kupanga kiteknolojia, tena teknolojia sahihi sana ambayo ina *precision* nzuri ambayo haitengenezi migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro mingi sasa tuliyonayo, kila ukituma timu iende *field* inatengeneza ramani yake. Unaweza ukakuta mgogoro mmoja una ramani sita. Fedha zimetumika za Serikali halafu wataalamu wetu hawa wanatuangusha sana. Naamini kwamba utaalamu walionao wataalamu wetu ni wa kusoma *GPS,* kutumia mashine hizi na kusoma Sera na Sheria ya Ardhi lakini siyo wataalamu wa mapori ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima kushirikisha wananchi. Ni jambo muhimu mno unapokwenda *site* kutaka kufanya ile *GN* ifanye kazi, wasikilize wale walio na ardhi yao. Hii imekuwa tofauti, anakuja mtu anajifanya ni mtaalamu. Sasa ni mtaalamu kweli wa mipaka ya mapori yetu? Wewe ni mtaalamu, umesomea wapi mapori yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukifanya hivyo, watunze utaalamu wanaopata shuleni kutumia *GPS* na hizi teknolojia na namna ya kusoma *GN,* lakini inapokuja kwenye majina ya maeneo ya watu, msikilize watu. Haiwezekani mnakuja mnatuambia hapa, yaani mnajifanya kwamba ni mafundi mpaka wa vijiji vyetu na majina yetu na vitongoji na milima eti. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri awaambie watu wake wawe na weledi na washirikishe wananchi. Tukifanya hivyo migogoro ya ardhi nchi hii itakuwa imekwisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro inataka weledi kwa sababu inaleta ugomvi. Watu wanachotaka ni tafsiri sahihi za hizi *GN*. Pia, namna ya kufanya hivi ni kuwa na Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi yenye bajeti kubwa sana. Tunaambiwa hapa na Mheshimiwa Waziri kwamba kati ya vijiji 12,318 ni vijiji 4,126 ndivyo vitakuwa na matumizi bora ya ardhi. Kwa hiyo, kuna vijiji zaidi ya 8,192 visipopata majawabu migogoro haitakaa iishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuamue kama tunataka kumaliza migogoro ni lazima Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi iwe na pesa nyingi sana. Tupime vijiji kwanza, tukishamaliza na vijiji vikawa na hati na matumizi bora ya ardhi tutakwenda kwenye hiyo *individual tabling* tunayotaka. Huwezi kuwa na *individua tabling* kama vijiji havifahamiki mipaka yake. Nchi hii ardhi yote tuliyonayo hata naogopa siku hizi kutaja *statistics.* Ardhi zimegawanyika sehemu tatu; ardhi ya vijiji, ardhi ya hifadhi na ardhi ya jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunaambiwa ardhi ya vijiji ni 70% sijui siku hizi imefika ngapi. Ardhi ya hifadhi tulikuwa tunajua ni 28% sijui siku hizi imefika ngapi na *general land* ilikuwa ni asilimia mbili, lakini siku hizi ni *vice versa.* Mheshimiwa Waziri ni Mwanasheria na Naibu wake ni Mwanasheria, wanafahamu

kuwa ardhi ikishaitwa hii ni ya kijiji ni ya kijiji. Ardhi ya kijiji kwa mujibu wa sheria yeye anafahamu, kuna aina tano ya namna ya kutambua ardhi ya vijiji, kwanza kama kijiji kina hati na imepimwa na hiyo inajulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa mujibu wa kifungu 22 ya Sheria ya Serikali za Mitaa, watu wa TAMISEMI, *that is known*. Ardhi nyingine ni kijiji kilichoanzishwa kwa ile Sheria ya *operation* vijiji. Nyingine ni ardhi ambayo wananchi wamekuwa wanakaa tu ama ardhi ambayo vijiji vimekubaliana ama ardhi ambayo watu wamekaa wanaishi kwa maisha ya kijijini kwa zaidi ya miaka 12 baada ya Sheria ya Ardhi kuwa imepitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lugha nyepesi, popote wanakoishi wananchi sasa ni ardhi ya vijiji *whether* wana hati ama hawana kwa mujibu wa sheria. Wakati mwingine Wizara na Mheshimiwa Waziri anafahamu, Kifungu 185 cha Sheria ya Ardhi, linapokuja suala la ardhi yeye ndio mkubwa kuliko Waziri mwingine yeyote. Sasa sijui wanaogopana ama sijui ni nini? Waziri aweke mguu chini, yeye ndiye mwenye dhamana ya ardhi, yeye ndiye anayetakiwa atutafsirie ardhi ya kijiji ni wapi? Ardhi ya hifadhi ni wapi? *General land* ni wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiona wale wa maliasili wanakuja kugombana na wanakijiji; amesema Mheshimiwa Kunambi hapa kwamba wanawachomea watu nyumba. Ukiona wale wanafika mpaka kwa wananchi, *there is something wrong,* hamfuati sheria. Kimsingi watu wa maliasili walitakiwa waende kwa Waziri waseme, tunaomba uje utuambie mipaka ya vijiji inaishia wapi? Halafu wao wapotee, hawarusiwi kwenda kwa watu. Waziri ndiye anatakiwa aje atutafsirie na kama ni fidia, yeye ndiye aje atuambie tunapataje fidia kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tukisimamia mipango hii na akasimama vizuri kama Waziri wa Ardhi, hakuna migogoro hapa. Mkiwaacha kila mtu achore ramani yake anavyotaka kama wanavyofanya wale watu wengine, sasa migogoro itaisha lini? Kwa mfano, Kiteto tumekuwa na mgogoro wa muda mrefu kati ya Manyara na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Ardhi 2015, juzi tu wamekuja timu kutoka Ofisi ya Takwimu, Wizara hii na Ofisi ya Waziri Mkuu, imetengenezwa ripoti ya kusema ni tathmini na mipaka, mkatuchorea ramani za vijiji na hati mkatupa. Halafu wengine wanakuja miaka mitatu baadaye wanasema wale walikosea. Sasa twende wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro mmoja unakuwa na ramani na ripoti sita au saba, wanawa-*confuse* wananchi *unnecessarily.* Hiyo waache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri aje Orkiush kwa ajili ya mgogoro wa Orkiush na Mkungunero. Sasa hivi tunachotaka ni tafsiri sahihi ya ramani ya Mkoa wa Manyara na Dodoma, *period*. Kwa hiyo, tunahitaji *equipment* ambazo ni *precision,* ambazo hazitakuwa na *error.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ule mgogoro nikikuletea ramani zake utashangaa sana, kuna michoro zaidi ya mitatu na tume tatu, kila mtu ana ramani yake. Hapo mwananchi atakwenda wapi? Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri akisimamia hilo tutatoka vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ipo kwa sababu wananchi hawashiriki. Nilikuwa nasoma hotuba yake hapa, mgogoro wa kwetu na Tanga huko Kilindi; kweli kwa mujibu wa *GN* inaonekana umemalizika, lakini *imagine GN* inatengenezwa, na unajua *GN* inavyosema, kwamba ikiwa mamlaka haijapewa *objection* yoyote kwa hiyo tunafanya hivi. Sasa wasipotutangazia, na tukiwa na *objection* tutaleta wapi kama mambo yanaishia kwenye *GN* na ofisini? Je, yule mwananchi ambaye alitakiwa kuleta *objection* ataona wapi? Wasimamie na tufuate utawala wa sheria. Tukifuata sheria vizuri migogoro hii itakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Mheshimiwa Waziri wakati mwingine ana mamlaka akiona hizi tume hazileti majawabu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mbunge, tunakushukuru.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, tunakutakia kila la heri Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Issa Juma Mtemvu atafuatia Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda ajiandae.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa mafungu yake mawili; Fungu Na. 48 na Fungu Na. 3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia nami nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya kwenye nchi yetu. Ni dhahiri kila Mtanzania anajua kazi inayofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa haraka nitumie nafasi hii kuipongeza sana Wizara kwa ujumla; kamisaa wetu Mheshimiwa Jerry William Silaa na kaka yangu Mheshimiwa Mizengo Pinda Geophrey, pia nisiache kwa watendaji wakiongozwa na Mhandisi Sanga, Katibu Mkuu; Naibu Katibu Mkuu pamoja na wataalam wao wote. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri ambayo na sisi Waheshimiwa Wabunge tunaithamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nijielekeze kwenye maeneo mawili tu. Eneo la kwanza ni eneo la urasimishaji likienda sambamba na migogoro ya wawekezaji dhidi ya wananchi wetu au ya maeneo. La pili, ni eneo hili ambalo wengi wamelizungumzia. Kuhusu Fungu Na.3 la Tume yetu ya Taifa ya Mipango na Matumizi ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la urasimishaji ni sehemu ambayo katika kipindi changu cha miaka mitatu, na huu wa nne, nimekuwa nikilisema kila tukiwa tunachangia bajeti. Naipongeza sana Serikali, imefikia pazuri, tofauti na tulipoanzia; na hapa

mlipofika mpaka leo mmepata mkopo wa Benki ya Dunia wa shilingi bilioni 345 na mmejielekeza nazo kwenye maeneo ya Dar es Salaam huko ili kuondoa migogoro kupitia dawati au Kliniki ya Ardhi. Pamoja na maeneo mengine, huko kwenye nchi yetu, mimi napongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwenye hili eneo, Waziri akiwa ni mdau wetu wa Dar es Salaam, pia naomba sana waongeze kasi. Kamati imesema ina shaka juu ya huu mradi wetu wa *LTIP* kama unaweza kwenda sawa kama tulivyokusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aongeze kasi kwenye madawati hayo ili mpaka tunafikia uchaguzi wetu Dar es Salaam, nami nishukuru sana viongozi wangu wa Mkoa wa Dar es Salaam wako hapa, wametambulishwa, nashukuru, lakini watambue wazi sasa hivi hii ndiyo agenda yetu Dar es Salaam. Urasimishaji kama hatutoboi na kule nje patakuwa ni balaa. Hili ni jambo jema, nimemwambia tukiwa ndani na tukiwa wawili; na hapa nalisema wazi kwenye Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine kwa ujumla wake ni hili jambo la usimamizi wa ardhi na wawekezaji. Nchi yetu imefanya sensa kwa zaidi ya mara tano hivi; mwaka 1967, tumefanya tena mwaka 1978. Mwaka 1967 ilikuwa na watu milioni 12, mwaka 1978 milioni 17, mwaka 1988 tukafanya tena tukawa na watu milioni 23, mwaka 2002 tukafanya tena sensa tukawa na watu milioni 34, mwaka 2012 na mwaka 2022 tukawa na watu milioni 61. Kwa sensa ya mwaka 2022 Bara ina watu milioni 59.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka kusema kwamba nimeona hoja ya wawekezaji, nami naipongeza sana Wizara, wamekuwa wanayo nia ya kuingiza wawekezaji 151 kutoka nje na wawekezaji 65 kutoka ndani, jumla yake ni takribani maombi 216, amesema Mheshimiwa Waziri, nampongeza sana. Amezungumza kuwa hawa wa nje wana matarajio ya kumwingizia mtaji wa zaidi ya dola milioni 58.95 au bilioni 152. Hili ni jambo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipo kwenye hao wa ndani ambao kwa sasa kwa mwaka huu wamewafikiria maombi yao

kama 65 hivi. Kwenye historia ya nchi yetu kuanzia miaka ya 1980 tumekuwa na wawekezaji uchwara. Hizi lugha ngumu sana, nitakuwa najitahidi kujifunza Kiswahili. Nataka nimpe mfano mmoja, tunaye mwekezaji wa tangu mwaka 1984 mpaka 1987 alifika ndani ya kijiji Jimbo la Kibaha Vijijini kwa ndugu yangu Mheshimiwa Mwakamo hapa, sisi wengine ni Wazaramo, wakati huo huo ni Waluguru; ndiyo humo humo kwetu kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwekezaji huyu ameingia akapewa ekari 200 vizuri tu. Alipopewa ekari 200 amekaa kwa kipindi cha zaidi ya miaka 15, anatoka anawaambia wananchi pale kwamba mimi nina ekari 2,500. Ekari 2500 ni kama vijiji viwili vya Lupunga na Kikongo, hatari sana. Vilevile wapo watu pale ndani ambao walikuwa ni sehemu ya ajira kwenye kulima mchicha kwenye ekari 200, na kesho yake wanakuja kuambiwa kuwa hata wewe tulikununua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida ni kwamba mwekezaji wa aina hii anafika anaulizwa, onyesha hati, hati haionyeshwi, anawaambia tu kwamba kuna hati. Sasa hebu onyesha pale nilipokuuzia mimi, anasema nilinunua mikorosho, kwangu hakuna mikorosho, nilipewa tu zawadi hata maeneo ambayo hakuna mikorosho, lakini kuna viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata juzi nilikuwa nasema hapa, kuwa nyie viongozi wakubwa, Katibu Mkuu na Waziri ni wa kuteuliwa, kila siku mnabadilishwa, lakini kuna wataalam wetu huku chini ambao ni changamoto. Sasa eneo kama hili nilitegemea *RC* wangu awe anafika ndani kwenye mashamba ili ajionee. Wanayetaka kumtoa leo ana mti wenye unene wangu, wanayetaka kumwingiza hajawahi kulima hata mchicha, wamempa leo ana miaka 40 ilhali sheria na sera inazungumza miaka 12. Wanasimamia sheria ya wapi? Kwa nini wananchi wanaonewa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiacha hoja hii, nilizungumzia sensa ili uweze kuona kwamba kama mwaka 1978 au 1988 ambapo kulikuwa na watu 23,000, leo watu 59,000 kwa mujibu wa mambo ya ardhi; watu 59,000 ambao ni vijiji viwili anawapeleka wapi hawa? Mheshimiwa Waziri hili analijua vizuri, atarajie kwenda

kule akamwokoe Mheshimiwa Mwakamo na akakiokoe Chama Cha Mapinduzi ndani ya Wilaya yetu ya Kibaha Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nilizungumza kuhusu Fungu Na. 3 – Tume ya Taifa ya Mipango. Wengi wamesema lakini mimi nitapenda kusema kwa takwimu. Mimi nimekuwa nikishangaa sana, na hapa nizungumze tu kwamba napongeza ule mradi wa *LTIP* wa dola milioni 150, takribani shilingi bilioni 345. Pamoja na mambo mengi, mwaka jana tulimwambia Waziri mwenye dhamana aliyekuwepo wakati huo, Mheshimiwa Dkt. Angellina Mabula, tukasema hizi ni fedha nyingi, wameweka mipango mingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie, wamekusudia kuingiza takribani vijiji visivyozidi 1,667 kwenye upimaji huu, tena baada ya maboresho, na vijiji hivi kwa thamani ya kupima kijiji kwa shilingi milioni 15, maana yake anatarajia kuweka shilingi bilioni 25, hazizidi hapo. Kwa hiyo, ndani ya hizo fedha zote za mkopo atatuambia hapa hajachukua zaidi ya shilingi bilioni 23, ndizo alizoziingiza kwenye kupima ardhi za vijiji, tutapima kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Olelekeita amemaliza kusema hapa, na Mheshimiwa mwingine ndugu yangu wa Dodoma amezungumzia kuhusu nia njema ya kupima. Kama tungepima, tungetambua wazi kwamba kuna maeneo ya malisho yangehitajika na tungejua ya kilimo, makazi, uwekezaji, miundombinu ya barabara, huduma za jamii na hifadhi za misitu. Mheshimiwa Olelekeita ameuliza ni asilimia ngapi hii? Hatujui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, kaka yangu Mheshimiwa Bashe, katika miaka yake miwili ametafuta shilingi bilioni 700 humu ndani. Ameanza na shilingi bilioni 249, mwaka wake wa kwanza tukamwekea shilingi bilioni 700, wa pili shilingi bilioni 900 na huu wa tatu shilingi trilioni 1.1, *over seven hundred billion*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jerry Silaa, miaka miwili anahitaji shilingi bilioni 120 kupima vijiji 8,400 alivyobakiza 120. Kwa nini yeye akose ndani ya Bunge hili? Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, *capacity* yake ya kufanya katika kipindi

cha mwaka mmoja ni *capacity* ambayo inaweza ikampa takribani vijiji 1400; na ukimpa kwa shilingi milioni 15 maana yake anahitaji shilingi bilioni kama 20. Sasa katika shilingi bilioni 20 leo wanampa shilingi bilioni tano! Kwa shilingi bilioni tano aliishia kupima vijiji 300. Sasa si ataishia vijiji 400! Tunakwenda wapi? Anahitaji miaka 19.6 au miaka 20 kupima vijiji vyote 8,400 vilivyobakia. Haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge humu ndani kwa nia njema tumsaidie Mheshimiwa Rais, maana siasa ya Chama cha Mapinduzi zipo ndani ya upimaji wa vijiji kutokana na faida ya upimaji wa vijiji hivyo. Tukipima vijiji ndipo tutaona vizuri, hata lile jambo zuri la kilimo la Mheshimiwa Bashe lingeenda vizuri. Tutajua anaishia hapa, wafugaji wanaishia hapa, wawekezaji wanaishia pale, huduma za jamii wanaishia kule, eneo la misitu linaishia pale, malisho yanaishia huku. Tunaanzia juu tunashuka chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, turudi kwenye vijiji. Kwa mwaka huu apewa shilingi bilioni tano kwa ajili ya maendeleo ili kupima vijiji 400, haimtoshi. *Capacity* yake ni vijiji 1,100 au 1,400. Tukimpatia shilingi bilioni 20 angalau atatumia miaka mitano kupima vijiji vyote 8,000 vilivyobakia. Hili ni jambo la msingi na jambo la muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nitumie tena nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kumwona yeye kama kamisaa anayetufaa kwenye Wizara hii. Anaendelea kuwa na macho makubwa ya kuona dira ya Taifa inakotaka kwenda. Tunaendelea kumwombea dua Mheshimiwa Rais ili Mwenyezi Mungu ampe karama kubwa, aliyonayo iongezeke mara dufu na Mwenyezi Mungu aendelee kumjalia hija na haja ya kuendelea kutuhudumia katika kipindi kinachokuja 2025/2030,…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** …tupo kwa ajili yake na tutahakikisha kura zote zinakwenda kwake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi, naunga mkono hoja kwa asilimia zote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa namwita Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, atafuatia Mheshimiwa Kilumbe Shabani Nge'nda na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara ajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niungane na wenzangu kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri Jerry Silaa kwa kazi kubwa ambayo anaifanya, hongera sana. Pili, nampongeza Mtendaji Mkuu wa Wizara hii Injinia Sanga kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Vilevile nawapongeza Wakurugenzi na Watendaji wengine katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa uteuzi ambao ameufanya. Wale ambao tunamwelewa Mheshimiwa Jerry Silaa, hatukushangaa kwa haya ambayo anayafanya. Mheshimiwa Jerry Silaa amekuwa *Mayor* wa Jiji la Dar es Salaam, na mengi ambayo yanafanyika leo Jijini Dar es Salaam ni mipango mizuri na mikubwa ambayo Mheshimiwa Jerry Silaa aliifanya, ambaye alishika umeya akiwa *Mayor* kijana kwa Afrika Mashariki. Kwa hiyo, ubunifu wake na ujasiri wake. Tunaona ujasiri wake kwa sababu hatukujua sisi kama kuna mapapa sita wa tasnia ya ardhi, lakini amewaleta hadharani. Amemchomoa papa mmoja baada ya papa mwingine. Vilevile na uzalendo wake, kwa sababu mengine angeyamaliza gizani tu lakini akaamua kuleta hadharani kwa manufaa ya nchi yetu. Si hivyo tu, na uthubutu, kwa sababu hivi vitu vinahitaji moyo wa uthubutu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, mimi nawapa moyo kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Macho ya Watanzania yanawaangalia na kila siku wanaombewa. Ndiyo maana kama alivyosema msemaji mmoja kwamba hata viongozi wa dini wanawaombea. Wameokoa mali za misikiti, wameokoa mali za makanisa, wameokoa mali za

wanyonge na wanasimamia haki. Hongera sana na Mwenyezi Mungu atawalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa kwanza utahusu ikama ya watumishi wa sekta ya ardhi. Kazi hii nzuri ambayo inafanywa huku juu na Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Kamishna na watu wengine, matunda yake yanaonekana kwa uchache sana huku chini kwa sababu ya upungufu mkubwa wa watumishi wa sekta ya ardhi katika maeneo yetu. Nimepitia baadhi ya taarifa, ikama ya watumishi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwenye kitengo cha ardhi ilitakiwa kuwe na watumishi wasiopungua watano. Kuwe na Afisa Ardhi, Afisa Mipango Miji, Mpima na Mthamini wa Majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Waheshimiwa Wabunge wote watakuwa mashahidi, katika maeneo yetu ni nadra sana kupata ikama kama hii. Kwenye Halmashauri yangu ya Mji wa Nanyamba tuna mtumishi mmoja tu kwenye kitengo hiki. Sasa migogoro inaanzia hapo, kwa sababu yeye hawezi akawa Afisa Ardhi wakati huo huo awe Afisa Mipango Miji, halafu achukue *tape* aende kuwa mpima na baadaye awe mthaminishaji. Kwa hiyo, naomba, ili kazi nzuri ambayo inayofanywa kule juu na Waziri na Naibu wake na watendaji wengine kule juu katika maeneo yetu ya upangaji, kwa mfano, kwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa, basi Wizara hii ipewe kibali maalum ili watumishi wa kada ya ardhi waweze kuajiriwa na kupunguza hili tatizo lililopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi sasa ifanye msawazo. Pamoja na uhaba mkubwa uliopo kuna maeneo mengine watumishi wa ardhi wamelundikana, wako wengi, na ndiyo maana sehemu nyingine ina wachache, kwa hiyo, ni muda muafaka sasa waangalie *staffing level* katika mikoa yetu, katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ili tuhakikishe kwamba na maeneo mengine tunapata watumishi wa kutosha ili mipango mizuri ambayo imetajwa, iliyowasilishwa na Waziri wetu, iweze kutekelezwa kwa umahiri na kwa ufanisi unaotarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili unahusu hii programu ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Ni mpango

mzuri na ni mradi mzuri ambao unatekelezwa katika maeneo yetu. Hata hivyo, tumeona hapa kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri pamoja na Kamati, kwamba bado kuna halmashauri hawajarejesha fedha ambazo walikopeshwa. Fedha zilizopelekwa ni shilingi bilioni 50 lakini hadi sasa zimekusanya shilingi bilioni 23.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mkopo ambao hauna riba, ni kama *revolving fund*. Zile halmashauri ambazo zimefanya vizuri tunawapongeza; na wameorodheshwa kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri, lakini zile halmashauri ambazo hawajarejesha, naomba TAMISEMI wasiwaachie Wizara ya Ardhi tu, washirikiane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa TAMISEMI kwa sababu alitoa tamko kwamba hadi tarehe 30 Juni hizi halmashauri ambazo hazijarejesha, basi wawe wamesharejesha, la sivyo, hatua nyingine zitachukuliwa. Kwa hiyo, naomba TAMISEMI na Wizara ya Ardhi watembee kwenye hili agizo lao ili wale ambao ikifika tarehe 30 Juni watakuwa bado hawajarejesha hizi fedha zikatwe moja kwa moja kutoka kwenye ruzuku zao ambazo wanapewa ili halmashauri nyingine waweze kukopeshwa na waweze kutumia katika mipango yao ya kuendeleza ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine unahusu mpango wa matumizi bora ya ardhi. Kwenye taarifa ya Waziri hapa amesema vizuri kwamba tuna vijiji 12,316 lakini vilivyopimwa ni vijiji 4,011, na kazi iliyobaki ni kwenye vijiji 8,305. Hapa nilikuwa natafuta fedha za kufanya kazi hii. Kwenye hii bajeti fedha hatuioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naiomba Serikali, kama alivyosema mchangiaji aliyepita, tutafute fedha kwa ajili ya shughuli hii muhimu na nyeti. Fedha hii tukiipeleka Wizara ya Ardhi tunaipeleka mara moja. Uzuri tukishapima vijiji vyote 8,305 vilivyobaki hatutarejea tena kama madarasa au nyumba za walimu, kwamba baadaye zitachakaa na tutakarabati. Tukishatoka na mpango wetu wa matumizi bora ya ardhi, utakuwa huo unatumika kwa miaka hiyo yote, tutakuwa tunafanya maboresho madogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo fedha ambayo inatakiwa takribani shilingi bilioni 125, naomba Serikali itafute mahali popote pale tuipe Wizara ya Ardhi ili kazi nzuri ambayo inafanywa na Waziri huyu mbunifu, Waziri mchapakazi, Waziri ambaye ana maono mapana, Waziri ambaye ana uthubutu, basi aweze kukamilisha kipindi hiki na aandike historia kwamba wakati wa uwaziri wake alikamilisha vijiji vyote 8,305 vilivyobaki. Hili linawezekana. Kama tumefanya hivyo kwenye Wizara nyingine, basi na Wizara hii ambayo ni nyeti, Wizara ya Ardhi, tutafute fedha ambazo zitakwenda kuleta matunda ambayo kwanza tutapunguza migogoro iliyopo sasa hivi kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vyetu tukipangilia vizuri na tukitengeneza mpango wa matumizi sahihi ya ardhi vijijini, hii migogoro ambayo ipo sasa hivi itapungua. Siyo hivyo tu, itakuwa rahisi wawekezaji watakapokuja tayari tutakuwa tumetenga maeneo mahususi kwa ajili ya uwekezaji na hivyo wawekezaji watapatra ardhi kwa kipindi kifupi na badala ya muda wanaoutumia sasa hivi kiutafuta ardhi kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali hii kwa sababu ni Serikali sikivu na kwa kuwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameamua kuisimamia ipasavyo sekta hii ya ardhi, nina matumaini makubwa kwamba kama mwaka huu itakosekana, basi tuiweke kwenye mipango yetu ili mwakani fedha hizi zipatikane. *Insha'Allah* kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu Waziri Silaa bado ataendelea kuwepo kwenye Wizara hii, akamilishe kazi yake na kwa ubunifu wake basi atakuwa ameandika kitabu kizuri kwamba alipokuwa Waziri wa Ardhi amekamilisha upangaji wa vijiji vyote 12,516 vya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa kuzingatia muda. Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Mwikwambe Waitara, Mheshimiwa Halima James Mdee, ajiandae.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kuendelea kutupatia afya na uhai wa kuendelea kuwatumikia wananchi waliotuchagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Mheshimiwa Jerry Silaa katika kuwakaribisha viongozi wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Dar es Salaam katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. nasema hivyo kwa sababu, kama angekuwa amepata nafasi hii kwa miaka minane iliyopita, basi nami ningekuwa miongoni mwa waalikwa maana nilikuwa Katibu wa CCM Dar es Salaam. Pia ukimsifu Mheshimiwa Jerry katika kazi anayoifanya, nipe na mimi sehemu kidogo ya sifa kwa sababu nimechangia malezi yake huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya kupata uhuru wa nchi yetu, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Baba wa Taifa letu alitangaza maadui watatu wakubwa wa Taifa letu na akatangaza mambo manne makubwa ambayo yanaweza yakafanyika ili tuendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadui hao watatu alitangaza; ujinga, umasikini na maradhi. Kila Mtanzania akawa anajua kwamba hawa ndiyo maadui wakubwa wa Taifa letu, lakini akasema ili tuendelee tunahitaji mambo manne; watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumza juu ya ardhi yetu tukitathmini maneno haya ya Baba wa Taifa letu. Yapo mambo ambayo mimi ningependa kutumia nafasi hii kwanza kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Vilevile, kumpongeza Waziri mwenye dhamana, ndugu yangu Mheshimiwa Jerry Silaa, Naibu wake *Comrade* Askari wa Jeshi Mheshimiwa Pinda pamoja na watendakazi wote wa Wizara. Ukijua kulaumu, ujue na kusifu maana haya mambo yote duniani yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma kabla ya juhudi zilizochukuliwa na Serikali hii chini ya uongozi wa Mama Dkt. Samia

Suluhu Hassan, Mkoa mzima tulikuwa na watu wanaomiliki ardhi kwa hati zilizo rasmi 5,426, mkoa mzima, lakini ndani ya muda wa kipindi kifupi ambacho maboresho makubwa yamefanyika na hiyo ni Julai, 2020 kuja Mei, 2024 wameongezeka watu 7,301. Kwa hiyo, kuna kazi kubwa. Kazi iliyofanyika tangu uhuru ni 5,426, kazi iliyofanyika kwa miaka mitatu 7,301 nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi ya CCM Ibara ya 74 imeelezea mambo muhimu ambayo Serikali ya CCM itayasimamia katika sekta ya ardhi. Ikasema, kwanza ni upangaji; pili, ni upimaji; na tatu; ni umilikishaji wa ardhi. Kazi hii ni muhimu sana. Ukishapanga ardhi na kupima ardhi unapata mambo mawili ndani ya jambo hilo, moja. Unaondoa migogoro ya matumizi ya ardhi; pili, unaongeza wigo wa kodi na pato la Taifa kupitia ardhi. Kwa hiyo, mimi nimtie moyo sana Mheshimiwa Waziri kwamba, kazi anayoendelea nayo ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi aongeze kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili nilitaka achukue changamoto hii. Kulikuwa na utaratibu wa kurasimisha makazi ambapo Halmashauri yangu ya Manispaa ya Kigoma Ujiji ambayo mimi ndiyo Mbunge, iliingia kwenye utaratibu huu, vikaja vikampuni vingi vingi vya kupima ili watu warasimishiwe makazi. Nashukuru mmechukua hatua maana kulikuwa na matatizo makubwa kwenye Kata ya Machinjioni, Lubuga, Bangwe, Kitongoni na Kibilizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watu wa Ofisi ya Ardhi pale wamefanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha yale matatizo yaliyokuwepo ambayo yametokana na yale makampuni yaliyokuwa yamepewa kazi, wameyarekebisha na watu wameanza kupata hati kwa kasi kubwa sana. Ahsante sana tunashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado nawaomba mwendelee na juhudi hii katika Kata ya Kibilizi ambayo maeneo ya Bushabani na Kigamboni bado yana tatizo na Kata ya Kitongoni kule Ujiji nayo bado ina tatizo. Mheshimiwa Waziri nataka niseme juhudi mlizozichukua ikiwa ni pamoja na kupunguza ada ya maombi kutoka 20,000 mpaka 5,000,

kupunguza ada ya utayarishaji wa hati kutoka 50,000 mpaka 25,000 na kupunguza kiwango cha kulipia *deed plan* kutoka 20,000 na kuwa *free,* haya mambo yamechochea sana wananchi wengi kujitokeza kupata hati. Kwa hiyo, endeleeni na jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nimalizie jambo moja. Kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 Ibara ya 74(e) kinaeleza hivi, "kuimarisha mfuko wa fidia ya ardhi ili uweze kufidia ardhi itwaliwayo (inayochukuliwa kutoka kwa wananchi) kwa matumizi ya umma na kwa uwekezaji." Hapa bado kuna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mfuko sijui upo au haupo! Sikusikiliza vizuri wakati unaunasoma, ukija hapa utanielezea vizuri kama upo na una kiasi gani cha fedha, maana hapa napo tunakumbana na matatizo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ya wananchi katika maeneo mengi inachukuliwa, na kufidiwa inakuwa shughuli. Wengine wamekaa ardhi yao imechukuliwa miaka mitano na hawajapewa fidia. Hili jambo linasononesha sana. Hivi leo nilivyosimama kuzungumza hapa kuhusu upanuzi wa Uiwanja cha Ndege wa Kigoma tayari kuna wananchi maeneo yao yamepimwa na wameambiwa wasiendeleze chochote wasubiri fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni zaidi ya miezi saba hawajapata fidia, hawawezi kujenga choo, mvua zinanyesha zinaharibu maeneo mbalimbali, wanasubiri fidia na fidia hazipatikani. Mbaya zaidi mnavyochelewesha kulipa fidia kwa mujibu wa sheria na taratibu za *evaluation* ikishapita miezi sita ni lazima mwongeze tena asilimia kwenye zile fedha. Kwa hiyo, chukueni maeneo ambayo mko tayari kuyalipia kwa sababu mtayalipia kwa kiwango hicho bila kuongeza gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo pale Kigoma la *Kigoma Special Economic Zone* nalo bado lina kelele kelele. Wapo wananchi wanalalamika, wengine wanasema hawajalipwa fidia, wengine wanasema tumelipwa, wengine wajanja wajanja wakaingia hapo. Mheshimiwa Waziri, hii ni kazi yako yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ni watumishi wa ardhi. Tunaomba Waziri atusaidie, ile ardhi watumishi wake watachochea sana mapato ya kodi ya ardhi kwenye nchi yetu. Kama tulivyotoa *priority* kwa watumishi wa *TRA* kuongezwa ili wakusanye kodi, na hawa waongezwe ili wawe wa kutosha na kodi iweze kupatikana nyingi kwenye ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shabani Ng'enda. Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima James Mdee.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Namshukuru Mheshimiwa Rais, ameanzisha Haki jinai na bahati mbaya sana hajafika katika Wilaya ya Tarime na Mkoa wa Mara, sijui kama maeneo mengine lakini kwangu haijafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Haki jinai ikienda kule Tarime, ikaenda maeneo ya Sirari itakutana na watu ambao wamepigwa na mipini. Ikienda Hifadhi ya Serengeti itakuta kuna wajane kule wana makovu, miguu na macho hawana. Ukienda kule Nyamongo kuna mambo mengi; wajane, yatima na walemavu, wote yaani raia na askari ni kama uwanja wa vita. Kwa hiyo, ningeomba hii Haki Jinai iende kule Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Waziri Mkuu alifanya ziara katika Mkoa wa Mara na Wilaya ya Tarime. Alisimama maeneo ya Nyamwaga ambako ni karibu na Machimbo ya *Barrick North Mara,* akatoa maelekezo kule na wananchi walijitokeza kuuliza maswali mbalimbali. Kuna fidia mbalimbali zimefanyika katika eneo lile kwa maana ya Nyamwaga yenyewe, Komarera, Nyakunguru, Kewanja na *Komarera North*. Pia ikaonekana Mthamini Mkuu wa Serikali alifanya tathmini katika maeneo hayo, lakini baadaye ikaonekana gharama ni kubwa, kwa hiyo, watu hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiongozi yeyote wa Serikali akifika katika maeneo hayo, hoja ya kwanza ya wananchi ni fidia ya *Komarera North*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi pamoja na wenzake naomba, jambo hili; nilikwenda pale kwenye Kliniki ya Ardhi nikaonana na watu wake. Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa yuko tayari, watu wa ardhi wapo tayari, aongee na mtu wa Madini watafute gharama wakasikilize hawa wananchi. Wananchi wanachanganya, kuna watu ambao wana haki na wengine hawana haki. Ukiwasikiliza utatenganisha mwenye haki na yule ambaye hana haki ili mwenye haki yake aweze kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wetu ni mgumu sana, kila akienda kiongozi hata kama una nia njema, ni lazima kwenye kikao chochote hoja ya fidia ya eneo hili iibuke. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ningeomba jambo hilo ilifanyie kazi na kwa kuwa wapo viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mheshimiwa Jerry tunafahamiana sana, tumekuwa *Mlimani Faculty of Science,* nilikuwa Mbunge wake, Mwenyekiti wake na Rais wake wa Chuo, Mwenyekiti wake wa Mtaa, tumegombea Ubunge.

Mheshimwia Mwenyekiti, sasa Mwenyekiti wa Mkoa yuko hapa, ili nisirudi tena Ukonga, Mzee fanya kazi kule Tarime, rahisisha mambo yaende sawasawa. Mimi nimezoea siasa, hata ukiniacha watu wakaanza kunishughulikia kule kwa fidia, maana yake nitarudi pale Kivule Mwembeni na sitakaa kimya tutasumbuana. Nakutakia kila la heri, chapa kazi, lakini weka nguvu kule Tarime ili watu wangu waweze kupata fidia, inakuhusu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Olelekaita amezungumza hapa, Mheshimiwa Waziri ni kweli katika vijiji 975, Jimbo la Tarime Vijijini nina vijiji saba. Shida kubwa ni watu kusikilizwa, yaani watu wenu wataalamu wakienda kule wana majibu, ramani na wameshachora mipaka. Unamwambiaje mtu kwamba siyo kwake na ameshakaa miaka 70, anakuonesha makaburi, mikahawa na kila kitu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani mwende mkawasikilize watu na mgogoro huu umesimama kidogo baada ya Wakuu wa Mikoa angalau kuelewa hali halisi ya kule kwetu,

lakini tunaomba mgogoro huu uishe, wananchi wasikilizwe, mpitie mipaka, kwa sababu hii nchi ni ya kwetu sote. Kama hifadhi wana haki na wananchi wana haki ya kuishi. Kwa hiyo, lazima Wizara iweze kufanya kazi kutusaidia vizuri katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza Mheshimiwa Rais, amefanya mabadiliko katika Mkoa wa Mara. Nataka nimwambie Kanali Mtambi na Kanali Surumbu Maulid, mapokeo ilikuwa ni kwamba tumepokea wanajeshi hapa, lakini nataka niseme na nadhani Wabunge wenzangu watanikosoa, lakini Mkuu wa Mkoa pamoja na *DC* wetu katika Wilaya ya Tarime ameanza vizuri. Amefanya ziara, amesikiliza watu na ni kwa kuwa anafanya kazi kama raia. Kwa hiyo, naomba waendelee kuchapa kazi na wawasikilize. Watu wa Wilaya ya Tarime na Mkoa wa Mara wanataka kusikilizwa, hawataki mabavu, ukiwasikiliza mtafanya kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la ardhi na mgodi, mimi kama Mbunge wa Tarime Vijijini ambako *Barrick* ipo kwa kweli wamefanya kazi kubwa sana. Mambo mengi yamefanyika na huduma za kijamii na watu wa Mgodi wa *Barrick* na watu wa Ardhi wakikaa vizuri. Kwa mfano, kule kwetu unalichukua eneo la mtu ambalo anajua kwamba chini kuna dhahabu, halafu unamwambia ekari moja ni shilingi 5,000,000 lakini mtu huyu huyu ukimpeleka eneo la Itiryo, kule Kiyongera ukienda unaambiwa ekari moja ni shilingi milioni 30. Sasa nakuuliza, hivi sina akili kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lenye dhahabu chini eka moja ni shilingi milioni tano, eneo la kuchimba choo eka moja ni shilingi milioni 30, wapi na wapi hii? Hata hivyo, ukiuliza watu wa Ardhi wanasema sisi tukija kama wawekezaji tukija Tanzania tunafuata sheria zenu. Kwa hiyo, tumegundua wanaoumiza wananchi wetu ni Serikali, Wizara ya Ardhi na wadhamini. Kwa nini msiweke bei kubwa? Mmtu anajua kwamba hapa kuna dhahabu, kwa nini msiweke bei kubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana leo ninaposema hapa, kwa mfano, nimesema nimwombe Mungu labda nizungumze taratibu. Maana yake humu nimeshalia sijasikilizwa,

nimerukaruka kichura sijasikilizwa, sasa sijui nifanye nini? Nimevua koti bado imekuwa ngumu. Sasa naongea kwa upole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tunapozungumza kuna msiba mkubwa sana pale Nyamongo. Tarehe 22 saa saba mchana vijana wangu waliji-*organize* kundi wakaenda kuvamia mgodi. Kwa hiyo, wamepambana na Polisi, wamekufa vijana wawili. Ninavyozungumza hapa, kesho wanazika. Kwa hiyo, hali ya kisiasa ni tete pale katika lile eneo zima la Nyamongo. Vile vile tarehe 01 mwezi wa tatu nilikuwa pale, Binti Neema Omari mwenye miaka 16 alipigwa risasi lakini nikaenda pale tukamtoa risasi mbili, tarehe 26 mwezi wa Nne, ameuawa mtu, tarehe 5 mwezi wa Tano ameuawa mtu, tarehe 22 mwezi wa Nne, sasa katika mazingira hayo maana yake vijiji vyote wanazika, na mgogoro ni nini? Mgogoro ni kwamba, katika kutoa yale maeneo ya wachimbaji, mikataba ni kwamba ukimlipa mwananchi mzawa shilingi milioni tano anahama. Hata hivyo, ana watoto, wakikua wakawa wakubwa wanaambiwa eneo letu ni hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu naomba katika eneo hili, kwenye mikataba mipya inayokuja ya kutoa maeneo ya watu tuwe na mikataba ya *shareholder*. Ni kwamba, kama mtu akichukua eneo la uchimbaji, awe na *share* katika uchimbaji ule ili wale watu waendelee kuishi kwa kadri ambavyo miaka inaenda. Akipewa fedha akashindwa ku-*survive* mmetengeneza mazingira magumu sana katika Wilaya ya Tarime, na kwa hiyo, inatusumbua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka niseme, nilitaka nizungumzie migogoro ya ardhi. Nimewaambia na watu wa Wizarani pale, kule kwetu ukienda pale Korotambe, miaka nenda miaka rudi wanagombana na watu wa Remagwe kule Pemba, na mgogoro haujawahi kwisha. Ukienda Mrito – Msege wanagombana, nenda Marasibora Rorya na Tarime Nyamberambalu wanagombana. Sasa maeneo hayo ndiyo ambayo Mheshimiwa Waziri anaweza akatufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri wa Madini na mgodi wamekubaliana, nadhani kama sikosei wiki ijayo kwa taarifa ya Mheshimiwa

Mavunde ni kwamba mtaongozana kwenda kutoa yale ambayo mgodi hawana uhitaji mkubwa ili yatwaliwe na kupewa vijana wachimbe (wachimbaji wadogo). Vilevile, Mheshimiwa Mama Dkt. Samia ameshapeleka gari la wachimbaji la madini, litawasaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mgodi wamekubali kuchukua vijana na kuwapeleka kwenye stadi za maisha *(VETA)* kwa gharama zao na kuwapa vitendea kazi. Hii pia itapunguza *tension* ya kuja hapa Bungeni kila siku kuwaambia watu wanauana kama kuku katika eneo lile ambapo kwa kweli kama watu Mkoa wa Mara na hasa Wilaya ya Tarime siyo jambo jema sana kwamba kila siku lazime uzike; kuna risasi, kuna mapanga. Siyo sawasawa. Pia kuna namna moja ambayo wanatakiwa wasaidiwe kuweza ku-*survive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Jerry kwamba hii Wizara ni kubwa sana na ina shida sana. Hata hivyo, nataka nimwambie, kwa namna ambavyo ulianza na nimekuomba uje kule Tarime na hasa kule kwenye maeneo ya Mgodi na maeneo mengine ufanye kazi ya ziada. Nataka nimwambie, tunataka migogoro ya wafugaji na wakulima iishe, tunataka ugomvi wa wakulima uishe. Ni kwa sababu watu wamemheshimu, ameanza vizuri na tunaomba aendelee vizuri, lakini kimsingi yaani kila ikija hapa Wizara ya Ardhi, Wizara hii haijawahi kuwa rahisi kwa sababu kila Mbunge hapa ana mgogoro katika jimbo lake, kila Mbunge hapa kwenye wilaya yake kuna mgogoro, kila Mkoa kuna mgogoro na bahati mbaya watu wake wanakula rushwa kweli kweli. Wanakula rushwa bila kunawa na wanaonea wananchi. Sasa hili ni lazima Mheshimiwa Waziri atengeneze mfumo kwa wale watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye halmashauri zetu katika idara ambayo haina nguvu sana ni Idara ya Ardhi. Kuna mtu mmoja tu aidha, mmoja na dereva na hana gari halafu anaamua peke yake. Hata hivyo, ardhi ni maisha. Pia, Baba wa Taifa alisema ukitaka maendeleo ni vitu vinne; uwe na watu, ardhi, uongozi bora na siasa safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siasa safi ipo, Mama Dkt. Samia ameweka mambo *level*, uongozi uko vizuri, ardhi ipo. Sasa ardhi hii isimamiwe, na Waziri ni mwenyeji katika watu ambao wamekuja kuelezea hapo Wizarani. Waziri ni mtu ambaye angalau katika matamko ya Mheshimiwa Baba wa Taifa naye anatajwa, ardhi. Kwa hiyo, naomba atoe heshima hiyo na sisi Wabunge tupate kutoa ushirikiano. Ukienda kwenye eneo la jimbo fulani, ita viongozi wa kisiasa, Wakuu wa Mikoa, *Ma-DC* na wananchi washirikishwe, migogoro mingine wanaijua mipaka yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, leo nimesema nichangie na hapo nimechangia kwa upole sana. Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri na viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam kile kitimoto kule kwenye jimbo langu mnisaidie kupunguza ili joto lisiwe kali sana, nisirudi Dar es Salaam. Ahsante sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waitara. Mheshimiwa Halima James Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitakuwa nyumbani zaidi na ninavyozungumza nyumbani maana yake ninazungumza Kawe. Kwanza, nilitaka Mheshimiwa Waziri anisaidie, mwaka 2023 mlisema kazi ambazo mlitarajia zitakamilika 2023/2024, ni pamoja na kukamilika kwa Mradi wa *Seven Eleven*. Sasa leo unatuambia umefika 35% na mnatarajia kumaliza 2026. Kwa nini mwaka 2023 mlilidanganya Bunge? Ama Serikali hamjui mipango wala hamna mipango, mnafanya kwa kubahatisha!

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mradi wa *Seven Eleven* ilikuwa na vipengele viwili; kulikuwa kuna *Seven Eleven One* ambayo hii ni miradi iliyoanza kipindi cha Dkt. Jakaya, ikakwamishwa Kipindi cha Mheshimiwa Dkt. Magufuli, ikafufuliwa kipindi cha Rais Mheshimiwa Dkt. Samia, ambapo ukwamishaji wake katika kipindi hicho cha Rais Mheshimiwa Dkt. Magufuli Mungu amlaze mahali pema Peponi, nchi ilipata hasara ya zaidi ya shilingi bilioni 199.9 kwa sababu kulikuwa kuna wakandarasi, kuna mikataba imeingia, mikopo na vurugu nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka tu tujue kwamba, *Seven Eleven One* gharama yake kipindi hicho ilikuwa shilingi bilioni 142, *Seven Eleven Two* ilikuwa shilingi bilioni 103. Sasa hivi mnatuambia kwamba *Seven Eleven* thamani yake ni shilingi bilioni 169. Sasa nataka nijue ni *one* ni *two* ama *combined*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo nadhani nitalizungumza kwa urefu kidogo ni suala la migogoro ya ardhi. Taarifa ya Kamati, ukurasa wa 28 inasema kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi inayotokana na Serikali kushindwa kupima na kupanga maeneo mengi nchini. Kamati inaishauri Serikali iendelee kutoa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungekuwa tunasoma *Hansard* za Bunge kwa Mabunge yaliyopita, hili ni Bunge la Kumi na Mbili, Bunge la Kumi na Moja, na Bunge la Kumi, hii sentensi inaweza ikawa imejirudia kwenye Mabunge mengi zaidi kuliko kipindi chochote. Ndiyo maana mimi nilisema hapa, Bunge lile lililopita kabla ya mwaka jana 2023 wakati wa Bajeti ya Ardhi inawezekana kabisa ama watumishi wana maslahi kwenye migogoro, ama vigogo wa Serikali wana maslahi katika migogoro, ama vigogo wa chama wana maslahi katika migogoro. Ndiyo maana leo pamoja na ngonjera zote tutakazoziimba, Bajeti ya Wizara ya Ardhi imepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana 2023/2024 matumizi mengineyo ambayo ndiyo *Other Charges* tunategemea yana-*facilitate* utendaji wa kazi wa watumishi ilikuwa shilingi bilioni 37.6, mwaka huu ni shilingi bilioni 36.6. Bajeti ya Maendeleo 2023/2024 ilikuwa shilingi bilioni 82, leo ni shilingi bilioni 70, unategemea nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maana yake ni kwamba, kuna mjumuiko wa pamoja wa hujuma, hii migogoro itokee, ili watu wazurure huko mtaani kujifanya wanasuluhisha kumbe wanatengeneza matatizo mengine. Kama tuna dhamira ya kusaidia hii Wizara, lazima tuoneshe kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mwaka jana 2023 tarehe 03 mwezi wa sita nilizungumza namna ambavyo *DDC (Dar es Salaam Development Cooperation)* Shirika la Maendeleo la Dar es

Salaam, mimi nimekuwa Mbunge miaka 10 Kawe, sijui hili shirika linafanya nini? Kuna mgogoro mkubwa sana ambao unagusa majimbo mawili; Jimbo la Kibamba na Jimbo la Kawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro huu unahusu mitaa saba ya Kiserikali. Napongeza tu kwa hatua kidogo ambazo Waziri ameweza kuonesha, kama Waziri, *well and good,* lakini kwangu mimi naona kama vile ni katone kwenye Bahari ya Hindi iliyojaa mapapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtaa wa Msumi, kwa mfano, kwa ndugu yangu pale Kibamba kwa eneo ambalo *DDC* wanasema watachukua, linaloingia kwenye mtaa ni 57.3% ya Mtaa wa Kiserikali. Huu mtaa una pori la Serikali ambalo ni *reserve,* linatengeneza 32%. Maana yake wakichukua eneo, itabaki 10%, ndiyo wananchi wakabanane kule. Mtaa wa Tegeta A, kwa ndugu yangu wa Kibamba ni 26.7%. Mbopo, Jimbo la Kawe, 48% ya eneo la Mtaa wa Mabwepande ni asilimia tano, Madale ni 5.9%, Kilangwa ni asilimia mbili, Makabe ni asilimia 0.38. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu anaitwa *DDC,* anasema ana hati aliyoipata mwaka 1981. Uzuri ni wananchi tokea mwaka 1980, 1979 wako pale. Kijiji cha Mabwepande kimetangulia, *DDC* wanasema kweli, walileta maombi, lakini walipewa masharti ambayo hawakuyatimiza wakaenda wakatengeneza hati yao mezani, ndio wanasema tuna hati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo husika, lina shule 17, za msingi 13 na za sekondari nne. Kuna Kituo cha Mafunzo cha Kilimo cha Serikali, kuna zahanati tatu, kuna viwanda vitano, kuna vituo vya mafuta viwili, kuna taasisi za kidini 20. Pia kuna Ofisi za Serikali za Mtaa saba, kuna ofisi za chama chenu, sitaki kutaja hapa, ila mjue ofisi za chama chenu zipo za kumwaga. Yapo maeneo ya maziko matano, kituo cha kulea watoto kimoja na visima vya maji viwili. Hawa watu walipewa hati mezani, ndiyo maana leo unakuta Kijiji cha Mabwepande kimepanuka mpaka Kibamba. Najua Mheshimiwa Waziri ana busara, naomba busara yake imwongoze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hati, hawa jamaa kwanza inasemekana kuna hati tatu; kuna ya mwaka 1981, kuna ya mwaka 1983, kuna Hati ya mwaka 1984. Hati hii ya 1984 ambayo ndiyo waliitoa kwenye Kijiji, kipengele kinasema walitakiwa watumie ardhi kwa kilimo na ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakitaka kubadilisha matumizi wa-*consult* mamlaka. Leo miaka 43 baadaye, nilipokuwa Mbunge wa Kawe hawakuthubutu kuleta pua kwa sababu walijua watakutana na kifaa. Leo nimeondoka wanaenda kupeleka pua kutaka kudhulumu kaya za watu laki mbili hivi, ni haki hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ya nchi hii ni mali ya umma. Bahati mbaya *sole fortunate* wameandika barua kwa Makamu wa Rais mara mbili, nimezungumza hapa, mwaka 2023 wakati dada yangu Mheshimiwa Angela ni Waziri hapa na Naibu wake wanajua, wakapuuza, hawajachukua hatua. Wanatajwa, Mheshimiwa Waziri, watu wanasema kumekuwa na upotoshaji na udanganyifu unaoendelea kufanyika na Mwenyekiti wa Bodi ya *DDC,* yuko rafiki yangu hapa ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, Mheshimiwa Mbunge wa Kawe Gwajima, Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamemwandikia Makamu wa Rais barua mbili wanalalamika, Dar es Salaam pale ni pua na mdomo na Wizara, Serikali iko wapi? Huwezi ku-*ignore* watu 200,000. Tu-*assume* wananchi wana tatizo, hivi kweli wewe umepata kahati kako mwaka 1981 hujaweka hata mbuzi, hujaweka hata kuku, hujaweka hata panya, miaka 43 baadaye unakuja unawaambia tu wananchi walipe pesa, *for what*? *Simply because* una-*connection* ndani ya Serikali! *We cannot allow that*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jerry alikwenda kwenye Kliniki ya Ardhi, Bunju. Nikuhakikishie tu wananchi wale wana matumaini makubwa sana naye. Mara ya kwanza alienda alivyoitwa na mwenezi wao, kuna *statement* akaitoa kuhusiana na ule mgogoro, lakini nashukuru baadaye Waziri ali-*revoke* akaja

akawasikiliza akaona kuna kitu. Naomba Waziri akasikilize hawa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wamezungumza hapa, Waziri akawasikilize wananchi, asiwasikilize wapambe wanaomzunguka wanampotosha kwa sababu wao ni wanufaika wakuu wa hii dhuluma. Wananchi wamepewa *Control Number* ya kulipia, eti wanaambiwa viwanja, sijui nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwenye yale maeneo kuna watu pia ni wavamizi. Kwa hiyo, kuna lugha inatumika, ooh, kuna watu *DDC* wamekubaliana nao kuwalipa, wale ni watu ambao waliingia pale kudhulumu watu wengine ambao wameshinda kesi mahakamani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wana foleni ya makubaliano na majambazi ili kuweza kuwanyima haki wenye haki. Namwomba Mheshimiwa Waziri, namwamini, Wakili, akawasikilize wananchi, kwani ana busara, tutamaliza mgogoro. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa ratiba yetu ya asubuhi hii. Kama ilivyo ada, nawapongeza wale ambao mmepata kuchangia kwa niaba yetu, mmeendelea kufanya kazi nzuri sana ya kuishauri Serikali na ninaamini mmefanya hivyo kwa sababu mnamshauri Waziri makini kabisa na ninaamini kwamba, atayafanyia kazi. Kwa hiyo, ninawapongeza sana na Mheshimiwa Jerry chukua *credit* hizo kutoka kwa Wabunge na kwa niaba ya wananchi. *(Makofi)*

Tutakuwa na mwendelezo wa mjadala mchana. Naomba niwatamke wachangiaji sita wa kwanza ili kuwawezesha kuwahi mapema muda huo. Tutakuwa na Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi na Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo na wengine watatamkwa muda huo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hili, ninasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 alasiri.

*(Saa 7.08 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na hoja ya Serikali ambayo ipo Mezani. Niliwataja wachangiaji wa kwanza jioni hii. Tutaanza na Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo atafuatia Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi jioni ya leo kuwa mchangiaji wa kwanza kwenye Wizara yetu ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nami nianze kama wenzangu kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo anaendelea kuyatekeleza majukumu ya Taifa hili kwa niaba ya Watanzania, lakini kwa jambo lililo Mezani kwetu, tumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutupatia Waziri na namna alivyoipanga timu yake ya Wizara ya Ardhi inavyoendelea kushughulika na matatizo ya wananchi na tunaona namna anakopita anavyoweza kufanya mambo mbalimbali na kumaliza changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi pia kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake yote ya Wizara, naamini kwa kweli katika Wizara ile yupo dada yangu pale Lucy kwa kuwa ametokea

Pwani najua nguvu na uwezo alionao juu ya kuzungumzia migogoro na naamini katika sehemu ya migogoro nitakayoizungumzia mingine yeye anaielewa vizuri zaidi. Kwa hiyo, namwomba yeye (Naibu Katibu Mkuu) amweleze vizuri Waziri ili aweze kusaidia kumaliza changamoto zilizopo Mkoa wa Pwani ambazo anazifahamu vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo waliochangia wakimwombea Mheshimiwa Waziri Ulinzi. Mimi niseme sisi Wabunge kwa niaba ya wananchi tuendelee kumwombea ulinzi wa Mwenyezi Mungu kwa sababu ulinzi wa mwanadamu siku zote una kikomo. Hata kama atapewa ulinzi wa namna gani, inawezekana mlinzi wake akasinzia na hayo ambayo tunapata mashaka nayo yakamkuta. Kwa niaba ya Watanzania sisi tulio hapa kwenye Bunge hili tuombe kwa kadiri tuwezavyo aweze kupata ulinzi wa Mwenyezi Mungu kwa sababu ukweli kabisa kazi ambayo anaendelea nayo kwenye majimbo yetu bila kumwombea hakika anaweza akapoteza mwelekeo na nguvu ya kupambana na matatizo ambayo anashughulika nayo ikapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo yote hayo ambayo nimeyasema, kwanza nitangulize ombi na ombi hili likiwa na sura ya kumkumbusha. Nakumbuka mimi na yeye tulikutana mara kadhaa, tulipanga ratiba ya kwenda jimboni, ilikuwa tarehe 09 lakini baada ya kukutana na majukumu ilishindikana. Ombi lile Mheshimiwa Waziri bado nalileta kwako nikikuomba sana sana sana ndugu yangu tuiweke vizuri ratiba ya kwenda Pwani na hasa katika Jimbo la Kibaha Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niseme kidogo, pia ndugu yangu wa Chalinze nilipomwambia nitachangia eneo hili akaniambia naomba umkumbushe atakapokuja Pwani asikose kufika Mbala. Ufike na pale Mbala ukamsaidie na lile tatizo ambalo na yeye linampa shida muda mrefu sana. Pia nakuomba, kwa sababu ulipanga siku moja kwenye haya maeneo mawili, ikiwezekana jitahidi sana kila jimbo lipe siku yake. Maana yake mzigo uliokuwa katika Kata ya Kikongo au katika Jimbo la Kibaha Vijijini siyo mzigo mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba Mheshimiwa Waziri atakapotoka kwenda pale kwa ajili ya kushughulikia, akatoa siku moja kwa maana ya majimbo mawili na uzito wa mambo yalivyo, inawezekana akapata rasha rasha. Mimi nataka aende akawasikilize Watanzania wa maeneo yale ya Kikongo kwa sababu kuna migogoro mbalimbali inatoka kwenye kata karibu tano au sita za jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Mtemvu hapa alipokuwa anachangia nikagundua kumbe na huyu naye ninaye kule. Kwa hiyo, namna alivyochangia ameigusa Kata ya Kikongo na ameeleza hali ambayo anaijua, nafikiri ni vizuri Waziri akaja kutusaidia. Baada ya eneo hili la kwanza ambalo nililitenga kama eneo la shukurani, na kuomba hali ambalo nimeomba, kwanza nitangulize maneno ya kwamba naunga mkono hoja kabla sijaanza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yangu ya kuchangia ambayo leo nimejipanga nayo ni maeneo yafuatayo: Kwanza kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameonesha majukumu ya Wizara katika kushughulikia migogoro, lakini ameanza pia kuzungumzia kwamba wanashughulika na suala zima la upimaji na umilikishaji wa masuala ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili pamoja na Mheshimiwa Waziri, naomba mfahamu kwamba kwa kadiri ambavyo mmeweza kutambua kama hii ni sehemu moja ya jukumu lenu, nafahamu kwamba suala zima la upimaji linakuwa chini ya Mabaraza ya Halmashauri, lakini tunafahamu kabisa tunapopewa hili jukumu la kwamba halmashauri zinatakiwa zipime na zipange ni katika suala zima tu la kutambua maeneo, kuwatumia wataalamu ambao wanatoka Wizara ya Ardhi waliokuwa ndani ya halmashauri husika, lakini pia kwenye utoaji wa maamuzi ya hapa pafanywe nini na hiki kifanywe nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zote za ardhi ni za kitaalamu, zinahitaji watu kutoka kwenye ofisi yako. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na jukumu hili kuwa linafanyika kwenye ngazi zile, ahakikisha analitupia jicho kwa sababu hapo ndipo panapoanza migogoro. Unakuta watu wanatambua

maeneo, wanayapanga, lakini kwenye matumizi ya upangaji ambao umekusudiwa unakwenda ndivyo sivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ndilo linalopelekea migogoro mingi ambayo inasababisha sasa Waziri hata sasa ashindwe kuwa na utulivu. Kila jimbo wanamhitaji yeye mtu mmoja; na hii ndugu yangu Waziri ni namna gani Watanzania na Wabunge wana imani na wewe na ofisi yako na siyo mtu mwingine yeyote. Kwa hiyo, jitahidi kutoa maelekezo kwa watu wanaokusaidia wafanane na wewe angalau kwa robo tatu ili waweze kupunguza kasi ya matatizo na wakupe muda wa kuweza kushughulika na masuala mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hivi kwa sababu gani? Tuna tatizo au suala zima la urasimishaji. Wananchi wanamiliki ardhi, tumetoa wenye sera ya kuzungumza kutakuwa na masuala ya urasimishaji kwenye maeneo ya miji ambayo haijapangwa. Tumetoa kibali kwa kampuni zifanye hizo kazi za kuwapimia watu na kuwapanga vizuri kwenye maeneo ya miji ambayo hayajarasimishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jimbo langu hasa katika Mji Mdogo wa Mlandizi kuna kampuni zimepewa majukumu ya kufanya jukumu hilo wameingia mitini, kwa lugha ya sasa. Wamewafanyia kazi nusu wananchi, ramani hazijulikani ziko wapi? Hawajui wamefika hatua gani, na wananchi wametoa pesa. Sasa tunaomba mtusaidie kututafutia hawa watu ambao walipewa dhamana ya kuja kufanya zile kazi wakazimalize na kama hawawezi kufanya hivyo, basi ofisi yako Mheshimiwa Waziri ione namna gani inaweza ikafanya jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kwenye suala zima hilo la upimaji na umilikishaji, nashukuru kwenye jimbo langu kuna jiji linaitwa Jiji la Kwala. Baadhi ya vijiji vimetambuliwa ambavyo vinakwenda kulitengeneza hilo Jiji la Kwala, lakini Mheshimiwa Waziri kazi ambayo imefanywa ya upangaji na upimaji kwenye eneo lile ukiangalia kwa haraka haraka tumekwenda kufanya kazi kwenye kipande ambacho wawekezaji wanaenda kuwekeza lakini watu walio jirani na maeneo hayo kazi hiyo haijafanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Jiji la Kwala tunapokwenda kupima maeneo tu ya viwanda lakini eneo la viwanda au eneo la uwekezaji jirani yake wapo wananchi wanaishi ambao nao ni vema wangeweza kupangwa vizuri mapema, kwa sababu tunapopanga kipande kidogo na tunatarajia liwe jiji, tutegemee kuweka mazingira ambayo siyo rafiki sana kwenye eneo ambalo linapakana na maeneo hayo. Nasema hivi kwa sababu gani? Kwenye Eneo la Kwala ambalo tumepanga kama eneo la jiji tumepima maeneo ya wawekezaji lakini bado kuna migogoro mikubwa ya ardhi. Wananchi wanaokabiliana na eneo hilo wapo wanaolalamika kwamba wako ndani ya eneo hilo. Sasa ni vizuri tufanye upimaji na tupange na kuvishirikisha vile vijiji vyote vya jirani vipangwe kwa pamoja ili visiharibike tena kwa sababu tunatarajia uje kuwa mji, na tukifanya hivyo tutakuwa tumemaliza migogoro mingi ambayo tunaizungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna suala zima la upangaji wa ardhi na matumizi bora ya ardhi. Vijiji vyote kwenye maeneo ya nchi hii, kwa mfano Jimbo langu la Kibaha Vijijini, vijiji vingi vilipangwa; wakapanga matumizi bora ya ardhi. Wakatambua wapi watakaa wafugaji, wapi watu watalima, wapi watu watawekeza viwanda, lakini cha kusikitisha, upangaji huu hausimamiwi na hausimamiwi kwa sababu gani? Anatokea mtu anataka kuwekeza kwenye eneo ambalo siyo lililopangwa kwa shughuli fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watumishi wa Wizara ya Ardhi wanaridhia kazi hiyo ifanywe tofauti na kilichokuwa kimepangwa. Jambo hili linaleta mgogoro mkubwa sana. Limesumbua kwenye Kata ya Ruvu na limepelekea mpaka kuwepo na mgogoro wa mpaka wa kata na kata kwa sababu hawakuheshimu mpango wa kijiji kimojawapo. Kwa hiyo, ni vizuri Mheshimiwa Waziri haya mambo yakaangaliwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ambalo nataka nichangie ni utatuzi wa migogoro. Hapa nitagusa kidogo eneo ambalo ndugu yangu Mheshimiwa Mtemvu amelizungumza. Eneo hili la migogoro tunajua tuna vyombo vinavyoshughulika na utatuzi wa migogoro ya ardhi. Kwanza, tunayo Mabaraza ya Ardhi lakini pia tuna Makamishna wa Ardhi ambao ndio

wanaweza kutusaidia kufanya hizi kazi lakini sasa hivi tunajua kabisa viongozi kwa mamlaka yao ma-*DC* na Wakuu wa Mikoa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mwakamo muda wako umeisha.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja nimalizie.

**MWENYEKITI:** Tafadhali hitimisha.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi pamoja na kusema haya, nimalizie tu kukuomba Mheshimiwa Waziri hii migogoro ambayo ameizungumza ndugu yangu, Mheshimiwa Mtemvu ambayo yote iko kwangu nakuomba unipangie ratiba nzuri twende tukaimalize kwa sababu Kikongo siyo pazuri panatuondolea amani na hali tutakayokwenda nayo mbele ambayo unaifahamu yote, siyo jambo jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, nilishasema naunga mkono hoja na narudia tena naunga mkono hoja, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Josephine Genzabuke atafuatia Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Mheshimiwa Ally Juma Makoa ajiandae.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwenye Wingi wa Rehema, alienijalia afya ya kusimama katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza naomba niunge mkono hoja. Baada ya kuunga mkono hoja naomba nichukue nafasi hii nami niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Jerry kwa kazi nzuri anayoifanya. Tumeshuhudia maeneo mengi amekuwa akifanya kazi nzuri ya kuwasaidia Watanzania, kuwatetea wanyonge na kurudisha haki za watu walioporwa haki

zao. Hongera sana Mheshimiwa Jerry kwa kazi nzuri unayoifanya ya kuwatumikia Watanzania. Pia naomba nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Ardhi kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Jemedari wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwaongoza na kuwatumikia Watanzania. Hakika mama huyu amekuwa ni mkombozi wa Watanzania. Kwa hiyo, tunaomba tuendelee kumwombea Mwenyezi Mungu amjaalie afya aendelee kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitajielekeza katika hoja moja tu, hoja ya migogoro ya mipaka katika maeneo mbalimbali. Migogoro ya mipaka imekuwa ni kilio kikubwa kwa Watanzania na hata ukiangalia kwenye jamii zetu watu wengi na hata wengine wanapelekea kuuana kutokana na mipaka ya ardhi. Kwa hiyo, ni namna gani unaweza kuona mipaka inavyoweza kuondoa amani kwa watu mbalimbali na hata kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika, ardhi haiongezeki kabisa kabisa na kwa hivi sasa badala ya kuongezeka ardhi inapungua. Ukiangalia mafuriko ya mwaka huu yameweza kumega ardhi kubwa kwenye mito, mito imemega ardhi, maziwa yamemega ardhi lakini vilevile bahari imemega ardhi kwa maana hiyo ni ukweli kabisa ardhi haiongezeki lakini watu wanaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Watu wanaongezeka na mahitaji yanaongezeka. Kwa mfano, kwa sasa hivi ukiangalia wanafunzi wanamaliza vyuo wanaelekea mitaani, vijana wanaotoka jeshini wakimaliza vyuo wanaelekea mitaani. Huku kwingine ajira inapungua, ajira pekee iliyobaki ni kwenye kilimo na huko huko kwenye kilimo ndiyo huko sasa ardhi haitoishelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimekuja na kilio cha kuiomba Serikali iongeze kasi ya kupima ardhi na kuweka mipaka.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Jerry kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kabisa naomba kazi ya kuwatumikia Watanzania kwa kupima ardhi na kuweka mipaka iweze kufanyika ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya yetu ya Kasulu upo mgogoro wa muda mrefu katika eneo la *Kasulu DC,* Kijiji cha Kagera Nkanda, Mvinza na Katoto. Huko kuna migogoro ya muda mrefu sana na mara ya mwisho nilitembelea vijiji hivyo mwezi wa Tisa. Wananchi wale waliniomba Waziri uweze kufika. Hivyo Mheshimiwa Waziri katika ratiba yako nakuomba sana na ninakusihi upange ratiba uweze kufika Kagera Nkanda Mvinza na huko kwingine ili uje ufanye mikutano. Tena naomba uitishe mikutano uwasikilize wananchi, ukishawasikiliza naamini utasema neno moja tu watapona, kwa sababu kilio chao ni kutaka kuwekewa mipaka ili waendelee kufanya shughuli zao za uzalishaji wa kilimo wakiwa na amani kuliko ilivyo hivi sasa unakuta ni migogoro ya ardhi na wakati mwingine wakilima mazao yao yanachomwa na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Waziri nirudie tena, naomba ufike Wilaya ya Kasulu, utakapokuja uje Kagera Nkanda, Mvinza na Katoto. Nafahamu ni mbali sana kufika katika vijiji hivyo na wakati mwingine unapita wilaya nyingine na watu wanaweza wasikupeleke kule wakakwambia Mheshimiwa kule hakufikiki, wewe bado ni kijana, fanya linalowezekana ufike kwenye maeneo hayo ambayo hayafikiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Josephine. Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, atafuatia Mheshimiwa Ally Juma Makoa na Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi ajiandae.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwa maneno ya Marehemu Mzee wetu Mwinyi; "Maisha ya binadamu ni hadithi tu hapa

ulimwenguni, ewe ndugu yangu kuwa hadithi nzuri kwa watu watakaosimuliwa habari zako.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nianze kwa maneno haya ili kumkumbusha Mheshimiwa Waziri juu ya umuhimu wa Kiongozi kuacha alama nzuri katika uongozi wake. Kwa muda mrefu Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukiishauri Serikali kuipima ardhi yote ya Tanzania na kuweka mipango bora ya ardhi. Hakuna asiyejua nchi yetu inakabiliwa na migogoro mingi hasa kati ya wakulima na wafugaji kwa upande mmoja na wananchi na hifadhi za Taifa kwa upande mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wenye mapenzi mema na Taifa hili tulitegemea kwamba tungetafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili ili wananchi wetu wasiumizane na ufumbuzi wa kudumu upo katika kuipima ardhi yote ya Tanzania badala ya kupima kijiji kimoja kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023 Wizara ilipata dola za Kimarekani 150,000,000 sawa na shilingi za Tanzania bilioni 405. Narudia, shilingi bilioni 405. Niliwahi kuzungumza na mtaalam mmoja wa upimaji akaniambia tunahitaji fedha kama shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kuipima ardhi yote ya Tanzania. Sasa tunaweza kupima juu ya utekelezaji wa jambo hili, ni jambo ambalo linawezekana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa badala ya Wizara kuzitumia fedha hizi, shilingi bilioni 405 kwa ajili ya kuipima ardhi, Wizara inashauriwa na watendaji wake itumie zaidi ya 70% ya fedha za mkopo kwa ajili ya kujenga kumbi za mikutano, kulipa posho za wafanyakazi, kugharamia semina na kununua kompyuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu, jambo hili siyo la busara hata kidogo. Hatuwezi kutumia fedha za mkopo kwa ajili ya shughuli za utawala. Kama Mheshimiwa Waziri ameshauriwa hivyo, nakumbuka maneno ya Mwalimu wangu akisema hivi; “Huu utakuwa ni mfano mzuri kwa ushauri mbaya aliopewa Mheshimiwa Waziri” Nasema, huu utakuwa ni mfano mzuri wa ushauri mbaya aliopewa Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, naomba autafakari vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri mambo mawili. Jambo la kwanza, naiomba Wizara ipime ardhi yote ya Tanzania na kuainisha maeneo ya mashamba, viwanda, maeneo ya wafugaji na kuweka miji ya kisasa katika kila Mkoa. Tusipolifanya jambo hili sasa, hatutaweza kulifanya miaka 50 inayokuja, kwa sababu ardhi itakuwa imeharibiwa sana kutokana na ujenzi mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naishauri Wizara, tutoe hati tuwamilikishe wananchi wanaostahili ili tukusanye mapato ya kutosha kwa ajili ya kugharamia maendeleo ya Taifa letu na kujenga Taifa linalijitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba Mheshimiwa Waziri na watendaji wako mlisikilize vizuri. Naomba nirudie maneno ya Mzee Mwinyi: "Maisha ya binadamu ni hadithi tu hapa ulimwenguni, ewe ndugu yangu, kuwa hadithi nzuri kwa watu watakaosimuliwa hadithi yako." Mheshimiwa Waziri nafikiri umenielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, umetoa sauti kwa kweli, ahsante sana. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Ally Juma Makoa atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi na Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo ajiandae.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii nami niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Ardhi. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa kuendelea kuhudumia nchi yetu kikamilifu. Nawapongeza pia Wizara chini ya Mheshimiwa Jerry Silaa kwa kazi ambazo tunaona zinaendelea. Kwa kweli Wizara inaendelea kuonyesha mabadiliko makubwa, kwa hiyo, tuendelee kumpa moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kazi anazozifanya Mheshimiwa Jerry Silaa pamoja na watendaji wa Wizara hii na wote wanaomsaidia kwa ujumla. Kikubwa tuendelee kumpa moyo kwamba hiyo ndiyo kazi aliyopewa na Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wewe utajiombea peke yako lakini yale machozi ya Watanzania ambayo unakwenda kuyatoa kwa furaha baada ya kudhulumiwa maeneo yao kwa miaka mingi yatakuwa ni maombi tosha kwako na wenzako wanaokusaidia. Endelea kufanya hivyo kwa sababu dhamira ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuona migogoro na dhuluma zote za wananchi wake zinaondolewa. Wewe na Wizara yako ndiyo umepewa dhamana ya kuweza kupanga vizuri matumizi ya ardhi katika nchi hii. Kwa hiyo, wewe endelea kufanya hivyo, sisi pamoja na Watanzania wengine tutaendelea kushuhudia yale ambayo unayafanya, lakini Mungu atakubariki kwa yale ambayo unayafanya kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishauri mwaka 2023 juu ya upimaji wa ardhi katika nchi yetu, na unakumbuka tuliongea maneneo mengi ya kushauri. Tumeona namna ushauri unachukuliwa. Nimeangalia hapa Tume ya Mipango ya Ardhi ya Taifa, Serikali imewapa fedha kwa 100% nao wamefanya kazi kwa zaidi ya 100%. Hii inaonyesha kwamba tunao watendaji wazuri, wakipewa rasilimali za kutosha watatufikisha pale tunapotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023 walipangiwa kupanga vijiji 210. Mpaka kufikia Juni, wamepima vijiji 339. Hii inaonyesha hata ukimpa fedha anazozihitaji shilingi bilioni 22 ili aweze kutupimia vijiji ambavyo kwa mwaka wana uwezo wa kupima vijiji zaidi ya 1,000, tukimpatia fedha hizo, maana yake atakuwa na uwezo wa kupima vijiji 1,640. Atachukua muda wa miaka mitano na miezi sita kukamilisha vijiji vyote 8,000 na zaidi vilivyobaki. Gharama ya vijiji vyote kama atapewa fedha kuvipima vyote, anahitaji shilingi bilioni 22 kila mwaka kwa miaka mitano, kutukamilishia upimaji wa vijiji 8,194. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona mambo haya siyo magumu kiasi hicho? Serikali imefanya mambo makubwa ya fedha nyingi. Suala la kupanga nchi ni suala la kuondoa migogoro, jambo

litakalowafanya wananchi kujipanga vizuri katika nchi yao, kufanya shughuli zao za kiuchumi bila bugudha na mwingiliano wa idara nyingine na wananchi. Tusipofanya hivi Mheshimiwa Jerry Silaa ataota mvi mpaka kwenye nyusi za kwenye macho. Migogoro itaendelea kuwepo na kuwepo bila mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali iwape Tume ya Mipango, hiyo shilingi bilioni 22 wapime vijiji 1,460 kwa mwaka ambapo baada ya miaka mitano na miezi sita suala upimaji na upangaji wa ardhi tutakuwa hatuliongei tena katika Bunge hili. Kwa hiyo, tunaomba tena Serikali ifanye hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliongelea ule mkopo wa shilingi bilioni 300, tukasema, katika fedha hizo ukiwapa hawa watu wa ardhi shilingi bilioni 100 na zaidi wanamaliza kesi yote. Kwa hiyo, ajenda hii ya kuongelea Bungeni muda wote masulala ya kupanga nchi itakuwa imeisha na itakuwa ni sifa kubwa kwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na itakuwa ni sifa kwa nchi na itakuwa ni sifa kwa Bunge letu, pia tutakuwa tumetekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa uhalisia wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaiomba Serikali ifanye hivyo, kwa sababu tazama katika ule mradi wa *LTIP* mpaka leo umeweza kupima vijiji 843. Kwa hiyo, kumbe tukiwapa nguvu Tume na hiyo miradi ya pembeni, hata hiyo miaka mitano haiwezi kufika. Haifiki. Kwa hiyo, tusaidie jambo hili liweze kwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anafahamu kule kwangu kuna mgogoro ule wa Mongoroma ambao kidogo juzi ulileta taharuki hapa. Mgogoro ule ni mdogo sana, Wizara ya Ardhi inatakiwa itupe elimu watumiaji wa ardhi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sekunde kadhaa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara nyingine zote na wananchi ni watumiaji wa ardhi, kwa maana hiyo, mtu ambaye atasimama na kuweza kusababisha tukapatana ni Wizara ya Ardhi. Sisi

hatuwezi kuwa tuna mgogoro, wananchi wana mgogoro na Wizara ya Maliasili halafu Maliasili ndiyo wakautatua ule mgogoro. Ni jambo ambalo haliwezekani. Wote ni waathirika, anayeweza kutatua mgogoro ule ni Wizara ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wanasema wamepeleka vigingi, wameshaweka vigingi kwenye maeneo ambayo wananchi wana kesi nao zaidi ya miaka 30. Maana yake kaamua tu yeye mwenyewe bila kushirikisha wananchi. Sasa hapa suluhisho litapatikana kwa wewe Mheshimiwa Jerry Silaa kufika Mongoroma haraka iwezekanavyo ili tumalize ile *issue,* na kikubwa zaidi ni agizo la Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba ufanye jambo hilo, ufike mpaka Mongoroma. Kondoa hapa ni saa moja tu umefika, mkutano wa saa moja, saa tatu uko zako Dodoma unaendelea na shughuli zako. Kwa hiyo, Mheshimiwa Jerry Silaa utakapokuja kuhitimisha uniambie ni lini tunafuatana kwenda kuwasikiliza wananchi wangu wa Mongoroma? Wana hamu sana na wewe ili waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wale wanashindwa kufanya kazi zao, wanashindwa kujenga majengo mazuri, wamecheleweshewa shughuli zao za kiuchumi miaka mingi, walishakuwa na kesi mahakamani, wakaona wanapoteza gharama, wakaachana na kesi hizo, leo tunasubiri maelekezo ya Rais ili wananchi wangu waweze kuwa na maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule ni mji siyo vijiji, ile ni mitaa, sasa kama ni mitaa sisi hatuhitaji mtuongezee eneo, tunahitaji mtoe vigingi vyenu mlivyoviweka kwenye maeneo ya wananchi, mpeleke kwenye hifadhi, sisi wananchi tutawasaidia kulinda hifadhi yetu baada ya kukubaliana kutoa vile vigingi vyenu kuweka kwenye eneo lenu ambalo tunaliheshimu na tunalifahamu na wananchi wanaliheshimu na wanalifahamu. Tukifanya hivyo tutakuwa tumeisaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, Mheshimiwa Waziri mwende mkamalize ule mgogoro wa mpaka uliopo kati ya Dodoma na Manyara kule Kondoa. Ule mgogoro msipoangalia

vizuri unaweza ukaleta maafa baadaye. Kwa hiyo, jitahidini kwa sababu tayari mmeshafanya kazi kubwa, kazi iliyobaki ni ndogo. TAMISEMI walishawaandikia namna ya kufanya kwenda kupima vile vijiji vitatu ambavyo viliingia Dodoma, mkamalize, mkaainishe ili wale watu waishi kwa amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahifadhi wa Mkungunero leo wana maeneo wanaogopa kwenda kulinda rasilimali za nchi kwa sababu wananchi wanawatisha na silaha za jadi. Ili kuondoa hilo, wananchi waonyeshwe kwao na wanyama waonyeshwe kwao mpaka uchorwe, ueleweshwe, mtangaze kesi iishe. Wote ni Watanzania, atakayeishi Dodoma aishi Dodoma, atakayeishi Manyara wote ni Watanzania wale wale, kwa maana hiyo, tunataka hilo mlifanye na Mungu awatie nguvu, awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, atafuatia Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi ajiandae.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii iliyoko mbele yetu. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo anaendelea kuwapigania wananchi wake wa Tanzania kuhakikisha kwamba wanamiliki ardhi na migogoro inapungua au inaisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wenzangu walivyosema, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayofanya, wote tumeona, Naibu Waziri na viongozi wote ambao wanakusaidia kazi ikiwemo Katibu Mkuu, Injinia Sanga na Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote, kwa sababu bila ushirikiano madhubuti haya yote mazuri ambayo leo tunayasema na kuyapongeza, basi yasingetokea. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Muhambwe, naishukuru Serikali na wewe mwenyewe Waziri na Kamishna wa Ardhi kwa jinsi ambavyo na mimi nimefaidika na

urasimishaji ulioboreshwa kwa kutengenezewa hati katika vijiji vyangu vya Kisogwe na Busunzu. Kwa kweli kwa niaba ya wananchi wa Kata ya Busunzu tunakushukuru sana. Kwa vile umetuonjesha vijiji viwili tu ilhali tuna vijiji 50, basi naiomba Serikali iliangalie jimbo hili la Muhambwe ili nasi tuweze kufaidika na kupangiwa ardhi yetu ili nasi wananchi wetu waweze kupata hati na kuweza kufaidika na hii keki ya Serikali ya kufanya ardhi yao iwe na thamani baada ya kupatiwa hati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, pamoja na mazuri yote yaliyoongelewa nina machache ya kuchangia kwenye hotuba hii. Ukurasa wa tisa wa hotuba yako umeongelea ukusanyaji wa maduhuli. Ni ukweli usiopingika kwamba ukusanyaji wa maduhuli umeshuka, mlijipangia kukusanya shilingi bilioni 300 lakini mmekusanya shilingi bilioni 136 sawa na 45% ya makusanyo. Mwaka huu nimeona mmejipangia kukusanya shilingi bilioni 250. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sababu iliyochangia kushuka kwa ukusanyaji wa maduhuli ni tamko la Wizara ya Fedha kusema makusanyo hayo yahamie TAMISEMI. Hii imeleta taharuki na imeleta kutokufahamu na imekuwa iko kwenye *dilemma* kwa sababu sasa pesa haikuweza kukusanywa vizuri. Naomba Serikali kupitia Wizara ya Fedha, waliangalie hili tamko na kulibadilisha ili Wizara ya Ardhi iendelee kukusanya haya maduhuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu kwanza ni jukumu lao la kisheria kuweza kukusanya haya maduhuli, pia, Wizara ya Ardhi ndiyo ina watumishi ambao wamesomea ardhi, wanafahamu taratibu za makusanyo hayo ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe, Serikali imeshaweka pesa nyingi sana kutengeneza mifumo kwenye Wizara yetu ya Ardhi. Tunao mfumo wetu wa *ILMIS* ambao umeunganishwa pamoja na mfumo wa ukusanyaji wa pesa ambao unaandaa taratibu zote za upangaji, upimaji, uthamini na umilikaji wa ardhi. Kwa hiyo, mfumo huu uko kwa pamoja ukifanya kazi zote za ardhi ikiwemo kukusanya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Ardhi ndiyo ina ile kanzidata ya nani anamiliki nini? Nani anamiliki wapi? Nani anapaswa kulipa nini? Kwa hiyo, kwa sababu zote hizi muhimu ambazo Wizara ya Ardhi inazo, naomba niishauri Serikali iliachie jukumu hili Wizara ya Ardhi, iendelee kukusanya hayo maduhuli ili hata hili lengo walilojiwekea la kukusanya shilingi bilioni 250 liweze kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tumempongeza Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo anaendelea kuziweka vizuri Kliniki za Ardhi. Tumetembelea kliniki mbalimbali anazokwenda, zile kliniki ziko katika ukweli na uwazi. Ni kweli kabisa imekuwa faraja kwa Watanzania ambao wamedhulumiwa kwa muda mrefu, Mheshimiwa Waziri amekwenda kurudisha furaha, amekwenda kurudisha mali zao zilizopotea. Takwimu hazisemi uongo, amesema ameshughulikia migogoro zaidi ya 7,000 na katika hiyo 4,500 ameweza kuimaliza na hii 2,000 inaendelea kufanyiwa kazi. Tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hiyo migogoro aliyoitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri leo yupo kesho hayupo, iko sababu ya makusudi kabisa ya kuweka mfumo wa kitaasisi ambao *whether* Jerry yupo au hayupo, mtu yeyote atakayekuja pale basi kuwe na mfumo maalum wa kuweza kufanya hii migogoro iweze kutatulika badala ya kusimama mmoja au kusimama watu wenye nia njema au nzuri, wachache wakabaki hawafanyi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba pamoja na kuwa wanafanya kazi vizuri sana, bado wako watendaji wachache ambao hawajaelewa nini Mheshimiwa Rais akiongelea kuhusu *4R*. Bado wanafikiria tuko wapi sijui, kwa maana bado wanadhulumu wananchi na bado wanakula rushwa. Kwa hiyo, kama Serikali itaweka mfumo wa kitaasisi ambao utashughulikia hii migogoro ya ardhi, basi tunaamini kabisa shida ya Watanzania na migogoro itaisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongezea kwenye suala hili la migogoro, wote tunafahamu jinsi gani wananchi ambao wana migogoro ya ardhi wanapata shida sana kwenye taasisi zetu za

kisheria. Kipo kivuli cha kusema migogoro ya ardhi ni kosa la madai, kwa hiyo, linachukuliwa kama kosa *light* sana. Ndiyo maana tunaona wako matajiri ambao wao wamekuwa sasa maarufu na umewaonesha hadharani jinsi gani wao ndio miamba wa ku-*forge documents* na hati kwa sababu wanajua hata wakienda Mahakamani, hilo ni kosa la madai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, kosa hili basi hizi taasisi iangalie jinsi gani inaweza ikaliweka ikawa ni kesi kali na likachukuliwa kama ni kesi za jinai ili hawa watu wanaofanya haya matatizo, basi waogope kufanya uvamizi wa hizi mali za wananchi. Wajue kwamba wakienda kwenye hizi taasisi, basi sheria kubwa itachukuliwa ili waweze kuacha kabisa hayo matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala ambalo limekuwa ni changamoto sana katika Bunge hili na Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakiendelea kulalamika, nalo ni juu ya fidia. Wizara ya Ardhi imepewa dhamana ya kufanya uthamini wa maeneo mbalimbali ambayo Serikali au taasisi inataka kufanya uwekezaji. Wizara imetimiza jukumu lake vizuri sana chini ya dada yetu Evelyne kuwasaidia hawa ambao wanataka kuwekeza au kufanya mradi pale kuweza kupata uthamini ambao ni halali ili Serikali na wananchi waweze kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko changamoto moja ya kucheleweshwa kulipa fidia ilihali mradi unaendelea kutekelezeka. Wengi wamesema hapa, kule kwetu Kigoma uwanja wetu wananchi wameshaambiwa wasiendeleze, lakini hawajalipwa fidia. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuliona hili na kuamua kuja na Waraka Na.1 wa 2024 kwa ajili ya uthamini ambao utasimamia taratibu nzima za uthamini wa hizi mali kabla ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuja na waraka ni jambo moja, lakini kuutekeleza waraka ni jambo la pili. Pia kuja na waraka ni jambo moja lakini kuusimamia waraka huu ni jambo la pili. Naiomba Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Waraka huu usimamiwe vizuri sana. Hamna sababu ya Wizara ya Ardhi kuhangaika na kufanya uthamini ilhali Serikali au taasisi inayotaka kuwekeza au

inayotaka kujenga mradi haina pesa ya kuwalipa wananchi. Mwananchi anaambiwa baada ya miezi sita tuta-*review* lakini hilo jambo halitekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu wanalia na wanalalamika kwani wameshapisha miradi lakini hawajalipwa pesa. Mheshimiwa Waziri nakuomba, huu Waraka umeutengeneza ili uweze kuleta tija kwa wananchi wetu wa Tanzania, basi usimamiwe kimadhubuti kuhakikisha kwamba kabla ya uthamini, taasisi au Serikali ijiridhishe na kuthibitisha kwamba inazo pesa za kuwalipa hawa wananchi ili baada ya uthamini, basi wananchi hawa waweze kupata pesa yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naungana na wenzangu wote waliosema kwamba mwarobaini wa hii migogoro ni kutengeneza matumizi bora ya ardhi ya nchi yetu na kuipanga nchi yetu ili kuhakikisha kila mtu anamiliki kipande chake. Wote wameonesha ukubwa wa hili tatizo kwa sababu wote tuna migogoro katika majimbo yetu. Migogoro ya wakulima na wafugaji ni matatizo ambayo yako karibu kila jimbo na yote yanatokea kwa sababu nchi yetu hatujaipima kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hapa katika taarifa zao, ni 33% ya nchi hii tu ndiyo imetengenezewa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Hii ni kama vijiji 4,000 hivi tu. Kwa hiyo, naiomba Serikali, kama Mheshimiwa Waziri ambavyo amekuwa akisema kila siku, tunahitaji shilingi bilioni 120 kuweza kuipima nchi yetu. Basi Serikali iweke nia ya dhati kabisa ya kuipatia Wizara hii shilingi bilioni 121 ili tuweze kuipima nchi yetu ili kuweza kupunguza migogoro ya ardhi katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza ajiandae.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami kuweza kuchangia hoja iliyopo Mezani. Awali ya yote naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, natumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyochukulia mambo yote ya kisekta kwa maslahi mapana ya Watanzania. Hata katika hii Wizara kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Waziri, yeye alipewa shilingi bilioni 450 kwa ajili ya kulipa madeni ya kandarasi na miradi. Hiyo inaonesha namna alivyo na dhamira njema ya kuondoa kero na migogoro ya ardhi iliyokuwepo kabla yeye hajaingia ama inayoendelea kwa ajili ya kuwanufaisha Watanzania walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Jerry. Mheshimiwa Halima Mdee wakati anachangia alisema kwamba anatambua Mheshimiwa Jerry ana hekima. Sasa mimi nikawa najiuliza, wale waliokuwa wanasema Mheshimiwa Jerry ni mzee waliangalia nywele zake, lakini wengine wakasema ni kutokana tu kwamba pengine ana matatizo mengi, lakini kumbe ni kutokana na hekima ndiyo maana nywele zake pia zimekuwa ni mzee wa hekima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nampongeza kwa sababu, hata kwa hii kliniki aliyoianza imeonesha manufaa makubwa sana na watu wamekuwa wakiikimbilia na hivyo ina tija na ina matokeo ya papo kwa papo. Hongera sana, hata kama tunakutwisha uzee, natambua kwamba wewe sio Mnyamwezi, lakini mzigo huu Mheshimiwa Rais alikuamini nasi tunakuamini. Endelea kuchapa kazi na wewe ndio Mnyamwezi kwenye eneo la ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri maeneo machache. Kwenye kazi alizopanga Mheshimiwa Waziri 2024/2025, mkazo umewekwa kwenye kupanga ardhi. Hapa tunaomba aongeze kasi kweli kweli na hii imezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi humu ndani. Mimi naona katika kupanga ardhi pale atakapofanya upimaji, hiyo ndiyo tutakuwa sasa tumezingatia lile eneo la matumizi bora ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa itapunguza gharama ya miradi kwenye sekta nyingine. Kwa mfano, kuna kipindi nilichangia huku kwamba wakati mwingine tunakuwa kama hatusomani, lakini utaona kabisa kuna wananchi wanaanzisha makazi mbali kabisa tofauti na wananchi wengine waliko. Wale wanahitaji baadaye wapelekewe huduma za msingi kama vile afya, maji, na shule shikizi zinazojengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tungekuwa na matumizi bora ya ardhi na maeneo yaliyopimwa kama ambavyo ameweka kama ni kipaumbele chake cha kwanza, ina maana gharama za kwenye sekta nyingine za kujenga shule shikizi, kujenga miradi ya maji ya kuwafuata wananchi watano ambao wamejitenga kabisa tofauti na makazi ya walio wengi, gharama nyingine za afya, zahanati zile za muda na kadhalika zingepungua kwa sababu, kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi, wananchi wengi walioko maeneo fulani wanatakiwa wapelekewe huduma za kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, eneo hili la kupanga ardhi kwa maana ya kupima, sisi kule kusini utakuwa umetusaidia sana. Sasa hivi wananchi kule tunaona kuna migogoro ya wakulima na wafugaji. Kama ardhi yote ingekuwa imepimwa, wale wafugaji hatusemi ni watu wabaya, lakini kwa vile wanaenda kwenye maeneo ambayo hawajatengewa wao kwa ajili ya kufuga na ndiyo migogoro inapoanzia. Kwa hiyo, hilo nalo lingekuwa limepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa suala la matumizi bora ya ardhi ni la msingi kwa sababu, tunaona hata kule kwenye Wizara za kisekta lipo lakini halisimamiwi vizuri. Tumeona hata wale Kamati ya Maafa ambayo tumeitungia sheria hivi karibuni, lile jambo la kudhibiti maafa pia litawezekana kama matumizi bora ya ardhi tutakuwa tumezingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo naomba nishauri ni kuwa na *land bank*. Ni muhimu sana kuwa na maeneo tunayoyapima na tusiyatumie kwa miaka 50 – 100. Najiuliza leo, ingekuwaje kama hapa Dodoma kusingewekwa akiba ya ardhi kwa ajili ya kujenga majengo ya Serikali? Tunaona yalivyojipanga

pale vizuri, ni kwa sababu waliofanya hivyo waliweka hiyo akiba na ndiyo maana Serikali imeweza kuhamia na yale maeneo yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kila eneo likiwa linavamiwa tu kiholela, haitafaa. Ni muhimu kuweka *land bank* na hayo maeneo yasiuzwe kwa ajili ya masuala fulani muhimu ya kimkakati ambayo yatakuja kutusaidia baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu, unatambua Idara ya Ardhi imehamishiwa Wizara ya Ardhi, lakini ni tofauti na *TARURA* na *RUWASA* ambapo tunaona wao mambo yao yanakwenda vizuri. Idara ya Ardhi, sawa wako kule, lakini wakienda kwa Mkurugenzi kuomba karatasi tunajua hawapati, wakienda kwa Kamishna *OC* hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tnatambua kazi kubwa anayoifanya, lakini Idara za Ardhi zilizopo kwenye halmashauri kwenye Serikali za Mitaa kule ambapo bado wengine wanaendelea kutumia zile ofisi, *OC* ni ngumu. Kwa hiyo, nao ni vizuri sasa, ili wale walioko kule wapime, na kushughulika na migogoro ya mipaka ya wilaya na wilaya ama vijiji na vijiji, ni vizuri wajengewe uwezo kwa maana ya kuwa na vifaa, pia hata hizo *stationery* ili waweze kufanya kazi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwenye hotuba yake amesema ujenzi wa jengo la biashara pale Masasi utaanza kwa bajeti hii ya 2024/2025. Tunamshukuru sana, na pia tunamshukuru pia sana Mheshimiwa Rais wetu. Sasa kuna madai ya fidia Uwanja wa Ndege Masasi. Uthamini ulishafanyika na imeshaenda kwa Mthamini Mkuu wa Serikali na wananchi wanaendelea kuwa na matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sasa, kabla ya Uwanja wa Ndege haujaamua kuchukua kipande kidogo kwa ajili ya kuanza shughuli zake, ni muhimu suala la fidia likawekwa vizuri, wananchi wale wakafidiwa ili shughuli zote ziendelee na wananchi kwa kweli wana matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amekuwa akitibu kwenye maeneo mengine, ni imani yetu pia Masasi atatufikia, na fidia ile wananchi watalipwa, hivyo shughuli ziendelee kama vile tunavyoendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwa kazi inaendelea, na iendelee maeneo mengine kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala dogo sana ambalo nilikuwa naomba na lenyewe ni muhimu pia. Waheshimiwa Wabunge wamezungumza huku kuhusu migogoro ya mipaka. Maeneo mengine kuna mgogoro wa mpaka kati ya mkoa na mkoa, wilaya na wilaya lakini wakati fulani unakuta migogoro kati ya kijiji na kijiji. Sasa hii kwa kweli siyo ya kumtoa Mheshimiwa Waziri Wizarani aende kule kwa sababu nchi yetu ni kubwa. Ni vizuri tu akatoa mwongozo na wale walioko kule kama ni suala la kwenda kutoa elimu, wakaenda wakaifanya ili wananchi waendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii migogoro wakati mwingine unaiona inatokea kwa msimu. Kwa mfano, katika maeneo ya uzalishaji kama kule kwetu, kipindi cha korosho unakuta sasa ndiyo mgogoro. Kwa sababu gani? Kwa sababu unajua upo ule ushuru ambao ndiyo pengine halmashauri za vijiji zimekuwa zikigombea. Kwa hiyo, ni vizuri hili likawekwa sawa ili kwa kweli kila mwananchi, kila Halmashauri ya Kijiji eneo lilipo, kwa mfano kama ni mgogoro wa kijiji na kijiji, ikatambua maeneo yake na ikaondoa hizo hali za sintofahamu ili kazi za wananchi ziendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi, siyo vyema nikagongewa kengele. Narudia tena kumpongeza Mheshimiwa Jerry na kaka yangu Mheshimiwa Pinda kwa namna walivyo. Kwa kweli wote ni watu wapole, na wamekuwa wakitusikiliza kila tunapowajia. Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki na kamwe msipandishe mabega, Watanzania wana matumaini sana na ninyi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Agnes. Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, atafuatia Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo ajiandae.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye katujaalia uhai na kutufanya tuweze kutoa mchango wetu kwenye Wizara hii ya Ardhi. Mchango wangu utakuwa kwenye maeneo kama matatu. Kabla sijatoa mchango wangu, naipongeza Wizara kwa maana ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wote. Nawahakikishia wako kwenye njia sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jerry kwa namna alivyoanza na namna anavyoendelea, nakumbuka Mwenyekiti mwenzangu wa halmashauri, anaenda vizuri. Namtia moyo na Mwenyezi Mungu aendelee kumlinda. Kwa namna mnavyoenda, nina kila sababu ya kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu kama kocha, amejua namna gani anaweza akapanga timu yake ili malengo anayoyatarajia na sisi Watanzania, matazamio yetu yaweze kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utakuwa kwenye maeneo matatu. Eneo la kwanza ni juu ya Mabaraza ya Ardhi. Kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 25 anaongelea Mabaraza ya Ardhi ambayo yameundwa kwa mujibu wa Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Sura Na. 216. Nawapongeza kwamba mpaka sasa kuna mabaraza takribani 139 yameundwa na katika hayo, mengi yanafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Mabaraza ya Ardhi kwa ngazi ya wilaya kufanya kazi, bado kuna changamoto. Naomba Wizara ione namna gani pamoja na kufanya kazi, iwasaidie ili wafanye kazi kwa ufanisi kwa sababu kufanya kazi ni jambo moja lakini kufanya kazi kwa ufanisi kufikia malengo ya wananchi ni jambo la pili ambalo ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, mabaraza haya hayana vifaa. Kukosekana kwa baadhi ya vifaa kwa mfano wanahitaji *photocopier*. Wanapohitaji kutoa *photocopy* kwa mfano, kuna maeneo wanaomba wateja watoe *photocopy* au wawachangishe ili wakatoe *photocopy*. Sasa tafsiri ya

mwananchi, anaona kama vile ameombwa rushwa, jambo ambalo halitoi tafsiri nzuri kwa Serikali. Kwa hiyo, pamoja na kuunda mabaraza haya, basi naomba Wizara ijitahidi kuhakikishe kwamba yanakuwa na vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwapa vifaa, Wenyeviti wa Mabaraza haya bado maslahi yao yana changamoto kubwa na muundo wao wa ajira una changamoto vilevile. Kwa hiyo, yajengwe mazingira ya kuwafanya Wenyeviti hawa wa Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya wawe *comfortable* na wa-*feel proud* kufanya kazi wanazozifanya kutoa haki kwa wananchi wetu na kuondoa manung'uniko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili la Mabaraza ya Ardhi, shida kubwa ipo kwenye Mabaraza ya Ardhi ya Kata. Kuna shida kubwa kwenye muundo wake, kuna shida kubwa kwa namna yanavyowezeshwa kuweza kufanya kazi jambo ambalo linasababisha migogoro mingi sana ya ardhi kwenye maeneo yetu. Nikitolea mfano Ukerewe, sisi ni eneo dogo la visiwa. Kilometa za mraba ambazo ni ardhi, tuna kilometa za mraba 640 na watu karibu 400,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaona katika kilometa ya mraba moja, inakaliwa na watu takribani 600, hivyo migogoro inakuwa mingi sana. Migogoro inakuwa mingi kwa sababu gani? Kwa sababu ufanisi wa mabaraza yetu ya ardhi ya kata ni mdogo sana. Hii ni kutokana na muundo wa mabaraza haya ama ni watu gani wanatengeneza mabaraza haya, wana mwongozo gani na wana utaalamu gani? Ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kumekuwa na mapendekezo mengi ama mabaraza haya yasimamiwe au haki kwenye mabaraza haya ipitie Mahakama zetu au namna nyingine yoyote ile. Mmekuwa na kigugumizi kufanya maamuzi kwenye eneo hili. Nashauri, kama haiwezekani kupitia Mahakama mabaraza haya kutoa haki, basi kiundwe chombo ambacho ni huru kama ilivyo taasisi nyingine ili iweze kujisimamia chini ya Wizara ya Ardhi ili mabaraza yetu ya ardhi ya kata yawe na ufanisi yaweze kutoa haki kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko na manung'uniko mengi sana ya wananchi huko chini kutokana na migogoro inayosababishwa na mabaraza yetu ya ardhi ya kata. Hima hima tafadhali Mheshimiwa Waziri, chukueni hatua haraka, fanyeni maamuzi ili kuweka mfumo mzuri kwenye mabaraza yetu ya ardhi ya kata ili wananchi wetu kule chini waweze kupata haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo natamani kuchangia ni juu ya mabadiliko ya Sera ya Ardhi. Natambua na kwenye hotuba umegusia, mko kwenye mchakato wa kufanya mabadiliko ya Sera ya Ardhi na hasa kwenye maeneo ya fukwe ili kuona namna gani sasa umiliki kwenye maeneo ya fukwe unaweza kuwezesha watu kuwekeza kwenye maeneo yale kama ni wafanyabiashara au namna nyingine yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri, wakati wakiendelea na mchakato huu na watakapofikia maamuzi kwenye mchakato huu wa mabadiliko ya Sera ya Ardhi wasiweke *uniformity* kwenye maeneo yote, wazingatie maeneo tofauti kulingana na mazingira. Maeneo kama Ukerewe ambayo ni visiwa ni sehemu ya makazi vilevile, kuna watu wanaishi pale, wamezaliwa pale, vizazi vyao vyote wanaishi pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haiwezi kuwa rahisi sana kwamba anakuja mwekezaji apewe tu au maamuzi yakafanyika akapewa eneo ama kisiwa. Jambo hili litaathiri sehemu kubwa ya jamii inayoishi kwenye maeneo yale. Kwa hiyo, wakati sera hii inafanyiwa mabadiliko izingatie maeneo tofauti kulingana na mazingira ili kwenye maeneo ya visiwa kama Ukerewe ambako pamoja na kwamba ni visiwa, lakini vilevile ni makazi ya wananchi, jamii husika ishiriki kwenye mchakato wote ili haki yao ya msingi isipotee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ambalo nilitamani kuchangia ni juu ya upimaji, upangaji na usajili wa ardhi. Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia na kuonyesha umuhimu wa maeneo yote ya nchi yetu kupimwa. Hili ni jambo la msingi sana kwa kuwa litatuondolea migogoro, kwa sababu kila eneo litajulikana kwamba eneo hili ni eneo kwa ajili ya shughuli gani? Jambo ambalo litatoa urahisi, na kama mtu mwingine

yeyote atakwenda tofauti na misingi ya maelekezo ya eneo husika, basi hatua zitachukuliwa. Hii itatuondolea migogoro mingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kutoa mkopo kwenye halmashauri ili ziweze kupima ardhi kwenye maeneo husika. Ukerewe ni miongoni mwa maeneo tuliyopata mkopo huo. Nimemfuata Mheshimiwa Jerry mara kadhaa ili aweze kutusaidia fedha nyingine, ingawa nimesikitika kwenye taarifa yake hakuitaja Ukerewe kama ni miongoni mwa halmashauri ambazo zimeshamaliza mikopo yake. Naomba nimhakikishie kwamba tumemaliza mkopo huo, na kwa sababu ametoa utaratibu mpya, basi tutaomba tufikiriwe kupata mkopo mwingine ili tuweze kupima maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukerewe kama ilivyo Zanzibar, ni Zanzibar nyingine ya Tanzania. Kama tutaipima tukatoa mwongozo mzuri, ikatumika vizuri, ni eneo zuri sana la utalii, na shughuli nyingi za kiutalii zinaweza kufanyika na kuliingizia Taifa hili kipato. Kwa hiyo, bado tunahitaji fedha nyingine ili tuweze kupima eneo letu lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kliniki yake anayoendelea nayo. Ushauri wangu kwenye eneo hili, hawezi kwenda kila mahali. Naomba sana, kama anaweza kutengeneza mfumo kwenye maeneo yetu kule wilayani na kwenye kata kuwe na kliniki za namna hiyo, ili watalamu kutoka wilayani pale, na kama italazimika labda mtalamu mmoja kutoka mkoani na kadhalika wakashiriki, basi maeneo yaliyoko chini kule vilevile kuwe na kliniki za namna hiyo ili kuweza kushughulikia migogoro mingine mbalimbali iliyoko kwenye maeneo yetu. Jambo hili litafanya jamii yetu iweze kuwa salama. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru. Nimalizie kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu, natambua kuwa una Katibu Mkuu bora sana…

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** …ninaamini watafanya mambo makubwa na Mwenyezi Mungu awajalie sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, atafuatia Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo na Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, ajiandae.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa maoni yangu kuhusu Bajeti ya Wizara ya Ardhi iliyo mbele yetu. Nami napenda nichukue nafasi hii kuwashuruku Mawaziri, Naibu Waziri na watendaji wao wote kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mfupi nimemwona Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wameonyesha umahiri mkubwa katika kushughulikia migogoro, na hasa mingine ambayo ilikuwa imeshindikana. Kwa hiyo, nina uhakika kwamba hata mawazo yetu tutakayoyatoa siku ya leo kuhusu bajeti ambayo ni tegemeo, fedha zinazoombwa zitajibu matatizo ya waliyonayo wananchi kuhusu mambo ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo machache. La kwanza napenda kuongelea kuhusu gharama za kufanya uhamishaji wa umiliki pale watu wanaponunua nyumba na wakitaka kubadili hati ili ziwe zao, gharama ni kubwa. Gharama hii ambayo inaitwa *Capital Gain Tax* ambayo inatozwa na *TRA* pale ambapo *evaluation* inafanywa ni kodi kubwa ambayo inawazuia wananchi wasiweze kubadili hati hizi na kuamua kukaa na hati za zamani. Hii kodi inakwenda kuanzia asilimia tatu, wengine wanalipa 20%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoomba, Wizara iliangalie jambo hili ili kodi ijulikane, kwamba ni asilimia tatu, nne ama kumi. *TRA* watoze *Capital Gain Tax* ambayo inawezesha wananchi ili hata wale ambao hawana uwezo wa kulipa na kuweza kubadili zile hati na umiliki uwe wa kwao badala ya kuendelea kukaa na hati za watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitaongelea zaidi kuhusu umilikishaji pandikizi. Mheshimiwa Waziri ameusoma vizuri katika ukurasa wa 18 aya ya 30 na kuendelea katika kitabu chake. Tunamshuru sana kwa kuleta kliniki hizi, ni nzuri sana. Tunamsifu na tunaendelea kumwombea. Asiogope, sala zinazidi kila kitu. Sisi wanyonge ambao tumeathirika na kuonewa kutokana na hiki kitu ambacho kinaitwa uwakilishaji pandikizi *(double allocation)* tutazidi kumwombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno nitakayoyasema leo naomba nisemee watu wote ambao wanapewa viwanja halafu wanadhulumiwa; ambao wanapewa viwanja halafu mtu unalipia mara mbili, na wako wengi. Ukienda pale, hivi inatwaje ile? *City Council,* Jiji pale, ukitaka kuona dhahma, nenda Kitengo cha Ardhi uone watu wanavyoteseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena wameweka taratibu, wanakwenda kata kwa kata, lakini dhahma ya watu utakayoikuta pale, utaona namna hiki kitengo cha ardhi katika jiji kinavyokuwa. Mimi nawaita zimwi kabisa la pembe mia. Hata yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri, ataona kwamba watu wana malalamiko mengi, na amesema namna wanavyopewa viwanja na kudhulumiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe historia yangu. Mimi ni mwathirika. Sasa kama Mheshimiwa Mbunge anafanyiwa hivi, je, watu wengine wa kawaida ambao wanasota pale inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilipewa kiwanja tarehe 16/06/2022. Nililipa tarehe 29/06/2022. Haikuchukua hata wiki mbili, nimelipa kwa *control number* 992000375444 na hii ni akaunti ya Mkurugenzi wa Jiji. Tunashukuru Jiji la Dodoma. Ni Jiji la Dodoma hapa siyo Arusha, akaunti ya Mkurugenzi wa Jiji Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka ilipokuja kliniki ya kwanza iliyoletwa hapa na Mheshimiwa Mabula nikaona hapa ni bora nikimbilie huko ili nami niende kutafuta haki yangu. Nilichokikuta kiwanja hiki kilishapewa hati mwaka 2021, nami nimelipa na yule amelipa. Sasa nasema haya mambo ni *criminal.* Unawezaje

ukanipatia *control number* mimi halafu ukampa mtu mwingine *control number* halafu Mkurugenzi anakaa pale ofisini anaangalia watu wake wanavyofanya uchafu wa namna hii? Hii ni *criminal case,* siyo kama ile aliyokuwa anasema Mheshimiwa Kunambi leo asubuhi. Wote tumepewa *control number,* mwenzangu analipa nami ninalipa. Yeye amepewa kiwanja, ana hati, lakini mimi sina hati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu sana, nilipokwenda kuomba hati kuna mtu mmoja anaitwa Mwakasitu pale halmashauri, nimepeleka *documents* halafu picha zimepotea. Miongoni mwa *issues* ambazo ziko pale ni kwamba wanapoteza *documents* za watu kwa makusudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yupo mwingine anaitwa Mwakajuja amekwenda na *documents,* nimepeleka *document* mara sita. Nenda wapige *photocopy,* na pale kwenu halmashauri ni ghorofa, unatembea panda teremka, panda teremka, nenda chumba hiki. Ndivyo wanavyowafanyia watu. Mimi nimetembea mpaka viatu vinaisha visigino. Amekimbia mpaka wamemhamishia Kigoma na *documents* zangu. Sasa nimeanza kwenye kliniki hii ya leo, hii ambayo ameileta, mpaka barua kwa Mkurugenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiseme mengi, kuna mtu ninamtaja, yuko hapa, nami nimesema nitawataja, anaitwa *Loveness*. Wamalize mgogoro, anipatie kiwanja changu kabla sijakwida mtu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kumwonyesha ni namna gani hii masijala inafanya. Hii masijala ambayo imejaa zimwi la mapembe inabakia ya nini? Kwa nini wasiindoe hii masijala? Zamani Mheshimiwa Lukuvi alishataka kuvunja masijala ya Dar es salaam kule, ninyi mnashindwa nini? Haina maana yoyote pale, wanatesa watu. Sio wote, sijasema kwamba ni wote, sio wote, lakini kusema ukweli mambo ninayoyasema nayasema kwa jazba kabisa nikitetea na watu wengine ambao wanasota namna hiyo. Kwa hiyo, naomba hizi taratibu ziangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu wana dharau. Mtu ukienda wanakutazama, kwa sababu wameshakula fedha, ili ukate tamaa, uache kiwanja chako na fedha yako ife. Nimesema yangu haifi na naomba na wengine wanaonisikiliza tusote, tutembee. Nimeshakwenda kwa Mheshimiwa Jerry na nimeshamwambia. Amenishika mkono amenipeleka, lakini hakuna chochote. Hata yeye inawezekana wanaona labda eeeh! Yaani vitu vidogo hivi twende kwa Mheshimiwa Waziri jamani! Kila mtu akiibiwa kiwanja aende kwa Waziri! Mapapa wa viwanja, kwa Waziri? Atakonda na wengine watasema ni mvi, hapana tutamkukondesha sisi wenyewe.

Mheshimwia Mwenyekiti, kupitia Bunge hili na maneno atakayoyasema, naomba kiwanja changu. Wako pale, wanasikia na nimewaambia kwamba ninakwenda kuyasema leo hii hii kwa kuwataja majina kwa sababu wamechosha. Wamenichosha na wanachosha wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwakagenda pale amepigwa. Siku nyingine nilimkuta Mheshimiwa Mabula, tulikutana kule, naye alishapigwa. Waheshimiwa Wabunge humu wananyamaza tu, lakini wameshapigwa na wale watoto. Unanunua, wanauza, wanatoa hati, *that is criminal*. Kwa nini wasiwachukuliwe hatua? Kwa nini wasipeleke mambo haya kwenye Mahakama? Wawashitaki watu hawa ambao wanafanya hivi? Huu ni wizi, ni wizi mkubwa. Kama ofisini nilikuwa na *control number* kwamba unalipa barabarani sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia juzi kuna mfanyabiashara mmoja alikuwa anaongea na *RC* Makonda, amemwambia kitu cha namna hii. Tunalipa fedha zinaingia kwenye *control numbers* za mifuko mingine. Serikali wana mikono mirefu, kwa hiyo, naomba wafanye uchunguzi ili walione hili. Wafanye uchunguzi na waondoe haya mambo ambayo wanafanyiwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wananyanyaswa na wanaibiwa na hao watoto halafu ukienda wanakutazama tu? Mimi jana aliniona, nilikuwa nimekasirika, nilitaka kukwida mtu kusudi waandishi wa habari waje, halafu watangaze kwamba kuna Mheshimiwa Mbunge Mzee mmoja amemkwida. Yaani

aliponea chupu chupu, nilitaka kumkamata kabisa shati. Hatuwezi kwenda namna hii, lazima tuonyeshe *reaction,* wasitunyanyase namna hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo sisemi mengi, nilikuja nimelibeba hili *purposely* kabisa, kwamba niseme kwa niaba ya wengine ambao hawana uwezo wa kuja hapa ili…

**MBUNGE FULANI:** Na faili lako la malipo.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshatembea na faili kila mahali ninapokwenda, utadhani naomba kazi. Mimi na faili langu kila mahali, kiwanja namba 653 kila mahali, kiwanja jamani nimelipa. Yaani kila mtu anakupiga teke. Huyu anakupiga teke huku na mwingine huku, haiwezekani. Tena nawaambia leo hii hii kiwanja changu nikipate, au kesho nikienda kwa Mkurugenzi nitapiga yowe kuanzia pale ghorofa ya kwanza. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, ahsante. Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, atafuatia Mheshimiwa Tauhida Gallos Cassian na Mheshimiwa Ally Issa Mchungahela ajiandae.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Wizara ya Ardhi. Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza napenda nimshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi alitilia mkazo kwenye masuala ya ardhi nchini Tanzania. Vilevile napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Jerry Silaa na Naibu wake Mheshimiwa Geophrey Pinda na watendaji wote wa Wizara ya Ardhi kwa kliniki ya ardhi waliyoianzisha, kitu ambacho awali hakikuwepo, hongereni sana. Tumeona jinsi ambavyo mnatatua matatizo ya wananchi wa Tanzania, matatizo ambayo mengi yanayohusiana na ardhi; migongano ya ardhi, *double allocation* na mengine mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kuchangia kama jinsi ripoti ya Kamati yetu ilivyosomwa hapa Bungeni. Mimi nikiwa kama Mjumbe wa Kamati tumekuwa tukiwasiliana na Wizara ya Ardhi, lakini tuna mapendekezo yetu ambayo tuliweka kama Kamati. Mapendekezo na ushauri wa Kamati uliosomwa leo hapa umeonyesha Mradi wa *LTIP* kwamba unasuasua, ina maana hauna kasi, hautekelezwi kama inavyopaswa kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *LTIP* ni mradi wa uboreshaji wa usalama wa milki za ardhi nchini. Mradi huu ni ule ambao una mkopo wa dola bilioni 150, sawa na fedha za Kitanzania shilingi bilioni 345. Fedha hizi ni za mkopo, hivyo Wizara ya Ardhi inatakiwa kwanza izitumie vizuri, lakini zaidi ya kuzitumia vizuri, mipango yake ya matumizi ijulikane, kwamba zimefanya kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ripoti ya Mheshimiwa Waziri aliyoisoma na kuiwasilisha hapa leo ameongelea Mradi wa *LTIP,* lakini hakuongelea kwa upana. Amesema unakwenda kuboresha hati za miliki nchini Tanzania, lakini kwenye ripoti yake ukurasa wa 60 ameelezea kuwa amepima vijiji 843.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023 wakati Bajeti ya Ardhi ilipopitishwa hapa tulitoa mapendekezo. Mradi huu ulikuwa unapima vijiji 250 kwa muda wa miaka mitano, Bunge likapendekeza, na kwenye mapendekezo ya Kamati tukapendekeza kuwa vijiji viongezwe. Hii ilikuwa ni mwaka 2023. Sasa kitu ambacho ninajiuliza, tangu mwaka 2023 mpaka sasa hivi, ni kama miezi kumi imepita. Leo kwenye ripoti Mheshimiwa Waziri ameandika kwamba tayari wameshapima vijiji 843.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tukiwa kama Kamati, tumetembelea Wilaya ya Ruangwa katika Kijiji cha Nkatila, na huko tukashuhudia utoaji wa hatimiliki kwa kile Kijiji. Pia tulitembelea Maswa. Hivi vijiji vingine 843 hatujavitembelea. Pia ningependa kujua kama hivi vijiji tayari vimeshapewa hati na Tume ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi, kwa sababu naona inakuwa ni ndoto ya ajabu kwa muda wa mwaka mmoja vijiji 843 viwe vimepimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi inahitaji kama shilingi bilioni 30 ili iweze kupima vijiji, lakini Tume hii imekuwa ikipewa fedha kidogo kwa ajili ya kupima vijiji hivyo. Matokeo yake ni kuwepo kwa migogoro ya ardhi ambayo haiishi Tanzania. Migogoro hii inatokana na sababu kwamba Watanzania wanakuwa hawajui maeneo wakalime wapi au wakafuge wapi. Vijiji vimepimwa lakini havijapangiwa matumizi ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo namwomba Waziri angaalie utaratibu wa kuweka kasi kwenye mradi huu wa *LTIP*. Katika hotuba yako umeeleza pia kuna ujenzi wa ofisi 25 za mikoa, lakini kwenye Ripoti ya Mheshimiwa Waziri ameonesha kwamba ndiyo kwanza mchakato unaendelea. Mheshimiwa Waziri, huu mradi ni wa miaka mitano, hizi ofisi utazijenga lini kwenye mikoa kwa muda mfupi? Sasa hivi huu mradi una kama miaka mitatu. Mradi umeanza toka mwaka 2022, hii ni 2024 ofisi hazijajengwa, bado zipo kwenye mchakato, mradi wa miaka mitano. Je, kuna uhakika wa kumaliza hizi Ofisi za Ardhi za Mikoa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachelea kusema kwamba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja, atuambie. Pia Mheshimiwa Waziri kwenye ripoti yake hajaweza hata kueleza huu mradi ambao mpaka sasa una miaka mitatu umetumia fedha kiasi gani? Tunashukuru kwa kliniki, ni za huo mradi, lakini tungependa kupata ufafanuzi, fedha za mradi zimetumika kiasi gani mpaka sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia leo ni suala la wale Wafanyakazi wa Mabaraza ambao wamefanya kazi kwenye Ofisi za Ardhi na walishastaafu, lakini hawalipwi fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wafanyakazi sio wengi, lakini wamekuwa wakidai malipo yao kwa muda mrefu sana. Wizara ya Ardhi haiwalipi na hawa watu walifanya kazi kwenye Ofisi za Ardhi kwenye Mabaraza. Ina maana waliisaidia Wizara ya Ardhi, lakini hawalipwi fedha zao. Wamekuwa wakipigwa danadana, leo wameenda huku, kesho nenda huku, tutawatumia *cheque,* lakini

Wizara ya Ardhi haijawekea umuhimu wa kuwalipa wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu walisaidia na walifanya kazi Wizara ya Ardhi, wangewekewa kipaumbele walipwe fedha zao, kwa sababu inaonekana kwamba watu wamefanya kazi wametumika, lakini kwa kuwa hawapo tena kwenye sekta ya ardhi, wanaonekana hawajafanya kitu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni zile halmashauri ambazo zilikopeshwa fedha kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Zipo halmashauri mbazo zilipewa hizo fedha, zimesharudisha, tunazipongeza sana. Pia zipo halmashauri nyingine zenyewe zimerudisha fedha nusu, bado zinadaiwa na nyingine hazijarudisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba zile halmashauri ambazo hazijarudisha zile fedha ziweze kurudisha ili halmashauri nyingine ziweze kukopeshwa na ziweze kuendelea na utaratibu wa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi inapopangwa inaondoa matatizo mengi, lakini fedha hizi halmashauri zilikuwa zimekopeshwa toka mwaka 2021 mpaka leo halmashauri hizo zinaendelea kukaa na mkopo huo na halmashauri nyingine zinashindwa kukopeswa kwa sababu fedha hazijarudishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulizungumza ni suala la Wizara ya Ardhi kuweka mfumo unaoeleweka kwa ajili ya bili za ardhi. Kama ilivyo kwenye Wizara ya Maji, mtu anapata bili yake mkononi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hitimisha, muda umeisha.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Taska Mbogo. Mheshimiwa Tauhida Gallos Cassian, atafuatia Mheshimiwa Ally Issa Mchungahela na Mheshimiwa Joseph Kakunda ajiandae.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia hoja ya Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme katika pongezi zangu hizi nilikuwa natafuta maneno ya kumwambia kaka yangu Mheshimiwa Jerry, lakini kati ya maneno nitakayompa kama zawadi leo akitoka hapa naomba aende akasome Kitabu cha 1Wafalme 3:16 – 24 akaangalie Hekima za Suleiman. Kila tukikaa tukimtafakari kwa umri wake, Mwenyezi Mungu amempa zawadi kubwa na kitu kikubwa. Amempa zawadi ambayo aliwahi kupewa Suleiman, zawadi ya hekima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya vitu ambavyo viongozi tunapaswa kuwa navyo ni pamoja na kuwa na hekima. Mungu hugawa kwa mafungu na mipango. Kati ya mipango aliyoifanya na katika fungu alilompa, kampatia fungu kubwa. Dada yangu Mheshimiwa Hokororo alisema mvi za Mheshimiwa Waziri ni hekima. Nampa jibu lake kwamba amempa Hekima za Suleiman. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo hekima nazo zitunzwe, zifanyiwe kazi kwa maslahi ya Watanzania. Ndani ya Bunge na Tanzania amekuwa Suleiman wetu. Akawasaidie Watanzania na awatendee haki, asiwe muoga, asiogope, sisi tunamwombea ulinzi. Tunamtegemea sana. Ili kazi ziende ndani ya Tanzania, ni lazima tukubali kama viongozi kuwa kafara, lazima kama viongozi tukubali kujitoa Watanzania wapone. Mama Dkt. Samia amekubali kujitoa kwa ajili ya Taifa la Tanzania. Amekuballi kubeba mazito, msalaba wa chuma na kuelemewa, lakini anasema Tanzania lazima iwe salama, Watanzania lazima wapone na matatizo yao lazima yatatuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu Mheshimiwa Waziri Jerry namwomba akubali kubeba ambacho Watanzania wanakitegemea kwake. Yeye kwetu amekuwa Isaka. Kati ya kondoo aliowaangalia Mama Dkt. Samia akaona kwamba, nani atakayekuwa kafara, yeye ndio amekuwa kafara ya Watanzania kwenye suala la ardhi. Ardhi ya Watanzania ili watu wagawane vizuri, Watanzania wanyonge wapate haki, Mtanzania asiyekuwa na fedha apate haki, lazima utoke kaka, lazima uwe kafara. Usiogope, hili ninakuhakikishia hakuna kitakachokudhuru, chozi la mnyonge ndiyo uponyaji wako, shukrani ya mnyonge ndio uzima na ulinzi wako ndani ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watakulinda kupitia maombi yao na shukrani zao, awatendee haki. Mfikirie mtanzania aliyekuwa mnyonge kila anapokwenda kwenye Mahakama na anaitafuta haki anaikosa. Yeye leo akawe mkombozi wake, Mungu atamlinda. Mwenyezi Mungu atampigania, hakuna kitu kitakachomdhuru wala mwiba utakaomtoga katika kutafuta haki ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo zilikuwa salama zangu kwake za kumpa moyo. Nina mambo manne ambayo nataka nizungumze siku ya leo katika mchango wangu. Jambo la kwanza, hapa nilikuwa nasoma *message,* kuna watu baada ya kusikia jina langu limetajwa wanatoka katika Halmashauri ya Ilala, wameniambia Mheshimiwa Tauhida sahau kila kitu, tunakuomba utusaidie. Tusemee kuhusu Kliniki ya Ardhi iendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo ambayo niliyoyapanga kuyasema ni pamoja na Kliniki ya Ardhi. Ile Kliniki ya Ardhi wakati inawekwa kuna watu wanatoka Zanzibar ambao waliolewa, walioa, wazee wao wanaishi Tanzania Bara, wamedhulumiwa wakati wazee wao wamefariki, unapoweka Kliniki ya Ardhi wanakuja kutafuta haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri atafute mzunguko wake endelevu kuona kila muda kipindi fulani kila mkoa, jimbo ikiwezekana na wilaya kuwe na hii Kliniki za Ardhi, kwani ni majibu tosha ya Watanzania. Hatuna njia rahisi ambayo tunaweza kutatua. Hii Kliniki ya Ardhi ndiyo imeenda kuleta majibu

fasaha kwa Watanzania, maana matatizo yao yanatatuliwa papo kwa papo na haki yao inapatikana papo kwa papo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, mipango mizuri ya ardhi na matumizi mazuri ya ardhi ni kitu ambacho kitaenda kuondoa migogoro ndani ya Tanzania. Migogoro ili iweze kuondoka, Waziri lazima akubali kuwa na matumizi mazuri ya ardhi, na ili mipango yetu iende vizuri, lazima kuna Wizara zikubali kushirikiana ikiwemo TAMISEMI, Kilimo na Mifugo. Wekeni mipango mizuri ambayo itaenda kumkomboa Mtanzania ili tuweze kwenda vizuri na tuweze kupata majibu mazuri kwenye matumizi mazuri ya ardhi. Ni lazima tuwe na mipango mizuri ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii angalia mifumo ya vijiji vyetu vilivyo, hata maendeleo kwenda kwao vinakawia. Kijiji kimoja kipo huku kingine kipo kule. Kufikiwa na miundombinu inakuwa kazi ngumu, Tanzania tunajipa mzigo mkubwa kwa sababu hatujipangi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umri wa Mheshimiwa Waziri ni mdogo, anaweza kukimbia, anaweza ku-*trot.* Akiona muda unakwenda, aache kwenda kwa miguu, a-*trot,* akimbie, ili Watanzania wapate majibu kazi ipate kwenda vizuri. Kwenye mifumo ya upangaji wa ardhi, hii itaenda kutupatia jibu pia itaondoa migogoro, kwani migogoro mingi inasababishwa na kutokujipanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza wenzetu waliotangulia kwenye Mji wa Dodoma, kwa sehemu kidogo wamejitahidi kupanga panga kidogo, lakini kuna maeneo mpaka leo, hivi vyote tunavyozungumza hakuna Afisa wa Ardhi anaona umuhimu wa kupanga mipango mizuri ya matumizi ya ardhi ndani ya halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri aangalie namna bora ambayo itaenda kuleta majibu endelevu. Hatutaki majibu ya muda mfupi. Wewe leo upo hapo, kesho unaweza ukapelekwa kwingine na kesho ukafanya mengine, bado Tanzania inakuhitaji kwenye sehemu tofauti. Sasa pale

tukiweka mipango endelevu kwamba ili ardhi itumike, na wananchi waweze kufanya kazi zao na kutumia ardhi katika shughuli zao, lazima tuhakikishe mipango mizuri ya ardhi inapangwa na inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niomba Mheshimiwa Waziri aimarishe kitengo chake cha utoaji wa hati. Kiimarishwe na kipewe nguvu. Kama hakina fedha, kipelekewe fedha, kama hakina gari kipatiwe magari, kama hakina kompyuta kipatiwe kompyuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro mikubwa ya wananchi wa Tanzania katika suala la ardhi ni pamoja na kutokupata hati kwa wakati. Muda anavyokawiza mtu kupata hati yake kwa wakati ambao yeye amemiliki kiwanja, hicho ndicho kinachosababisha hao madalali waliokuwepo ndani ya Wizara, hao makanjanja wanaotumika, ndio wanaobadilisha matumizi ya mtu mmoja kwenda mtu mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ana uwezo wa kutoa maamuzi magumu, amsaidie Mheshimiwa Rais wa Tanzania, kwani anapambana, anatafuta fedha kwa ajili ya bajeti zetu, anaweka kila namna ya mipango kuona kila Wizara inafanya vizuri. Waziri kazi yake ni kupanga na kumshauri Rais ili tuweze kutoka hapa tulipokuwepo. Kama kuna wafanyakazi wabovu watolewe, tunataka tuone anaondoa wafanyakazi wabovu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wanalalamikiwa wabovu wapo chungu mzima.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha tafadhali.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja, namtakia kila la heri Mheshimiwa

Waziri, tuna matumaini na imani kubwa juu ya ufanyaji wake wa kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tauhida Gallos Cassian. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Ally Issa Mchungahela, atafutiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga ajiandae.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kunijalia uhai na afya njema. Nawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Lulindi kwa kuniombea dua njema; mamshukuru mke wangu na wanangu kwa ujumla kwa kuniombea dua njema; na pia nawashukuru wananchi wote wema, kwa kuniombea dua njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, mchango wangu nitajikita katika eneo moja tu, hili litakuwa ni eneo la upimaji wa ardhi na mipango miji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi iliyopimwa inaweka mipango mizuri ya matumizi yake. Ardhi iliyopimwa inatuonesha waziwazi wapi pa kujenga nyumba za kuishi, kulima, kufuga, kujenga viwanda, kuweka miundombinu ya kupumzika na michezo *(recreation centers)*. Pia inaweza kuweka wazi wazi wapi pa kujenga shule, hospitali, ofisi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi iliyopimwa inaonesha waziwazi wapi ni maeneo ya akiba, na pia inaonesha kila kitu kinachohusiana na ardhi. Ardhi iliyopimwa ndugu zangu ni fedha, na ardhi iliyopimwa ni dhamana. Benki itakukopesha kirahisi ukiwa na ardhi iliyopimwa. Ardhi iliyopimwa ni kinga ya umaskini. Ukishakuwa na njaa utauza ardhi yako kirahisi lakini hali kadhalika unaweza ukaiwekeza kirahisi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi iliyopimwa ni kinga ya majanga. Kipindi cha mafuriko ardhi iliyopimwa inaonyesha miundombinu wapi pa kwenda kukabialiana na majanga hayo; ardhi iliyopimwa inatuonesha wazi wazi wapi tutapata maji kwa maana ya zimamoto, wanafahamu ni wapi tutaenda kuchukua

maji kwa ajili ya kuzima moto, pia vifaa na vitendea kazi vitapita kwenye maeneo gani katika ardhi hiyo ili kufikia janga mahali lilipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi iliyopimwa ni kinga kwa tetemeko; ardhi hii imekuwa ni bora sana wakati wa matetemeko kwa sababu nyumba zimewekwa kwa mpangilio kiasi kwamba hata itakapoanguka nyumba moja kutakuwa na ugumu kwa nyumba nyingine kuathirika, kama kwa watu walioko kwenye nyumba za karibu karibu kama zile ambazo ardhi hazijapimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ardhi iliyopimwa ni njia na kinga ya kuondokana na magonjwa. Kipindi cha mvua maji hayawezi kutuama na kusababisha magonjwa yanayosababishwa na uchafu kama vile kipindupindu, malaria na magonjwa mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ardhi iliyopimwa ni kinga ya migogoro. Kukiwa na ardhi iliyopimwa aghalabu huwa inakuwa na migogoro. Pia ardhi iliyopimwa ni urithi thabiti na kizazi kinachokuja, kwa nini nimeongelea haya? Nimeongelea haya kwa sababu hakuna kitu chochote cha muhimu kama nchi hatujaweka mipango yetu vizuri kwenye ardhi. Ardhi ni urithi mkubwa wa asili kwa dunia ambao tumepewa kuliko maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijikite kwenye Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali, inayoonyesha matumizi hafifu ya ardhi. Kwa ripoti ya mwaka 2023 inaonyesha kwamba, Tanzania kiasi cha ardhi kilichopimwa ni 25% pekee. Pia ripoti inaonesha kuwa, kuna makazi holela takribani 70%, kwa maana hiyo wananchi wa Tanzania 70% wanakaa katika makazi holela. Hili siyo jambo dogo hata kidogo. Nafikiri tunajua jinsi gani tunatakiwa tuanze kujielekeza katika eneo la kupima ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia utafiti uliofanyika katika halmashauri mbalimbali umeonesha, kumekuwa na uibukaji wa maeneo yasiyokuwa rasmi. Majengo yanayojengwa katika maeneo yasiyopimwa, kwa maana hiyo makazi holela, kwa mfano ripoti ya *New Urban Agenda*, inaonyesha kabisa kuna

takribani nyumbani 1,444,000 kwa makazi holela. Sasa ukichukulia idadi ya nyumba ambazo tumezijenga, unaweza ukaona ni kwa kiasi gani tunaishi katika makazi holela. Hili siyo jambo jema, hususan wakati kunapotokea masuala ya majanga, kama nilivyozungumza hapo mwanzo, na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Ripoti ya Utekelezaji wa Wizara imetuonesha kwamba, kwa miaka tofauti tofauti kumekuwa na nyumba zilizojengwa kwenye makazi holela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2019/2020 takribani nyumba au majengo 348,918; mwaka 2020/2021 kuna takribani nyumba 741,645 holela na mwaka 2022 takribani nyumba 452,806 ambazo ni holela. Kwa hali hii inaonesha wazi wazi kwamba, tatizo hili ni kubwa, kama nilivyoanza kulizungumza hapo mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, makazi holela yameonekana katika halmashauri zote. Halmashauri ya Arusha inaongoza. Ni kitu cha kushangaza sana, lakini ndiyo inayoongoza kwa makazi holela. Takribani 95% ya makazi yaliyopo ni holela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kuzungumza hayo niliyoyazungumza, kutokana na ufinyu wa muda, naishauri Wizara kujielekeza moja kwa moja katika kuharakisha upimaji wa maeneo ya nchi, ili kupata uhakika wa ardhi iliyopo kwa vizazi vinavyokuja hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Issa Mchungahela. Sasa namwita Mheshimiwa Joseph George Kakunda na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, ajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kutoa pongezi nyingi sana kwa Serikali kwa ujumla, hususan Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, timu yote ya Wizara pamoja na

Kamati husika kwa jinsi ambavyo wamechambua haya mambo mpaka wamefika leo kutoa hotuba nzuri hivi. Namushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa umahiri wake. Nampongeza sana kwa umahiri wake na ninawapongeza viongozi wote waliohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile 4R za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan zinatuhusu Watanznaia wote, lakini Sekta hii ya Ardhi hasa hasa inahusika zaidi na R ya tatu na R ya nne. Katika R ya nne, Kulijenga Taifa, hatuwezi kulijenga vizuri upya Taifa kwa maana ya miradi ya miundombinu, majengo ya biashara na makazi, majengo ya huduma za jamii na huduma za jamii kwa ujumla na ujenzi kwa ujumla bila kufanya maboresho makubwa kwenye Sekta ya Ardhi au *Land Reforms*. Hatuwezi kupata maendeleo endelevu katika nchi *(Sustainable Development)* bila kufanya *land reforms*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaalamu mmoja wa maboresho ya Sekta ya Ardhi duniani aitwaye Raleigh Barlowe katika andiko lake lililochapishwa mwaka 1953 katika *Journal of Farm Economics*, *Volume* ya 75, Na. 2, Uk. 173 – 187 katika mada iitwayo, *Land Reform and Economic Development,* amesema, ninanukuu: "*Land reform is often treated as a necessary or highly desirable condition for economic development, although it might also be viewed as a partial consequence of the development process.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba maboresho ya Sekta ya Ardhi ni sharti muhimu la maendeleo ya kiuchumi, ingawa vilevile wakati mwingine maboresho ya Sekta ya Ardhi yanaweza kufanyika kupitia matokeo ya mchakato wa maendeleo. Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo analolishauri mtaalamu huyu ni kwamba, ili tupate maendeleo ya haraka ni lazima maendeleo hayo yawe *guided* na maboresho ya Sekta ya Ardhi. Siyo maendeleo yapatikane kwanza halafu ndiyo tuje tuboreshe Sekta ya Ardhi. Hayo ndiyo makosa ambayo tumeyafanya miaka yote ambapo Sekta ya Ardhi imekuwa nyuma ya maendeleo ambayo wanayafanya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tumepata matatizo mengi ya kuwa na ujenzi holela katika miji mingi, makazi duni, holela, nyumba zisizo na viwango ambazo zimekuwa zikisababisha ajali mara nyingi, makazi yasiyo na huduma za miundombinu, migogoro mingi ya ardhi, watu wetu kukosa dhamana kwa ajili ya kukopa kwenye benki, watu wa vijijini kukosa dhamana hata kama wana Hati za Kimila na hizi Hati za Kimila hazitambuliki na benki. Haya ni matatizo ambayo yamesababishwa na kutokuwa na *land reforms* ambazo zina-*guide* maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi chache ambazo ni muhimu sana kwa Wizara hii. Juzi katika semina wametupitisha kwenye Sera ya Ardhi ambayo imefanyiwa mapitio na wametuahidi kwamba, baada ya sera sasa watakuja na Mkakati wa Taifa wa kutekeleza Sera ya Ardhi. Hii ni tofauti na walivyofanya mwaka 1995, baada ya kuwa tumepata Sera ile ya Ardhi ya mwaka 1995 walikuja wakatengeneza Sheria za Ardhi, mwaka 1999.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sera ilifuatiwa na Sheria badala ya mkakati. Kwa hiyo, baada ya Sheria ya Mwaka 1999 ndiyo wakaja wakatengeneza kitu kinaitwa Mkakati wa Kutekeleza Sheria. Mimi nilikuwepo katika Timu ya Wataalamu ya MKUKUTA wakati ule na tulikuwa tunabishana na Wataalamu wa Sekta ya Ardhi, tunawaambia mmefanya makosa, utekelezaji kwenye Sekta ya Ardhi utakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana utekelezaji wa Sekta ya Ardhi kuanzia mwaka 1999 mpaka sasa mwaka 2024 bado hawajapata mafanikio makubwa kwa sababu walikosea. Kwa sasa hivi kama unakuja na ile *plan continuing* kwamba, unatoka kwenye sera, halafu unakuja kwenye mkakati, halafu baadaye unakwenda kwenye sheria, halafu ndiyo uje kwenye mpango, hapo kitakuwa ni kitu kizuri. Nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake yote, ninaamini sasa mambo haya yatakuja kuwa mazuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi ya pili naitoa kwenye Wilaya ya Sikonge. Nimearifiwa na Kamishna Msaidizi wa Ardhi wa

Mkoa wa Tabora kwamba tayari mpango umeshakamilika. Ifikapo mwaka 2026 vijiji vyote vya Wilaya ya Sikonge vitakuwa vimepimwa, mipango ya matumizi bora ya ardhi na kwa kweli, hatua hiyo ni kubwa sana. Haijafanyika kwa muda mrefu, hii ni pongezi kubwa sana kwa Wizara ya Ardhi. Nampongeza Kamishna Msaidizi wa Ardhi, aendelee na Mpango huo ausimamie ili uweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwneyekiti, nina ushauri katika maeneo machache. Ninaishauri Wizara ya Ardhi, iandae mkakati wa kutekeleza hii sera mpya ambayo imewasilishwa juzi. Mkakati wa sera uandaliwe kwa umakini mkubwa kugusa maeneo yote ili sera itekelezeke vizuri zaidi, halafu baada ya hapo wafanye mapitio makubwa ya kuja na sheria mpya za ardhi. Baada ya sheria waje na mpango wa mwaka mmoja, mipango ya miaka mitano na mipango ya muda mrefu, miaka 20 na kuendelea, ambayo itai-*transform* sekta ya ardhi iweze kusaidia maendeleo ya nchi yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna sababu kwa nini mtu wa mjini apate Hati ya Ardhi ambayo inatolewa na Wizara ya Ardhi, halafu mtu wa kijijini apate Hati ya Kimila. Katika mabadiliko ya sheria mtakayoyaleta ni muhimu sana itolewe Hati ya Ardhi Mjini na Vijijini, ili mtu wa mjini awe na uwezo wa kukopa benki na mtu wa kijijini awe na uwezo wa kukopa benki. Huu utaratibu wa Hati za Kimila hautambuliwi na benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima mwatendee haki Watanzania wote wanaoishi mijini na vijijini. Ardhi yote inayomilikiwa na wananchi ipimwe ili kila kipande ambacho anamiliki mwananchi kijulikane ili kuondoa migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali ije na mpango wa ujenzi wa nyumba bora. Haiwezekani tangu uhuru hatujaweka *ultimatum* ya ujenzi wa nyumba bora. Zamani kulikuwa na Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wanasimamia mipango ya ujenzi wa nyumba bora, lakini Serikali kwa ujumla haijaja na mpango mahususi wa kuwasaidia wananchi wawe na ujenzi wa nyumba bora, tofali za kuchoma na mabati. Mnaweza mkawa na

mpango wa ruzuku kwa ajili ya vifaa vya ujenzi ili Watanzania wa-*transform* waje kuwa na nyumba bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, tuna mgogoro wa mpaka kati ya Tabora na Singida. Mgogoro ule ni kama vile umeisha, kilichobaki ni kuweka *beacon* na wawekaji wa *beacon* ni Wizara ya Ardhi. Naomba mje kwenye mpaka wa Tabora na Singida mweke *beacon* hata kesho ili kuondoa mgogoro wa mpaka kati ya Tabora na Singida ambao umekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, nilikuwa na maeneo haya ya ushauri ili kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa 100%. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa George Kakunda. Mheshimiwa Francis Isack Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu sana kwa sababu, hakuna jambo lolote linafanyika bila ardhi. Chochote kile tunachokifanya katika nchi hii au duniani, kinafanyika juu ya uso wa ardhi. Kwa hiyo, ni sekta au ni Wizara ambayo inabeba maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza tu kwa kumpongeza ndugu yangu Mheshimiwa Jerry. Pongezi alizozipata ni nyingi, lakini anastahili. Kwa hiyo, naomba tu kama walivyopongeza, hasa Mheshimiwa Tauhida, nami ni hivyo kama Mheshimiwa Tauhida alivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita zaidi kwenye jimbo langu. Yako mambo mengi ya kusema, lakini kubwa nataka tu niseme juu ya migogoro midogo midogo na mikubwa ya mipaka na mashamba. Naanza na shamba moja kubwa lililopo Kata ya Kinyangiri, linaitwa Shamba la Makometi. Shamba hili ni mali ya Wizara ya Mifugo, lina hati, lakini limekuwa shamba pori kwa muda mrefu na mnafahamu madhara ya mashamba pori. Mashamba pori wananchi huwa wanaingia huko. Sasa, pale wananchi wa kutosha wameshaingia, wengine wamejenga humo, wengine wanalima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, japo bado kuna eneo kubwa limebaki, lakini mimi nakuomba Mheshimiwa Waziri, shamba hili sasa uende ukatambue upya mipaka, lakini kubwa zaidi uwatambue wale wananchi ambao wako mle kwa sababu, wameachwa muda mrefu. Maeneo yao mengine yameshakuwa makubwa kama kitongoji sasa, kwa hiyo, angalau hayo maeneo yarasimishwe na eneo kubwa la shamba pori lililobaki Wizara ifanye jambo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wizara imeshindwa, basi ituachie sisi Halmashauri ya Mkalama ili tulipangie matumizi ya maendeleo kwa sababu, tumekuwa tukililinda kwa muda mrefu, maana sasa Wizara haifanyi chochote. Matokeo ni wananchi wetu wanaingia halafu baadaye watakuja kutolewa, watakuja kupata shida sana, watakosa mahali pa kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sasa kuna wengine wamezaliwa humo wanaamini hayo ndiyo maeneo yao. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aje Mkalama atambue mipaka ya shamba hili la Makometi, shamba pori, ambalo lilikuwa ni kituo cha mifugo. Wananchi ambao wameingia humo watambuliwe wafanye mambo yao kwa uhuru, lakini eneo lililobaki basi Wizara ifanye kitu ama itukabidhi Halmashauri tuendelee nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu migogoro ya mipaka kati ya Wilaya ya Mkalama na Wilaya za jirani. Upo mgogoro wa mpaka kati ya *Singida DC* kwa ndugu yangu Mheshimiwa Ighondo pale katika Kijiji cha Ntondo. Kuna mgogoro pale unasumbua sana wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mgogoro kati ya Wilaya ya Iramba na Mkalama, katika Kijiji cha Kisana, Kata ya Gumanga. Kijiji kizima wameingia, karibu kitongoji kimeingia kwetu, lakini wao kwa sababu asili yao ni kule Iramba, wanataka waendelee kutii mambo ya kule wakati tayari wako kwetu. Kwa hiyo, naomba migogoro hii ifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mgogoro kati ya Kijiji cha Milade na Wilaya ya Ikungi katika Kijiji cha Munyu; upo mgogoro kati ya Kijiji cha Milade na Kijiji cha Mgungia; pia upo mgogoro

kati ya Kijiji cha Maruga, Iramba, na Tumuli. Hii yote ni migogoro kati ya Wilaya ya Mkalama na Wilaya nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Wilaya ya Mkalama inapakana na mikoa miwili; inapakana na Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Arusha. Huu mpaka wa Mkoa wa Manyara na Arusha na Wilaya yangu ya Mkalama imekuwa ni tatizo kubwa na la muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza swali hapa Bungeni na nikajibiwa kwamba, watakwenda wataalamu kule, lakini mpaka hivi ninavyoongea mgogoro huu haujaisha. Mgogoro huu una madhara makubwa. Wako Wahadzabe wanaishi kule katika Kata yangu ya Mwangeza, hawa watu bado wanakula asali, nyama na mizizi, na kwa kuwasaidia imepatikana miradi, tukaamua tuwawekee mizinga kule ili tuwapatie asali, maana zamani asali ilikuwa inapatikana kwenye vichuguu. Siku hizi hakuna asali ya kwenye vichuguu, kwa hiyo, tukawapatia mizinga, lakini wenzetu wa Mkoa wa jirani wakaja wakateka, wakavunja ile mizinga wakisema kwamba eneo lile ni lao wakati siyo lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aje Mkalama, aje Mkoa wa Singida, atuite. Aite Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, na sisi Wabunge wote twende kwenye mpaka tutambue. *GN* ipo, mipaka huwezi kuhamisha, ile *GPS* huwezi kuihamisha, tusomeeni pale mpakani ili kila kitu kieleweke. Sisi tumeshajiandaa maana unaweza ukawakosa wapigakura au ukaongezewa wapigakura. Sasa ukweli ukishasimama pale mambo yote yataeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri jambo hili alichukulie maanani, limeanza muda mrefu sana mpaka tumenyang'anywa mnada pale Kijiji cha Endaragati na wenzetu wa Manyara wakauchukua ule mnada, tuna uhakika ni wa kwetu, tukisoma ninajua kabisa ule unarudi. Kwa hiyo, ndugu yangu Mheshimiwa Flatei ajiandae tu pale, yale mapato atayakosa iwapo Waziri atakuja kusoma vizuri ule mpaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba niongelee suala la Baraza la Ardhi, Mabaraza ya Ardhi ya Kata. Nchi yetu ni kubwa sana. Baraza la Ardhi la Wilaya kushughulikia migogoro ya Wilaya ni mzigo mkubwa sana. Nakuomba Mheshimiwa Waziri arudishe ile *system* ya Mabaraza ya Ardhi ya Kata kutoa hukumu, lakini ayaboreshe, yapelekewe Wenyeviti ambao ni *professional* kama yalivyo Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu hatuna upungufu wa *human resource*. Wako vijana wengi mtaani wamesoma sheria, wamesomea uhakimu, wanasubiri ajira. Haya Mabaraza ya Ardhi ya Kata yakiimarishwa haki itatendeka kule chini. Kitendo cha mwananchi mnyonge kwenda kwenye Baraza la Ardhi la Wilaya ni mgogoro mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeshuhudia, mwenyewe niliuziwa ardhi na jamaa, halafu kumbe katuuzia wawili akataka anidhumulu kwa sababu mimi ni Mbunge, nitaogopa wapigakura. Nikaona hebu ngoja niende kwenye Baraza la Ardhi la Wilaya nikapate haki yangu. Mwaka mzima na siyo makusudi, wale Wenyeviti wameelemewa na kesi. Maana uende ukasajili, utoke hapo uwaite mashahidi, wewe usikilizwe, asikilizwe mwenzako, alete mashahidi wake, sijui yaani mpaka ule mlolongo wa kesi uje uishe ni mwaka na yote hiyo ni gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wanyonge wengi wameamua kuacha hizi kesi, wamedhulumiwa. Amekosa nauli yake mwenyewe, lakini leo anatakiwa abebe mashahidi, abebe sijui watu gani wakasikilize kesi. Inafika mahali wanaamua kuacha. Kama mimi Mbunge nimetoka jasho, mwaka mzima, kila siku ninachoma mafuta na siyo makusudi, siyo kwamba wale Wenyeviti wanafanya makusudi, ana mlolongo wa kesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anakaa kuanzia saa nne mpaka saa 12 jioni kusikiliza kesi za ardhi. Sasa nakuomba Mheshimiwa Waziri arudishe Mabaraza ya Ardhi ya Kata yatoe hukumu, ila yaboreshwe, yapelekewe Mahakimu *professional* ili watoe hukumu. Haya Mabaraza ya Wilaya yawe Mabaraza ya Rufaa, yatakayoshindikana kule kwenye Kata ndiyo yaende kwenye Wilaya. Hapo tutakuwa tumemsaidia mnyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanyonge wanateseka sana, wengi wameacha ardhi zao na watu wenye fedha wanafanya makusudi kabisa. Anachukua ardhi, anajua huyu atashindwa tu njiani kwenye kesi. Wale Wenyeviti hata rushwa hawachukui, wale ni kwamba, tu ile nenda rudi, nenda rudi, wananchi wanaamua kuacha, lakini ukweli ni kwamba, wameelemewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza wale Wenyeviti wanafanya kazi kubwa. Naomba niwapongeze, nimeshuhudia mwenyewe wanafanya kazi kubwa sana, kwani migogoro ni mingi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, arudishe Mabaraza ya Ardhi ya Kata yatoe hukumu. Maana sasa hivi yanafanya usuluhishi tu, hayatoi hukumu. Kwa hiyo, kwanza hayaheshimiki, lakini wapelekewe Mahakimu *Professional* ili watu wetu wapate haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata haya Mabaraza yatalinda hata hiki ambacho Wabunge wamekisema kila kona kwamba, tupime ardhi. Tukishaipima haioneshi kwamba wahalifu watakosekana. Wako watu watataka kuvamia eneo limepangwa la malisho wao wanataka walime, wengine eneo la viwanda, wao wanataka wajenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya Mabaraza ya Ardhi ya Kata kama yatakuwa yamewezeshwa vizuri, ndiyo yatakayotatua hii migogoro huko chini. Hata hiyo ardhi ukiipima itabaki kuwa salama kwa muda mrefu na itakuwa imewasaidia Watanzania. Kwa hiyo, ndugu yangu Mheshimiwa Waziri naomba sana kwa hili, aje Mkalama, atupimie mipaka na sehemu nyingine nchi itulie. Apime ardhi kama alivyosema, lakini awezeshe haya mabaraza ili wanyonge wa nchi hii wapate haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kumpongeza, hongera sana. Unajua kijana anapofanya vizuri, anasababisha mama aendelee kutuona vijana kwamba, tunaweza. Kwa hiyo, anatuwakilisha vizuri na ninampongeza mama yangu kwa jicho lake la kuona. Bunge hili ni kubwa, lakini akaona na amepatia, na muda wote hesabu za mama ni za uhakika, zinafunga magoli. Mama endelea kupiga hizi hesaby za uhakika ili wananchi wa Tanzania waendelee kufaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtinga. Waheshimiwa Wabunge, tunaelekea mwisho wa ratiba yetu ya jioni hii. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao mmepata kuchangia kwa niaba yetu na kwa niaba ya Watanzania, lakini pia ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na timu yako ya wataalamu ambao mmeendelea kupokea maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge.

Jambo moja tu la msingi ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelisisitiza ni kwamba, kama Wizara hii ingekuwa gari, basi kipuri kipya kwenye gari hili ni wewe Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu, lakini kwa sehemu kubwa timu ni ile ile. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wana imani kubwa na nyie, lakini wana mashaka kwenye maeneo ya huko kwenye utekelezaji ambako kwa muda mrefu imekuwa *business as usual* na wewe umekuja na Sera ya *Business Unusual*. Kwa hiyo, tunaamini wataalamu wako wanaokusaidia wamefuatilia mjadala huu na watahakikisha kwamba ndoto yako na ndoto ya Mheshimiwa Rais inatimia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninaahirisha Kikao cha Bunge mpaka Siku ya Jumatatu tarehe 27 Mei, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.00 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 27 Mei, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*